Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 19 Mei, 2014**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na mkutano wetu wa Kumi na Tano kikao cha leo ni kikao cha kumi na mbili. Katibu.

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na :-

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**NAIBU WAZIRI WA WAZIRI WA UJENZI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 76

**Serikali Kujenga Nyumba za Walimu**

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA** aliuliza:-

Shule nyingi za msingi zina upungufu mkubwa wa nyumba za walimu na hivyo kusabaisha walimu kuishi katika mazingira magumu na kutoripoti katika shule kama Nyamsebehi, Mnekezi, Shilabela, Buyagu, Kageye, Ntono na Nyasalala katika jimbo la Budana.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga nyumba za walimu katika shule hizo na nyingine ili kuboresha mazingira ya walimu kufanya kazi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lolesia Jeremeah Bukwimba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imedhamiria kukabiliana na tatizo la nyumba za walimu nchini kwa kuanzisha mpango wa endelevu wa kujenga kwa awamu kila mwaka. Kwa mwaka huu wa fedha 2103/2014 Serikali imetenga shilingi bilioni 20 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu katika halmashauri 40 na kila halmashauri imetengewa shilingi milioni 500.

Aidha, kati ya mwaka 2009, hadi mwaka 2012 Serikali ilitoa katika mamlaka katika Serikali za Mtaa shilingi 12.9 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu kupitia *program* ya Mpango wa Maendeleo ya Msingi na Mpango wa Maendeleo ya elimu ya Sekondari na Halmashauri ya Wilaya ya Geita ilipata shilingi milioni 134.
Serikali itaendelea kutenga fedha za ujenzi wa nyumba kupitia *program* za Mpango wa Maendeleo Elimu ya Msingi na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari na Ruzuku ya Maendeleo katika mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuajiri na kuwapanga walimu kadiri wanavyohitimu na kulingana na uwiano wa mahitaji kwa halmashauri kila mwaka.

Aidha, Serikali imefanya maboresho makubwa katika mazingira ya kuwapokea walimu wapya kila wanapopangwa. Kwa ajira mpya ya mwaka 2014 Halmashauri ya Wilaya ya Geita ilipangiwa walimu wa shule za msingi 341 na hivi sasa taarifa tulizonazo wameripoti walimu 340 na walimu wa shule za sekondari 124 waliopangwa na walioripoti hadi sasa ni walimu 120. Walimu

hawa wamepangwa pia katika shule za msingi alizozitaja Mheshimiwa Mbunge za Buyagu, Kayege, Mneke, Mtono na Nyamisebei.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Naibu spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri kwa sababu inaonyesha kwamba ina mpango mzuri kwa ajili ya ujenzi wa nyumba. Sasa ningependa kujua kwamba je, kati ya hizo halmashauri 40 zilizotengewa fedha kwa kila halmashauri milioni 500. Halmashauri ya Wilaya ya Geita ipo katika mpango huo?

La pili, kwa kuwa walimu wanaishi katika mazingira magumu sana hawana nyumba hawana kitu chochote na mazingira yao ni magumu sana katika shule nilizotaja kwa kweli walimu wetu hawa wanaishi katika mazingira magumu sana. Ningependa kuuliza Serikali kwamba haioni sasa ni wakati muafaka wa Serikali kuweka utaratibu maalum wa kuweza kuwapa hata kama ni kiasi cha fedha kwa ajili ya kuwawezesha hawa walimu waliopo katika mazingira magumu sasa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ambalo anahitaji kujua kama je, Wilaya ya Geita imo kwenye mpango huu wa awali. Katika mkoa wa Geita tumeanza na wilaya kama Mbogwe, ambazo ndiyo wilaya mpya ambazo bado ziko katika mazingira magumu kama ambavyo nimeeleza.

Mgao huu wa halmashauri 40 tumeanza na zile ambazo ziko katika mazingira magumu, baadaye tutakuja kwenye halmashari ambazo zinahitaji pia kuboreshwa kama ambavyo tumeeleza Geita kwa sababu ina walimu wengi wa kutosha. Kwa hiyo, bado tumeendelea kuiweka katika mpango ambao mwaka huu kupitia Bajeti ya fedha ambayo tumeitenga tunaweza pia kutoa majibu hayo.

Swali la pili, sikuweza kulielewa vizuri, nilikuwa naomba arudie, aliweke vizuri ili niweze kumpa majibu sahihi.

**NAIBU SPIKA:** Kwa kifupi Mheshimiwa Lolesia.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Nilikuwa napenda kuuliza kwamba kuwepo posho maalum kwa ajili ya walimu walioko katika mazingira magumu ningependa kujua.

Je, Serikali mpango huo inao?

**NAIBU SPIKA:** Yaani walimu walio katika mazingira magumu kama kule Kongwa hivi una mpango gani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Naibu Spika, swali hili nimepata kulijibu mara nyingi na kulifafanua mara nyingi kwa sababu pia hata walimu wetu wanahitaji kujua mwelekeo wao kwenye utumishi hasa walio katika mazingira magumu. Ni kweli kwamba Serikali tunao mpango wa kuhakikisha kwamba walimu wetu wanakuwa katika mazingira mazuri.

Hatukutenga fedha kwa ajili ya kumlipa mwalimu mmoja mmoja kwa sababu walimu hawa baadaye watahama kutoka kwenye mazingira ambayo tumeyabaini kuwapeleka kwenye maeneo mengine kwa hiyo, lile suala la kifedha linaweza kuwa gumu katika hamisha mara kwa mara. Tulichokifanya ni kuhakikisha kwamba maeneo yote ambayo yana mazingira magumu tumefanya uboreshaji wa kuhakikisha kwamba walimu hawa wanapofika pale mazingira yawe mazuri, ikiwemo na mpango wa ujenzi wa nyumba.

Kazi hii tumeifanya pia kwa shule za sekondari na za msingi pale ambapo tumeanzisha *program* ya ujenzi wa nyumba zile 1200 na sasa tumeanza na shule 264 tutakuja na shule 528 na baadaye 408 ili kuzifanya shule hizi kuwa miundombinu inayoridhisha kwamba mwalimu anapofika kwenye maeneo anakuta mazingira yako vizuri. *(Makofi)*

Mpango wa pili ni huu ambao nimeueleza tumeanza na kutenga fedha bilioni 20 kwa ajili ya Halmashauri hizi 40 kila Halmashauri tumeitengea milioni 500 kwa lengo la ujenzi wa nyumba ili mwalimu akifika aweze kukuta mazingira yanaendelea kuwa vizuri.

Lakini mpango wa tatu, ni ule ambao sasa Halmashauri zenyewe kupitia mabaraza yao, lazima tumewaagiza kutenga fedha kwa ajili ya kuboresha mazingira ya shule zilizo pembezoni ili mwalimu anapokwenda aweze kufanya kazi yake vizuri mahali salama.

Lakini huku pia Serikali ikiendelea kuboresha maslahi yao kupitia mpango ambao umeanzishwa kuanzisha bodi ya motisha na mishahara ambayo imeundwa na iko ya chini ya utumishi kwa lengo la kuboresha mafao yao watumishi wote katika mamlaka ya Serikali za mitaa wakiwemo walimu. Haya yote matatu, na mipango ambayo sisi tunaendelea kuipanga itasaidia sana kwenye maeneo yaliyopo pembezoni kuwawezesha watumishi wetu kuishi na kufanya kazi yao vizuri zaidi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Waziri lakini ni ukweli usiofichika kwamba tatizo la makazi kwa wafanyakazi wa Halmashauri hasa katika Halmashauri zilizoko pembezoni bado

ni tatizo. Nataka kumwambia Mheshimiwa Waziri hivyo haoni sasa kwamba sasa iko haja ya kuitumia *LAPF* ambayo inakusanya mafao ya watendaji wa Halmashauri waweze sasa kujiingiza kuongea nao, ninyi Serikali waweze kujenga hizi nyumba za wafanyakazi kwa mkopo.

Badala ya fedha zao ambao watendaji wa Halmashauri wanazichanga kwa *LAPF* kujenga magorofa hapa Dar es Salaam, Dodoma na kadhalika ili fedha hizi sasa muweze kuzikopa kwa ajili ya kujengea hizi za wafanyakazi?

**NAIBU SPIKA:** Majibu ya swali hilo kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya *LAAC*. majibu hayo yatatoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, Mheshimiwa Majaliwa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikiri kwamba *LAPF* ni moja ya taasisi zilizoko ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI. Moja kati ya majukumu yake ni kutoa mafao kwa wananchama wake ikiwemo na mipango mbalimbali ambayo ipo imewekwa na *LAPF* pamoja na uwekezaji. Wazo hili ni nzuri na sisi ofisi ya Waziri Mkuu hatujazungumza na *LAPF* pekee, tumezungumza na mifuko yote ya hifadhi ambayo pia watumishi wa halmashauri zetu nchini wanaingia pia kwenye mifuko hiyo.

Kwa hiyo, mazungumzo hayo yameshafanywa na tumeanza kuona kila mfuko utakuwa umeweka program za ujenzi wa nyumba ikiwemo na *LAPF, NSSF, PPF* ni miongoni mwa wale ambao sasa wameamua kuwekeza kwenye majengo ili watumishi wetu waweze kupata nafasi za kujengewa nyumba za kupanga.

Lakini iko *program* pia katika mifuko hii, wanaanza sasa kuingiza *program* za watumishi hawa mmoja mmoja kupata nyumba za kukopa kwenye mifuko hiyo. Kwa hiyo, nalichukua hilo wazo kwa sababu *LAPF* ni yetu tuweze kuiwekea mkakati huu na kuwashauri ili waweze kujenga nyumba kwa ajili ya watumishi wetu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Wahesimiwa Wabunge, kwa sababu leo ni Wizara ya Elimu na Mafunzo na Ufundi, maswali mengine tutayashughulikia kwenye uchangiaji. Swali linalofuata ni la Wizara hii ni la Mheshimiwa Riziki Said Lulinda, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Lindi, Mheshimiwa Riziki.

Na. 77

**Kujenga Barabara ya Mchinga – Mnyangara**

**MHE. RIZIKI S. LULIDA** aliuliza:-

Barabara ya Mchinga – Kijiweni – Kineng'ene Nangaru – Mkwajuni hadi Matapwa hadi Mnyangara ni mbaya sana na imekuwa na kero kwa wananchi:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NAS SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Saidi Lulida, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli hali ya barabara ya Mchinga, Kijiweni, Kinengene, Nangaru, Mkwajuni, Matapwa, mpaka Mnyangara, siyo ya kuridhisha na hivyo kuleta adha kwa wananchi wanaotumia barabara hiyo.

Kwa kuzingatia hali hiyo, Serikali katika mwaka wa fedha wa 2012/2013 ilitenga shilingi milioni 112.1 kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya Mchinga hadi Kijiweni kilomita 37.3 na mkandarasi aliyepewa kazi ya matengenezo ya barabara hiyo alisimamishwa kazi na kulazimu Halmashauri kutafuta mkandarasi mwingine ambaye hivi sasa anaendelea na kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014 Serikali ilitenga shilingi milioni 57.3 kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya Mchinga, Kijiweni yenye urefu kilomita 57.3 na kazi ya ukamilishaji inaendelea. Aidha, shilingi milioni 81.0 zilitengwa kwa ajili ya matengenezo ya kawaida na sehemu korofi katika barabara ya Mipingo, Mnyangara yenye urefu wa kilomita 8.5 na kazi ya matengenezo inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa barabara hiyo, Serikali katika mwaka wake wa fedha 2014/2015 imetenga shilingi milioni 71 kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya Mkwajuni, Mipingo, Matapwa yenye urefu wa kilomita 16 na shilingi milioni 96 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya Chikonji – Nangaru, yenye urefu wa kilomita 22.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba Serikali inatambua adha wanayopata wananchi kuhusu barabara hiyo na imekuwa ikitenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kuifanyia matengenezo ili kuweza kupitika katika kipindi chote.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri amekiri kuwa mkandarasi aliyepewa kazi ya barabara ya Mchinga – Kijiweni kuwa ni mbabaishaji na barabara ameiacha kama alivyoiacha, na mpaka hii navyozungumza haijaendelezwa ile barabara na kuwa matumizi ya gharama ya pesa kwa barabara ile kuwa hayana maana yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri alitembelea Lindi na kujionea mwenyewe jinsi kazi zinavyofanyika, barabara za Lindi kuwa mbovu na akaahidi mwenyewe kuwa daraja la Mchinga atalisimamia na kuhakikisha kero ya daraja la Mchinga zimekwisha kwa vile huwezi kwenda Mchinga, pana mkondo wa bahari pale. Maji yakijaa wananchi hawawezi kwenda Mchinga. Sasa wanawake wakitaka kwenda kujifungua kwenda hospitali Mchinga B, hawawezi kwenda Mchinga A sasa.

Je, Waziri anatoa tamko gani kuhakikisha madaraja haya mawili ya Mchinga na la Mnyangara linapitika?

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya majibu ya baadhi ya Mawaziri wetu, hasa wa barabara wanajibu majibu ambayo hayawafanyi wananchi waridhike. Juzi tumepata majibu mabovu kutoka kwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Lwenge, kuwa barabara ya kutoka Nangurukuru kwenda Liwale, wananchi wanatembea kutoka Dar es Salaam mpaka Masasi, Masasi wanakwenda Liwale, anasema Serikali haina mpango. Majibu haya ni ya kifedhuli yanaudhi na yana kero.

**NAIBU SPIKA:**Mheshimiwa Lulida swali lako sasa moja kwa moja.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Je, Waziri atakuwa tayari kuomba radhi kwa wananchi wa Lindi kwa majibu ambayo hayakuwafurahisha?

**NAIBU SPIKA:** Matarajio yangu Serikali inatoa majibu ya ukweli na siyo kuwafurahisha tu wananchi. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali moja hili lingine kwa sababu Mheshimiwa yuko hapa atanisaidia. Kwanza nataka kukiri haya yote anayosema Mheshimiwa Lulida ni kweli mimi nimekwenda mimi nilikuwa sijui maana ya bavua mimi natoka Kilimanjaro bavua nilikuwa sijui maana yake

nikauliza bavua ni kitu mimi nikafikiri bahari ambayo inakuwepo wakati mwingine haipo wakati mwingine unaikuta na nini.

Hivi tunavyozungumza sasa hivi hapa mimi nimezungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Lindi, Mheshimiwa Grace Mbarouk.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri na mimi sielewi bavua ni kitu gani maana na mimi natoka Dodoma hapa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Ndio hiyo nayokueleza unajua mimi naieleza kwa lugha hiyo kwa sababu mimi sijui wakina Saida Mtanda na Riziki Lulida na wenzake wanaweza wakaeleza. Ni kwamba kuna wakati ambapo maji yanakupwa na kuna wakati maji yanakuwepo kuna wakati maji yanahama yanaondoka pale kwa kifupi ndiyo hiyo bavua inazungumzwa hapo. Sasa kipindi hiki kipindi tunachokizungumza sasa hivi mvua zinanyesha kule si za kawaida yaani ndiyo tatizo la msingi lililoko pale.

Hata kama mkandarasi anataka kufanya kitu chochote pale kazi hiyo haiwezi kufanyika. Nataka aniamini Mheshimiwa Riziki Lulida maana tumecheki na Engineer, tumecheki na Mkurugenzi Mtendaji leo hii asubuhi nimezungumza naye na anafahamu nasema nini. Nimetaka kujua hizi hela ambazo nazieleza hapa zimekwenda na ziko katika Halmashauri zimeshaingia katika akaunti yao. Huyu mkandarasi huyu mwingine anayezungumzwa hapa tulimkataa tukasema hatumtaki huyu nikacheki.

Je, alipewa hela, amechukua hela amekwenda nazo? Hakupewa hela, hela hizo ndizo zitakazotumika pale. Kwa hiyo, mkandarasi aliyeko hapo, huyu mkandarasi kinachomfanya sasa hivi ashindwe kuendelea Mheshimiwa Lulida ni kwa sababu sasa hivi mvua zinanyesha.

Kwa hiyo, ndiyo tatizo kubwa lililoko pale na aniangalie macho yangu, aangalie midomo yangu hili jambo hili tutalisimamia kwa sababu tumekwenda sisi wenyewe mimi nimekwenda nimehusika na jambo hili. Sasa hela zilizokwenda katika Halmashauri hii Bajeti yao, ilikuwa ni shilingi milioni 617, fedha ambazo *so far* zimeshakwenda pale milioni 268,715,000. Zungumza habari ya daraja unafahamu kwamba ni jambo kubwa hilo linazungumzwa pale, kwa hiyo linahitaji hela nyingi. Bajeti tuliyoipitisha sasa hivi ni bilioni mia mbili na, mwaka huu unaopita wa fedha tunaozungumza zilikuwa bilioni 151 ndizo zilizopelekwa kwa Taifa zima kwa nchi nzima.

Kwa hiyo, nataka nimdhibitishie tu kwamba hili jambo halitakuwa ni la kubabaisha hivi kama anavyosema hapa wananchi hawa wanapata shida

sana pale kwa hiyo, hatuwezi kupuuza yale yanayozungumza na Mheshimiwa Mbunge. Sasa hili lingine la pili mzee, hili kidogo na mimi….

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, nakushukuru Mheshimiwa Lwenge, swali la Mheshimiwa Lulida la pili linasema majibu yako ya juzi la barabara ya Nangurkuru Liwale majibu hayakufurahisha wananchi kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa swali lake alikuwa anauliza ni lini na nikaelezea kwamba kwa sasa hatuna mpango wa kujenga barabara hii lakini nikasema katika mipango ya baadae tutaiweka barabara hii kwa sababu sasa tumeanza kujenga barabara kuu. Nikasema kwa Mkoa wa Lindi tumeshajenga kilometa 333, bado kilometa 14 tu kumaliza barabara kuu. Nikasema tutakapomaliza hizi, ndiyo tutaingia awamu ya pili ya kujenga barabara za Mkoa.

Kwa hiyo, kama lugha ya kusema ukweli imewaudhi wananchi, naomba radhi. Habari yenyewe ni kwamba kwa sasa, maana kwa mwaka huu wa fedha hatuna mpango wa barabara hiyo. Lakini tutaijenga katika mipango ya baadaye.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Lulida habari ndiyo hiyo. Mheshimiwa Said Mtanda kwa ufupi sana.

**MHE. SAIDI MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa fursa niulize swali dogo la nyongeza. Barabara ya Mnyangara, barabara ile inayotoka Nangalu kwenda Milola baada ya kuonekana Mvua ni nyingi na mimi Mbunge kufanya mkutano na niliomba Halmashauri yangu isitishe shughuli hizo za ujenzi wa barabara wakati wa mvua kwa sababu fedha za wananchi zitateketea bila sababu yoyote ili kupisha mvua iishe na juzi niliagiza Halmashauri yangu wakandarasi wale baada ya kuridhika kwamba mvua hakuna sasa warudi kazini. Nimehakikishiwa juzi wamerudi kazini sasa swali.

Kwa kuwa barabara ya Nangalu hivi sasa wananchi baada ya kulima ufuta, barabara ya Nangalu haimo kabisa katika *program* hii ya fedha kutoka pale Moka kwenda Nangalu.

Je, Serikali iko tayari kuchukua hatua za dharura za kunusuru barabara hii ambayo haimo na fedha zake hazimo kama barabara zile nyingine zilivyotajwa ili wananchi waliolima ufuta mwaka huu wawe na uhakika wa kupeleka mazao yao sokoni? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri sijui kama utaifahamu barabara hiyo ya Nangalu huko kunakotajwa. Majibu kwa kifupi tafadhali!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu kama ifuatavyo:-

Kwanza Wabunge wote hawa wawili naomba niwashukuru sana kwa kazi nzuri ambayo wanafanya katika eneo lao hili ambalo tumezungumza hapa, wanafuatilia kwa karibu sana yeye na mwenzake wote wanafanya kazi nzuri sana. Mimi huu uelewa wote nilionao hapa umetokana na jinsi ambavyo wamekuwa wanafuatilia jambo hili. Sasa ninashukuru pia kwamba wanajua kwamba kuna tatizo hili la mvua ambazo zinanyesha hapa nah ii kwa kweli tunajibu kwa Halmashuri zote nchini.

Kwa sasa hivi ni kama vile kazi tumesimamisha kwa sababu ya mvua zinazonyesha, *otherwise* tukiruhusu waende pale watafanya halafu kesho unarudi kifusi kimebebwa na kila kitu kimeondoka halafu badaye tunarudi na hela zimeshalipwa pale.

Kwa hiyo, kule ambapo mnaona kwamba kumekuwaje, ni pale ambapo tunaona hali ni mbaya watoto hawawezi kwenda shule hawawezi kwenda sokoni wala hawawezi hospitali wala maeneo ya ibada na maeneo mengine, ndiyo tunajaribu kui- *intervene* kufanya vile. Hata hivyo, tunawaomba tuvute subira kidogo tutamaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuhusu barabara hii inayozungumzwa hapa anayosema Mheshimiwa Mtanda, ni kweli kama unavyosema ninaweza nisiwe na upeo mpana hasa kwa barabara hii anayozungumza. Lakini Bajeti zetu zinaendeshwa *in terms of priorities* na *normally priorities* hatu-*determine* sisi Wizara, ni kule kule. Kuna kitu kinaitwa *O and OD (Opportunities and Obstacles to Development)*.

Kwa hiyo, kama Halmashauri ikiona kwamba kwa kweli ni *priority you have to re-arrange your priorities* ili kuifitisha hii sasa iingie pale. Nikiruka tu hapa nikasema kwamba nitakwenda kufanya nitapata matatizo kwa sababu Mheshimiwa Said Mtanda ni mmoja mfuatiliaji sana, atanibana tena mbavu hapa.

Niseme tu kwamba nalichukua hili jina la hii barabara, tutakwenda kuangalia na hii Bajeti niliyotaja hapa. Tutakwenda kuangalia na vipaumbele vyao, kwa sababu hizi nyingine zote kama tulivyoeleza. Hapa tayari zimeshapangiwa na fedha zake zimekwenda pale ili na hii barabara iweze kuinginzwa katika mpango na tuweze kuishughulikia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana. Tuhamie Ofisi ya Rais Utawala Bora, swali litaulizwa na kaka yangu Mheshimiwa Hezekiah Ndahani Chibulunje, Mbunge wa Chilonwa.

Na. 78

**Nyumba za Watumishi wa Ikulu Chamwino Kutelekezwa**

**MHE. HEZEKIAH NDAHANI CHIBULUNJE** aliuliza:-

Kwa kuzingatia nia ya kuhamia Dodoma, Serikali ya Awamu ya Kwanza ilijenga nyumba kadhaa za watumishi wa Ikulu ndani ya Kijiji cha Chamwino Ikulu ambazo tangu wakati huo zimetelekezwa bila kukaliwa na mtumishi yoyote.

(a) Je, ni sababu zipi zilizopelekea nyumba hizo zisitumike na waliokusudiwa na kusababisha uharibifu mkubwa kwa nyumba hizo kutokaliwa kwa muda mrefu?

(b) Je, Serikali ipo tayari kuzikabidhi nyumba hizo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, ili zikarabatiwe na kutumiwa na watumishi wengine wa Serikali badala ya kuziacha ziendelee kuharibika?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII JINSIA NA WATOTO (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS UTAWALA BORA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa nchi Ofisi ya Rais Utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hezekiah Ndahani Chibulunje, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba za watumishi zilizopo Ikulu Ndogo Chamwino, zimedhamiriwa kuwa makazi ya muda ya watumishi wasaidizi na washauri wa Mheshimiwa Rais wakati wanapokuwa Chamwino.

Nyumba hizo hutumika kwa kutegemea ratiba ya Mheshimiwa Rais anapokuwa Dodoma. Hivyo, kuchakaa kwake kumetokana siyo tu na nakutokaliwa na walengwa bali pia nyumba hizi zimejengwa muda mrefu na kutokana na ufunyu wa fedha, imeshindikana kuzifanyia ukarabati.

Hata hivyo, Serikali inaendelea kuzikarabati kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Aidha, katika mwaka wa fedha 2014/2015 zimetengwa fedha shilingi bilioni mbili kwa ajili wa ukarabati wa nyumba hizo pamoja na mazingira yake.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika jibu la sehemu (a) kwamba nyumba zilizojengwa ndani ya kijiji cha Chamwino ni sehemu ya Ikulu Ndogo na ni kwa ajili ya makazi ya muda ya watumishi wanaombatana na Mheshimiwa Rais anapokuwa katika Ikulu hiyo. Hivyo, basi haziwezi kukabidhiwa kwenye Halmashauri ya Chamwino ili zitumiwe na watumishi wengine wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kuwa Chamwino ni Wilaya mpya yenye Changamoto nyingi likiwemo tatizo la ukosefu wa nyumba za kuishi watumishi na kulazimisha baadhi yao kuishi Dodoma Mjini.

Serikali imewasiliana na Uongozi wa Shirika la Nyumba la Taifa na kuwaomba wajenge nyumba za kupangisha Chamwino. Shirika hilo limekubali, Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino inaombwa kuwatengea viwanja na kuwasilisha rasmi maombi ya kujengewa nyumba na Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)*.

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri lakini niseme tu kwamba pamoja na kukubaliana naye madhumuni ya kujenga zile nyumba pale Chamwino dhumuni kubwa lilikuwa ni kusukuma mchakato wa kuhamia Dodoma na mara zote Serikali imekuwa ikitamka hapa Bungeni kwamba azma ya Serikali ya kuhamia Dodoma iko palepale.

Lakini wakati huo huo Wizara na Idara za Serikali zinaendelea kujenga Dar es salaam. Baadhi ya Taasisi na Idara za Serikali zilizokuwa zinafanyia kazi hapa Dodoma, zinarudishwa Dar es salaam na hivi karibuni Idara ya Maendeleo ya Ushirika ambayo ilikuwa kwa muda mrefu sana hapa Dodoma imeamuliwa kurejeshwa Dar es salaam.

Sasa nauliza, ni upi hasa uhalisia wa Serikali juu ya suala hili la kuhamia Dodoma?

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kutupa hii changamoto ya kutenga viwanja kule Chamwino. Namhakikishia kwamba viwanja vipo isipokuwa sasa namwomba awape msukumo Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)*, ili liweze kuja haraka Chamwino na kujenga nyumba za watumishi wa Halmashuri ya Wilaya?

**NAIBU SPIKA:** Jibu ya swali hilo pamoja na ombi, Mheshimiwa Waziri Sofia Simba tafadhali!

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII JINSIA NA WATOTO (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimkubalie kuhusu ombi lake na Mheshimiwa George Mkuchika ameshaanza kulifanyia kazi na ndiyo maana wameombwa wawapangie viwanja ili kusudi Shirika hilo liweze kuanza kazi hiyo mara moja.

Swali lake la pili ni kuhusu kuhamia Dodoma, ni kweli Serikali bado ina azma ya kuhamia Dodoma na masuala ya kuhamia yanakwenda kidogo kidogo zipo Wizara ambazo tayari wako hapa Dodoma. Kwa mfano, TAMISEMI tayari iko hapa Dodoma na nyingine kidogo kidogo zitahamia kufuatana na rasimali fedha ambazo tunazo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge ahsante sana, tuendelee na Wizara ya Katiba na Sheria, Swali la linaulizwa na Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mbunge wa Kasulu Mjini.

Na. 79

**Kutunga Sheria Dhidi ya Wahujumu Uchumi**

**MHE. MOSES J. MACHALI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutunga sheria kali dhidi ya wezi na wahujumu uchumi nchini ikiwemo ya kuwanyonga hadi kufa?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moses J. Machali, Mbunge wa Kasulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, makosa ya wizi yanadhibitiwa na Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Suraya 16. Makosa hayo yapo ya aina nyinga na yanaainishwa katika sura ya 27 ya Sheria ya Kanuni za Adhabu. Makosa hayo ni kama vile wizi wa kawaida, kwa mtu kuchukua kitu cha mtu mwingine bila ridhaa yake, wizi wa kuaminiwa au wizi unaofanywa na mtu aliye katika Utumishi wa Umma.

Makosa yana adhabu zinazotofautiana zikianzia faini, kifungo cha muda mfupi au cha muda mrefu kinachoweza kufikia miaka kumi na tano jela, kwa kutegemea uzito wa mazingira ya kosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, makosa ya uhujumu uchumi yanadhibitiwa na Sheria ya Uhujumu Uchumi, Sura ya 200. Makosa hayo yameanishwa katika

jedwali la kwanza la sheria hiyo kama ilivyo kwa makosa ya wizi, makosa ya uhujumu uchumi yapo ya aina mbalimbali.

Baadhi yake ni kusababisha hasara kwa mamlaka na makosa yaliyo chini ya sheria ya uhifadhi wa wanyamapori. Endapo mtu atatiwa hatiani kwa kosa la uhujumu uchumi anaweza akhukumiwa kwa kifungu kisichozidi miaka 15 Jela, kulipa faini au vyote kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaamini kwamba, Sheria zilizopo ni kali vya kutosha na zitaendelea kufanyiwa marekebisho kwa kadri itakavyohitajika. Pamoja na ukweli huu, nia ya kutoa adhabu ni kuzuia na kudhoofisha uhalifu. Kuwarekebisha waharufu na kurejesha mali iliyoibwa au kuhujumiwa.

Mheshimwia Naibu Spika, kwa mujibu wa sheria za nchi yetu, hivi sasa adhabu ya kunyingwa hadi kufa hutolewa kwa kosa la uhaini au kuua kwa kukusudia. Serikali kwa sasa haina mpango wa kutunga sheria inayotoa adhabu ya kifo kwa wezi na wahujumu uchumi.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, matukio kama ya *Richmond,* matukio kama ya wizi wa fedha za Rada, matukio pia kama toleo jipya sasa hivi *Escrow* wizi wa Akaunti ya *Escrow* na hali kadhalika kuna taarifa kwamba hata viti ambavyo viliandaliwa kwa ajili ya Bunge Maalum kwamba kiti kimoja kimetumia takribani shilingi milioni moja na nusu. Haya yote ni matukio ambayo yanaonekana kwamba yana *element* za uhujumu uchumi fedha za wananchi. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Machali una uhakika na *figures* zako?

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumza hivyo kwa sababu ipo minong'ong'ono ndiyo maana ninasema yanasikika pia mambo haya.

**NAIBU SPIKA:** Tukizungumzia habari za minong'ong'ono katika Bunge hili Waheshimiwa Wabunge tutaipotosha nchi yetu, tutawapotosha wananchi wetu, ni vizuri kujiridhisha kama Wabunge tukaongea kitu ambacho kinaeleweka. Endelea moja kwa moja Mheshimiwa.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru nafikiri taarifa zinaweza zikawekwa hadharani tukajua, lakini pia matukio kama ya uhujumu wa miradi mbalimbali ambayo iantekelezwa kwenye maeneo

mablimbali ya nchi yetu, miradi ya maji na ujenzi wa barabara na kwingineko ina *element* za wizi na uhujumu wa uchumi ndiyo maana barabara nyingine kwa muda mfupi unakuta zimevimba zinaanza kuharabika. Nilikuwa naomba niulize Wizara ya Katiba swali la kwanza.

Je, Waziri anaona kwamba inaingia akilini kusema kwamba Serikali haioni umuhimu wa kutunga sheria kali ya kuweza kuwanyonga wale wote watakaodhihirika wamepora fedha za Umma na matokeo yake wananchi wanapata shida na umaskini unaendelea kuwatafuna?

Swali la pili, kwa mujibu wa taarifa ya *Legal and Human Rights Centre* ya mwaka 2013, ukurasa wa 28, inaonyesha wazi kwamba, matukio ya wananchi kujichukulia sheria mikononi yamezidi kuongezeka. Kule Mwanza unaona kuna watu 195 na kwingineko. Ni wazi Sheria zilizopo zimeshindwa kuweza kukidhi matakwa ya Jamii.(*Makofi*)

Sasa swali langu ni kwamba, je Serikali itakuwa tayari kuweza kutunga sheria nyingine, kuleta muswada ama kuzifanyia marekebisho sheria zilizopo kutoa fursa kwa wananchi kwenye vijiji mbalimbali pale itakapodhihirika kwamba kuna uhujumu wa miradi amnbayo inatekelezwa na Serikali, iweze kuwaruhusu wananchi kuju…

**NAIBU SPIKA:** Swali sasa!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Ndiyo nauliza swali! Iweze kuwaruhusu wananchi kujiundia chombo cha kufanya *assessment* ya miradi na ikibainika chombo kile kiweze kutoa adhabu kwa kusema kwamba hapa wametuhujumu na Serikali pengine kupitia Mahakama waweze kuunda chombo cha kuweza kuchunguza iwapo haki haikutendeka katika utelekelezaji wa miradi mbalimbali. Ni kwa nini Serikali isifanye marekebisho ya sheria hizo?

**NAIBU SPIKA:** Maswali marefu sana sana, maswali marefu muno! Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, jitahidi majibu yawe mafupi tafadhali!

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali kadhaa ya Mheshimiwa Moses Joseph Machali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ulivyosema maswali yake kidogo yamekuwa ni marefu muno na haijulikani anauliza nini lakini najaribu kuelewa, kwamba kwanza kwa nini baadhi ya kesi ambazo amezitaja zisichukuliwe kama ni za uhujumu uchumi na kutolewa adhabu ya mtu kunyongwa.

Napenda kusema baadhi ya kesi alizozitaja kwa mfano kesi ya *Richmond* bado iko Mahakami na kwa mujibu wa taratibu zetu isingekuwa vyema kuizungumzia hivi sasa.

Kuhusu miradi ambayo anaizungumzia kama ujenzi wa barabara, ukarabati wa ukumbi wa Bunge, nataka kumfahamisha Mheshimwia Machali kwamba, nchi yetu inaongozwa kwa utawala wa sheria na sheria imeanisha ni makosa gani yanachukuliwa kuwa ni ya uhujumu uchumi.

Kwa hiyo, kama kuna matukio yoyote ambayo yanaonekana kukiuka sheria, basi ni vyema matukio hayo yakafikishwa kwenye vyombo vya sheria ili Mahakama ziweze kuamua kama hayo yanaangukia katika makosa ya uhujumu uchumi au makosa mengine ya wizi ambayo yana sheria zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu taarifa aliyoinukuu hapa, na jinsi ambavyo jamii inatakiwa kufanya vile alivyopendekeza yeye. Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika jamii yetu hivi sasa kupitia Wizara mbalimbali na mipango ya Serikali wananchi wanahamasishwa wafennye Ulinzi Shirikishi kuwe na Polisi Jamii, utaratibu huu umefanya kazi vizuri katika maeneo mengi na kama kuna matukio ya namna hiyo bado tunapenda kutoa wito kwa wananchi wasijichukulie sheria mikononi bali wayafikishe haya katika vyombo vinavyohusika na Serikali itachukua hatua muafaka.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Kwa majibu haya, Waheshimiwa Wbunge. Kwa sababu ya muda tuendelee na swali la Wizara ya Ujenzi, Swali la Mheshimiwa Abdul Rajab Mteketa, Mbunge wa Jimbo la Kilombero, kwa niaba yake Dkt. Haji Mponda, tafadhali!

Na. 80

**Ujenzi wa barabara ya Lami toka Kidatu – Ifakara hadi Mliba**

**MHE. DKT. HAJI H. MPONDA (K.n.y. MHE. ABDUL RAJAB MTEKETA)** aliuliza:-

Je, ni lini barabara inayotoka Kidatu – Ifakara na Ifakara hadi Mlimba itajengwa kwa kiwango cha lami kwa kuwa barabara hizo ni uti wa mgongo wa Jimbo la Kilombero?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdul Rajab Mteketa, Mbunge wa Jimbo la Kilombero, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli barabara hii ni uti wa mgongo kwa Jimbo la Kilombero na taifa kwa ujumla. Barabara ya Kidatu-Ifakara yenye urefu wa kilometa 73.26 ni sehemu ya barabara kuu ya Mikumi – Kidatu - Ifakara – Mahenge, yenye jumla ya urefu wa Kilometa 178.08. Barabara ya Ifakara Mlimba, yenye urefu wa Kilometa 150 ni sehemu ya barabara ta Mkoa inayojulikana kwa jina la Ifakara, Taveta, Madeke, yenye urefu wa kilometa 231.53.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi wa barabara ya Kidatu-Ifakara, kilometa 73.26 kwa kiwango cha lami umekuwa ukitekelezwa kwa awamu. Katika awamu ya kwanza Serikali ilijenga kilometa 10 kutoka kijiji cha Kiberege njia panda ya Magereza, Gereza la Kiberege hadi Kijiji cha Ziginali, ambapo kazi hii ilikamilika mwaka 2006. Katika awamu ya pili, Serikali ilijenga kilometa 6.17 kutoka eneo la Kibaoni Ifakara hadi Ifakara Mjini ambapo ujenzi huo ulikamilika mwaka 2008. Aidha, katika awamu ya tatu, Serikali imeshaanza utekelezaji wa mpango wa ujenzi kwa kiwango cha lami eneo la kutoka kibaoni, Ifakara hadi Iziginali kilometa 16.8, ili kuunganisha lami iliyowekwa katika awamu ya kwanza na ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 Serikali iliweza kupata fedha kwa msaada kutoka Serikali ya Marekani kupitia shirika lake la maendeleo la *USAID* kwa ajili ya kugharamia kazi ua upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Mikumi – Kidatu- Ifakara kilometa 103.3 kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

Kuhusu utekelezaji wa ujenzi wa barabara ya Ifakara, Taveta, Madeke, kupitia Mlimba, kilomita 150 kwa kiwango cha lami, Serikali imepanga kuitekeleza kwa awamu. Awamu ya kwanza itahusisha upembuzi yakinifu na usanifu kwa kina kwa sehemu ya barabara kutoka Ifakara hadi Kihansi, kilomita 126, ili kuunganisha na sehemu ya barabara ya lami kilomita 24 iliyojengwa hapo awali kati ya Kihansi na Mlimba. Taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi hiyo zinaendelea.

Aidha Serikali itaendelea na kazi ya kuimarisha sehemu korofi ili barabara hii iweze kupitika kwa kipindi chote cha mwaka.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Hussein Haji Mponda, swali la nyongeza. Ah! Mheshimiwa Mteketa ameshawasili, haya Mheshimiwa Mteketa swali la nyongeza.

**MHE. ABDUL RAJAB MTEKETA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri aliyotoa Ndugu Naibu Waziri. Lakini nataka kujua kwamba,

barabara hiyo ya kutoka Kidatu mpaka Ifakara, inafadhiliwa na nani? Ni kwa sababu kila siku tunaambiwa, mara wako wafadhili hao, mara *USAID*, mara nani. Lakini kitu hakieleweki, toka mwaka 2010 tunalilia hiyo barabara.

Pili, vilevile nataka kujua barabara hii ya kutoka Ifakara kwenda Mlimba inafadhiliwa na nani? Vilevile ni kwa sababu barabara hizo ni uti wa mgongo katika jimbo letu la Kilombero. Naomba majibu tafadhali.

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri Ujenzi, Kidatu Ifakara, Ifakara Mlimba, nani mfadhili?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:**Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Abdul Mteketa, kama ifauatavyo:-

Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mteketa kwa namna ambavyo ameuwa anafuatilia sana ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami, kwa miaka mitatu mfululizo amekuwa anaulizia manedeleo ya barabara hii.

Kuhusu suala la nani anafadhili. Tuna ufadhili wa shirika la Marekani *(USAID)*, kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara yote kutoka Mikumi mpaka Ifakara.

Pamoja na kuimarisha sehemu ile ambayo ilishajengwa siku nyingi ya lami, ili tupate barabara ambayo ni imara zaidi. Lakini kwa sehemu kubwa ya barabara hii kwa sasa inafadhiliwa na Serikali ya Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Haji Mponda, ulilianzia swali hili, hebu limalizie, swali dogo fupi.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:**Mheshimiwa Naibu Spika,nakushukuru, mwendelezo wa barabara hiyo hiyo inaitwa T16, baada ya kutoka Ifakara, inaelekea Mahenge na nyingine inaelekea Kilosa Mpepo na Serikali imetuambia, upembuzi yakinifu unaendelea, kipande kile cha Ifakara mpaka Kilosa Mpepo, Lodilomecha.

Swali langu ni lini kazi hiyo ya upembuzi yakinifu itakamilika?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu maswali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Haji Mponda, kama ifauatavyo:-

Kwa sasa hivi, barabara ya kutoka Ifakara mpaka Mahenge inafanyiwa tathimini ya zabuni kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kufanya usanifu. Kwa hiyo, baada ya muda si mrefu mhandisi mshauri ataanza kazi hiyo. *(Makofi)*

Na. 81

**Uhitaji wa Mawasiliano Tarafa ya Msangano.**

**MHE. JOSEPH R. SELASINI (K.n.y. MHE. DAVID E. SILINDE)** aliuliza:-

Mawasiliano ni moja kati ya nguzo za kuchochea maendeleo katika nchi:-

Je, ni lini Tarafa nzima ya Msangano ambayo ndiyo Makao Makuu ya Wilaya ya Momba pamoja na Kata za Kapele, Chilulumo, Mkulwe na Nzoka, zitapatiwa mawasiliano?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa David E. Silinde, Mbunge wa Mbozi Magharibi, kama ifuatavyo:-

Kwanza nakubaliana naMheshimiwa Silinde kwamba mawasiliano ni kichocheo muhimu sana cha maendeleo. Kwa umuhimu huo Wizara inashirikiana na watoa huduma ya mawasiliano kupeleka huduma hiyo katika maeneo mbalimbali nchini.

Aidha Wizara imeanzisha mfuko wa mawasiliano kwa wote, ambapo pamoja na mambo mengine, utaharakisha kazi ya kupeleka mawasiliano vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia mfuko wa mawasiliano kwa wote, iliainisha maeneo ya tarafa za Msongano, pamoja na Kata za Kapele, Chilulumo, Mkulwe, Nzoka, Nyimbili, Chitete na Nambizo, katika wilaya ya Mbozi kuwa miongoni mwa maeneo yenye uhitaji wa mawasiliano. *(Makofi)*

Katika zabuni ya awamu wa kwanza iliyotolewa mwezi Machi, 2013, Kata ya Chilulumo na Nyimbili, zilipata mzabuni ambaye ni kampuni ya Tigo. Kazi ya upelekaji Mawasiliano ikiwa ni pamoja na ujenzi wa minara ya Mawasiliniano, inatarajiwa kukamilika mwisho wa mwezi huu wa tano mwaka huu 2014 kwa Kata ya Nyimbili na mwisho wa mwezi Juni, 2014 kwa kata ya Chilulumo.

Katika zabuni ya kwanza (a), iliotolewa mwezi Februari, 2014, kata za Chitete na Nambizo, zilipata mzabuni, ambaye ni kampuni ya *Vodacom*, ambapo kazi ya upelekaji mawasilino, inatarajiwa kukamilika kabla ya mwezi Novemba, mwaka huu 2014.

Maeneo ya Tarafa ya Msongano pamoja na Kata za Kapele, Mkulwe na Nzoka, yameingizwa katika mpango wa zabuni ya awamu ya pili inayotarajiwakutangazwa na kutekelezwa katika mwaka ujao wa fedha.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika,nashukuru kwa majibu mazuri pamoja na kazi nzuri ambayo Serikali imefanya. Lakini pamoa na hayo naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza, ni lini maeneo yaliyosalia ya Kapele, Mkulwe na Nzoka, yatapelekewa huduma hii ya mawasiliano?

Swali la pili, ni kwamba kuna mwingiliano mkubwa sana wa mawasiliano kati ya kampuni za mawasiliano za Tanzania na zile za nchini Kenya hususan *Safari Com,* hasa maeneo ya Rongai, Tarakea, Ubetu, Useri na Mashati kule Rombo, jambo ambalo linaleta usumbufu mkubwa sana kwa watumiaji wa huduma hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujua, ni lini Serikali itahakikisha kwamba imerekebisha kasoro hii, ili wananchi wa Rombo badala ya kupata mawasiliano ya *Safari Com,* wapate mawasiliano ya kampuni zilizo hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Selasini, Mbunge wa Rombo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika,la kwanza, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, kwamba maeneo yaliyobaki ya jimbo la Mbozi Magaribi yatapata mawasiliano katika mwaka unaokuja wa fedha na yameshaingizwa katika mpango wa tenda zinazofuatia.

Kuhusu swali la pili, kwamba upo mwingiliano wa mawasiliano kati ya mawasilino ya kampuni za simu za Tanzania na mawasilino ya kampuni za simu za Kenya, katika eneo la jimbo la Rombo, ambalo baadhi ya maeneo yake yanapakana na nchi ya Kenya, ni kweli tatizo hilo lipo, na lipo katika maeneo mengi tu ya mipakani, mpaka wa Tanzania na Burundi, Tanzania na Rwanda, Tanzania na Uganda, ni dhahiri kwamba mawimbi ya mawasiliano hayatambui mipaka ya nchi.

Kwa hiyo, watu wa mipakani wanaweza kupata mawimbi ya mawasilino ya minara na makampuni yaliyo katika nchi nyingine.

Hata hivyo, Serikali imezishauri na kuzishawishi kampuni za simu zenye minara katika maeneo ya mipaka yetu kuongeza nguvu katika minara hiyo ili kuhakikisha kwamba minara iliyopo upande wa Tanzania ina nguvu.

Kwa hiyo, Watanzania wanapata mawasiliano kwa urahisi katika minara iliyo ndani ya nchi yao, badala ya minara iliyoko nje ya nchi. Ambapo matokeo yake wanapata mawasiliono kwa gharama kubwa kwa sababu wanapata *network* ambayo ni ya *roaming*.

Kwa hiyo, kazi hiyo tumeifanya ya kuzishawishi kampuni za simu zenye minara ya maeneo ya mipakani, kuongeza nguvu katika minara hiyo, na Serikali katika mpango huu wa kupeleka mawasilino vijijini, imeweka msisitizo mkubwa, kuhakikisha kwamba maeneo ya mipakani ya Tanzania yanapata mawasiliano ya uhakika kama mkakati wa kuongeza usalama kwa nchi yetu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda tunaendelea na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

Na. 82

**Matumizi na Manufaa ya Lugha ya Kiswahili.**

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA (K.n.y. MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE)** aliuliza:-

Kiswahili ni lugha mojawapo iliyopewa kupaumbele Barani Afrika na Duniani kote, na tayari vyombo vya habari na vyuo kadhaa duniani vimeanza *program* na mafunzo ya Kiswahili:-

(a) Je, Tanzania imejiandaa vipi kuhakikisha kuwa lugha hii inatumika ipasavyo kwenye mikutano ya *AU* na *UN*?

(b) Je, lugha hii inawanufaishaje Watanzania ambao ndiyo wazawa wa Kishwahili?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatafutia ajira za nje wanafunzi wote waliosoma shahada za Kiswahili?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nyambari C. M. Nyangwine Mbunge wa Tarime lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imeanzisha *program* ya mafunzo ya Kiswahili katika Vyuo Vikuu vya Dar es Salaam na Dodoma ambavyo vinatoa Shahada za Umahili, yaani *MA* na Shahada za Uzamivu *(Ph.D.)* katika Kiswahili.

Chuo Kikuu cha Zanzibar pia kimeanzisha *program* ya Shahada ya Uzamivu. Nia ni kupata wataalam wa fani za ufasili na ukalimani ambao utatumika kwenye mikutano ya Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa na kuhakikisha kuwa lugha hii inatumika ipasavyo.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika,lugha ya Kiswahili inawanufaisha watanznai akwa kupata ajira za ndani na nje ya nchi, wengi wameajiliwakufundisha Kiswahili tangu shule za msingi, sekondari, vyuo vikuu, na kwa wageni mbalimbali wanaotembelea nchi yetu. Pia wengi wameajiriwa katika nafasi mbalimbali za vyombo vya habari, kwa mfano Magazeti nchi Iran na China, *Televisheni* na Redio mfano *VOA*, *BBC*, Radio Japan, hali kadhalika Redio China. Wapo wanaonufaika na mauzo ya vitabu vya Kiswahili vya hadithi na taaluma mbalimbali.

(d) Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la la Serikali ni kutangaza nafasi za kazi zinapotokea ama za ndani au nje ya nchi. Kimsingi jukumu la kuomba ajira yoyote ni la mhitimu mwenyewe.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA**:Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, namshukuru pia Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu aliyotoa. Tanzania tuna Baraza la Kiswahili (BAKITA), ambalo lina jukumu la kukuza nakuimarisha Kiswahili.

Je, Serikali inalisaidiaje Shirika hili au Baraza hili kufanya kazi hii ya kudumisha Kishwahili?

Swali la pili, Tanzania ndiyo asili ya Kiswahili, ndiyo chimbuko la lugha ya Kiswahili. Lakini kuna nchi nyingine za Afrika Mashariki na nchi nyingine zinabaka nafasi hiyo, kwa kupeleka wataalam nje, kwenye vyombo alivyovisema *Voice of America (VOA), BBC* na ukisikiliza kishwahili chao siyo Kiswahili sanifu. Ni Kiswahili kibovu kibovu hivi. Nafasi hiyo wanaichukua hawa wengine, sisi tunaangalia tu. Kwa nini tunaangalia hivi na hatuchukui hatua yoyote?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa maswali yako. Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, ambaye na yeye amefanya kazi katika vyombo hivyo vya kimataifa. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Rweikiza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) lina jukumu kubwa la kuendeleza Kiswahili hapa nchini, sisi kwa upande wa Serikali, mwaka hata mwaka tumekuwa tukitenga Bajeti ili kuwezesha Baraza hili linakuwa na uwezo wa kufika sehemu zote za Tanzania na kuendeleza kukuza Kiswahili.

(b), kwamba chimbuko la Kiswahili ni Tanzania na kwa nini vyombo vya habari vingi vya kimataifa vimekuwa na waandishi au watangazaji wanaotumia Kiswahili kibovu kibovu kama alivyouliza. Unapoomba kazi katika shirika la utangazaji la *BBC* ama *VOA* ama redio Japan kwa mfano, hawachukui kutokana tu unajua kuzungumza Kiswahili.

Pia wanaangalia na uwezo wako mwenyewe wa utambuzi wa mambo.

Kwa hiyo, kunakuwa na *interviews,* kunakuwa na vitu vingi ambavyo wanaviangalia. Kwa hiyo, inawezekana kabisa mtu akawa Kiswahili chake ni cha wasiwasi kidogo, lakini uwezo wake wa utambuzi wa mambo ya kimataifa ukawa ni mkubwa zaidi.

Kwa hiyo, wakam-*consider* huyu, kuliko huyo ambaye anaongea Kiswahili cha kawaida tu kama cha Mnyaa, ama cha Chacha Mariba Nyangwine, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Pamoja na muda kuwa mdogo nisipompa Profesa Kulikoyela K. Kahigi, swali la nyongeza hatanisamehe. Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kahigi, swali fupi.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Tatizo linalokifanya Kiswahili kisitumike katika mikutano ya kimataifa ni ukosefu wa wakalimani makini. Sasa Serikali ina mpango gani wa kuwapa mafunzo wanafunzi wetu wa Vyuo Vikuu ambao wanachukua Kiswahili, ili wapate mafunzo ya ukalimani makini, waweze kufanya kazi hiyo ya ukalimani katika mikutano ya kimataifa?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kahigi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri yeye pia ni mwalimu na anafundisha Chuo Kikuu cha Dodoma hivi sasa Kiswahili, na nadhani atatumia nafasi hiyo kwa uzuri zaidi kuwajengea uwezo vijana ili wawe na utambuzi mzuri na wawe wakalimani wazuri katika mikutano ya kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa nyongeza tu ni kwamba, mikutano ya kimataifa, kwa mfano, *United Nations* wanapokuatana, kwa sababu kishwahili bado hakijawa *authorized* kama lugha rasmi pale, lakini wale wakalimani ambao wanakwenda pale, wanatakiwa kulipwa. Siyo umoja wa mataifa wanaolipa. Kwa mfano, Tanzania tukitaka tutumie Kiswahili, pale katika Umoja wa Mataifa, katika mikutano ile, inabidi tulazimike kulipa.

Hata hivyo, mimi nashukuru kwamba Profesa Kahigi, kwa uwezo wako ulio nao na kwa sababu ni Mwalimu wa Chuo Kikuu cha Dodoma, nafahamu unatoa mchango mkubwa sana pale na mimi ni miongoni mwa wanafunzi wako. Utatumia nafasi hiyo ili tupate nafasi bora zaidi, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Tuhamie Wizara ya Maliasili na Utalii.

Na. 83

**Kuhifadhi Historia ya Mji wa Bagamoyo**

**MHE. ZAYNAB M. VULLU** aliuliza:-

Katika juhudi za kuenzi na kuhifadhi historia ya mji wa Bagamoyo, tarehe 20Julai, 2009 Serikai ilianza ukarabati wa lililokuwa Boma la Mjerumani; lakini ukarabati huo umeenda kwa kusuasua kwa muda mrefu sasa.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha ukarabati wa boma hilo katika muda muafaka?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kulikarabati jengo la Kale la *Father House* lililopo Chuo cha Uongozi wa Elimu, *ADEM,* Bagamoyo ili kulinusuru na kuporomoka au kutoweka kabisa?

**NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zaynabu M. Vullu, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, mwaka 2009 ilianza kukarabati boma la Mjerumani, baada ya boma hilo kuwa limebomoka kutokana na mvua ya *El-Nino* mwaka 1998. Katika ukarabati huu, Wizara hutoa wataalam na Wizara ya Ujenzi hutoa fedha kwa ajili ya kazi hiyo. Ukarabati huo umekuwa ukikabiliwa na changamoto za ufinyu wa Bajeti. Hata hivyo, Wizara yangu itaendelea kufanya ukarabati wa boma hilo kwa kadiri fedha zitakavyopatikana.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu jukumu lake ni kuhakikisha kuwa majengo yote yanahifadhiwa kwa mujibu wa Sheria, hayabomolewi wala kubadilishwa muonekano wake bila kufuata Kanuni za uhifadhi wa majengo ya kihistoria.

Hata hivyo, Wizara kwa kushirikiana na taasisi za umma, dini na watu binafsi, wanaomiliki majengo ya kihistoria, huyafanyia ukarabati pale inapobainika mmiliki wa jengo ameshindwa kufanya ukarabati kutokana na ukosefu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, jengo hili bado linamilikiwa na Taasisi ya dini, *ADEM Bagamoyo* na Serikali itakuwa tayari kutoa msaada pale itakapokuwa imeombwa na taasisi hii.

**MHE. ZAYNAB M. VULLU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa masikitiko makubwa sana kutoka kwangu binafsi na kwa wananchi wa jimbo la Bagamoyo, sijaridhishwa na majibu ya Mhehsimiwa Naibu Waziri. Majibu yake ni yale yale ambayo mimi nimemwuliza swali, ametoa kwenye swali ameweka kwenye majibu!

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatakiwa ionyeshe juhudi zake za kutaka kuimarisha na kutunza hifadhi ya Mambo ya Kale. Kwani jengo hili wamesema walitoa fedha mwaka 2009, hadi leo ni miaka mitano! *(Makofi)*

Je, Serikali kweli iko *serious*, katika kutaka kulikarabati jengo hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, jengo hili tu kwa taarifa yako, lina historia kubwa sana katika nchi yetu. Jengo hili ndilo lilikuwa Makao Makuu. Kwa maana nyingine, Ikulu ya Mjerumani wakati anatutawala hapa Afrika Mashariki. Wakati huo ilikuwa inaitwa *Dotch East Africa*. Kwa maana ya kwamba Tanganyika, Rwanda na Burundi, Mjerumani ndiyo akaweka Ikulu yake pale Bagamoyo. Sasa ikiwa ikiwa Serikali haiwekei umakini katika kulikarabati hili jengo kwa kweli inasikitisha sana. Nataka tu nimwambie Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, yale mabati aliyozungushia, mengine wananchi wanajisaidia kwa kwenda kuhifadhi…

**NAIBU SPIKA:** Sasa swali.

**MHE. ZAYNAB MATITU VULLU:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali tayari nilishamwuliza, nilikuwa natoa ufafanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa taarifa yake Waziri ADEM haiko chini ya taasisi ya dini. *ADEM* ni taasisi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Kwa maana ni chuo kinachotoa Mafunzo ya Uongozi kwa waalimu. Ninachoomba, Serikali ituambie, imeweka mkakati gani?

Kwa maelezo yake amesema taasisi za dini na watu binafsi. Kama wanataka kuipa ile *Fathers' House,* kuikabidhi kwenye taasisi ya dini, basi naomba wafanye mazungumzo ya haraka ili taasisi hiyo iweze kuwa chini ya uongozi wa dini, ahsate sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, nashukuru. Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi sana tafadhali, muda hauko upande wetu na bado tuna maswali mawili.

**NAIBU WAZIRI WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Zaynab Vullu, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iko *serious,* na Serikali inajua umuhimu wa jengo hili. Jengo hili lilikuwa linatumiwa na Gavana wa kwanza wa Kijerumani na baadaye akaja kulitumia Gavana wa Kiingereza, na baadaye likaja kutumika na Mkuu wa Wilaya wa kwetu baada ya kupata uhuru. Mkuu wa Wilaya aliacha kulitumia mwaka 1998 baada ya ile mvua ya *el-nino* kulibomoa jengo hili.

Hata hivyo nataka nimhakikishie tu. Sisi kama Serikali, kwa maana ya Wizara ya Maliasili na Utalii, pamoja na Ujenzi tuliona umuhimu wa jengo hili na mwaka 2009 tulianza kufanya ukarabati jengo hili. Hata hivyo namwambia Mheshimiwa Mbunge mwenzangu kuwa tatizo kubwa hapa ni ufinyu wa Bajeti. Lakini mwaka huu tarehe 8 Februari, 2014 Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo ilikutana na wataalam wa wizara yetu. Tulizungumza na tukakubaliana baadhi ya mambo ya msingi ya kuyafanya katika maeneo yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa yake tumetenga Bajeti ndogo. Nataka nimhakikishie tu kwamba umuhimu wa jengo lile sisi kama Wizara ya Maliasili na Utalii na kama Serikali kwa ujumla tunatambua na tutalishughulikia kwa kadiri ya uwezo wetu, kuhakikisha linakaa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujibu swali lake la 'B' kama ifuatavyo. Jengo hili la *ADEM,* nataka nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge ajue, liko chini ya taasisi ya *Roman Catholic,* ndimo walimokuwa wanakaa waasisi wa dini siku za nyuma.

Kwa utaratibu, maeneo haya ya kihistoria huwa yanamilikuwa na Serikali, taasisi za dini, hata watu binafsi. Kama watu binafsi au taasisi za dini zimeshindwa kuyaendeleza huwa kuna utaratibu wanaomba kwenye Wizara yetu na sisi tunakuwa tayari kuwasaidia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana, tuhamie Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa maswali mawili yaliyobaki. Sasa ni swali la Mheshimiwa Bernadetha Kasabago Mushashu, Mwalimu Mushashu, swali.

Na. 84

**Malipo ya Wazabuni wa Chakula Kwenye Magereza**

**MHE. BERNADETHA KASABAGO MUSHASHU** aliuliza:-

Wazabuni wanaotoa huduma ya chakula kwenye Magereza hawajalipwa malipo yao ya huduma hiyo kwa muda mrefu sana, jambo linalosababisha malalamiko mengi.

(a) Je, Wazabuni hawa wanaidai Serikali kiasi gani cha fedha tangu mwaka gani?

(b) Je, Serikali itawalipa wazabuni hawa?

**NAIBU WAZIRI WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bernadetha Kasabago Mshashu, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu 'A' na 'B' kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba wazabuni wanaotoa huduma za chakula kwa wafungwa magerezani hawajalipwa madai yao ya huduma hiyo kwa muda mrefu. Madai hayo ni ya tangu Julai 2009 na yameendelea mpaka mwezi wa Aprili 2014. Jumla ya madai yao ni bilioni thelathini na nne nukta mbili. Aidha madai ya wazabuni hao yaliyohakikiwa ni ya kipindi cha Julai 2009 hadi Juni 2012 ambayo ni bilioni kumi na mbili nukta tatu (Sh. bilioni 12.3).

Mheshimiwa Naibu Spika, madeni haya yametokana na ufinyu wa Bajeti inayotengwa kwa chakula cha wafungwa mwaka hadi mwaka katika kutekeleza majikumu ya lazima ya Jeshi la Magereza. 'B', nia ya Serikali ni kuyalipa madeni yote haya, na kwa kuanzia Serikali italipa madeni ambayo tayari yameshahakikiwa.

**MHE. BERNADETHA KASABAGO MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Serikali imeshindwa kuwalipa wazabuni hawa kwa takriban miaka sita sasa, tangu mwaka 2009 hadi sasa mwaka 2014 na hivyo kusababisha baadhi ya wazabuni hawa kufilisika, na wengine nyumba zao kupigwa minada kwa sababu wameshindwa kurejesha mikopo ya benki. Kwa sababu thamani ya Shilingi kwa maka 2009 ni tofauti kabisa na thamani ya Shilingi mwaka 2014.

Je, Serikali iko tayari kuwalipa wazabuni hawa asilimia fulani ili kufidia ucheleweshwaji wa malipo hayo kwa miaka sita?

Swali la pili, kwa kuwa wazabuni hawa wanadai Wizara yako bilioni thelathini na nne, lakini unasema tangu mwaka 2009 mmeshahakiki madeni ya bilioni kumi na mbili nukta tatu; lakini wazabuni hao wameteseka kwa muda mrefu na wamevumilia.

Je ni lini hasa, unipe muda, Serikali itaweza kuwalipa hata hayo madeni ambayo yameshahakikiwa?

**NAIBU WAZIRI WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mushashu kama ifuatavyo.

Ni kweli kwamba kwa bahati mbaya sana kumetokea baadhi ya hawa wazabuni ambao wameshafilisika kutokana na deni hili na wengine kupoteza mali zao. Swali la kuwalipa deni mpaka sasa bu kuwalipa deni ambalo wametukopesha, na deni ambalo limehakikiwa hivyo hivyo ni lile ambalo limetokana na deni halisi. Swali 'B', ni kwamba ni lini tutawalipa hayo yaliyohakikiwa. Mpango wa Serikali ilikuwa ni kuhakikishwa kwamba tunalipa madeni ya wazabuni sit u ya chakula cha wafungwa lakini pia ya madai mengine kabla ya mwaka huu wa fedha kumalizika. Ikishindikana bado tunashauriana, kutokana na ugumu wa Bajeti, lakini ikishindikana tutatoa tarehe nyingine ambayo tunategemea kufanya hivyo.

**NAIBU SPIKA:** Tuendelee na swali la mwisho kwa siku ya leo, mtaona muda hauko upande wetu Waheshimiwa Wabunge. Swali hilo linaulizwa na Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola, Mbunge wa Mwibara.

Na. 85

**Serikali kufunga vifaa vya kisasa**
**(Closed Circuit TV)**

**MHE. KANGI ALPHAXARD LUGOLA** aliuliza:-

Je, kuna sababu gani kwa Serikali kutofunga vifaa vya kisasa *(Closed Circuit Television)* ili kuzuia na kudhibiti uhalifu nchini hususan katika Miji mikubwa ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Tanga, Moshi, Morogoro na Mbeya?

**NAIBU WAZIRI WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola, Mbunge wa Mwibara, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa ufungaji wa vifaa vya ulinzi vijulikanavyo kama *Closed Circuit Television* ni muhimu katika kupunguza uhalifu wa aina mbalimbali kwenye miji mikubwa hapa nchini.

Ni kwa kutambua umuhimu huo Jeshi la Polisi katika *program* yake ya maboresho inatekeleza jukumu lake la msingi la ulinzi kwa kuwa na miradi 27 ya *ICT* ukiwemo mradi wa kufuatilia taarifa za Usalama Barabarani ambao unaitwa *Integrated Road Traffic Management Information System.* Hata hivyo ufanisi wa jukumu hili unakwamishwa na ufinyu wa Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufungaji wa vifaa hivi vya ulinzi katika maeneo mbalimbali ni jambo mtambuka linaloshirikisha wadau mbalimbali wakiwemo Wizara ya Miundombinu, Mipango miji, Serikali za Mitaa na watu binafsi. Huu ni mradi mkubwa ambao unahitaji utafiti wa kutosha wa kimuundo, kisheria na rasilimali fedha. Wizara yangu ni mshauri na msimamizi wa kazi ya mradi huu katika kudhibiti uhalifu, yaani *Crime Monitoring*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kufanya uchambuzi wa mapendekezo ya kibiasha ya sekta binafsi ili kuwekeza teknolojia hii na miundombinu yake katika kutimiza malengo ya usalama wa nchi. Aidha wakati Serikali ikijipanga kusimamia ufungaji wa *CCTV* kwenye maeneo muhimu, natoa wito kwa taasisi binafsi na makampuni kufunga vifaa hivi hasa katika maeneo ya biashara zao na yenye mikusanyiko ya watu wengi. *(Makofi)*

**MHE. KANGI ALPHAXARD LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimesikitishwa sana na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa sababu majibu yake yana maneno 237 na kati ya maneno hayo ni maneno 58 tu ndiyo yamezungumzia swali langu la *CCTV* ambayo ni sawa na asilimia 24.5. Lakini maneno 179 ambayo ni asilimia 75.5 yamezungumzia mambo ya *ICT* ambayo sikuuliza. Sasa swali la kwanza. Kwa nini asilimia 75 zitoe majibu ya swali ambalo mimi sikuuliza. Swali la pili. Ile aya ya mwisho, Serikali inasema kwamba inakaribisha wawekezaji kufanya kibiashara sekta binafsi. Ile sentensi ya mwisho anasema anatoa wito kwa taasisi, makampuni na watu binafsi kufunga vifaa hivi kwenye mikusanyiko mingi. Tulianza kubinafsisha huduma za ufagiaji maofisini, tukaona haitoshi tukabinafsisha masuala ya kukusanya ushuru, tukaona haitoshi tukabinafsisha mashirika ya umma, tumemaliza ubinafsishaji kila mahala sasa Serikali inakwenda kubinafsisha suala la ulinzi na usalama wa nchi. Jambo ambalo ni hatari. Wizara hii sasa Waziri amekuwa ni mtu wa watu binafsi. Kazi hii ni kazi ya Jeshi la Polisi, ni ulinzi na usalama wa nchi na Waziri Kazi yako si kazi ya mambo ya watu binafsi. *(Makofi)*

Mheshimimiwa Spika, watu hao binafsi ndio tunaowadhibiti, ndio wanaofanya uhalifu pamoja na jamii, inakuwaje ndio washughulikie suala la ulinzi na usalama? Sasa swali langu la mwisho, kwa nini Serikali imeamua kubinafsisha suala la Ulinzi na Usalama wa nchi yetu?

**WAZIRI WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali kadhaa ya Mheshimiwa Kangi Lugola, kwa pamoja

kama ifuatavyo. Tunafahamu kwamba kazi kubwa ya Serikali yoyote duniani ni suala la ulinzi na usalama wa raia wake, sisi tunajua hilo.

Kwa kutambua hilo, Serikali sasa iko katika mazungumzo na makampuni mbalimbali yenye teknolojia hii kuhusu suala zima la *Public Surveillance Systems.* Lakini alichokisema Naibu Waziri ni kuwaomba tu, kama tulivyofanya hapa Bungeni, kuna *CCTV System* yetu, kikitokea kitu tunaweza tukasaidiana tukajua.

Hata hivyo sisi tunataka kuweka kwa ajili ya *public* nzima. Sehemu zile ambazo ni *crime prone* tunazianza na tuna miradi mingi. *Pilot* moja itaanza Dar es Salaam hivi karibuni na tunataka kuweka katika mji wa Zanzibar, Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, Dodoma na Arusha. Katika miji hii mikubwa tutaanza nayo baadaye, utaratibu huu ni wa kawaida. Tutasambaa sehemu nyingi ambazo tunaona hali ya uhalifu inakuwa kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ni la kawaida, na nchi nyingi duniani zinafanya. Marekani kule wanakuambia *Big Brother is Watching* na kweli huwezi ukafanya kitu mahala, baada ya muda watajua ni nani amefanya nini. Kwa hiyo, jambo hili Kangi Lugola nasema tuvumilie, tunaendelea nalo na tuko katika hatua za *advanced* kabisa, karibu utaliona mitaani, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. KANGI ALPHAXARD LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika Swali la kwanza halijajibiwa. Kwa nini robo tu ndiyo amejibu swali langu na robo tatu amejibu mambo mengine ambayo sikuuliza, hajajibu.

**WAZIRI WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, uzito wa swali unaweza kuwa katika robo vile vile na robo tatu likawa halina uzito wowote. Nashukuru.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa *CCTV* zinasaidia sana si katika suala la uhalifu mijini tu. Nakumbuka jambo moja hivi sasa nchini ambalo linamaliza uhai wa wananchi ni ajali za barabarani. Katika nchi nyingi zinafungwa barabarani na kwa kuwa Serikali mara nyingi tunasema haina uwezo.

Je, Wizara yake itakuwa tayari sasa kufunga *CCTV* barabarani, katika njia kuu zote ili ku-*monitor* magari yanayokwenda kwa kasi na yanayosababisha ajali na kwa njia ya *PPP* ikiwa Serikali haina fedha?

**WAZIRI WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Eng. Mnyaa kama ifuatavyo.

Kama nilivyosema na pengine ndiyo sababu Kangi anasema hakujibiwa moja kwa moja *CCTV,* nilisema jambo moja ambalo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Wizara ya Uchukuzi tunalisimamia ni kuhakikisha kwamba haraka iwezekavyo tunaweka *Car Tracking System* kwa kufunga hizo *system* sehemu zote. Hii itatusaidia kwa ajali lakini pia hasa kwa kuya-*track* magari ambayo wakati mwingine yanapeleka bidhaa nje halafu wakajifanya wanazizungusha ndani na kutukosesha kodi kubwa sana. Kwa hiyo hili tunalishughulikia hivi sasa na utekelezaji wake uko karibu sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge naomba niwashukuruni sana kwa kipindi hiki cha maswali, tumeshapitiliza muda kidogo sasa turudi kwenye utaratibu. Nina matangazo ya haraka haraka kama yafuatayo.

Wageni 56 ambao ni wageni wangu, wanafunzi 53 na walimu wanne kutoka Sekondari ya *St. John* Kilimatinde Singida, kule kwenye jimbo la Mheshimiwa John Chiligati. Pale walipo wananfunzi wa *St. John* simameni. Ahsanteni sana na Katibuni sana Dodoma, karibuni muone shughuli za Bunge zinavyoendelea. Wanaongozwa na mwalimu wao Mkuu, mwalimu Kanungha. Ahsante sana, karibu sana Head Master. Hii ni shule ya Sekondari kule Kilimatinde, ni moja ya shule nzuri kabisa katika kanda ya Kati.

Tuna wanafunzi 82 kutoka Shule ya Msingi Mazengo, Dodoma, pale mlipo Mazengo, karibu sana wanangu, karibuni sana. Karibuni muone Bunge lenu linavyofanya kazi, ahsanteni sana. Tuna wananfunzi 60 kutoka Chuo Kikuu cha Sebastian Kolowa cha Tanga, inaelekea watakuwa wako *basement,* wamekosa nafasi huku juu.

Wanafunzi 75 kutoka Chuo cha Mipango Dodoma, wanafunzi wa mipango na wenyewe ibaelekea labda wako huko. Tunaye mgeni wa Bunge letu, Mgeni wa Mheshimiwa Spika, anaitwa Musambai Joseph ambaye ni Katibu wa Bunge la *Count* la Vihiga kutoka Kenya. Karibu sana Katibu. Waheshimiwa kama mnavyojua, baada ya Katiba Mpya ya Kenya, imeanzisha *Counties 47,* kwa hiyo wana mabunge ya *counties 47* yenye Spika, Naibu na Katibu wa Bunge na kadhalika, lakini pia wana mabunge mawili ya taifa.

Kwa hiyo, kwa ujumla wana mabunge 49. Wana Bunge la kawaida na Bunge la *Senate* pia. Hayo ni mambo ya Kenya hayo. Wageni 11 wa Mheshimiwa Mheshimiwa Gosbert Blandes, ni Mheshimiwa Wales Mashanda, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe, pale ulipo usimame, Katibu

sana. Mheshimiwa Baba Paroko Padre Alovatus Alfred Mulengela wa Parokia ya Nyakaiga, karibu sana. *(Makofi)*

Mwisho katika wageni wake, sio kwa umuhimu, ni Mwalimu wake Mheshimiwa Gosbert Blandes wa Shule ya Msingi kule Kyabanga ambaye alimfundisha Hisabati Shule ya Msingi kule Kayungu mwaka 1978. Mwalimu Mary Rubunga Alfred. Karibu sana Mwalimu, karibu sana Bungeni, tunakushukuru sana. Ulimfundisha Hisabati Mheshimiwa Gosbert Blandes, lakini baadaye hakuendelea na Hisabati tena, akasoma mambo mengine! Tunakushukuru, lakini mwanafunzi wako anafanya kazi nzuri hapa Bungeni. Tunakupongeza sana Mwalimu.

Wageni wa Mheshimiwa Ezekia Wenje, ni Ndugu Yared Awando – *Branch Manager* wa *Jubilee Insurance,* Mwanza. Karibu sana. Mwinginei ni Ndugu Haule Reward – *Branch Manager* pia wa *Jubilee Insurance,* Dodoma. Karibuni sana. Hawa *Jubilee Insurance* ndio wanaoshughulikia Bima yetu ya Afya inaelekea.

Wageni wa Mheshimiwa Susan Lyimo – Waziri Kivuli wa Elimu, ni Ndugu Elizabeth Msokia. Karibu, pale ulipo; Ndugu Mwemezi Makumba na Ndugu Godfrey Bonaventura, karibu pale mtakapokuwa mpo.

Wageni wa Mheshimiwa Sylvester Mabumba, ni Mjumbe Msuri Mjumbe – Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mfenesini Unguja. Karibu sana Mwenyekiti; na Ndugu Mgeni Mussa Haji, Katibu wa CCM, Wilaya ya Mfenesini Unguja. Karibuni sana nyinyi wote wawili.

Wageni wawili wa Mheshimiwa Lolensia Bukwimba, pale walipo naomba wasimame. Ahsante sana. Pia naomba nitambue uwepo wa Maofisa wote wa Wizara ya Elimu, wakiongozwa na Katibu Mkuu Elimu, kama mmeishaingia hapa ndani naomba msimame wote kwenye *Gallery,* karibuni sana. Tunatambua uwepo wenu; sikupata orodha yenu lakini nawashukuru sana kufika kwenu. Karibuni sana Dodoma.

Waheshimiwa Wabunge, sasa ni matangazo ya kazi. Ofisi ya Utawala Bunge, inaomba niwatangazieni kwamba Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wanafanya maonyesho ya shughuli wanazozifanya, ikiwa ni pamoja na vitabu na machapisho mbalimbali, taarifa mbalimbali kuhusu wahitimu wa Chuo hicho pamoja na programu zinazotolewa katika Chuo hicho. Maonyesho hayo yanafayika nyuma ya jengo la Utawala kwenye uwanja wa tafrija leo, tarehe 19 Mei, 2014. Wabunge mnakaribishwa kuona mambo mengi mapya ya kujifunza. Chuo Kikuu cha Dar es Salalam wanayo maonyesho yao nyumba ya jengo la utawala pale, tunaombwa tupitie pale Waheshimiwa Wabunge, tuweze kujifunza nini wanafanya.

Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo ya Maendeleo ya Jamii, saa 7.00 mchana mkutane leo, Ukumbi wa Msekwa 'C'. Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Ukumbi wa Msekwa 'C' saa 7.00 mchana.

Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo saa 7.00 mchana mkutane katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Kama yatajitokeza matangazo mengine yatakuja, tutaendelea kutangaziana kadri muda unavyokwenda. Katibu!

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2014/2015 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na shughuli yetu. Taarifa nilizonazo ni kwamba tuliishia na Mwenyekiti wa Kamati kusoma maoni ya Kamati. Kwa hiyo, sasa hapa namwita Msomaji wa Maoni ya Kambi ya Upinzani, moja kwa moja Mheshimiwa Susan Lyimo, akimaliza, tutaanza na uchangiaji na mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Gosbert Blandes. Mheshimiwa Susan Lyimo!

### Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Upinzani kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mhe. Susan A. J. Lyimo, Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2014/2015, Kama Ilivyosomwa Bungeni

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili nieweze kusoma maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kutoa shurani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kusimama hapa leo hii. Kipekee nimshukuru sana Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe, kwa kuniamini na kunirudisha tena katika nafasi hii ya Uwaziri Kivuli wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Mwisho lakini siyo kwa umuhimu, niwapongeze wale wote walioteuliwa kuunda Baraza Kivuli, na tunawaambia watani zetu, kazi ndiyo kwanza imeanza na UKAWA ndiyo mpango mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu sana tumeonya na kushauri juu ya hatari inayolinyemelea Taifa letu kutokana na Serikali ya CCM kuharibu mfumo wetu wa elimu. Tunasikitika kwamba ushauri wetu, maonyo na nasaha tulizotoa zilibezwa kwa kishindo ndani na nje ya Bunge, sasa siyo maonyo tena wala utabiri, bali ukweli umeonekana jinsi mfumo huu ulivyoporomosha elimu yetu.

Ni jambo la kusikitisha kwamba leo hii asilimia 70 ya watoto Kitanzania wa umri kati ya miaka saba mpaka 16 hawawezi hata maana ya rangi tatu za bendera ya Taifa. Vile vile ni mwanafunzi mmoja, au pungufu kati ya 10 wa darasa la tatu, anayeweza kusoma hadithi kwa Kiingereza ya kitabu cha Darasa la Pili. Aidha, ni mwanafunzi mmoja tu kati ya wanne wa Darasa la Tatu, anayeweza kusoma kwa ufasaha kitabu cha Darasa la Pili kwa Kiswahili. Takwimu hizi zimetolewa na ripoti ya tathmini ya mwaka wa Shirika lisilo la Kiserikali, linaloshughulikia masuala ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka nane ya Utawala wa Mheshimiwa Rais Kikwete, kiwango cha ufaulu katika ngazi ya Msingi na Sekondari, kimeendelea kushuka na kwa mujibu wa takwimu za Serikali zinazopatikana kwenye kitabu cha *BEST*. Katika kipindi hiki, kiwango cha kufeli kilifikia kiwango cha kilele mwaka 2012, pale ambapo asilimia 65.5 ya wanafunzi wa Kidato cha Nne walipopata alama sifuri.

Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni ilisema mwaka jana, 2013 kwamba watalaam wa masuala ya Elimu wanabashiri kwamba kiwango cha kufeli kinaweza kupanda hadi kufikia asilimia 95 kama hakutakuwepo na ujanja wa kufuta matokeo na kuyapanga upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili limetokea mwaka huu na tumeona matokeo haya yakipandishwa hadi kufikia asilimia 58.9 kutokana na upangaji upya na alama na madaraja ya kufaulu. *(Makofi)*

Mhehsimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba kiwango cha kufaulu hakikupanda, bali kilipandishwa ili kufuta aibu ambayo imekuwa ikiikumba Serikali ya CCM tangu awamu ya nne iingie madarakani. Watanzania wanapashwa kuelewa kuwa mchezo unaofanywa na Serikali ya CCM wa kuchezea madaraja na alama za kufaulu utaligharimu sana Taifa hili huko tuendako kwa sababu mfumo wetu wa elimu utakuwa unatoa Wahitimu ambao wanafaa hapa Tanzania peke yake lakini wasio na sifa katika wigo wa Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli ulio wazi kuwa mufumo wetu wa elimu, umepitwa na wakati. Kiwango cha wastani wa kusoma shuleni ni miaka tisa,

lakini wa kwetu ni miaka saba pekee. Matokeo yake watoto wetu wanamaiza shule wakiwa wadogo, na bila kuwa na maarifa na stadi za msingi za kuweza kuwafanya wajitegemee. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikitoa mapendekezo kadhaa ili kuboresha mfumo wetu wa Elimu hapa nchini. Mapendekezo haya, ni pamoja na:-

(i) Wigo wa elimu ya msingi upanuliwe ili watoto wakae shuleni kwa muda usiopungua miaka tisa, kama ilivyo katika viwango vya Kimataifa;

(ii) Elimu ya msingi iunganishwe na Elimu ya Mafunzo ya Ufundi ili kwamba vijana wetu wanapomaliza Elimu ya Msingi, wawe na maarifa na stadi za kufanya kazi itakayofanya wajitegemee popote walipo;

(iii) Watoto wetu waanze shule mapema;

(iv) Miundombinu ya elimu iboreshwe; maslahi ya Walimu yaboreshwe;

(v) Wakala wa ukaguzi uanzishwe; na

(vi) Fedha za ruzuku kwa wanafunzi zifike kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie Serikali ya CCM ilivyoshindwa kutekeleza Ilani yake ya Uchaguzi kwa Awamu zote mbili kuboresha elimu na maslahi ya Walimu nchini. Ibara ya 92(h) na (j) ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, 2005 na 2010 inasema kwamba CCM inatambua elimu ni haki ya msingi kwa kila mwananchi na ndiyo ufunguo wa maendeleo. Ili kuendeleza sekta hii, Serikali ya CCM itazingatia ipasavyo suala la ubora wa elimu, kama inavolishughulikia katika suala la wingi na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muhula wote wa kwanza wa miaka mitano wa utawala wa awamu ya nne, yaani 2005 – 2010, Serikali ya CCM imeshindwa kabisa kutekeleza ilani yake ya uchaguzi kuhusu elimu bora kwa Watanzania. Hii ni kwa sababu kiwango cha ufaulu kimekuwa kikishuka kwa miaka yote mitano ya muhula wa kwanza ya utawala wa Serikali ya CCM, kama inavyoonyeshwa hapo juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maslahi ya Walimu, Serikali ya CCM imeshindwa kutekeleza Ilani yake yenyewe ya kuboresha maslahi ya Walimu kama ilivyoahidi katika Uchaguzi Mkuu wa 2010. *(Makofi)*

Kwa mujibu wa Chama cha Walimu CWT, hadi kufikia Desemba, 2013, madai ya Walimu ambayo hayakulipwa, yalifikia Shilingi biloni 61. Hili

limethibitishwa na Naibu Waziri wa TAMISEMI juzi tarehe 17 Mei, katika kipindi cha 'Jambo Tanzania,' kinachorushwa asubuhi cha *TBC1*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi (Mheshimiwa Dkt. Kawambwa), imeahidi kuwa italipa madeni haya ya Walimu katika mwaka wa fedha. Serikali itambue uzuri wa mfumo wa elimu utategemea ubora wa Walimu wake. Kwa mantiki hiyo, Serikali haina budi kuwathamini Walimu kama kweli Serikali inakusudia kuboresha elimu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kulielezea Taifa kupitia Bunge hili kwamba, Serikali iliyoko madarakani sasa hivi ina *record* mbaya katika masuala ya elimu hapa nchini. Tumeona jinsi ambavyo ufaulu umekuwa ukishuka kwa kasi, tangu Serikali hii iingie madarakani. Aidha, matatizo ya maslahi duni ya Walimu yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka. Kwa vyovyote vile, Watanzania wasitegemee jambo jipya katika Elimu ikiwa watu ni wale wale, wenye mawazo yale yale wataendelea kutawala.

Napenda kuwaambia Walimu pia kwamba wasikate tamaa, bado wanayo nafasi ya kuchagua Serikali nyingine itakayojali maslahi yao. Lakini Serikali hiyo kamwe isitokane na CCM tena, kwa kuwa CCM imedhihirisha kwa vitendo kwamba imeshindwa kutoa elimu bora kwa watoto wetu na pia imeshindwa kutatua kero za muda mrefu za Walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Niabu Spika, Serikali ya CCM ilivyotumia fedha za Umma vibaya kwa kuunda Tume za Uchunguzi wa Matokeo Mabaya ya wanafunzi wa Kidato cha Nne, mwaka 2010/2012 na kutotumia mapendekezo ya Tume hizo katika kuboresha elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa vipindi tofauti, yaani mwaka 2010 na 2013, imeunda Tume kuchunguza sababu za kushuka kwa viwango vya ufaulu, ingawa *report* za Tume zinazoundwa kuchunguza sababu za kushuka kwa ufaulu hazijawekwa hadharani, na hivyo hazijulikani kwa wananchi ambao ni wadau wake wakuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Mei, 2013, Serikali ilitangaza kufutwa kwa matokeo ya Kidato cha Nne ya mwaka 2012 kutokana na kushuka mno kwa viwango vya ufaulu, ambapo zaidi ya asilimia 65 ya wanafunzi walipata daraja sifuri. Miezi sita baadaye, yaani Novemba, 2013, Serikali hiyo hiyo ilitangaza kubadili viwango vya ufaulu ambapo pamoja na mambo mengine, daraja la sifuri lilifutwa na badala yake kuwekwa daraja la tano, kama kiwango cha mwisho cha ufaulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, baada ya kelele nyingi kupigwa juu ya kufutwa kwa daraja la sifuri na kuanzisha daraja la tano, Serikali hii iliamua kubadili msimamo wake na hivyo daraja la sifuri likabaki na daraja la tano likaondolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwa makini utaona kwamba Serikali haikutumia mapendekezo ya Tume mbili ilizounda katika kufanya uamuzi wa kubadili matokeo ya Kidato cha Nne mwaka 2012, na pia haikutumia mapendekezo ya Tume hizo katika kubadili viwango vya ufaulu. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa maelezo katika Bunge hili, ni kwa nini ilitumia vibaya fedha za Umma kwa kuunda Tume ya Profesa Mchome ya 2013, wakati Tume ya Ndugu Liboy ilikuwa imeishafanya kazi hiyo mwaka 2011? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa Rai kwa Serikali, kuacha kufanya mambo yanayohitaji utaalam kwa ajili ya kujitafutia sifa za kisiasa. Suala la Elimu lisichukuliwe kama agenda ya kisiasa, kwani kwa kufanya hivyo tunaiua elimu yetu bila kujua, ama kwa kujua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama elimu bora ni ufunguo wa maisha, basi elimu mbovu ni ufunguo wa matatizo. Tatizo kubwa la Serikali hii ni kutofuatilia na usimamizi mbovu na kamwe siyo sera. Suala la kujiuliza, ni kwa nini Shule Binafsi zinafanya vizuri? Tanzania tumefika hapa na ni lazima mabadiliko makubwa yafanyike ili kunusuru elimu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa Mwanafunzi wa kuelewa vizuri au kwa ufasaha lugha anayoitumia kujifunzia na ule wa Mwaimu kwa mweledi katika lugha anayotumia kufundishia haupewi uzito unaostahili. Ni kawaida kukuta Mwalimu darasani akifundisha kwa lugha ambayo hata yeye mwenyewe haijui vizuri, na wanafunzi kutahiniwa katika hali hiyo hiyo. Tatizo hili linakumba hata Vyuo vyetu Vikuu.

Wote tunaelewa umuhimu wa lugha ya kujifunzia na kufundishia, na hii ndiyo sababu Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kwamba katika Bajeti ya Wizara ya Elimu ya Mafunzo ya Ufundi, katika mwaka wa fedha Serikali itenge fungu maalum kwa ajili ya uwekelezaji katika weledi wa lugha ya kufundishia na kujifunzia. Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kuchagua lugha moja itakayotumika kwa kufundishia, yaani kati ya Kiingerezda na Kiswahili ili watoto wetu wawe na weledi mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ruzuku mashuleni linatokana na Tanzania kuridhia kutekeleza mipango ya maendeleo ya elimu, ambao ni Mpango wa Maendeleo ya Elimu (MMEM) na ule wa (MMES) wa Sekondari. Lengo lilikuwa ni kuziwezesha Shule za Umma za Msingi na Sekondari, kuwa na

uwezo wa kujiendesha na kusimamia utoaji wa Elimu katika kiwango kinachostahili. Katika utekelezaji wa mipango yote miwili ilikubalika kwamba itolewe ruzuku ya Sh. 10,000/= kwa za Shule za Msingi na Sh. 25,000/= kwa kila mwanafunzi wa Shule ya Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzoefu umeonyesha kwamba mpango huu wa ruzuku mashuleni hautekelezwi ipasavyo, jambo linalopoteza ndoto ya maendeleo katika elimu. Kwa mfano, katika Awamu ya Kwanza ya utekelezaji wa Mpango wa Elimu wa (MMEM) ni kiasi cha wastani wa Sh. 6,000/= tu ndicho kilichofika shuleni badala ya Sh. 10,000/= kama ilivyopangwa na Sh. 16,384/= tu, badala ya Sh. 25,000/= kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kujiuliza ni kuwa katika hali hii ni vipi itawezekana katika kupata matokeo makubwa na ya haraka katika elimu? Hii maana yake ni kwamba badala ya kuwa na *Big Result Now*, tutakuwa na *Bad Result Now,* na hali ndivyo ilivyo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya Ukaguzi bado ni mbaya, uwezo wa Serikali kukagua shule hauridhishi. Kwa mujibu wa Haki Elimu, ni takriban asilimia 19 tu za Shule za Msingi hukaguliwa kwa mwaka na asilimia 21.4 tu ya Shule ya Sekondari hukaguliwa. Hii maana yake ni kwamba takriban asilimia 80 ya Shule zote za Msingi hazikaguliwi, na asilimia 70 ya Shule Sekondari hazikaguliwi. Kama hali ya ukaguzi ndiyo hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaihoji Serikali, tutegemee nini katika elimu yetu?

Mheshimwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu mfumo wa elimu unavyochangia tatizo la ajira nchi. Tatizo la ukosefu limeendelea kuwaumiza vichwa vijana na wazazi wengi nchini hasa wale wanaohitimu Vyuo vya Elimu ya Juu. Wengi wa vijana hawa wamejikuta wakitumia muda mwingi barabarani kusaka ajira bila mafanikio. Wataalam na wachambuzi wa masuala ya kijamii wanaliangalia tatizo la ukosefu wa ajira nchini kwa upana zaidi wakihusisha zaidi na mfumo mbovu wa elimu. Wanasema mfumo wa elimu uliopo hauendani ya hali halisi ya kichumi iliyopo nje ya mfumo wa shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa elimu na hasa mitaala haihusishi ujuzi wa stadi za kazi mbalimbali za uzalishaji, yaani *work production skills,* na hivyo Wahitimu wengi kukosa ujuzi na stadi zinazohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, Kambi ya Upinzani inashauri yafuatayo:-

(i) Uwepo utaratibu wa kufundisha fani zinazomwezesha mhitimu kujiajiri kama vile ufundi, ufugaji, uvuvi na nyinginezo. Hii itasaidia kupunguza vijana wanaokaa mitaani bila ajira na hatimaye

kuijitumbukiza kwenye vitendo vya uhalifu na ukosefu wa maadili. *(Makofi)*

(ii) Mheshimiwa Spika, wakati umefika sasa, kwa Serikali kuanda utaratibu utakaowezesha vijana wengi zaidi wanaohitimu kidato cha nne, na sita kujiunga na Vyuo vya Ufundi Studi *VETA*, na hata vyuo vya maendleo ya jamii, yaani *FDCs* ambavyo vimetapakaa nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu Mpango wa Matokeo Makubwa wa *Big Result Now*. Kambi Rasmi ya Upinzani inaunga mkono mipango yote yenye lengo la kuleta mageuzi chanya kwenye Sekta ya Elimu. Mpango huu wa *BRN* ni sehemu ya jitihada za Serikali ya Tanzania kuinua uchumi wake kutoka uchumi wa chini mpaka uchumi wa nchi yenye uchumi wa kati. Mpango umeingizwa nchini kwa kurudufiwa kutoka nchi ya Malaysia. Tunatambua jinsi mpango huu ulivyoinua uchumi na uwajikaji wa utendaji nchini humo. Katika Afrika, mpango huu unafuatwa na nchi za Nigeria na Rwanda, ambao umeonyesha mafanikio makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo na mikakati yote iliyooanishwa ni mizuri, lakini tunadhani mikakati hiyo imekuwepo kwa muda mrefu. Kilichokosekana ni utekelezaji na ufuatiliaji wake. Hivyo tungelipenda kufahamu ni mbinu gani mpya, ambazo Serikali na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi inakuja nazo safari hii ili tuelewe kupata matokeo makubwa sasa kwa kujiuliza masuala yafuatayo:-

(i) Kiapo walichokula Maafisa Elimu kinasaidia nini, kama hakuna fedha?

*(ii)* *Copy* za Mitihani ya zamani, yaani *Past Papers,* na ambazo zimesambazwa Mashuleni, zinamsaidiaje Mwanafunzi kuelewa?

(iii) Mwalimu ambaye ni mtekelezaji mkuu wa mpango huu, amemotishwaje?

(iv) Hatari inayolinyemelea Taifa kutokana na Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa, ni ukweli kwamba msisitizo umewekwa kwenye kuongeza kiwango cha kufaulu katika mitihani ya Taifa.

(v) Hatari iliyopo ni kwamba Walimu wataanza sasa kufundisha ili Wanafunzi wafaulu mitihani.

(vi) Wanafunzi watasoma kwa lengo la kufaulu mitihani tu badala ya kujifunza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tungelipenda Wizara izingatie angalizo hili kuona namna ambavyo *BRN* haitaharibu ari ya Wanafunzi kwa lengo la kujua mambo badala ya kukariri ili wafaulu mitihani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashauri Mikataba ya Utendajii kazi katika kila ngazi ya elimu iwekwe wazi ili kwa atakayeshindwa kutekeleza wajibu wake, ijulikane na awajibike. Hivyo kama kweli tunataka kupata mafanikio katika Sekta ya Elimu kama walivyopata wenzetu wa Malaysia, hatuna budi kubadilika katika utaratibu wetu wa utendaji kazi.

Kama tumeweza kuiga nadharia ya mpango, basi tuige pia hata utaratibu wao wa ufanyaji kazi ili tupate matokeo makubwa na mazuri kama wao. Tusije tukawa kama Namibia, walipoambiwa na Rais wao kuwa wanataka kufikia mwaka 2020 wawe kama wenzao wa Ulaya, baada ya mwezi mmoja tu wasichana wakawa Mitaani wemevalia kama wenzao wa Ulaya, yaani walivaa *min-skirt* au nguo fupi na walipoulizwa walisema, tayari tumeanza kuwa kama wenzetu wa Ulaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ubadhirifu wa fedha za Umma katika Sekta ya Elimu unavyodidimiza elimu yetu. Kwa muda mrefu sasa maendeleo ya elimu katika Taifa letu yamekuwa yakirudishwa nyuma na kuathiriwa sana na uwekezaji kidogo na ufinyu wa Bajeti unatokana na upotevu wa fedha za elimu katika njia ya badhirifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Report* ya Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, wakati wa Ukaguzi wa Fedha ya ruzuku shuleni, ilibainika kuwa jumla ya Shilingi bilioni 1.36, zilizopokelewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, fedha hizo bado hazijapelekwa shuleni kwa ajili ya utekelezaji. Pia jumla ya Sh. 496,000,000/= zilitumika kwa ajili ya matumizi yasiyohusiana na matumizi ya fedha ya ruzuku za shule, kama vile kulipa posho. Taswira hii ni mbaya katika kuboresha elimu na suala la kujiuliza ni hatua gani zimechukuliwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, *Report* ya *CAG* ilionyesha pia kwamba katika Halmashauri 13, jumla ya Shilingi billioni 1.4 zilzitengwa kwa ajili ya kuekeleza shughuli ya MMEM, hazikutumika hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha 2012/2013.

Kama vile haitoshi, Shilingi bilioni 21 ilizotolewa kwa ajili ya Mamlaka ya Serikali ya Mamlaka ya Serikali Mitaa 60 kwa ajili ya uekelezaji wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMESS), kwa malengo ya kuongezd ubora wa elimu na kupanua wigo wa wanafunzi kupenda kuendelea na masomo ya Sekondari. Hata hivyo, ni Shilingi bilioni 11.2 kati ya hizo sawa na asilimia 51 ndizo zilizotumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa *Report* hiyo, jumla ya Shilingi bilioni 2.6 zilizotengwa kwa ajili ya shughuli za mfuko wa kuchochea maendeleo ya Jimbo hazikutumika katika sampuli za Mamlaka ya Serikali za Mitaa 66. Hizi ni fedha zilizokusudia kuleta maendeleo katika Majimbo ikiwemo elimu. Kama fedha hizi zingetumika katika Sekta ya Elimu, zingeweza kutengenza zaidi ya madawati 17,333 kwa bei ya Sh. 150,000/= kwa kila dawati na kusaidia zaidi ya wanafunzi 34,666 kukaa juu ya madawati badala ya chini kama kila dawati lingekaliwa na wanafunzi wawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutoa misamaha mikubwa ya kodi kwa Sekta mbalimbali, mfano *report* ya CAG imebainisha kuwa hadi kufikia Juni, 2013 misamaha ya kodi iliyoidhinishwa ni kiasi cha Shilingi trilioni 1.5. Fedha hizi ni nyingi na zilikuwa na uwezo wa kujenga shule 300 zenye miundombinu iliyotimia kama maabara, maktaba na vifaa vya kujifunzia na kufundishia kwa gharama ya Shilingi bilioni tano kwa kila shule. Kwa hiyo, wakati Serikali inalia kushindwa kuhudumia wananchi wake kwa kuwapa elimu bora kwa kisingizio cha umasikini, bado inapoteza fedha nyingi sana kwa kisingizio cha misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukikusanya fedha zote ambazo tumesema, utaona kwamba tunapoteza Shilingi trilioni 1.5. Kama kiwango hiki cha fedha kingetumika kujenga nyumba za walimu peke yake kwa gharama ya Shilingi milioni 50 kwa kila nyumba, Serikali ingejenga zaidi ya nyumba 30,757. Kiwango hiki kingepunguza au kuondoa kabisa tatizo la makazi ya Walimu hasa maeneo ya vijijini na tumeona jinsi gani Wabunge wakilia kuhusu matatizo makubwa ya nyumba za Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kuhusu ajira za Walimu zisizozingatia uwiano wa mahitaji. Uhaba wa Walimu ni moja ya sababu zinazochangia wanafunzi kushindwa kujifunza vizuri na kuelewa mada za masomo mbalimbali. Katika kuabiliana na changamoto hii, Serikali katika mwaka huu wa fedha imeajiri jumla ya Walimu 17,928 kati yao na kuwasambaza katika shule mbalimbali za Msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaunga mkono jitihada hizi kwani baada ya kuajiri Walimu wapya 17,000 mwaka 2014 tatizo la shule kukosa Walimu limepungua.

Hata hivyo, Mikoa ya Kanda ya Ziwa bado ina matatizo makubwa ya Walimu. Upangaji wa Walimu Kimkoa, Kiwilaya na Kishule ni lazima uzingatie mahitaji ya Walimu kwenye eneo fulani ili kuwe na tija na ajira hizo na vilevile kuondoa manung'uniko katika maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ajira hizo, bado kuna upungufu mkubwa na Walimu wengi huko Mitaani hawajapata ajira. Kambi ya Upinzani

inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili, ni lini watatoa ajira kwa Walimu hawa ambao bado wamezaa Mitaani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaunga mkono maendeleo yanayofanyika katika kupanua elimu ya juu nchini kwani kuanzia mwaka 2006 hadi 2013 vimeongezeka Vyuo 20 na idadi ya wanafunzi waliodahiliwa imefika 133,000. Hata hivyo, bado bado udahili ni mdogo sana ukilinganisha na nchi nyingine katika Bara la Afrika.

Takwimu zinaonyesha kwamba Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye udahili wa chini kabisa katika Vyuo Vikuu. Kwa mujibu wa taarifa ya *SARUA* yaani *Southern African Region University Association* ushiriki wa Watanzania katika elimu ya juu, yaani wastani wa watu wenye elimu ya juu ni 2% tu tukiwa mbele ya nchi za Malawi na Msumbiji. Hii ni aibu kubwa ukizingatia Tanzania ina *population* ya watu milioni 45 na Vyuo Vikuu 50. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ubora wa elimu ya juu Tanzania unatia shaka kubwa sana. Kwa mfano, utafiti uliofanywa na Baraza la Ushirikiano la Vyuo Vikuu, yaani *Inter-university Council for East Africa* kwa kushirikiana na Baraza la Biashara la Afrika Mashariki unaonyesha kuwa asilimia 39 tu ya wahitimu wa Vyuo Vikuu Tanzania ndiyo wenye maarifa na stadi zinazoweza kuwafanya waajirike.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa takwimu za *SARUA Tanzania* ni miongoni mwa nchi zilizo Kusini Mashariki mwa Afrika ambazo zinachangia kidogo sana katika kuzalisha maarifa kupitia machapisho katika majarida ya kitaaluma na kisayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Bodi ya Mikopo kujitahidi sana kulipa fedha za Walimu, bado kuna ucheleweshaji na kusababisha usumbufu mkubwa sana kwa wanafunzi na Uongozi wa Vyuo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulipa posho za wanafunzi kwa wakati ili kuondokana na migomo, maandamano, uvunjifu wa amani ambavyo vinaathiri ubora wa elimu katika Vyuo vyetu vya Elimu ya Kuu. *(Makofi)*

Aidha, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuongeza fedha kwa ajili ya kuwasomesha Wahadhiri wa Vyuo Vikuu katika Shahada ya Uzamivu yaani *Ph.D* kwa kuwa kumekuwa na kilio cha siku nyingi kwa Wahadhiri wetu kutoendelezwa katika ngazi ya uzamivu na sababu zinazotolewa ni gharama kubwa kulipia masomo yao. Hali hii imefanya Wahadhiri wengi kubaki na Shahada za Uzamili kwa muda mrefu na hata kustaafu katika ngazi hiyo. Hivyo ubora wa elimu katika Vyuo vya Elimu ya Juu unaathirika kwa kuwa unakuta mwanafunzi wa Shahada ya Uzamili *(Masters)* wanafundishwa na Mhadhiri mwenye Shahada ya Uzamili badala ya Mhadhiri mwenye *Ph.D.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna shaka kuwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni Chuo kikongwe zaidi hapa nchini. Chuo hiki pamoja na sifa kilichojijengea ndani na nje ya nchi kinaendelea kukumbwa na matatizo lukuki ikiwa ni pamoja na miundombinu mibovu, majengo, ubovu wa vyoo na mabafu katika mabweni. Pamoja na matatizo hayo, bado Chuo hiki hakijafanyiwa ukarabati kwa kipindi kirefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Wizara itoe maelezo juu ya hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa ahadi aliyoitoa Mheshimiwa Rais alipofika kwenye maadhimisho ya Chuo Kikuu kwamba Serikali itatenga fedha za kutosha katika bajeti ili kukamilisha ujenzi wa Kituo cha *Student Centre* katika *Campus* ya Mlimani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanzoni mwa mwaka 2012 Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kiliwafukuza wanafunzi 50 lakini hadi sasa kuna wanafunzi 15 hawajarejeshwa. Hii ndiyo kusema kwa mujibu wa Sheria za Chuo, wanafunzi hawa wanapaswa kuanza mwaka wa kwanza wa masomo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inalaani kitendo hicho cha ukatili cha kuwanyima watoto wa Kitanzania maskini haki yao ya kupata elimu kwa visingizio mbalimbali. *(Makofi)*

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua sababu zilizosababisha Serikali ya CCM kuwadhulumu haki yao watoto hawa na vilevile tunataka Serikali kuwarudisha vijana hawa bila masharti. Kama wamegundua masomo yao, basi waelezwe na wale waliorudishwa wapewe stahili zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi pamoja na kuvisimamia moja kwa moja Vyuo Vikuu hapa nchini vilivyo chini ya Wizara tajwa, inayo pia wajibu wa kuhakikisha kuwa Vyuo Vikuu vilivyo chini ya Taasisi nyingine za Umma na Binafsi vinaendeshwa kwa viwango vinavyohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani imepokea taarifa ya mgogoro mkubwa katika Chuo cha Mtakatifu Joseph, Tawi la Songea uliopelekea kufungwa Chuo hicho kwa muda mgogoro huu kuwa ni kushindwa Uongozi wa Chuo kusimamia mfumo wa uendeshaji wa usimamizi wa Vyuo Vikuu. Kambi yetu ilifahamishwa kuwa Uongozi wa Serikali ya wanafunzi uliandika barua kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Desemba, 2013. Hata hivyo, tuna taarifa kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri ametembelea Chuo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Chuo hiki inadaiwa kuwa wanafunzi wanapofiwa au wanapopata matatizo ya ujauzito au matatizo mengine huwa hawapewi fursa ya kufanya *special papers* kama ilivyo katika Vyuo vingine. Vilevile wamekuwa wakicheleweshewa vyeti vyao, kwa mfano waliomaliza

mwaka 2013 mpaka leo hawajapewa vyeti vyao na hivyo kuwafanya washindwe kupata ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inatarajia kupata majibu ya kutosha na utekelezaji makini wa Serikali na kutolea maelezo ni kwa jinsi gani wametekeleza matatizo yanayokikumba Chuo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee Chuo cha Madini Dodoma. Chuo cha Madini yaani *Mineral Resources Institute* ni miongoni mwa Idara zilizo chini ya Wizara ya Nishati na Madini ambayo haina mamlaka kamili inayojitegemea kimuundo. Chuo hiki kilianzishwa miaka ya 78 hakina muundo wa uongozi tangu kuanzishwa kwake kama Taasisi ya kitaaluma. Hali hii imesababisha matatizo makubwa ya kiutendaji na kitaaluma, mfano kufeli kwa wingi kwa wanafunzi; mwaka 2012/2013 walifeli wanafunzi 55; na mwaka 2013/2014 wanafunzi 67, kwani kila Mkuu wa Chuo anapoingia anajiundia Idara na kuchagua Watendaji wa kukaimu. Kambi ya Upinzani inaomba Serikali kupitia Wizara hii kufuatilia kwa kina matatizo yaliyopo Chuoni hapo ili kunusuru vijana wetu na adhira hii ya kufeli shuleni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchambuzi mfupi wa bajeti wa bajeti ya Elimu. Ni wazi kuwa bajeti ya Wizara ya Elimu imeongezeka kutoka Shilingi bilioni 689 hadi Shilingi bilioni 799 mwaka huu na bajeti ya matumizi ya maendeleo inaonekana kuongezeka kutoka Shilingi bilioni 72 mwaka 2013 na kufikia Shilingi bilioni 454 mwaka 2014, huku bajeti ya matumizi ya kawaida ikionekana kushuka kutoka Shilingi bilioni 612 kwenda 344. Kimtazamo sura ya bajeti hii ina uwiano mzuri kwa maana ya ongezeko la bajeti na magawano ya matumizi ya maendeleo na yale ya kawaida. Hii ni kama ambavyo wadau wengi na hata Wabunge walivyokuwa wakishauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, inaonyesha kwamba bajeti ya maendeleo ni asilimia 57 wakati ile ya kawaida ni asilimia 43. Lakini ukiangalia utaona kwamba kimsingi ongezeko hilo limetokana na mabadiliko katika upangaji wa baadhi ya vifungu ambavyo hapo awali vilipangwa katika bajeti ya kawaida. Kwa mfano, fedha za Bodi ya Mikopo zimeondolewa kwenye bajeti ya matumizi ya kawaida *sub-vote 7001 - Higher Education* na kuhamishiwa katika bajeti ya maendeleo *sub-vote 1003*. *(Makofi)*

Uchambuzi unaonyesha kuwa bado hakuna uwekezaji wa kutosha katika miradi ya maendeleo kwa kuwa sehemu kubwa ya bajeti yake inakwenda kugharamia mikopo ya elimu ya juu. Shilingi bilioni 307 kati ya Shilingi bilioni 454 ya bajeti ya maendeleo ya Wizara zinakwenda kulipia mikopo ya elimu ya juu. Hii ni sawa na asilimia 68 ya bajeti nzima ya maendeleo. Hivyo, tunaweza kusema kwamba fedha iliyopangwa kwa shughuli za maendeleo mwaka 2015

ni ndogo kuliko iliyotengwa mwaka 2013/2014 wakati changamoto bado ni nyingi. Hivyo Wizara hii wala isijisifu kwamba imeongeza fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kama nilivyoeleza hapo awali, elimu ya Tanzania hasa kwa Shule za Msingi na Sekondari imeshuka kwa kasi ya ajabu katika mihula yote miwili ya utawala wa Serikali ya Nne. Hali hii inadhihirisha kwamba Serikali ya CCM imeshindwa hata kutekeleza Ilani yake ya Uchaguzi kuhusu elimu bora kwa Watanzania.

Aidha, sababu kubwa ni udhaifu wa kiuongozi zaidi kuliko sababu nyingine yoyote inayotajwa na Serikali. Uongozi dhaifu umepelekea misamaha ya kodi na hivyo kupoteza fedha nyingi ambazo zingeweza kuboresha elimu yetu. Udhaifu huu umesababisha ubadhirifu wa fedha za elimu, ufanyaji wa maamuzi katika masuala ya msingi ya elimu bila kuzingatia mapendekezo ya Tume mbalimbali ambazo ziliundwa kuchunguza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Karl Marx alivyosema, "*force is the midwife of every old society pregnant with a new one.*" Ikiwa na maana kwamba matumizi ya nguvu ni lazima kwa mama aliyefikia siku za kujifungua na asijifungue na kwamba bila kumpasua wote wawili mama na mtoto watakufa, ila ukimpasua au mmoja anaweza kupona au wote wanaweza kupona.

Hivyo hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema, bila kufanya mageuzi makubwa katika mfumo wetu wa utawala, kuna hatari kubwa ya Taifa kuangamia kwa kuwa wananchi wasio na elimu bora ya kuwawezesha kukabiliana na mazingira yao ili kumudu maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyopendekeza mwaka jana, 2013 tunarudia kupendekeza tena kwamba Serikali ianzishe chombo cha udhibiti wa Elimu na Mafunzo ya ufundi, yaani *Tanzania Education and Training Regulatory Authority* ambacho kitaweka viwango vya ubora wa elimu kwa mujibu wa mitaala iliyopitishwa na Serikali kudhibiti utungaji, usahihishaji na upangaji wa matokeo ya mitihani, kudhibiti gharama za elimu, ada na michango mingine baina ya Shule na Taasisi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kulitaarifu Bunge hili na wananchi kwa ujumla kwamba kudorora kwa elimu nchini kunatokana na Serikali kuwa na viongozi wababaishaji, wasemaji wa maneno mengi, wasiotekeleza wanayosema na kukosa ufuatiliaji. Hivyo, Wizara hii inahitaji kufanyiwa mabadiliko makubwa, vinginevyo Tanzania itaendelea kudidimia kielimu na hivyo kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana Makatibu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wakiongozwa na Oliver Mwikila na kipekee namshukuru

sana Ndugu Onesfo Mbuya kwa kushirikiana nami hatua kwa hatua wakati wa maandalizi ya hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha kwa niaba ya Kambi ya Rasmi ya Upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mhe. Susan J. A. Lyimo, Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa 2014/2015, Kama Ilivyowasilishwa Mezani**

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI MHE. SUSAN ANSELM JEROME LYIMO (MB), KUHUSU MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA 2013/2014 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KATIKA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2014/2015**

1. **UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Kanuni ya 99, kanuni ndogo ya (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2013, napenda kuchukua nafasi hii kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

**Mheshimiwa Spika,**Kwa muda mrefu sana, tumeonya na kushauri juu ya hatari inayolinyemelea Taifa letu kutokana na Serikali ya CCM kuharibu mfumo wetu wa elimu. Tunasikitika kwamba ushauri wetu, maonyo na nasaha tulizotoa, zilibezwa kwa kishindo ndani na nje ya Bunge. Sasa si maonyo wala utabiri tena bali ukweli umeonekana jinsi ambavyo mfumo wetu wa elimu uliyoporomoka. Ni jambo la kusikitisha kwamba leo hii asilimia 70% ya watoto wakitanzania wa umri kati ya miaka 7 – 16 hawawezi kuelezea hata maana ya rangi tatu za bendera ya Taifa (ukitoa nyeusi). Vile vile ni mwanafunzi mmoja au pungufu kati ya 10 wa darasa la tatu anayeweza kusoma hadithi kwa kingereza katika darasa la pili. Aidha, ni mwanafunzi mmoja tu kati ya wanne katika darasa la 3 anayeweza kusoma kwa ufasaha kitabu cha darasa la pili kwa Kiswahili. Takwimu hizi zimetolewa na Ripoti ya Tathmini ya Mwaka ya Shirika lisilo la Kiserikali linaloshughulikia Masuala ya Elimu la UWEZO ya mwaka 2012.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha miaka 8 ya utawala wa Rais Kikwete, kiwango cha ufaulu katika ngazi ya msingi na sekondari kimeendelea kushuka. Kwa mujibu wa Takwimu za Serikali zinazopatikana kwenye kitabu cha takwimu

za elimu (Basic statstics in Education in Tanzania - BEST), katika kipindi hiki kiwango cha KUFELI huku kulifikia kilele mwaka 2012 pale ambapo 65.5% walipata daraja '0' . Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilisema mwaka jana kwamba kuna wataalamu wa masuala ya elimu wanabashiri kwamba kiwango cha kufeli kinaweza kupanda hadi kufikia 95% kama hakutakuwa na ujanja ujanja wa kufuta matokeo na kuyapanga upya. Na hili limetokea na tumeona matokeo ya 2013 yakipandishwa hadi kufikia asilimia 58.9 kutokana na upangaji upya wa alama na madaraja ya kufaulu.

**Mheshimiwa Spika,** Ukweli ni kwamba kiwango cha kufaulu hakikupanda bali kilipandishwa ili kufuta aibu ambayo imekuwa ikiikumba serikali tangu awamu ya nne iingie madarakani. Watanzania wanapaswa kuelewa kuwa mchezo unaofanywa na serikali ya CCM wa kuchezea madaraja na alama za kufauli utaligharimu sana taifa hili huko tuendako kwa sababu mfumo wetu wa elimu utakuwa unatoa wahitimu ambao wanafaa hapa Tanzania pekee lakini wasio na sifa katika wigo wa kimataifa.

**Mheshimiwa Spika,**Pamoja na wabunge na wadau mbalimbali wa elimu kupiga kelele kuhusiana na upangaji mpya wa alama na madaraja, bado Wizara imeendelea kutekeleza mpango wake na hivyo matokeo ya 2013 ya Kidato cha 4 yamepangwa kwa kutumia alama mpya za ufaulu. Sababu za kuporomoka kwa mfumo wetu wa elimu zinajulikana na zimeainishwa katika tafiti mbalimbali na ripoti za tume za uchunguzi kuhusu matokeo mabaya ya mitihani ya kidato cha nne za mwaka 2011 na 2013.

## 2. MFUMO DUNI WA ELIMU NCHINI

**Mheshimiwa Spika,** Ni ukweli ulio wazi kuwa mfumo wetu wa Elimu umepitwa na wakati. Ni wazi kuwa watoto wetu wanaanza shule ya msingi kwa kuchelewa sana na wanakaa shuleni kwa muda mfupi. Kiwango cha wastani duniani cha muda wa kusoma shuleni ni ni miaka 9 lakini wa kwetu ni miaka 7 pekee. Matokeo yake watoto wetu wanamaliza shule wakiwa wadogo na bila kuwa na maarifa na stadi za msingi za kuwafanya wajitegemee.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikitoa mapendekezo kadhaa ili kuboresha mfumo wa elimu hapa nchini. Mapendekezo haya ni pamoja na:

i. Wigo wa elimu ya msingi upanuliwe ili watoto wakae shuleni kwa muda usiopungua miaka tisa kama ilivyo katika viwango vya kimataifa,

ii. Elimu ya msingi iunganishwe na elimu ya mafunzo ya ufundi ili kwamba vijana wetu wamalizapo elimu ya msingi wawe na

maarifa na stadi za kufanya kazi itakayowafanya wajitegemee popote walipo.

iii. Watoto waanze shule mapema.

iv. Miundombinu ya elimu iboreshwe.

v. Maslahi ya walimu yaboreshwe.

vi. Wakala wa ukaguzi uanzishwe.

vii. Fedha za ruzuku kwa wanafunzi zifike kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kwamba Serikali imechukua mapendekezo iliyoyatoa kuhusu kubadili mfumo wa Elimu yetu kuyaingiza katika Sera mpya ya elimu. Hata hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kuyafanyia kazi mapendekezo hayo na sio kuyaingiza tu katika Sera bila utekelezaji.

**3. SERIKALI YA CCM ILIVYOSHINDWA KUTEKELEZA ILANI YAKE YA UCHAGUZI KWA AWAMU ZOTE MBILI KUBORESHA ELIMU NA MASLAHI YA WALIMU NCHINI.**

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 92(h) na (j) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 -2010 inasema kwamba; "*CCM inatambua kwamba, elimu ni haki ya msingi kwa kila mwananchi na ndio ufunguo wa maendeleo. Ili kuendeleza sekta hii Serikali ya CCM itazingatia ipasavyo suala la ubora wa elimu, Kama linavyoshughulikiwa suala la wingi, na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Elimu iliyoandaliwa na kuendeleza maslahi ya walimu*"

**Mheshimiwa Spika,** Elimu ya Tanzania kwa sasa, imeporomoka mara dufu na hali ya maisha ya walimu ni mbaya zaidi kuliko ilivyokuwa mwaka 2005 wakati CCM ilipoahidi kuboresha elimu na maslahi ya walimu. Katika hotuba ya Kiongozi wa Upinzani Bungeni hapa bungeni mwaka jana wa fedha 2013/2014, alisema kwamba mwaka 2007 miaka miwili tu baada ya Serikali ya awamu ya nne kushika madaraka, ufaulu wa vijana wetu wa kidato cha nne ulikuwa asilimia 90.3. Mwaka 2008 ufaulu ulishuka hadi asilimia 83.6, mwaka 2009 ufaulu uliendelea kushuka hadi kufikia asilimia 72.5 na mwaka 2010 ufaulu uliporomoka kwa kasi zaidi hadi kufikia asilimia 50.4

**Mheshimiwa Spika;**Kwa muhula wote wa kwanza wa mikaka mitano ya Utawala wa awamu ya nne yaani 2005 -2010; Serikali ya CCM imeshindwa kabisa kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM kuhusu elimu bora kwa watanzania. Hii ni kwa sababu kiwango cha ufaulu kimekuwa kikishuka kwa miaka yote mitano ya

muhula wa kwanza wa utawala wa Serikali ya CCM kama nilivyoonyesha hapo juu.

**Mheshimiwa Spika,**Kuhusu maslahi ya walimu, Serikali ya CCM imeshindwa kutekeleza ilani ya CCM ya kuboresha maslahi ya walimu kama ilivyoahidi katika Uchaguzi Mkuu wa 2010. Miaka yote mitano ya muhula wa kwanza wa utawala wa awamu ya nne wa Serikali ya CCM ilikuwa ni miaka ya adha kubwa kwa walimu iliyotawaliwa na migomo na kesi dhidi ya walimu kwa sababu ya kudai stahili zao ambazo Serikali ilishindwa kuzilipa. Kwa mujibu wa Chama Cha Walimu (CWT), hadi kufikia mwezi Disemba 2013, madai ya walimu ambayo hayakulipwa yalifikia shilingi bilioni 61. Ombi la CWT kwa Serikali kuongeza mishahara ya walimu kwa asilimia 50 lilimekataliwa na walimu wameendelea kupuuzwa.

**Mheshimiwa Spika**,Katika hotuba yangu nikiwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani katika bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi katika mwaka wa fedha 2012/2013 nilitoa angalizo kwamba; endapo walimu wataachwa na kinyongo kwa kutolipwa madai yao na kama walimu wataamua kulipa kisasi kwa kuwafundisha watoto vitu visivyo halisi basi kuna hatari kubwa ya kuja kuwa na kizazi kisicho na elimu kabisa, na hatimaye kuwa na Taifa lisilojiweza katika nyanja zote na hapo ndipo kutakuwa na ANGUKO KUU LA NCHI (Total State Collapse).

**Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, imeahidi kuwa italipa madai haya ya walimu katika Mwaka wa fedha 2014/2015. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini ahadi hii itatekelezwa na kwamba fungu hili limetengwa katika bajeti hii ili tuondokane na kadhia hii. Serikali itambue, "Uzuri wa mfumo wa elimu unategemea ubora wa walimu wake". Kwa mantiki hiyo, Serikali haina budi kuwathamini walimu kama kweli serikali inakusudia kuboresha elimu nchini. Walimu wamekata tamaa, na tusipokuwa makini hali hii itaambukizwa kwa watoto wetu, familia zao na hatimaye sehemu kubwa ya jamii pia itakata tama. Jambo hili ni hatari kwa uchumi na ustawi wa taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,**Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kulieleza Taifa kupitia Bunge hili kwamba, Serikali iliyoko madarakani sasa hivi ina rekodi mbaya katika masuala ya elimu hapa nchi. Tumeona jinsi ambavyo ufaulu umekuwa ukishuka kwa kasi tangu Serikali hii iingie madarakani. Aidha, matatizo ya maslahi duni ya walimu yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka. Kwa vyovyote vile watanzania wasitegemee jambo jipya katika elimu ikiwa watu walewale wenye mawazo yale yale wataendelea kutawala. Napenda kuwaambia walimu pia kwamba, wasikate tamaa bado wana nafasi ya kuchagua Serikali nyingine itakayojali maslahi yao lakini Serikali hiyo isitokane na CCM tena kwa kuwa CCM imedhihirisha kwa vitendo kwamba imeshindwa

kutoa elimu bora kwa watoto wetu na pia imeshindwa kutatua kero za muda mrefu za walimu.

**4. SERIKALI YA CCM ILIVYOTUMIA VIBAYA FEDHA ZA UMMA KWA KUUNDA TUME ZA UCHUNGUZI WA MATOKEO MABAYA YA WANAFUNZI WA KIDATO CHA CHA NNE YA MWAKA 2010 NA 2012 NA KUTOTUMIA MAPENDEKEZO YA TUME HIZO KATIKA KUBORESHA ELIMU YA TANZANIA.**

**Mheshimiwa Spika,**Kwa miaka mitatu mfululizo, elimu ya Tanzania, na hasa kwa ngazi ya elimu ya msingi na sekondari, umekuwa ukiporomoka kwa kasi ya ajabu. Kufuatia kuporomoka huko, na hasa kushuka kwa viwango vya ufaulu, Serikali kwa vipindi totauti (mwaka 2010 na 2013) imeunda Tume kuchunguza sababu za kushuka kwa viwango vya ufaulu. Ingawa ripoti za tume zilizoundwa kuchunguza sababu za kushuka kwa ufaulu hazijawekwa hadharani na hivyo hazijulikani kwa wananchi ambao ni wadau wakuu wa elimu.

**Mheshimiwa Spika,** Mwezi Mei, 2013 Serikali ilitangaza kufutwa kwa matokeo ya kidato cha nne ya mwaka 2012 kutokana na kushuka mno kwa viwango vya ufaulu ambapo zaidi ya asilimia 65 ya wanafunzi walipata daraja sifuri na kuamuru matokeo hayo kupangwa upya. Miezi sita baadaye, yaani Novemba, 2013 Serikali ilitangaza kubadili viwango vya ufaulu ambapo pamoja na mambo mengine, daraja la sifuri lilifutwa na badala yake kuweka daraja la tano kama kiwango cha mwisho cha ufaulu. Hata hivyo baada ya kelele nyingi kupigwa juu ya kufutwa daraja la sifuri na kuanzishwa daraja la tano, Serikali iliamua kubadili msimamo wake na hivyo daraja sifuri likabaki na daraja la tano likaondolewa.

**Mheshimiwa Spika**, Baada msererekо wa matokeo mabaya ya mitihani kwa wanafunzi wa sekondari na hususan kidato cha nne Seriakali ilifanya mambo yafuatayo:

i. Serikali iliunda tume ya mwaka 2010 chini ya uenyekiti wa Ndugu Francis Liboy kuchunguza sababu za kufeli kwa wanafunzi. Kabla ripoti ya Tume hiyo kutolewa, Serikali iliunda Tume nyingine kuhusu jambo hilohilo la kufeli kwa wanafunzi mwaka 2012 chini ya uenyekiti wa Profesa Sifuni Mchome.

ii. Serikali ilifuta matokeo ya kidato cha nne ya mwaka 2012 na kuyapanga upya kabla Ripoti ya Tume ya Uchunguzi ya Prof. Mchome kutolewa na hivyo mapendekezo ya tume hiyo hayakuzingatiwa wakati wa kubadili matokeo hayo.

iii. Serikali ilibadili viwango vya ufaulu ikiwa ni pamoja na kufuta daraja sifuri na kuanzisha daraja la tano. Hata hivyo baada ya pingamizi kubwa kutoka kwa wadau wa elimu Serikali ilibadili msimamo wake na kurejesha daraja la sifuri na kufuta daraja la tano.

**Mheshimiwa Spika,**Ukiangalia kwa makini, utaona kwamba Serikali haikutumia mapendekezo ya tume mbili ilizoziunda katika kufanya uamuzi wa kubadili matokeo ya kidato cha nne ya mwaka 2012 na pia haikutumia mapendekezo ya tume hizo katika kubadili viwango vya ufaulu. Hivyo, fedha zilizotumika na tume hizo zilipotea bure kwa kuwa mapendekezo hayo hayajafanyiwa kazi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa maelezo katika Bunge hili, ni kwa nini ilitumia vibaya fedha za umma kwa kuunda tume ya Prof. Mchome ya 2013 wakati Tume ya Ndugu Liboy ilikuwa imeshafanya kazi hiyo mwaka 2011?

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa rai kwa Serikali kuacha kufanya mambo yanayohitaji utaalamu kwa ajili ya kujitafutia sifa kisiasa. Suala la elimu lisichukuliwe kama ajenda ya kisiasa kwani kwa kufanya hivyo tunaiua elimu yetu bila kujua.

**Mheshimiwa Spika,**Ni vema kabla Serikali haijafanya maamuzi ya jambo linaloathiri maisha ya watanzania wengi kama hili la mitihani ikaleta kusudio la kufanya hivyo bungeni ili wabunge ambao ni wawakilishi wa wananchi wajadili na kuishauri Serikali Ipasavyo. Hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kufuta uamuzi wake wa kubadili viwango vya ufaulu na badala yake iboreshe mazingira ya kufundisha na kujifunza.

**Mheshimiwa Spika,**Kama elimu bora ni ufunguo wa elimu basi, elimu mbaya ni ufunguo wa matatizo. Tatizo kubwa la serikali hii ni kutofuatilia na usimamizi mbovu na kamwe si sera. Mbona shule za binafsi wanafanya vizuri? Tanzania tumefika hapo na ni lazima mabadiliko yafanyike ili kuinusuru elimu yetu.

## 5. UWEKEZAJI KATIKA LUGHA YA KUJIFUNZA NA KUFUNDISHIA

**Mheshimiwa Spika,**Umuhimu wa mwanafunzi kuelewa kwa ufasaha lugha anayotumia kujifunzia na ule wa mwalimu kuwa mweledi katika lugha anayotumia kufundishia haupewi uzito unaostahili. Ni kawaida kukuta mwalimu darasani akifundisha kwa lugha ambayo hata yeye mwenyewe haijui vizuri na wanafunzi kutahiniwa katika hali hiyo hiyo.

**Mheshimiwa Spika,**Lugha ya kiingereza mathalani, ndiyo lugha ambayo inatumika kufundishia na kujifunza kwa masomo yote (Ukitoa somo la Kiswahili) kwa ngazi ya sekondari hapa nchini. Lakini cha ajabu ni kwamba imekuwa ni kawaida kukuta walimu na wanafunzi wakiwa na ujuzi mdogo wa lugha hii ambayo tumeruhusu itumike. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali serikali ianze kuwekeza katika kuwajengea weledi wa lugha walimu, kwa kutenga bajeti maalumu ya kuwapa mafunzo maalumu ya lugha ya kiingereza

walimu wanaokwenda au ambao wanafundisha kutumia lugha hii na kununua vitabu na vifaa maalumu vya kufundishia na kujifunzia lugha hii, ili kuwasaidia wanafunzi pia. Wazo hili ni muhimu ili kuwezesha wanafunzi kuelewa mada na hatimaye kujifunza vizuri.

**Mheshimiwa Spika,**Ni kwa sababu hii Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kwamba katika Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi katika mwaka huu wa fedha 2014/2015, Serikali itenge fungu maalumu kwaajili ya uwekezaji katika weledi wa lugha na hasa ya kiingereza ambayo ndiyo inatumika kama lugha ya kufundishia na kujifunzia lakini imekuwa ni kikwazo kikubwa katika kufundisha na kujifunza. Kambi ya upinzani inaishauri serikali kuchagua lugha moja itakayotumika katika kufundishia yaani kati ya kiingereza na kiswahili.

## 6. UPUNGUFU WA RUZUKU SHULENI

**Mheshimiwa Spika,**Suala la Ruzuku Mashuleni linatokana na Tanzania kuridhia kutekeleza mipango ya maendeleo ya elimu ambayo ni Mpango wa maendeleo Elimu ya Msingi(MMEM) na Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES). Lengo lilikuwa kuziwezesha shule za umma za msingi na sekondari kuwa na uwezo wa kujiendesha na kusimamia utoaji wa elimu katika kiwango kinachostahili. Katika utekelezaji wa Mipango hiyo ya maendeleo ya elimu, ilikubaliwa kuwa itolewe ruzuku ya shilingi 10,000/= kwa kila mwanafunzi wa shule ya Msingi na shilingi 25,000/= kwa kila mwanafunzi wa shule za sekondari.

**Mheshimiwa Spika,**Uzoefu unaonyesha kwamba Mpango huu wa ruzuku mashuleni ambao ulitegemewa kufanya mageuzi ya maendeleo katika sekta ya elimu hautekelezwi ipasavyo jambo ambalo linapoteza ndoto ya maendeleo katika elimu. Hii ni kwa sababu viwango vya ruzuku vilivyopangwa kwa kila mwanafunzi havitolewi kwa ukamilifu.Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na shirika lisilo la kiserikali la Hakielimu kiasi cha ruzuku kinachotolewa, licha ya kuwa pungufu na kile kilichopangwa, bado kiasi hicho kimekuwa kikipungua kwa mfululizo kwa awamu zote tatu za utekelezaji wa mpango. Kwa mfano katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM I), ni kiasi cha wastani wa shilingi 6,497 tu ndicho kilichofika shuleni badala ya shilingi 10,000/= iliyopangwa. Kiasi hicho kilipungua hadi kufikia wastani wa shillingi 5,500 katika awamu ya pili ya utekelezaji wa mpango huo (MMEM II). Aidha, kiasi cha ruzuku iliyofika mashuleni katika awamu ya tatu (MMEM III) kiliendelea kupungua hadi kufikia wastani wa shilingi 3,580 tu badala ya kiwango cha 10,000/= kilichopangwa.

**Mheshimiwa Spika,**Hali hii inazikumba pia shule za sekondari ambazo nazo zinapokea wastani wa sh. 16,384 tu badala ya 25, 000 kwa mwaka kwa kila

mwanafunzi kama mpango unavyoelekeza. Ikumbukwe tu hapa kuwa viwango hivi ni wastani tu wa hali ya utoaji ruzuku shuleni, lakini katika hali halisi ziko shule nyingi ambazo hupata chini ya wastani wa shilingi 1500/= kwa mwanafunzi kwa mwaka. Swali la kujiuliza ni kuwa, katika hali hii ni vipi itawezekana kupata matokeo makubwa kwa haraka katika elimu? Hii maana yake ni kwamba badala ya kuwa na *'Big Results Now' tutakuwa na 'Bad Results Now'* na hali ndivyo ilivyo sasa.

**Mheshimiwa Spika,**Ni wazi katika mazingira haya, utekelezaji wa malengo ya kuboresha elimu hautafanikiwa. Serikali imekuwa ikitoa majibu yaleyale ya uhaba wa fedha kila inaposhauriwa juu ya umuhimu wa kupeleka fedha za ruzuku zilizokamilika na kwa wakati. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaliomba Bunge hili kuiondoa Bajeti ya Elimu katika Mjadala wa Bunge kama fedha za ruzuku katika shule za Msingi na Sekondari hazikutengwa kwa ukamilifu wake.

**Mheshimiwa Spika,**Ni muhimu sana kuangalia kwa undani bajeti ya ruzuku kwa shule za umma ambayo imekuwa haifiki kamili na kwa wakati hivyo kuzorotesha utekelezaji wa mipango ya shule ya kuboresha elimu. Kuzungumza bungeni kwa ukali na hisia ni hatua moja ya kukemea, lakini ni muhimu kuonesha wananchi kwa vitendo kwa kuzuia kupitisha bajeti ambayo haizingatii na kulenga kuboresha elimu kwa maslahi ya watanzania walio wengi.

## 7. UKAGUZI WA SHULE NA TAASISI ZA ELIMU

**Mheshimiwa Spika,**Hali ya ukaguzi bado ni mbaya. Uwezo wa serikali kukagua shule hauridhishi. Kwa mujibu wa Hakielimu, ni takribani asilimia 19.1% tu ya shule zote za msingi ambazo hukaguliwa kwa mwaka. Kwa upande wa shule za Sekondari ni asilimia 21.4 tu ya shule za sekondari ambazo hukaguliwa kwa mwaka. Hii maana yake ni kwamba takribani asilimia 80% ya shule zote za msingi hazikaguliwi na takribani asilimia 70 ya shule za sekondari hazikaguliwi.Kama hali ya ukaguzi ndivyo ilivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaihoji Serikali; tutegemee nini katika Elimu?

**Mheshimiwa Spika,**Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inarudia kuishauri tena Wizara na Serikali kwa ujumla kuhusu umuhimu wa shule kukaguliwa mara kwa mara ili kujua kama malengo na dira ya elimu itafikiwa. Kambi ya upinzani inahoji tena wakala wa ukaguzi ambao ungekuwa suluhisho la tatizo kwani tunaamini uwepo wake ungeongeza ufanisi na tija katika sekta hii na kwa vyovyote vile tungeona mabadiliko makubwa sana. Swali ni je mpango huu umeishia wapi?

## 8. MFUMO WA ELIMU UNAVYOCHANGIA TATIZO LA AJIRA NCHINI

**Mheshimiwa Spika,**Tatizo la ukosefu wa ajira limeendelea kuwaumiza vichwa vijana wengi nchini, hasa wale wanaohitimu vyuo vya elimu ya juu. Wengi wa vijana hawa wamejikuta wakitumia muda mwingi barabarani kusaka ajira bila mafanikio.

Kwa upande mwingine, familia wanazotoka vijana hawa, pia zimejikuta katika mfadhaiko mkubwa baada ya kutumia raslimali zao kuhakikisha watoto wao wanapata elimu na hatimaye ajira, lakini bado wanaendelea kuwa tegemezi baada ya kuhitimu masomo yao.

**Mheshimiwa Spika,**Serikali kwa upande wake inasema kuwa tatizo la ajira linasababishwa, pamoja na mambo mengine, na kasi ndogo ya ukuaji wa nafasi za ajira katika uchumi, na uwezo mdogo wa kuajirika miongoni mwa nguvu kazi inayoingia katika soko la ajira.

**Mheshimiwa Spika,**Wataalamu na wachambuzi wa masuala ya kijamii wanaliangalia tatizo la ukosefu wa ajira nchini kwa upana zaidi, wakilihusisha zaidi na mfumo mbovu wa elimu. Wanasema mfumo uliopo wa elimu hauendani na hali halisi ya kiuchumi iliyopo nje ya mfumo wa shule na vyuo.

**Mheshimiwa Spika,**"Badala ya kufundisha wanataaluma na watu wenye ujuzi maalumu, mkazo umekuwa zaidi kwenye nadharia kuliko mafunzo kwa vitendo. Hata sera zetu za elimu zimelenga zaidi katika kuzalisha wasomi ambao huduma zao haziakisi mwenendo halisi wa kiuchumi katika soko la ajira," anasema mmoja wa wachambuzi hao.

**Mheshimiwa Spika,**Mfumo wa elimu, na hasa mitaala, haihusishi ujuzi na stadi zap kazi mbalimbali za uzalishaji (work/production skills) na hivyo wahitimu wengi kukosa ujuzi na stadi zinazohitajika katika mfumo halisi wa kiuchumi kwenye jamii yao. Kwa kiasi kikubwa mfumo huu huwaelekeza zaidi wasomi kwenye kupata ajira za maofisini na sio kujiajiri wenyewe.

**Mheshimiwa Spika,**Ili kukabiliana na changamoto hii, inashauriwa kuwa nguvu zaidi ielekezwe kutoa mafunzo ya ufundi na stadi nyingine za kazi katika mazingira ambayo vijana wanaishi ili kuwaandaa kujiajiri pale wanapohitimu mafunzo yao. 'Hii itawasaidia kuwapatia kipato lakini pia kutoa ajira kwa wenzao ambao hawajabahatika kupata ujuzi huo, na wakati huo huo kutoa mchango chanya kwa jamii inaowazunguka."

**Mheshimiwa Spika,**Ni vema kurejea maswali aliyowahi kuuliza Waziri wa zamani wa Elimu, Marehemu Jackson Makweta wakati akichambua hali ya elimu nchini katika miaka 50 ya uhuru (1961-2011). Alisema: Je, vijana wetu wanasoma kwa

malengo? Je, elimu itolewayo nchini inakidhi malengo yao? Kama haikidhi kwa nini umma wa nchi hii uendelee kugharamia elimu isiyo na manufaa?"

**Mheshimiwa Spika,**Kambi ya Upinzani inashauri yafuatayo:
Uwepo utaratibu wa kufundisha fani zinazomuwezesha mhitimu kujiajiri kama vile ufundi, ufugaji, uvuvi, na nyingine. Hii itasaidia kupunguza idadi ya vijana wanaokaa mitaani bila ajira na hatimaye kujitumbuzika kwenye vitendo vya uhalifu na ukosefu wa maadili.
**Mheshimiwa Spika**,Wakati umefika sasa kwa serikali kuandaa utaratibu utakaowawezesha vijana wengi zaidi wanaohitimu Kidato cha Nne na Sita kujiunga na vyuo vya Ufundi Stadi (VETA) na hata vyuo vya maendeleo ya jamii (FDC) ambavyo vimetapakaa nchi nzima. Vyuo zaidi vijengwe na kupewa uwezo wa kuzalisha wahitimu bora katika fani mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** Ni lazima idara za elimu kwenye halmashauri ziwezeshwe ili ziweze kutoa ushauri wa kielimu kwa vijana waliopo shuleni ili wachague kozi zinazowafaa badala ya kujiingiza kwenye kozi ambazo zimeshakuwa na wahitimu wengi na wasio na ajira.

**Mheshimiwa Spika**,Serikali pia inapaswa kuweka mkazo zaidi katika kuvisaidia viwanda vinavyochechemea ili kulinda ajira zilizopo. Ni muhimu kuwekeza zaidi katika viwanda hivi na usimamizi mzuri wa raslimali ili kuongeza uzalishaji.

**Mheshimiwa Spika,**Kwa kuwa tatizo la ajira linalochangiwa na maandalizi yasiyo na dira kwa vijana wanapokuwa shuleni na vyuoni, ni lazima wadau mbalimbali, wakiwemo wasomi wa ngazi mbalimbali, mashirika ya kijamii, mashirika yasiyo ya kiserikali na taasisi za ustawi na usalama wa jamii washirikishwe katika mipango ya serikali ya kukabiliana na changamoto hii. Makundi haya pia yashirikishwe katika kufanya tathmini ya utekelezaji wa mipango mbalimbali iliyowahi kupendekezwa siku za nyuma.

## 9. MPANGO WA MATOKEO MAKUBWA WA *'BIG RESULTS NOW'* (BRN)

**Mheshimiwa Spika,**Mpango huu ni sehemu ya jitihada za serikali ya Tanzania kuinua uchumi toka nchi yenye uchumi wa chini mpaka nchi yenye uchumi wa kati. Mpango umeingizwa nchini kwa kurudufiwa toka nchini Malaysia. Malaysia Ambayo wakati inapata uhuru ilikuwa katika kiwango sawa na Tanzania katika maendeleo ya kiuchumi kwa sasa ni nchi iliyoendelea na rekodi ya juu kiuchumi barani Asia. Katika Afrika mpango huu unafuatwa na nchi za Nigeria na Rwanda na umeonyesha mafanikio makubwa.
**Mheshimiwa Spika,**Katika kutekeleza mpango huu, serikali imeanza na wizara sita wizara ya elimu na mafunzo ya ufundi ikiwa ni mojawapo. Ukiangalia malengo na mikakati ya mpango huu ni wazi kuwa umelenga katika njia mpya za ufanyaji kazi katika nia nzima ya kuimarisha utendaji.

**Mheshimiwa Spika,**Akizindua mpango huu jijini Dar es Salaam Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi alisema mpango umebainisha Mikakati tisa (9) muhimu ili kuinua ufaulu kutoka 31% na 43% kwa Elimu ya Msingi na Sekondari hadi 60% kwa mwaka 2013, ufaulu wa 70% kwa mwaka 2014 na hatimaye ufaulu wa 80% au zaidi ifikapo mwaka 2015. Mikakati hiyo tisa ni pamoja na Utoaji mafunzo kwa walimu kuhusu ufundishaji mahiri wa stadi za Kusoma,Kuandika na Kuhesabu, utoaji wa tuzo kwa shule zilizofanya vizuri na kuwa na Kiongozi cha usimamizi wa shule.

**Mheshimiwa Spika,**Malengo na Mikakati yote iliyoanishwa ni mizuri lakini tunadhani mikakati hiyo imekuwepo muda mrefu kilichokosekana ni utekelezaji na ufuatiliaji wake. Hivyo tungependa kufahamu ni mbinu gani mpya ambazo serikali hususani wizara ya elimu na mafunzo ya ufundi inakuja nazo safari hii ili tueweze kupata matokeo makubwa sasa kwa kujiuliza mambo yafuatayo:-

**Mheshimiwa Spika,**Katika uzinduzi wa mpango huu tulishuhudia wakurugenzi wa elimu na maofisa elimu wa mikoa yote ya Tanzania wakila kiapo na kutoa ahadi zao za kuleta matokeo makubwa katika maeneo yao ya kazi kuanzia, mitihani ya darasa la saba na kidato cha nne itakayofanyika baadae mwaka huu. Tunadhani ahadi hizi ni ngumu kuzitekeleza kwa kipindi hiki kifupi. Tunasema hivyo kwa sababu katika hotuba ya Waziri yaliyotekelezwa mpaka sasa tangu mpango huu uanze mapema mwaka jana ni mambo machache mno. Hivyo ni vigumu kuweza kuona mabadiliko makubwa kwa kiasi kilichoahidiwa na viongozi wetu wa elimu.

**Mheshimiwa Spika,**Moja ya hatua za utekelezaji alizozitaja waziri wa elimu ni pamoja na kupeleka mashuleni kopi za mitihani ya taifa ya miaka ya nyuma ili wanafunzi waweze kuzoea maswali ya mitihani na kuongeza ufaulu. Nadhani ingekuwa sahihi zaidi kama wizara ingepeleka kopi za vitabu vinavyokosekana mashuleni pamoja na vifaa vingine vya kufundishia kwani mara nyingi usomaji wa kutumia mitihani unachochea kukariri badala ya kuelewa.

**Mheshimiwa Spika,**Mipango yote hii haiwezi kutekelezwa pasipo kuwepo na jitihada za mwalimu. Kwa kiasi kikubwa matokeo mabaya ya sasa yanachangiwa na walimu waliokata tamaa na hali ngumu ya mazingira ya kazi. Sijui serikali imejipangaje na hilo kwani katika kutekeleza mpango huu yameanishwa majukumu mengi zaidi kwa mwalimu bila kuonyesha ni kwa namna gani mwalimu huyu atamudu kuyatekeleza katika mazingira yale yale yaliyoshindikana hapo awali.

**Mheshimiwa Spika,**Katika mikakati ya matokeo makubwa motisha kwa walimu ni kipaumbele cha mwisho namba 9. Huduma gani bora zimepangwa kwa walimu, kwani mpaka sasa madai ya msingi ya walimu yaliyopelekea mgomo

mkubwa mwaka jana 2012 hayajatekelezwa.Aidha stahili za walimu zimeendelea kuwa ni changamoto kubwa. Mpaka mwezi Disemba 2013 walimu walikuwa wanaidai serikali zaidi ya shilingi bilioni 60 na mpaka sasa deni hili halijalipwa. Katika hali kama hii matokeo makubwa yanapatikana vipi?

**Mheshimiwa Spika,**Ikumbukwe kwamba, unapozungumzia ulipaji wa madeni ya walimu hizi ni stahiki zao za msingi ambazo walipaswa kuwa wamelipwa kwa wakati kama wanavyolipwa wafanyakazi wa wizara nyingine.Wataalamu na wadau wa elimu wameonya mara nyingi kuhusu madhara ya kutomjali mwalimu na matokeo ya sasa yanadhihirisha hilo. Kimsingi, bado hatujaona mipango madhubuti ya kumwezesha mwalimu ili aweze kuleta matokeo makubwa tunayoyatarajia.

**Mheshimiwa Spika,**Hatari inayonyemelea taifa kutokana na Mpango wa Matokeo Makubwa sasa ni ukweli kwamba msisitizo umewekwa katika kuongeza kiwango cha kufualu katika mitihani ya taifa. Motisha wote umelenga hapo. Hatari iliyopo ni kwamba walimu wataanza sasa kufundisha ili wanafunzi wafaulu mitihani na wanafunzi watasoma kwa lengo ka kufaulu mitihani badala ya kujifunza. Tungependa wizara izingatie angalizo hili ili kuona namna ambavyo BRN haitaharibu ari ya wanafunzi kujifunza kwa lengo la kujua mambo badala ya kukariri ili wafaulu mitihani.

**Mheshimiwa Spika,**Tunashauri mikataba ya utendaji kazi katika kila ngazi ya elimu iwekwe wazi ili kwa atakayeshindwa kutekeleza wajibu wake ijulikane atawajibikaje. Katika uzinduzi wa mpango huu tulishuhudia wakurugenzi na maofisa elimu kutoka mikoa yote Tanzania wakitoa ahadi zao kwa kiapo kwa yale watakayoyatekeleza lakini hatukusikia endapo watashindwa kuwajibika kwa yale waliyoahidi, watawajibika vipi. Hivyo kama kweli tunataka kupata mafanikio katika sekta ya elimu kama waliyopata Malaysia hatuna budi kubadilika katika utaratibu wetu wa utendaji kazi. Kama tumeweza kuiga nadharia ya mpango basi na tuige pia utaratibu wao wa ufanyaji kazi ili tupate matokeo mazuri kama wao, tusije kuwa kama Namibia walipoambiwa na rais wao kuwa anataka kufikia 2020 wawe kama wenzao wa Ulaya na baada ya mwezi mmoja wasichana wakawa mitaani wamevalia kama wenzao wa Ulaya(nguo fupi) na walipoulizwa wakasema tunaanza kuwa kama wenzetu wa Ulaya.

## 10. UBADHIRIFU WA FEDHA ZA UMMA KATIKA SEKTA YA ELIMU UNAVYODIDIMIZA ELIMU YA TANZANIA.

**Mheshimiwa Spika,**Kwa muda mrefu sasa maendeleo ya elimu katika Taifa letu yamekuwa yakirudishwa nyuma na kuathiriwa sana na uwekezaji kidogo na ufinyu wa bajeti unaotokana na upotevu wa fedha za elimu kwa njia ya ubadhirifu. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa

mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2013, inaonyesha kwamba; kuna mingi ya matumizi mabaya au usimamizi mbaya wa rasilimali ambao unachangia sekta ya elimu kuendelea kupokea kiwango kidogo cha fedha na hivi kuendelea kufanya vibaya kila mwaka.

**Mheshimiwa Spika,**Wakati wa ukaguzi wa fedha za ruzuku za shuleni, ilibainika kuwa jumla ya **shilingi bilioni 1.36** zilipokelewa na Mamlaka za serikali za Mitaa lakini fedha hizo bado hazijapelekwa shuleni kwa ajili ya utekelezaji hivyo kuchelewesha utoaji wa huduma zilizokusudiwa. Pia jumla **shilingi milioni 499** za ruzuku zilitumika kwa matumizi yasiyohusiana na matumizi ya fedha za ruzuku ya shule kama vile kulipa posho. Taswira hii ni mbaya katika kuboresha elimu na swali la kujiuliza ni hatua gani zimechukuliwa?

**Mheshimiwa Spika,**Ripoti ya CAG ilionyesha pia kwamba; katika Halmashauri kumi na tatu (13), jumla ya **shilingi bilioni 1.14** zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza shuguli katika MMEM hazikutumika hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha 2012/2013. Kama vile haitoshi, **shilingi bilioni 21.87** zilitolewa kwa Mamlaka za serikali za Mitaa sitini (60) kwa ajili ya utekelezaji wa maendeleo ya elimu ya sekondari (MMES) kwa malengo ya kuongeza ubora wa elimu na kupanua wigo wa wanafunzi kupenda kuendelea na masomo ya sekondari, **ni shilingi bilioni 11.21** tu kati ya hizo (sawa na 51%) ndizo ilizotumika. Kwa hiyo kiasi cha Sh. Billion 10.7 (sawa na 49%) ya fedha zote zilizopokelewa hazikutumika hadi mwisho wa mwaka 30 Juni, 2013. Tafsiri ya fedha kutotumika ni kuwa zinapaswa kurejeshwa hazina na kuwa kuwa shughuli zilizokusudiwa kufanywa na fedha hizo hazikufanyika. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa maelezo kama fedha hizo ambazo hazikutumika kwa malengo yaliyokusudiwa zilirudishwa hazina au la.

**Mheshimiwa Spika,**Kwa mujibu wa Ripoti ya CAG, jumla ya **shilingi bilioni 2.6** zilizotengwa kwa ajili ya shughuli za Mfuko wa kuchochea Maendeleo ya Jimbo hazikutumika katika sampuli ya Mamlaka za serikali za Mitaa sitini na sita (66). Hizi ni fedha zilizokusudiwa kuleta maendeleo katika majimbo ikiwamo elimu. Kama fedha hizi zingetumika katika sekta ya elimu zingeweza kutengeneza zaidi ya madawati 17,333 kwa bei ya shilingi 150,000 kwa kila dawati, na kusaidia zaidi ya wanafunzi 34,666 kukaa juu ya madawati badala ya chini kama kila dawati litakaliwa na wanafunzi wawili.

**Mheshimiwa Spika,**Serikali imeendelea kutoa misamaha mikubwa ya kodi kwa sekta mbalimbali, fedha hizo ni fedha ambazo serikali ingeweza kuzikusanya na kuzitumia katika shughuli za maendeleo. Mfano ripoti ya CAG imebainisha kuwa hadi kufikia 30 Juni 2013, misamaha ya kodi iliyoidhinishwa ilifikia kiasi cha **shilingi trilioni 1.52.** Hizi fedha ni nyingi na zilikuwa na uwezo wa kujenga shule 300 zenye miundombinu iliyotimia kama maabara, maktaba na vifaa vya kujifunza na kufundishia kwa gharama za **shilingi billion 5** kila shule. Kwa hiyo wakati serikali inalia kushindwa kuhudumia wananchi wake kwa kuwapa elimu bora kwa

kisingizio cha umasikini, bado inapoteza fedha nyingi bure kwa kisingizio cha misamaha wa kodi.

***Mheshimiwa Spika**,*Kimsingi pamoja na mianya hii katika usimamizi wa fedha za umma, ripoti ya CAG inathibitisha ukweli wa hali ulivyo katika elimu yetu. Mfano, mapitio ya utendaji wa elimu katika shule za Msingi na Sekondari yamebaini kuwa, Mamlaka za Serikali za Mitaa hazikuwa na miundombinu ya shule ya kutosha katika shule za msingi na sekondari. Ukaguzi pia umebaini kuwa, shule za msingi na sekondari, zina upungufu wa walimu ambao huathiri sana ubora wa elimu. Tatizo hili limepelekea nchi kushindwa kufikia lengo la kitaifa la uwiano wa 1:45 (Wanafunzi 45 kwa mwalimu mmoja).

**Mheshimiwa Spika,**Mwelekeo unaonesha kwamba walimu wengi hawaripoti katika vituo vyao vya kazi hasa vijijini kutokana na miundombinu duni iliyopo vijijini. Sasa ukikusanya fedha hiyo ambayo haikutumika pamoja na misamaha kama ilivyoainishwa hapo juu, utaona serikali inaruhusu zaidi ya **shilingi trilioni 1.54** kupotea bila kufanyiwa kazi. Kama kiwango hiki cha fedha kingetumika kujenga nyumba za walimu peke yake kwa gharama ya shilingi milioni 50 kila nyumba, serikali ingejenga zaidi ya nyumba 30,756. Kiwango hiki kingepunguza au kuondoa kabisa tatizo la makazi ya walimu hasa maeneo ya vijijini.

**Mheshimiwa Spika,**Kupanga ni kuchagua, na nilazima serikali iachane na tabia ya kufanya kila kitu kila wakati. Tunatambua kuwepo kwa mpango wa matokeo makubwa sasa BRN, serikali ijikite kwenye kusimamia rasilimali hizi zinazopotea badala ya kukimbilia kutoa visingizio vya umasikini na uhaba wa bajeti. Kwa msingi huu, hatutegemei serikali kuja na visingizio vya namna hii katika bajeti ya mwaka huu wa fedha 2014/15. Sekta ya elimu ipangiwe kiwango cha kutosha kushughulikia changamoto zilizopo ili kuboresha elimu nchini.

## 11. AJIRA ZA WALIMU ZISIZOZINGATIA UWIANO WA MAHITAJI KIMKOA

**Mheshimiwa Spika,**Uhaba wa walimu ni moja ya sababu zinazochangia wanafunzi kushindwa kujifunza vizuri na kuelewa mada za masomo mbalimbali kwa muda muafaka hapa nchini. Katika kukabiliana na changamoto hii, serikali imekuwa ikiajiri walimu kila mwaka na katika mwaka wa fedha 2013/2014 serikali imeajiri jumla ya **walimu 17,928** na kuwasambaza katika katika shule mbalimbali za msingi.

**Mheshimiwa Spika,**Tunaipongeza serikali kwa jitihada hizi kwani baada ya kuajiri walimu wapya 17,928 mwaka 2014 kwa shule za msingi, tatizo la uhaba wa walimu limepungua. Kitaifa hivi sasa uwiano wa mwalimu kwa mwanafunzi kwa shule za msingi za serikali umepungua toka 1:44 ulivyokuwa mwaka 2013 hadi kufikia 1:40 kwa mwaka 2014. Hata hivyo pamoja na jitihada hizi, bado ugawaji

wa walimu hauna uwiano kwani bado mikoa mingi hususan ya kanda ya Ziwa bado ina upungufu  kama; (Mwanza, Shinyanga, Geita, Simiyu, Mara na Kagera) na mikoa ya kanda ya magharibu (Rukwa, Kigoma na Tabora) bado ina uwiano mkubwa zaidi ya 1:40. Hakuna hata mkoa mmoja kutoka kanda hizi ambao umefikia lengo la kitaifa tofauti na mikoa ya kanda ya mashariki (Pwani, Dar es salaam na Morogoro) na kaskazini (Kilimanjaro, Tanga na Arusha) ambayo yote imevuka lengo la kitaifa la uwiano wa 1:40.

**Mheshimiwa Spika,**Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kuwa, Serikali Igawe Walimu kwa Kuzingatia Mahitaji. Mikoa ya Kanda ya Ziwa na Kanda ya Magharibi bado ina uhaba wa walimu. Upangaji wa walimu kimikoa, kiwilaya, na kishule lazima uzingatie mahitaji ya walimu kwenye eneo fulani ili kuwe na tija ya ajira hizo katika kuboresha mazingira ya ufundishaji darasani.

## 12. ELIMU YA JUU

**Mheshimiwa Spika,**Kambi Rasmi ya Upinzani inaunga mkono maendeleo yanayofanyika katika kuboresha elimu ya juu nchini. Takwimu zinaonyesha kwamba katika kipindi cha chini ya mika kumi, tangu 2006, vyuo vya elimu  ya juu vimeongezeka kutoka vyuo 30 mwaka 2006 hadi vyuo 50 kufikia mwaka 2013, na idadi ya wanafunzi waliodahiliwa imefikia 135,367. Hata hivyo bado udahili ni mdogo sana ukilinganisha na nchi zingine katika bara la Afrika. Takwimu zinaonyesha kwamba Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye udahili wa chini kabisa katika vyuo vikuu. Kwa mujibu wa taarifa ya SARUA (Southern African Regional Universities Association), ushiriki wa Tanzania katika elimu ya juu (yaani wastani wa watu wenye elimu ya juu) ni asilimia mbili (2%) tu tukiwa mbele ya nchi mbili tu za Malawi (1%) na Msumbiji (1%).

**Mheshimiwa Spika,**Ubora wa elimu ya Juu Tanzania unatia shaka kubwa. Kwa mfano, utafiti uliofanywa na Baraza la Ushirikiano wa Vyuo Vikuu Afrika Mashariki (Inter - University Council for East Africa - IUCEA) kwa kushirikiana na Baraza la Biashara la Afrika Masharika (East African Business Council), na kuripotiwa katika Gazeti la The East African la Mei 10-16, 2014, unaonyesha kuwa ni asilimia 39 tu ya wahitimu wa vyuo vikuu Tanzania ndio wenye maarifa na stadi zinazoweza kuwafanya waajirike.

**Mheshimiwa Spika,**Kwa mujibu wa takwimu za SARUA, Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizopo kusini na mashariki mwa Afrika ambazo zinachangia kidogo sana katika kuzalisha maarifa kupitia machapisho katika majarida ya kitaaluma na kisayansi (‘*Peer Reviewed Journals*’). Kwa mfano, kwa mfano kwa mwaka 2010, watafiti wa Tanzania walichapisha makala (articles) 120 pekee ukilinganisha na makala 347 kwa Botswana, nchi ambayo ina vyuo vikuu visivyozidi vitano na idadi ya watu wasiozidi milioni mbili.

**Mheshimiwa Spika,**Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa wito kwa Serikali kuwekeza katika ubora wa elimu ya juu. Pamoja na bodi ya mikopo kujitahidi kulipa fedha kwa wanafunzi bado kuna ucheleweshaji na kusababisha usumbufu mkubwa sana kwa wanafunzi na uongozi wa vyuo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulipa posho za wanafunzi kwa wakati ili kuondosha migomo, maandamano na uvunjifu wa amani ambavyo vinaathiri ubora wa elimu katika vyuo vya elimu ya juu hapa nchini. Aidha Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali kuongeza fedha kwa ajili ya kuwasomesha wahadhiri wa vyuo vikuu katika shahada ya uzamivu (PhD) kwa kuwa kumekuwa na kilio cha siku nyingi kwa wahadhiri wetu kutoendelezwa katika ngazi ya uzamivu. Sababu zinazotolewa ni gharama kubwa kulipia masomo ya uzamivu. Hali hii imefanya wahadhiri wengi kubaki na shahada za uzamili kwa muda mrefu na hata kustaafu katika ngazi hiyo. Hivyo ubora wa elimu katika vyuo vya elimu ya juu unaathirika kwa kuwa unakuta wanafunzi wa shahada ya uzamili (Masters Degree) wanafundishwa na mhadhiri mwenye shahada ya uzamili badala ya mhadhiri mwenye PhD.

## 12.1. HALI KATIKA VYUO VIKUU HAPA NCHINI

### *i. Chuo Kikuu cha Dar es salaam*

**Mheshimiwa spika,** hakuna shaka kuwa Chuo kikuu cha Dar es salaam ni chuo kikongwe zaidi hapa nchini, chuo hiki pamoja na sifa kiliyojijingea ndani na nje ya nchi, kinaendelea kukumbwa na matatizo lukuki, ikiwa ni pamoja na miundombinu mibovu ya majengo, ubovu wa vyoo na mabafu katika mabweni. Pamoja na matatizo haya bado chuo hiki hakijafanyiwa ukarabati kwa kipindi kirefu na hivyo kuhatarisha usalama wa wanafunzi

**Mheshimiwa spika,** Kambi rasmi ya upinzani bungeni inaamini kuwa ubora wa elimu unatokana pia na kuwepo kwa mazingira rafiki ya kujifunza na kufundishia, Hivyo tunaitaka serikali kutoa kauli ni lini haswa miundombinu hii itafanyiwa ukarabati? Aidha, Wizara itoe maelezo juu ya hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa ahadi aliyoitoa Rais Jakaya Kikwete alipifika kwenye maadhimisho ya Chuo Kikuu ya Serikali kutenga fedha za kutosha katika bajeti ya kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Wanafunzi (Student Center) katika Kampasi ya Mlimani; Je, ni kiwango gani cha fedha kimetumika katika mwaka wa fedha 2013/2014 na kiasi gani kimetengwa kwa mwaka wa fedha 2014/2015?

**Mheshimiwa Spika,** Ikumbukwe kuwa mwanzo mwa mwaka 2012, chuo kikuu cha Dar es salaam kiliwafukuza wanafunzi 50, hadi sasa baada ya miaka miwili kuna wanachuo 15 hawajarejeshwa chuoni, hii ndiyo kusema kwa mjibu wa sheria za chuo, wanafunzi hawa wanapaswa kuanza mwaka wa kwanza wa masomo, kambi rasmi ya upinzani bungeni inalaani kitendo hicho cha ukatili wa

kuwanyima watoto wa watanzania masikini haki yao ya kupata elimu kwa visingizio mbalimbali. Kambi rasmi ya upinzani Bungeni inataka kujua sababu zilizosabsha serikali hii ya CCM kuwadhulumu haki yao watoto hawa wa watanzania masikini. Vile vile tunaitaka serikali kuwarudisha chuoni vijana hawa bila masharti na kama wamegundua makosa yao basi waelezwe na wale waliorudishwa wapewe stahilli zao.

**Mheshimiwa spika,** Chuo kikuu cha Dar es salaam kwa ukongwe wake kinapaswa kuendelea kupewa hadhi yake, miongoni mwa mambo ambayo yalikiletea heshima chuo hicho, ni pamoja na shughuli na mijadala mbalimbali za kitaaluma ambayo siyo tu ilielimisha jamii lakini pia ilisaidia kutoa mwelekeo wa Taifa letu.

### ii. Chuo Cha Mtakatifu Joseph - Songea

**Mheshimiwa Spika;**Kambi rasmi ya upinzani bungeni ilipokea taarifa za mgogoro wa chuo Kikuu cha Mt. Joseph tawi la Songea, mgogoro uliopelekea kufungwa kwa chuo kwa muda. Mgogoro huu ulielezewa kuwa ni kushindwa kwa uongozi wa chuo kusimamia mfumo wa uendeshaji na usimamizi wa vyuo vikuu jambo ambalo limekuwa ni chanzo cha matatizo mbali mbali pale chuoni. Kambi yetu imefahamishwa kuwa uongozi wa serikali ya wanafunzi uliandika barua kwa Mh. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya ufundi mnamo tarehe 23 desemba 2013 juu ya matatizo ya chuo na nakala kutolewa kwa Mkuu wa Mkoa Ruvuma na Mkuu wa Wilaya Songea.

**Mheshimiwa Spika;**Taarifa zilizoifikia ofisi ya kambi rasmi ya upinzani ni kuwa mnamo tarehe 7 februari mwaka huu Naibu waziri wa Elimu, Mh. Jenister Mhagama alikutana na viongozi wa serikali ya wanafunzi na baadhi ya wanafunzi wa chuo cha St. Joseph, Songea ili kusikiliza matatizo yao. Mh. Naibu waziri alikiri kupelekewa tayari baadhi ya malalamiko ya wanafunzi na kuwa tayari alikwisha agiza vyombo husika kama TCU kutatua matatizo yale na tayari kamati imeshatumwa kushughulika na swala hilo.

**Mheshimiwa Spika.**Kambi rasmi ya upinzani imepokea taarifa kuwa kinyume kabisa na mambo aliyoyasema Mh. Naibu waziri mengi hayakufanyiwa kazi na wanafunzi wanaendelea kuteseka. Aidha chanzo cha mgogoro ilikuwa kunyang'anywa nyadhifa na kusimamishwa masomo kwa viongozi wa serikali ya wanafunzi (Rais na Waziri mkuu wa serikali ya wanafunzi) baada ya kuonekana wakitetea maslahi ya wanafunzi. Wanafunzi hao wamerudishwa katika masomo lakini nyadhifa zao hazitambuliwi na utawala wa chuo na hivyo wanafunzi kutokuwa na uwakilishi wawapo chuoni. Je utawala wa chuo unapata wapi mamlaka ya kutengua uongozi wa wanafunzi uliochaguliwa kidemokrasia na kuvunja katiba ya serikali ya wanafunzi na kutotii maelekezo ya

TCU ya kuwa na serikali ya wanafunzi isiyoingiliwa katika majukumu yake na utawala?

**Mheshimiwa Spika;**Katika chuo hiki imedaiwa kuwa wanafunzi wanapofiwa au wanapopata ujauzito (kwa wanawake) au matatizo mengine yanayowalazimu kushindwa kufanya mtihani wanachukuliwa kama waliofeli somo husika na hivyo kutakiwa ku rudia muhula unaofuata badala ya kupewa mtihani maalumu(special paper) kama ilivyo utaratibu wa vyuo vikuu nchini.

**Mheshimiwa Spika;**Kuna haja ya kuangalia mfumo huu wa uendeshaji wa chuo hiki ili kuhakikisha watanzania wanapata elimu yenye tija kwa taifa badala ya baadhi ya watu kuleta propaganda katika mambo ya msingi kabisa kama hili la Elimu na kuishia kulalamikia ufaulu wa wanafunzi kumbe hata walimu wanaoandaliwa katika baadhi ya vyuo kama hiki ni mbovu.

Kambi rasmi ya upinzani inatarajia majibu na utekelezaji makini wa matatizo yote yanayokikumba chuo cha Mt. Joseph, Songea ambayo kati ya hayo yapo mengi ambayo yanatendeka katika matawi yote ya Chuo kikuu cha Mt. Joseph, Tanzania.

### iii. Chuo cha Madini Dodoma (Mineral Resources Institute).

**Mheshimiwa Spika;** Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi pamoja na kuvisimamia moja kwa moja Vyuo na Vyuo Vikuu vilivyopo chini ya Wizara tajwa moja kwa moja inao wajibu pia wa kuhakikisha Vyuo na Vyuo Vikuu vilivyo chini ya Taasisi zingine za umma na za binafsi vinaendeshwa kwa viwango vinavyohitajika.

**Mheshimiwa Spika,**Chuo cha Madini(Mineral Resources Institute) ni miongoni mwa idara zilizo chini ya Wizara ya Nishati na Madini ambayo haina mamlaka kamili inayojitegemea kimuundo. Chuo hiki kilichoanzishwa miaka ya 1978 kina matatizo mbalimbali kama ifuatavyo ambayo Wizara ina wajibu wa kutoa majibu wakati wa majumuisho na kuchukua hatua za za haraka.

**Mheshimiwa Spika;** Kukosekana kwa muundo katikia Chuo cha Madini tangu kuanzishwa kwake kama taasisi ya kitaaluma (Chuo cha ufundi) kunasababisha matatizo makubwa kiutendaji na kitaaluma (mfano kufeli kwa wingi kwa wanafunzi 55 mwaka 2012/2013, 67 mwaka 2013/2014 muhula wa kwanza) kwani kila mkuu wa chuo anapoingia anajiundia idara na kuchagua watendaji wa kukaimu.

Kambi ya Upinzani inaomba serikali kupitia wizara hii mkufuatilia kwa kina matatizo yaliyopo chuoni hapo haraka ili kunusuru vijana wetu.

## 13. UCHAMBUZI MFUPI WA BAJETI YA WIZARA YA ELIMU 2014/15

**Mheshimiwa Spika,**Ni wazi kuwa bajeti ya wizara ya elimu imeongezeka kutoka **shilingi bilioni 689.7** mwaka 2013/14 hadi **bilioni 799** mwaka huu 2014/15. Na bajeti ya matumizi maendeleo inaonekana kuongezeka kutoka **shilingi bilioni 72** mwaka 2013/14 hadi **shilingi bilioni 454** mwaka 2014/15 huku bajeti ya matumizi ya kawaida ikionekana kushuka kutoka **shilingi bilioni 612** mwaka jana hadi **shilingi bilioni 344** mwaka huu 2014/15. Ki-mtazamo sura ya bajeti hii ina uwiano mzuri kwa maana ya ongezeko la bajeti na mgawanyo wa matumizi ya maendeleo na yale ya kawaida. (bajeti ya maendeleo ni 57% na kawaida ni 43% ya bajeti ya wizara. Lakini kimsingi ongezeko hilo limetokana mabadiliko katika upangaji wa baadhi ya vifungu ambavyo hapo awali vilipangwa katika bajeti ya kawaida kwa mfano fedha za bodi ya mikopo zimeondolewa kwenye bajeti ya matumizi ya kawaida **Sub vote 7001 (Higher education - 270900)** na kuhamishiwa katika bajeti ya maendeleo **sub vote 1003 (Policy and Planning)**

**Mheshimiwa Spika,**Uchambuzi unaonesha kuwa bado hakuna uwekezaji wa kutosha katika miradi ya maendeleo kwakuwa sehemu kubwa ya bajeti yake inakwenda kugharamia mikopo ya elimu ya juu. Shilingi bilioni 307 kati ya bilioni 454 ya bajeti ya maendeleo ya wizara zinaenda kwenye kulipia mikopo ya elimu ya juu, hii ni sawa na asilimia 68% ya bajeti nzima ya maendeleo 2014/15. Hivyo tunaweza kusema fedha iliyopangwa kwa shughuli ya maendeleo mwaka 2014/15 ni kidogo kuliko iliyotengwa mwaka 2013/14 wakati changamoto bado ni nyingi.

**Mheshimiwa Spika,**Katika bajeti ya maendeleo ya wizara tunaona shilingi bilioni 15 zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo elimu ya msingi na bilioni 12 kwa ajili ya maendeleo ya sekondari. Hatahivyo tunajua kuwa utaratibu wa kusimamia utekelezaji wa miradi hii upo chini ya ofisi ya waziri mkuu TAMISEMI na wizara inabaki kama mtungaji na msimamiaji sera. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji, ni kwa nini kiwango hiki kinatengwa chini ya wizara wakati msimamizi na mtekelezaji wa shughuli za maendeleo zinasimamiwa na TAMISEMI?

## 13. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,**Kama nilivyoeleza hapo awali, elimu ya Tanzania hasa kwa shule za msingi na sekondari imeshuka kwa kasi ya ajabu katika mihula yote miwili ya utawala wa Serikali ya awamu ya nne. Hali hii inadhihirisha kwamba Serikali ya CCM imeshindwa hata kutekeleza ilani yake ya uchaguzi kuhusu elimu bora kwa watanzania. Aidha, tumeona kwamba tatizo kubwa la kuporomoka kwa sekta ya elimu hapa nchini kunatokana na udhaifu wa ki-uongozi zaidi kuliko sababu nyingine zinazotajwa na Serikali. Uongozi dhaifu umepelekea misamaha ya kodi na hivyo kupoteza fedha nyingi ambazo

zingeweza kuboresha elimu yetu. Mapungufu katika uongozi yamesababisha usimamizi dhaifu katika sekta hii kiasi cha kusababisha ubadhirifu wa fedha za elimu, ufanyaji wa maamuzi katika masuala ya msingi ya elimu bila kuzingatia mapendekezo ya tume mbalimbali ambazo ziliundwa kuchunguza mapungufu mbalimbali katika sekta ya elimu.

**Mheshimiwa Spika,**Kama Karl Marx alivyosema, '**Force is the midwife of every old society pregnant with a new one"** ikiwa na maana kwamba matumizi ya nguvu ni lazima kwa mama aliyefikia siku za kujifungua na kwamba bila kumpasua wote wawili mama na mtoto watakufa, ila ukimpasua wote au mmoja anaweza kupona, vivyo hivyo na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasema bila kufanya mageuzi makubwa katika mfumo wetu wa utawala kuna hatari kubwa ya Taifa kuangamia kwa kuwa na wananchi wasio na elimu bora ya kuwawezesha kukabiliana na mazingira yao ili kumudu maisha yao.

**Mheshimiwa Spika,** Kama tulivyopendekeza mwaka jana, tunarudia kupendekeza tena kwamba Serikali ianzishe chombo cha udhibiti wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi (Tanzania Education and Training Regulatory Authority - TETRA) kitakachoweka viwango vya ubora wa elimu kwa mujibu wa mitaala iliyopitishwa na Serikali, kudhibiti utungaji, usahihishaji na upangaji wa matokeo ya mitihani, kudhibiti gharama za elimu (ada na michango mingine) baina ya shule na taasisi nyingine za elimu za uma na binafsi ili kuwa na mfumo mmoja wa elimu unaoeleweka kuliko sasa ambapo kuna tofauti kubwa za kimfumo baina ya shule na taasisi za elimu binafsi na zile za umma.

**Mheshimiwa Spika,**Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kulitaarifu Bunge hili na wananchi kwa jumla kwamba kudorora kwa elimu nchini kunatokana na Serikali kuwa na viongozi wababaishaji , wasemaji wa maneno mengi, wasiotekeleza wanyosema na kukosa ufuatailiaji. Hivyo, Wizara hii inahitaji kufanyiwa mabadiliko makubwa vinginevyo Tanzania itaendelea kudidimia kielemu na hivyo kiuchumi pia.

**Mheshimiwa Spika,**Baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha.

Susan Anselm Jerome Lyimo (Mb)
**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI NA WAZIRI KIVULI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**
17 Mei, 2014

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Susan Lyimo kwa maoni yako kwa niaba ya Kambi ya Upinzani Bungeni. Tunawashukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa kama mnavyoona, Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Kawambwa na Naibu wake Mheshimiwa Jenista Mhagama wako tayari kupokea maoni yetu kwa wale watakaopata nafasi ya uchangiaji. Maombi niliyonayo ni mengi sana, kwa hiyo, sishauri mtu yeyote kuniandikia kuomba nafasi kwa vile nafasi imejaa.

Sasa tunaendelea na wachangiaji kama nilivyosema, na mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes. Lakini kabla hajasimama, palikuwa na Waratibu saba wa kutoka Jimboni kwa Mheshimiwa Blandes hawakusimama wakati ule, pale mlipo hebu simameni Waratibu wa Elimu Kata saba wale, karibuni sana Bungeni, naomba kutambua uwepo wenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Blandes karibu sana, lakini kumbuka na Mwalimu wako Mary Alfred anakusikiliza. Endelea Mheshimiwa, una dakika saba! *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. GOSBERT BEGUMISA BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mungu kwa kumleta Mwalimu wangu, Mwalimu Mary Alfred katika Bunge hili. Mwalimu usiwe na wasiwasi, kazi naichapa hapa na Karagwe wananiamini sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuchangia kidogo. Kuna mawazo kwamba viwango vya ufaulu vimeshuka. Inawezekana Msemaji wa Kambi ya Upinzani hajapitia mwongozo wa matumizi ya viwango vya ufaulu na utaratibu wa kutunuku matokeo ya Kidato cha Nne na Kidato cha Sita. Napenda baadaye nimpe nakala hii ili apitie aone viwango vya ufaulu kwamba ni vizuri na havijabadilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie matokeo ya ufaulu ya mwaka 2013 katika Wilaya ya Karagwe. Katika Shule za Msingi Wilaya ya Karagwe ilipata nafasi ya 73 kati ya nafasi 151. Ni ufaulu mzuri na wa hali ya juu sana, nawapongeza sana Walimu. *(Makofi)*

Upande wa Sekondari, Wilaya ya Karagwe ilikuwa ya 51 kati ya Wilaya 152. Ni kazi nzuri sana ambayo imefanywa na Watendaji, wazazi pamoja na Mbunge wao. Naomba tuongeze bidii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumza kwa mara nyingi sana na Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Ufundi, Mheshimiwa Kawambwa, nimekuwa nikimuuliza, ni kwa nini Mkoa wa Kagera haujapatiwa chuo cha *VETA*?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikoa yote Tanzania ukiondoa Kagera peke yake ndiyo ambayo haina Chuo cha *VETA* pamoja na hii Mikoa mipya ambayo

imeanzishwa juzi. Namtaka Mheshimiwa Waziri anaposimama hapa anionyeshe kwenye bajeti yake fedha kwa ajili ya ujenzi wa *VETA* Mkoa wa Kagera na vinginevyo nitawaomba Waheshimiwa Wabunge tusipitishe bajeti hii kwa sababu ni bajeti ya ubaguzi inayobagua Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilikuwa kwenye ziara Jimboni kwangu, nimekutana na Walimu wapya ambao wameajiriwa juzi. Kuna kilio Walimu wapya bado hawajalipwa mishahara yao. Nataka nijue ni kwa nini Walimu wapya hawajalipwa mishahara na mnawaweka katika mazingira magumu?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kwamba mishahara ya Walimu imekuwa ikisuasua sana ukilinganisha na Idara nyingine kwa mfano Mifugo na Afya, utakuta kuna tofauti kubwa sana. Mwalimu anapoanza na mtu wa Afya au Mifugo, tofauti ya mishahara unakuta siyo chini ya Sh.140,000/=. Kwa maana hiyo mishahara inapopanda, Walimu wanazidi kuwa chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kuna *Income Tax* imekuwa ni kubwa. Walimu wanalipa *Income Tax* kubwa kiasi kwamba wanaondoka nyumbani na fedha kidogo sana. Naomba Serikali ituambie ni kwa nini kuna tofauti ya mishahara hii kati ya Walimu na kada nyingine wakati wote wamemaliza *form four* au *form six* pamoja, wamekwenda kozi ya miaka miwili kwa pamoja lakini Walimu wanaendelea kudidimizwa na kuwa chini?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumezungumza sana hapa ndani ya Bunge, kuna posho za Walimu waliopanda madaraja; Mwalimu anapopanda madaraja anapanda na posho zake au stahili zake. Lakini kwa masikitiko makubwa, Walimu mpaka sasa hivi unakuta wamepanda miaka miwili au mitatu hawajalipwa posho na stahili zao, ni kwa nini? Mheshimiwa Waziri utueleze na tunataka fedha hizi Walimu wapewe, kwani ni haki yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kwamba kuna posho ya madaraka au *responsibility allowance* na hasa kwa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi na Sekondari na hizi wanastahili kupewa kwa sababu ni haki yao na iweze kuwatia motisha na wenyewe Walimu Wakuu wanalia hawajapata fedha hizi. Tunataka tuzione kwenye bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilituahidi kwamba itakuwa inawapa Walimu posho ya mazingira magumu, lakini mpaka leo hii hatuoni kitu ambacho kimefanyika. Sambamba na hilo Walimu wana kilio cha nyumba za Walimu, hawana mahali pa kuishi. Utakuta Walimu wanne au watano au sita wanakaa kwenye kajumba kamoja. Tunataka tujue, tatizo hili litatatuliwa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna madai sugu ya Walimu, tumepiga kelele hapa ndani ya Bunge, Serikali imeahidi kwamba mtakuwa mmelipa madai ya

Walimu kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha. Lakini ninavyozungumza leo hapa, hata Waratibu Elimu Kata ambao wako hapo juu wametoka Karagwe wanajua Walimu wao wana madeni mengi sana. Kwa nini mnaendelea kuwakopa Walimu wetu? Wapeni fedha zao za madai na ikiwezekana muwape na riba *(interest)* kwa sababu mmechelewesha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu wetu wamekuwa wakiwa kazini lakini hawajapatiwa mafunzo kazini. Wakati mwingine tunawalaumu kwamba ufaulu wao wanafundisha chini ya viwango. Walimu hawa wanahitaji kupewa mafunzo kazini ili waende na wakati. Kwa mfano, kuna Walimu wa zamani, ukimwambia afundishe somo la *TEHAMA* hawezi. Kwa hiyo, ni vizuri mkawapa mafunzo Walimu ili na wenyewe waweze kufundisha vizuri watoto wetu.

Pia kuna Walimu waliojiendeleza. Hawa Walimu wanaojiendeleza wapandishwe madaraja mara moja wasisubiri kupandishwa vyeo kwa mkupuo na wengine. Mwalimu akitoka Chuo amejindeleza, hapo hapo apandishwe na apewe stahili zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo sugu la mabweni hasa kwa upande wa wasichana; wasichana wetu na wanafunzi wetu wanapata mimba na kudhalilishwa kwa sababu ya kutembea umbali mrefu kutoka majumbani kwenda mashuleni. Tunataka Serikali ituambie ni lini itamaliza tatizo hili la mabweni ya wasichana na ikiwezekana na ya wavulana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ni kwamba watoto wetu wanakwenda shuleni kuanzia saa 12.00 asubuhi na wanatoka shuleni kwenye saa 9.00 au saa 10.00 au saa 11.00, hawa watoto wanashinda na njaa; Serikali ina mpango gani wa kuwapatia chakula? Mtu akiwa na njaa hawezi akasoma akaelewa. Nataka hayo kwanza Mheshimiwa Waziri anapokuja ku-*wind up* ahakikishe kwamba anayaweka vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la Baraza la Mitihani kushusha ufaulu; mimi nimepitia mwongozo huu ambao nimeonyesha hapa. Nimejiridhisha kwamba kiwango cha chini cha ufaulu mpaka sasa hivi ni alama ya 'D' wala haijabadilika. Tangu zamani ilikuwa ni hivyo! Kwa hiyo, mtu mwenye mawazo kwamba ufaulu umeshuka, siyo kweli. Bila 'D' ni kwamba huyo mwanafunzi akiwa chini ya 'D" anakuwa hajafaulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia, kuna kigezo cha mtahiniwa kufaulu. Mtahiniwa kwa mujibu wa mwongozo huu ni lazima awe na *credit* ya *'D'* au awe na *'D'* moja na ikiwezekana awe na 'D' mbili angalau na *credit* nyingine moja. Tangu zamani ndivyo ilivyokuwa, nashangaa mtu anaposema kwamba vigezo zimeshwa. Inawezakana hajasoma vizuri, hajafanya *research*, ningeomba wenzetu wakafanye *research* vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru, nasema nitaunga mkono hotuba hii nitakapoona fedha za *VETA* Kagera zimewekwa hapo. Vinginevyo sitaunga mkono. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Gosbert Blandes. Mchangiaji wetu wa pili atakuwa Mheshimiwa James Mbatia, Mheshimiwa Peter Serukamba ajiandae. Mheshimiwa Mbatia, dakika saba.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza na Matokeo Makubwa Sasa. Yako malengo tisa ya Matokeo Makubwa Sasa kwenye Wizara ya Elimu. Lakini zoezi hili wakati linafanyika kwenye Matokeo Makubwa Sasa mwaka 2013 walitoa mtihani kwa ajili ya Matokeo Makubwa Sasa, mtihani wa Shule ya Msingi uliofanyika tarehe 9 Julai, kuona hayo Matokeo Makubwa Sasa yanafanyaje kazi.

Katika mtihani wa Kiingereza, hata jina la Wizara ni shida. Umeandikwa *Ministry of Education and Vocation Training Improvement, Test Examination*. Ukisoma humu ndani, anakwambia "*In 1964 the Tanganyika and Zanzibar united to from…" Not to form, "to from." (Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitai-*table* Mezani. Yapo matatizo mengi sana. Ukija mtihani wa Kiswahili unasema, "Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi; jina la Wizara halijulikani. Halafu wanasema "mkakati wa kuboresha taaluma, matokeo makubwa sana." Halafu wanaandika mtihani wa kujipima Darasa la Saba; saba ya maandishi na saba ya kirumi, Saba VII. Ukienda humu ndani kwenye Kiswahili chenyewe ndiyo kasheshe tupu.

Mheshimiwa Naibu Spika, njoo kwenye mtihani wa Hisabati, nami napenda sana Hisabati. Nilipeleka huu mtihani kwa Profesa wa Chuo Kikuu ch Dar es Salaam, Mtihani wa Darasa la Saba, Profesa ameniandikia hapa kwamba, "nimetumia muda wa saa mbili na dakika tatu kufanya mtihani huu bila ya kuandika majibu kwenye karatasi, na mtihani wenyewe haufanyiki. Yaani ni madudu matupu yako kwenye mtihani huu. Nina-*challenge* wenzangu ambao ni Maprofesa na wengine wanajua Hisabati, wafanye mtihani huu waweze kupata mia kwa mia, mimi nitawapa Shilingi milioni 10 ndani ya Bunge hili." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni hatari kubwa sana! Haya ndiyo Matokeo Makubwa Sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtihani huu wamefanya majaribio, nimekwenda Baraza la Mitihani, hata kule Wizarani wakati wa kuulizia hii mwaka jana, 2013…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbatia, namwona Mheshimiwa Profesa Muhongo anakuangalia kwa umakini sana!

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Ni sawa hata yeye niko tayari aufanye, akipata mia nampa Shilingi milioni 10. Ninatampa na nitau-*table* huu mtihani pale Mezani. Haya ni madudu ya kutisha. Najua Profesa Muhongo ni mtaalamu wa miamba, lakini na mahesabu anayajua, nitampatia vilevile afanye huu mtihani. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2013 nilipotoa hoja hapa, Mheshimiwa Waziri alisema maoni ya Waheshimiwa Wabunge na wadau wengine, yamechukuliwa na rasimu ya mwisho ya Sera ya Elimu inapekekwa kwenye Baraza la Mawaziri Machi, 2013. Waziri aliliambia Bunge lako Tukufu, Bunge hili kwa mujibu wa Ibara ya 63 linaisimamia Serikali. Kwa hiyo, hata Bunge lenyewe limekuwa haliheshimiki. Kama Bunge lilipitisha hii, Waziri alisema ndani ya Bunge Machi, 2013, leo hii kwenye hotuba yake ukurasa wa saba anasema kwamba, wanakamilisha, liko kwenye hatua za mwisho kwenye Baraza la Mawaziri, sasa 2014. Mwaka jana alisema Machi, 2013. Sasa wapi ni wapi? Serikalini ni madudu, ndani hata ya Bunge linapitisha madudu; hii ni hatari tu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waliunda Kamati kwa ajili ya kuangalia ufaulu. Ukisoma ripoti hii ya mwaka 2010/2011 Taarifa kuhusu kushuka kwa kiwango cha Ufaulu wa Mitihani ya Taifa, Kidato cha Nne 2010, ukisoma humu ndani, majibu yote yamo humu ndani japo mengine ni ya ajabu ajabu, Kamati nyingine ya kazi gani? Ripoti zipo zimewekwa kwenye mafaili, hakuna chochote kinachofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni mambo ya kusikitisha, ni mambo ya kutisha, katika nchi yetu elimu ni dhaifu kupindukia. Elimu ni mapigo ya moyo wa Taifa. Mapigo ya moyo yakienda kinyume na maumbile yake, uhai hupotea. Kwa hiyo, uhai wa Taifa la Tanzania unapotea kwa sababu tumeshindwa kuwekeza kwenye elimu, wanafunzi wetu wanashindwa kufikiri yakinifu, *power of reasoning* katika nchi yetu imekwenda chini sana kwa sababu elimu ni dhaifu kwa kiwango cha kutisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni lazima tulikiri na hili halina suala la Chama wala nini, hapana! Sasa tufanye nini? Napendekeza tumwombe Mheshimiwa Rais aunde Tume ya Kudumu ya Elimu nchini, kwa sababu kwa hali inavyokwenda sasa, ni mbaya sana. Tume hii napendekeza ihakikishe ubora wa elimu nchini na kudhibiti mambo yote yanayotokana na kusababisha

kutetereka kwa ubora wa elimu nchini. Yaani tuiite *Education Quality Assurance and Control. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu yake yawe nini? Moja, kuangalia ubora wa elimu, kuidhinisha mambo ya mitaala, kuhariri vitabu, naweza nikapongeza magazeti au vyombo vya habari angalau wao wana wahariri wa magazeti na sekta mbalimbali. Nchi hii haina wahariri wa vitabu. Hakuna Jopo la Wahariri wa Vitabu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu lingine, wafanya tafiti za kisayansi kuhusiana na malengo ya elimu, kufanya maamuzi juu ya masuala mbalimbali ya elimu kama vile lugha gani itumike katika kufundishia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana kule Kigoma Walimu wa Mikoa minane wamekutana, wametoa *dead line* mpaka tarehe 30 ya Juni, wawe wamelipwa malimbikizo yao ya Shilingi bilioni 61. Nawaunga mkono, ni haki yao kwa sababu Sekta ya Elimu ndiyo inayowekeza kuliko sekta nyingine zote na ndiyo sekta kuu ya uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza pia jukumu lingine liwe kungalia marupurupu katika Sekta ya Elimu na kuangalia mambo ya ngazi za mishahara na mambo mengine. Yako mengi ambayo nimeyapendekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda na ninaomba, elimu isiwe ni bidhaa ya kuuza sokoni, elimu ni huduma. Sasa kuna hizi shule za watu binafsi, nao wanatozwa kodi, *skills and development levy*, mara *working permit*, sasa unaenda kutoza kodi kwenye elimu, maana yake nini wakati hii ni huduma na wala siyo biashara? Huwezi ukafanya elimu kana kwamba ni bidhaa unayouza sokoni. Hii ni hatari kweli kweli! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli utatuweka huru. Naomba tukubali ndugu zangu kwa moyo wa unyenyekevu, elimu yetu ni dhaifu sana, elimu yetu imeshuka sana! Taifa hili ni letu sote, tuhakikishe kwamba tunakuwa wakweli, *accept the reality and deal with it*. Kama hatuwezi tuka-*accept reality* tunarushiana maneno, elimu haina itikadi.

Kama elimu imeshuka sote tunaumia! Tukubali *class* yetu tulioko huku Bungeni na wengine wengi, watoto hawapati elimu hii. Hata watoto wangu hawapati elimu hii! Ni watoto wa walalahoi Watanzania. Kwa hiyo, *class* yetu hii kwa sababu tunawapa watoto wetu elimu iliyo bora, tumesahau *class* nyingine, tumesahau wale walala hoi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa heshima kubwa Bunge hili lichukue nafasi yake ya kuisimamia Serikali ili tupate elimu kwa ajili ya vizazi. Tuangalie malengo yetu ya elimu miaka 20 ijayo, miaka 100 ijayo na hasa

wakati huu wa mabadiliko makubwa ya Sayansi na Teknolojia ili kizazi kijacho na hasa nikirejea kwenye hoja yangu niliyowahi kuleta kwenye Bunge lako Tukufu mwaka 2013, iangalieni, ifanyieni kazi. Hata kama hampendi sura yangu, hampendi mawazo yangu, hayo mawazo niliyoyatoa kule ni kwa maslahi ya Watanzania na siyo kwa maslahi yangu binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili nimelitoa kwa moyo wa unyenyekevu, tuwe wazalendo kwa Taifa hili, tuwe wakweli kwa Taifa hili, na ukweli utatuweka huru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa James Mbatia. Mheshimiwa Peter Serukamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Jasson Rweikiza.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru kwa kunipa nafasi. Naomba nianze kwa kusema elimu ya Tanzania iko *ICU*. Niwaombe Bunge hili tuache siasa kwenye elimu, niwaombe Bunge hili tutafakari kwa kina, tutatue tatizo la elimu na tatizo la elimu siyo la mtu mmoja hapa, bali ni tatizo la Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi siyo wa kwanza kutafakari tatizo la elimu. Mwaka 1981 wakati wa Rais Regan, *Secretary of State* alikuwa anaitwa Belz aliamua kuunda Tume ya Elimu. Siyo kwamba Tume hazikuwepo, aliunda Tume iliyofanya kazi kwa miezi 18 kuangalia mfumo wa elimu wa nchi ya Marekani na wakaja na ripoti. Kwa mtu ambaye anasoma, akasome hiyo ripoti, inaitwa *A Nation at Risk*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mataifa makubwa yanajichunguza. Wanasema sababu ya kuunda ile Tume, ni kwamba aligundua *education system was failing to meet the national need for competitive work force*. Maana yake nini? Tukikaa hapa tuko *busy,* tunataka kupitisha bajeti; sawa bajeti itapita, lakini tunaua *generation* ijayo*. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii nenda Darasa Kwanza mpaka Darasa la Saba, anayoyasema Mheshimiwa Mbatia yapo, hata kama hatuyapendi. Leo nenda Vyuo Vikuu, watu wetu wanaomaliza Vyuo Vikuu ni *disaster,* tukubaliane. Lakini tumeamua kuwa wabinafsi na ni kwa sababu wote tuliokaa humu ndani tulio wengi watoto wetu hawasomi hizi elimu. Tuwe wakweli. Kama Taifa hili tumeamua kwa sababu unajiangalia wewe tu na familia yako, mengine basi, tunaua Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanini nasema hivyo? Mimi nimefanya *research* kwenye nchi 35, Tanzania ni ya mwisho kwa ufaulu. Wako watu wanasema ufaulu wetu ni mzuri. Nchi ambazo zimeendelea, China, Korea Kusini, Kuwait, Sweden, Peru, Mexico, zote ufaulu ni asilimia 60 *and bove.* Lakini sisi tunataka tuje hapa tushangiliane kwa sababu ufaulu mmoja anasema ni asilimia 20 na mwingine anasema hapana ni asilimia 30. Bado ni ndogo sana!

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitaka kujua, tunalo tatizo hapa la bajeti. Bajeti ya mwaka huu, 2014 kwenye Sekta ya Elimu wamepanga Shilingi trilioni 4.7, ni jambo jema sana. Lakini katika fedha hizi, zinazokwenda kweye *recurrent* ni Shilingi trilioni 2.67, zinazokwenda kwenye maendeleo ni Shilingi bilioni 800. Lakini katika Shilingi bilioni 300 ni kwa ajili ya *Loan Board*. Maana yake ni kwamba tunakwenda ku-*invest* kwenye *education only* Shilingi bilioni 500. *(Makofi)*

Ndugu zangu kama kuna *resource* ya kwanza mbayo lazima Taifa tuwekeze. ni elimu. Msiniambie barabara, sijui gesi; kama huna elimu, Taifa hili tutashangaana siku moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia hali halisi ya matokeo yetu, inashuka. Lakini unaona *measures* tunazofanya ni za ku-*solve* tatizo la leo ili Watanzania wasiseme watoto wamefeli sana. Tukubali waseme ili tujisahihishe. Nchi hii haina Wakaguzi, Walimu hawalipwi, vitabu ni tatizo, watoto wamelundikana madarasani, hatuwezi kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba niseme kwamba, nitaungana na James Mbatia kwa tofauti, nimwombe Waziri Mkuu, kama Waziri wa Elimu ameshindwa, aunde Tume ya Elimu ichunguze matatizo yetu ya elimu kuanzia *Kindergarten* mpaka *University.* Tujichunguze upya! Hii habari ya kuunda Tume kuangalia kwanini watu wamefeli sana, una-*solve* tatizo moja; unaunda Tume kwa ajili ya kuangalia madeni una-*solve* tatizo moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni Taifa, tukubali tuunde Tume ya elimu ya watu waliobobea kwenye elimu iangalie mfumo wetu wa elimu *in its totality,* itufanyie hiyo kazi ili tuanze upya. Kama mnadhani unaweza uka-*solve* tatizo la elimu; leo nunua vitabu, tumepata vitabu vya rada, tunakuja tunatamba sana hapa! Tumejenga madarasa mapya, tunakuja tunatamba, hatuja-*solve* tatizo la elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo letu la elimu ni kubwa sana. Tunahitaji kuwekeza kwenye elimu! Mimi nasema ndugu zangu Waheshimiwa Viongozi kama kuna jambo tunacheza nalo ni elimu.

Naombeni sana, hapa tusianze kubishana kwamba mambo yetu ni mazuri, ufaulu wetu ni mzuri, hii *BRN* ni nini? *BRN* haiwezi kuwa kwenye hali hii ya elimu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, chukua vijana waliomaliza *University* wote, tuwalete hapa tuwaambie waandike barua za Kiingereza, *fifty percent of it* watashindwa! *(Makofi)*

Tukubaliane, dunia hii ni kijiji, watoto hawa wataenda kushindana au watashindana na watoto wa sisi viongozi? Watoto wetu wanasoma *South Africa*, wanasoma Nairobi, Uingereza, labda! Kama Taifa hili tunalipenda, naomba sana tuunde Tume ya Elimu ichunguze mfumo wetu wote wa elimu tujue tuna matatizo wapi. Hii habari ya ku-*solve* tatizo moja moja haitatui tatizo letu la elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nitaomba niunge mkono nitakapokuja kuambiwa tunaunda lini Tume ya Elimu. Nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Peter Serukamba. Anafuata Mheshimiwa Jasson Rweikiza. Lakini kabla hajaongea Waheshimiwa Wabunge najua wengi hatufahamiani vizuri, itoshe tu kusema kwamba Mheshimiwa Rweikiza ni mmiliki wa shule Nane, lakini pia shule zake mbili zimepata *best performer* kwa mwaka huu katika hizo nane. Pia *best male student* wa 2013 ambaye yuko katika picha mojawapo ya hotuba Mheshimiwa Waziri, anatoka katika moja ya shule zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Jasson Rweikiza, tafadhali!

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii na pia kwa maelezo uliyotoa kuhusu uhusika wangu katika sekta ya elimu. Ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kwa moja niungane na Mheshimiwa Blandes kwamba sitaunga mkono hoja ya bajeti hii kama Kagera hatupewi Chuo cha Ufundi cha *VETA*. Juzi, Alhamis niliuliza swali kuhusu Chuo cha Ufundi, Kagera. Majibu niliyopewa yalikuwa ni ya kawaida tu; bajeti, nini, lakini nasema leo kwamba sitaunga mkono bajeti hii kama hatupati majibu humu ndani jioni hii kuhusu Chuo cha *VETA* Kagera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wanamaliza Elimu ya Msingi, Elimu ya Sekondari, hawana pa kwenda, wanakaa tu. Naomba wapate Chuo wajifunze ufundi na stadi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, utoaji wa elimu katika nchi yetu kama ulivyosema, kuna Shule za Serikali na Shule za binafsi. Nitangaze maslahi kwamba mimi namiliki shule kadhaa na kuziendesha na sheria imepitishwa hapa ndani baada ya Serikali kuamua kwamba shule binafsi zishiriki katika utoaji wa elimu. Kwa hiyo, shule hizi zipo kihalali na inasaidia sana.

Ukiona matokeo mazuri, vijana wanaofanya vizuri karibu wote ni wa shule binafsi. Hii siyo siri, ni wa shule binafsi. Sasa Wizara haisaidii shule hizi hata kidogo! Hakuna ruzuku, sawa; hatutaki ruzuku; lakini kodi zilizopo kwenye shule za binafsi ni za kutisha, ni za hatari. Amesema Mheshimiwa Mbatia na ninaungana naye mkono. Kodi ni nyingi sana! Mnataka kuziua hizi shule? Kuna kodi ya Mapato ambayo ni ya kawaida, *Pay As You Earn (PAYE)*, kuna *Skills Development Levy (SDL),* kodi ya vifaa mbalimbali, kodi ya majengo; hizi shule mnaziua! Lengo ni ziendelee kufanya kazi au zife? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ninapoongea nina barua ya shule yangu moja pale Dar es Salaam kwamba sitapata mtihani wa *Form Two* na wa *Form Four* unaotolewa na Baraza la Mitihani wa kujipima unaotoka mwezi ujao kama sijalipa kiwango cha Sh. 650/= kwa kila mwanafunzi kwa ajili ya michezo ya UMISETA. Sasa wapi na wapi? Michezo na mitihani inaenda wapi na wapi? Kwanini wanafunzi wasipewe mitihani kwa sababu ya UMISETA?

Mheshimiwa Naibu Spika, shule yangu nyingine iko Bukoba, iko Mahakamani imeshitakiwa na watu wa Idara ya Zimamoto. Sasa mimi sijaunguliwa shule, sijawaita waje kuzima moto; wamenishitaki kwamba sijalipa michango ya kuzima moto. Hizo fedha zinatoka wapi? Michango, michango, kodi, kodi, kila kukicha! Mnafikiri kwamba shule zina fedha nyingi sana za kulipa kodi na michango hii? Kutoka wapi? Mzigo kwa shule na mzigo kwa wazazi. Maana shule ikizidiwa inaongeza ada. Mzazi akiona hawezi, anaondoa mtoto shuleni; shule inakufa mtoto anakosa elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nafikiri kwamba Wizara ingeweka mpango maalum kusaidia shule hizi. Serikali peke yake haiwezi, ndiyo maana imeruhusu shule binafsi ziwepo na zinafanya vizuri sana. Isaidie shule hizi ziweze kusimama na kutoa elimu bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee ukaguzi wa shule. Hapa ukisoma hotuba ya Waziri amezungumzia ukaguzi, hotuba ya Kamati ya Huduma za Jamii imezungumzia ukaguzi haufanyiki na pia hotuba ya Waziri Kivuli imezungumzia ukaguzi; huwezi kutoa elimu bila ukaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru umeeleza kwamba shule zangu zinafanya vizuri. Ninachokiongea, sikiongei kutoka hewani tu, nakijua. Huyo mwanafunzi bora ni wa kwangu kutoka katika shule yangu moja ya Sekondari,

*Form Four* wa mwaka 2013. Shule nyingine ya msingi iko Bukoba ni shule ya 11 Tanzania nzima. Katika shule 16,000 ni shule ya 11, imepewa cheti cha *best perfomer* mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachokisema nakijua. Huwezi kutoa elimu kwa kugushigushi tu bila ukaguzi. Tangu Ukoloni tunajua umuhimu wa ukaguzi. Kagua shule hizi! Hakikisha Walimu wanahudhuria, wanafuata mitaala, vitabu vipo, majengo yapo! Maana unaweza kusema nina shule kumbe majengo haina! Hakikisha Madawati yapo! Mnasema shule zipo, lakini haina madawati, wanasomaje wanafunzi hao? Kwa hiyo, nasema Wizara lazima iwe na mkakati maalum kusimamia ukaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nashangaa Mheshimiwa Dkt. Kawambwa, Waziri wa Elimu ni Mwalimu; alikuwepo Mheshimiwa Mulugo, ni Mwalimu; leo yupo Mheshimiwa Jenista Mhagama, ni Mwalimu; Prof. Sifuni ni Mwalimu, wote ni Walimu. Kwa nini hamjui mambo hayo? Siyo mpaka uwe Waziri wa Elimu ndiyo ujue. Tunajua kwamba bila ukaguzi shule haziwezi kwenda. Simamieni ukaguzi vizuri ili tupate matokeo mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo kwamba hatuna fedha, siyo ya kweli. Wizara hii ya Elimu inapata fedha nyingi sana. Hadi kufikia tarehe 31 Machi ilishapokea Shilingi bilioni 486.6 kwenye bajeti. Asilimia 80 ya bajeti yake walizoomba na kupitishiwa. Fedha za kutosha! Kwa nini hawakagui shule? Wakague shule hizi, tupate ufanisi katika elimu. Kwa hiyo, sikusema hii kodi ya kukagua, kila mwaka hupewi mtihani hadi uchangie ukaguzi. Mimi shule zangu zimekukaguliwa mara ya mwisho mwaka 2005. Baada ya hapo, hamna ukaguzi. Shule zinakwenda, zinadidimia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kusema kwamba nitaunga mkono baada ya kupata majibu sahihi katika mambo ambayo nimesema. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deogratias Ntukumazina, atafuatiwa na Mheshimiwa Arfi.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKUMAZINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nianze kwa kuunga mkono hoja ya Waziri wa Elimu, lakini mbele ya Waziri Mkuu niseme kwamba sasa hivi hatuna Wizara ya Elimu. Huwezi kuwa na Wizara ya Elimu kama Elimu ya Msingi imeondolewa, Elimu ya Sekondari imeondolewa, wanaondoa sasa Elimu ya Watu Wazima; shule zile zote za *demonstration* zimeondolewa kwenye Vyuo vya Ualimu, huwezi kuwa na elimu. Lakini sitaki kuendelea kuwa mlalamikaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2013 nilijiita Yohana Mbatizaji aliyekuwa anapiga kelele huko nyikani kuhusu ujio wa Bwana wetu Yesu Kristo sisi ambao ni Wakristo. Sasa nataka leo nitoe ushauri kwamba iliyokuwa Wizara ya Elimu baada ya kuondolewa hayo yote, naomba ibadilike iwe *centre of excellence,* yaani iwe chimbuko au kitovu cha mawazo mazuri ya kielimu. A *good educational ideas* kama ilivyo Tume ya Mipango ambayo ni *centre* ya kutoa mawazo mazuri ya kiuchumi.

Idara ya Mipango iliyopo sasa Wizara ya Elimu, naomba iongozewe utafiti, wafanye utafiti na waone ni masomo gani ambayo wanaweza kuyaongeza ili watoto wetu waweze kuwa ni *critical thinkers* kuwa ni *system thinkers* kuliko kuwa *robot* kama walivyo sasa. Tuendeleze falsafa ya Mwalimu ya *Education for self reliance* ambayo mle ndani walikuwa wanazungumzia kwamba umwandae mtoto awe ni mdadidisi au mbunifu kuliko sasa ambavyo hatuna elimu ya kujitegemea. Bahati nzuri, pale sasa kiutaalam Wizara Elimu ni *top header;* ina Maprofesa watatu, ina Madaktari, hao wanaweza sasa wakatusaidia kuwa *centre of excellence.*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa mfano Prof. Bararusesa alikuwa *mis-allocated,* alikuja baada ya hayo yote kuondolewa, wakamwita Kamishna. Kamshina ni cheo cha Magereza, ni cheo cha Polisi, ni cheo cha Ardhi. *Title* nzuri ya elimu ni *Chief Educational Officer.* Sasa tukishaanzisha *centre of excellence,* naomba Prof. Bararusesa mmwite *Chief Educational Officer.*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ushauri huo, niende sasa kwenye mchango wangu. Bajeti ni tatizo sana kwa Wizara ya Elimu kama bado ipo. Kwa mfano, ukaguzi kama alivyosema Mheshimiwa Rweikiza, huwezi kuwa na maendeleo ya elimu bila ya ukaguzi. Mwaka 2013 nilishauri kwamba tununue pikipiki badala ya kuendelea kutumia magari ambayo hawana mafuta, tuimarishe ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mwalimu *by profession,* nimefanya utafiti, mwanafunzi anapokuwa pale Chuoni anatakiwa asome kwa siku 270 za darasani pamoja na *weekends.* Halafu kati ya hizo siku 270, siku 210 ni za darasani, siku 60 za *block teaching practice*. Lakini kwa sababu bajeti mbaya, bajeti ndogo sana, nasikia vijana wanasoma kwa siku 140, siku 20 za *BTP* na matokeo yake ni Walimu wanaotoka ambao hawakuandaliwa vizuri, *barefoot teachers* au *half cooked teachers.*

Sasa niende kwenye Vyuo Vikuu. Vyuo Vikuu vina matatizo ya bajeti makubwa sana. Tunapata *OC* ndogo, nasema tunapata kwa sababu mimi ni Mwenyekiti wa Chuo Kikuu cha Muhimbili *(MUHAS)*. Tunapata *OC* ndogo, tunapata fedha za maendeleo kidogo sana na ni Vyuo Vikuu vyote. Sasa

lazima elimu ishuke kama bajeti ni tatizo kubwa sana. Twende kwenye Maktaba.

Nampongeza sana Dkt. Mchalazo, anajitahidi sana kusambaza huduma ya Maktaba. Tunazo Wilaya 133, lakini kwa sababu ya bajeti amefikia Wilaya 19 tu, bahati nzuri na Ngara imo, na Tarafa mbili tu ya Moshi na Lulenge ambayo ni Tarafa yangu. Lakini imekuwa hivyo kwa sababu mimi nimejitahidi sana kushirikiana na Dkt. Mchalazo kwa kuibana Halmashauri yetu kutoa majengo na kukarabati majengo ndiyo maana tuna Maktaba mbili Ngara. Lakini ni Wilaya 19 tu zina Maktaba. Baba wa Taifa alitaka kueneza Maktaba vijiji vyote, sasa tumheshimu Baba wa Taifa.

Jambo lingine ambalo ningependa nilizungumzie niwaunge mkono ndugu zangu Wabunge wa Kagera kwamba kwa kweli tunahitaji Chuo cha Ufundi *(VETA)*. Ni Mkoa tu peke yake ambao hauna Chuo hicho. Kwa hiyo, mimi naunga mkono, wenzangu wamesema hawataunga mkono, lakini mimi naunga mkono, lakini natoa ushauri huo kwamba hatuna Wizara ya Elimu lakini ijigeuze iwe kama Tume ya Mipango ambayo ni *centre of excellence* kwa mawazo ya kiuchumi. Tunahitaji sasa tuboreshe elimu kwa kutumia Kitengo hicho cha Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Ntukumazina. Sasa ni Mheshimiwa Said Amour Arfi na atafuatiwa na Mheshimiwa Betty Machangu.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi nami nichangie katika hoja iliyokuwa mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na wenzangu waliotangulia kwamba bila ya kuitazama Wizara ya Elimu kwa ujumla wake, bado tuna tatizo kubwa katika nchi yetu. Wizara ya Elimu ambayo leo tunaishambulia hapa, Wizara ambayo kazi yake kubwa ni kusajili shule, ndiyo kazi ambayo inafanya Wizara ya Elimu. Inasajili Shule za Msingi, Shule za Sekondari, Vyuo na kadhalika, lakini haina mamlaka ya moja kwa moja na hizo shule. Shule zinasimamiwa na kitu kingine tofauti kabisa na Wizara ya Elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama hili hatuwezi kulirekebisha, bado tutaendelea kupiga kelele katika eneo hili la elimu. Ni lazima Wizara hii irudi kama ilivyokuwa, iweze kusimamia shule kwa sababu Waziri wa Elimu leo yupo tu na anabeba lawama nyingi kuhusu kuporomoka kwa elimu lakini hana mahusiano ya moja kwa moja na shule. Leo tuna Maafisa Elimu wa Mikoa wamekaa kwenye Sekretarieti ya Mkoa, kazi yao ni kuratibu taarifa tu, lakini

hawana mahusiano yoyote kwa shule. Sasa hili kama hatutaliangalia kwa ujumla wake bado tuna tatizo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunafanyaje katika mazingira haya ambayo Wizara haipati fedha za kutosha? Nitataka nipate maelezo. Katika bajeti ya mwaka 2013/2014 fedha ambayo iliidhinishwa na Bunge lako ni zaidi ya Shilingi bilioni 72. Fedha waliyopata ni Shilingi bilioni 14, mnatarajia nini? Miujiza gani mtakayofanya ili muweze kupata hayo matokeo makubwa kwa mtiririko huu wa kibajeti?

Mheshimiwa Naibu Spika, bado mipango yetu mingi tunawategemea wahisani. Wahisani katika bajeti iliyopita waliahidi kutoa Shilingi bilioni 53, lakini fedha waliyotoa wahisani ni Shilingi bilioni tisa, asilimia 15. Mna matarajio gani, mnategemea muujiza gani mtakaofanya ili tuweze kupata matokeo makubwa sasa? Ni lazima tuliangalie hili kwa umakini mkubwa sana.

Cha ajabu mwaka huu mnaomba fedha na mnawategemea wahisani ambao wameshindwa, wamewapeni Shilingi bilioni tisa, mnawaomba Shilingi bilioni 71, watu wa ajabu kabisa! Ni lazima tutengeneze mfumo wa kujitegemea sisi wenyewe kwa fedha zetu za ndani katika kuendeleza na kuwekeza kwenye elimu, vinginevyo Taifa hili linakufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nirudie kuangalia matatizo katika maeneo yangu. Moja, ni mgawanyo wa elimu. Nalieleza hili kwa sababu ni lazima nilipeleke katika Wizara ya Elimu. Pamoja na kwamba najua huzisimamii hizi shule, lakini mgawanyo wa Walimu una athari za moja kwa moja katika matokeo ya wanafunzi. Nitolee mfano, nina shule pale katika Halmashauri ya Mji ya Mapinduzi, ina wanafunzi 200, ina Walimu 12. Lakini kuna Shule ya Wiyimbi iko katika Halmashauri ya Nsimbo ina wanafunzi 200 na Walimu watano; iko Shule ya Ugala ambayo iko katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda, ina wanafunzi 600 na Walimu 20, Shule ya Mnyaki ambayo iko katika Halmashauri ya Nsimbo, ina wanafunzi zaidi ya 1,000 ina Walimu 15. Tunatarajia nini katika hali kama hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, mgawanyo wa Walimu ambao hauko sawia hauwezi kutoa matokeo mazuri. Shule nyingine ambazo zina Walimu wa kutosha, zitafanya vizuri na shule nyingine hazitafanya vizuri kwa sababu ya upungufu wa Walimu. Kibaya zaidi ni utaratibu huu ambao Wizara umeuanzisha wa michepuo. Huko nyuma sisi wakati tunasoma, Mwalimu alikuwa na uwezo wa kusomesha madarasa yote, vipindi vyote. Leo Walimu wanajifunza masomo mawili tu ya kufundisha. Kwa hiyo, unakwenda shuleni unakuta shule ina Walimu wa *arts* tu peke yake, hakuna Walimu wa sayansi, unatarajia nini? Kwa hiyo, Wizara kama ilivyokuwa imependekezwa ni lazima tuyaangalie hayo yote kwa ujumla wake ndiyo tunaweza tukafaulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni huyu mtoto ambaye anaanza kusoma. Mtoto unayemwingiza Darasa la Kwanza anapewa masomo manane na mzigo wa vitabu anabeba huyu mtoto. Hatumsaidii huyu mtoto! Ni lazima tujenge utaratibu kwamba mtoto huyu anayesoma Darasa la Kwanza basi afundishwe hayo masomo matatu; kusoma, kuandika na kuhesabu. Kwa lugha gani, nalo hili ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi wenzangu wamezungumzia, nilikuwa na pendekezo sitaki kurudia takwimu, lakini nilikuwa na pendekezo kwamba Ofisi zetu za Waratibu wa Kata zipanuliwe, angalau katika kila Kata kuwepo na Mkaguzi atakayekuwa na eneo dogo na shule chache ambazo anaweza kuzipitia badala ya kuwangojea Wakaguzi ambao hawana magari, hawana mafuta na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nimalizie Shule ya Mpanda *Girls.* Shule hii ni ya Kitaifa na ni ya "*A" level*. Shule hii mwaka 2010 wamejenga madarasa manne ambayo mpaka leo hayajatumika. Shule hii uwezo wake ni kupokea wanafunzi 800, ina wanafunzi 351 wa kike. Hosteli za kutosha zipo, Walimu hakuna na shule hii haitumiki inavyotakiwa. Pia kuna tatizo la Walimu hususan wa sayansi. Kuna jengo zuri na la kisasa na maabara, lakini hakuna vifaa. Hakuna vifaa vya maabara wala kemikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule hii iko pembezoni. Pamoja na kwamba sasa inaanza kuvamiwa na makazi ya watu, haina uzio, haina gari la wagonjwa, gari la shule pamoja na kwamba jana nimeambiwa kwamba wamefanikisha kuzindua *Dispensary* pale shuleni wakati Mbio za Mwenge zilizopita pale Mpanda Mjini, wamezindua. Kwa hiyo, nadhani tatizo hilo litakuwa limepungua, lakini bado shule hii inahitaji kupata gari ili iweze kuwahudumia wanafunzi ipasavyo na kuihudumia shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie. Nina shule ambazo kwa miaka minane au tisa sasa nimekuwa Mbunge nimezisemea mwaka nenda mwaka rudi. Nina Shule ya Msingi Uhuru, nina Shule ya Msingi Majengo na Shule ya Msingi Katavi, zote zina madarasa matatu matatu na zina darasa la kwanza mpaka la saba, tunatarajia kitu gani Mheshimiwa Waziri?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Arfi. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Betty Machangu atafuatiwa na Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Mimi naongea kwa uchungu sana kwa sababu bajeti ya Wizara ya Elimu imekuwa inaendelea kupungua ilikuwa asilimia 20 mwaka 2008 ikaendelea kupungua mwaka 2009 ikawa asilimia 19 tangu mwaka 2011 mpaka leo imekuwa ni asilimia 17. Kama kweli tunataka maendeleo ya nchi hii, ni lazima tu-*invest* kwenye elimu kama walivyosema wenzangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutoa vibali vya kujenga Vyuo Vikuu nami nawaunga mkono kabisa. Basi hivyo Vyuo Vikuu lazima vi-*match* na uanzishwaji wa viwanda. Kwa hiyo, Serikali inapokaa, Wizara ya Elimu inatoa vibali vya kujenga Vyuo Vikuu, Waziri mwingine ambaye anakaa kwenye Baraza la Mawaziri na huyu Waziri wa Elimu washauriane ili iwezekane kabisa kuanza pia viwanda kwa sababu kwenye hivi Vyuo Vikuu wanafunzi wana-*graduate* kila mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, tumeanzisha Shule za Awali katika kila Shule ya Msingi na tumefanikiwa vizuri na nimeona Mheshimiwa Rais anapongezwa kule Abuja na aliyekuwa *Former Prime Minister* wa Uingereza Bwana Brown, nami pia nampongeza Mheshimiwa Rais. Lakini sera ya hii Shule ya Awali iko wapi? Hatuongei kisera na kimkakati, hawa wanafunzi wa Shule ya Awali wanafundishwa na nani? Mwalimu anayefundisha Shule ya Awali lazima awe kweli ana taaluma ya kufundisha Shule ya Awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema samaki mkunje angali mbichi, tukiendelea kwa mtindo huu kwamba Mwalimu wa kawaida ndio anamfundisha mwanafunzi wa Shule ya Awali hatutapata wanafunzi bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwa niliyokuwa nataka kuchangia, kuna kilio kikubwa kabisa cha kufeli wanafunzi katika masomo ya sayansi, yaani Hisabati, Fizikia na Kemia. Lakini pia kuna kilio kikubwa cha ukosefu wa Walimu wa sayansi. Kule Mkoani Kilimanjaro tuna ukosefu wa Walimu wa Sayansi 898 ambao ni asilimia 45 ya mahitaji. Masomo ya Sayansi lazima yaende sambamba na Maabara. Kama hakuna Maabara, masomo ya Fizikia, Kemia na Baioloji yanafanyikaje? Hiyo mitihani itafanyikaje? Kwa hiyo, naomba Serikali iliangalie hili, hatuwezi kwenda kwa mtindo huu bila Maabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka pia nichangie jambo la ukaguzi. Wenzangu wameliongea nami naomba nisisitize kwamba jambo ambalo linawafanya wanafunzi pia wanafeli ni kwa sababu ya kukosa ukaguzi. Ukaguzi huu unatakiwa uwe ukaguzi makini. Ukaguzi makini maana yake ni nini? Ukaguzi unasaidia kuiongoza Serikali kujua *performance* ya shule za zake. Ukaguzi huu lazima ufanyike ukiwa na dhamira na lengo la kuchochea mabadiliko chanya katika *performance* ya shule. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kama ukaguzi hautafanyika kwa makini, kama matokeo ya ukaguzi hayatakuwa na mrejesho kwa wale wahusika ama walengwa, kama ukaguzi hautakuwa na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya wale waliofanya ukaguzi, yaani *recommendations* na kama ukaguzi hautakuwa na tathmini, yaani *monetary and valuation,* ukaguzi huu utakuwa hauna maana. Kwa hiyo, naomba Serikali iliangalie hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ripoti ya *CAG* inasema, ingawa Idara za Ukaguzi zinakuwa ni matatizo kiofisi, hazina Ofisi za kutosha, hazina vifaa vya kutosha, lakini pia ripoti inasema kuwa Wakaguzi na wenyewe wanachangia wanafunzi kufeli. Kwa sababu wanasema katika kitabu chao cha Ukaguzi, kuna mambo 148 ambayo yanatakiwa yatiliwe mkazo. Lakini katika hayo mambo hakuna hata jambo moja linaloelekeza *performance* mbaya ya wanafunzi kama kipaumbele. Kwa sababu ilitakiwa wanapokwenda kukagua sasa, *performance* mbaya ya shule au *performance* mbaya ya wanafunzi iwe ni kipaumbele katika ukaguzi. Badala yake wakienda kule ndiyo watagua *capitation* imefanyikaje? Majengo yamekuwaje? Wanasema hata ripoti nyingine, *special audit* iliyofanyika kwa shule 110 katika zile shule hakuna hata ripoti moja iliyotaja utoro wa wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo unaweza kuona kwamba ukaguzi nao unachangia kwa wanafunzi hao kufeli. Laiti ingekuwa wana-*communicate* hiyo *information* ya ukaguzi vizuri, kwa mfano Serikali wanatakiwa kupeleka ripoti hii kwa shule zilizokaguliwa, kwa Bodi za shule, kwa wazazi kupitia hizo Bodi lakini pia watoe taarifa kwa Umma kupitia Waandishi wa Habari na Umma wenyewe unaweza kuwa unachangia namna ya kuboresha. Ndiyo maana unakuta shule imekuwa ya mwisho kwenye mitihani mwaka huu na mwaka kesho inaendelea kuwa ya mwisho au inapanda kidogo tu kwa sababu yale mapendekezo ya ukaguzi, zile *recommendations* kwamba kuna hili na hili hayafanyiwi kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine linalofanya wanafunzi wanafeli pia ni ukosefu wa chakula shuleni. Ziko familia ndugu zangu ambazo hawali nyumbani kwao yaani hakuna chakula nyumbani kwa hiyo mtoto anaponea kile chakula anachokula shuleni. Taarifa za Umoja wa Mataifa na Shirika la Chakula Duniani linasema, duniani wako wanafunzi wa shule ya msingi milioni sitini na sita ambao wanakaa na njaa kwa siku na 23% ya wanafunzi hawa wanatoka Afrika. Wako wanafunzi milioni sabini na tano ambao wamefikia umri wa kwenda shule lakini hawaendi shule na kati yao 55% ni wasichana na wanasema 47% wako Afrika. Kama tutatoa chakula shuleni imeonyesha kuongeza mahudhurio, imeonyesha kupunguza utoro lakini pia imeonyesha kusaidia wale watoto wenye matatizo ya chakula nyumbani kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili watoto wa kike wanaokula chakula shuleni inawasidia sana kwa sababu akikaa nyumbani ana mambo mengi ambayo anafanya yanamfanya hata asiweze kusoma. Tunasema mtoto akikaa shuleni muda mrefu zaidi, akiwa na *more years in school* inamsaidia kuepukana na ndoa na mimba za utotoni na hatimaye itamsaidia yeye kiuchumi kwa sababu akisoma hata kama hatapata kazi lakini ataweza kufanya hata shughuli yoyote ya kumsaidia. Hata hivyo, huyu mtoto wa kike sasa anaweza kufanya maamuzi kwa sababu amepata elimu, hata akifikia umri wa kuolewa, anaweza kuamua sasa nataka kuolewa na ninataka nizae watoto wawili au watatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo tunasema kwamba elimu yetu iko kinadharia sana kwa hiyo wanafunzi wakimaliza vyuo hawana ajira kwa hiyo tunataka kutoa elimu ambayo itamsaidia mwanafunzi akitoka pale akaanze biashara. Ni sawa na mimi ninaunga mkono lakini naomba tuliangalie hili kwamba huyu mwanafunzi anaye-*graduate* chuo cha Tumaini au Dar es Salaam, tunamwambia akafanye biashara mikopo yenyewe ya Benki Serikali haijaweka namna ambavyo mikopo ile itakuwa na *interest* ndogo za kukopa. *Interest* ni kuanzia kumi na na nane mpaka ishirini na moja, huyu mwanafunzi anayemaliza chuo anawezaje kukopa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niiombe Serikali ile Sheria tuliyoiweka ya *PPP*, tukubaliane kwamba Kanuni ziwe tayari kule kwenye Wilaya wafanyabiashara waanzishe viwanda.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Betty Machangu. Sasa ni Mheshimiwa Chacha Mariba Nyangwine, yeye ni Mwalimu lakini pia ni mchapishaji wa vitabu na ni mtunzi wa vitabu pia, Mheshimiwa Nyangwine tafadhali.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE**: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii ambayo ni nyeti katika maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nianze kuongelea suala la madaraja kama ilivyowasilishwa na Mheshimiwa Blandes na Msemaji wa Kambi ya

Upinzani katika Wizara hii. Haya madaraja yamepangwa kwa msingi kwamba yawe ya kudumu. Ukiangalia katika nchi nyingine, haya madaraja yanapangwa kuanzia elimu ya awali mpaka elimu ya vyuo vikuu. Katika nchi yetu ya Tanzania tulikuwa tunapanga haya madaraja kuanzia ngazi ya Diploma na kuendelea lakini yamerudishwa katika elimu ya msingi na sekondari. Mimi sina ubishi na haya madaraja kabisa, kama yatafuatwa na yasibadilike yatatoa msingi mzuri katika kuinua elimu Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na hayo, mimi napenda kuishauri Wizara hii, masuala yote ambayo Wabunge wanayaongelea inaonekana kabisa kuna tatizo katika elimu yetu ya Tanzania. Ni vizuri zaidi tukayaangalia yale yote ambayo yanatolewa na Wabunge tukayafanyia kazi tangu Kamati ya Kudumu ya Huduma za Jamii ya Bunge hata maoni ya Upinzani waliyoyatoa na yale Wabunge waliyoyachangia, ni muhimu sana ili kuelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tufahamu, kuna Mheshimiwa Baba yangu pale ameongelea suala la masomo mengi katika shule za msingi hasa darasa la kwanza kwamba mtoto wa darasa la kwanza anaanza kusoma historia, uraia, sayansi inakuwa ni mzigo mkubwa sana.

**MBUNGE FULANI:** Kweli.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Ukiangalia katika nchi zilizoendelea na kabla elimu yetu haijaharibika kiasi hiki, mtoto alikuwa anasoma masomo matatu kuanzia darasa la kwanza mpaka darasa la tatu, anasoma Kuandika, Kuhesabu na Kusoma, vitu vitatu tu hapo vilikuwa vinamjenga sawa. Mtoto wa sasa hivi anaanza darasa la kwanza anarundukiwa masomo mengi mpaka anakosa uwezo wa kuyabeba. Kwa hiyo, hilo ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala lingine ambalo tumelisahau na Waheshimiwa Wabunge naomba hili mlifahamu kabisa, elimu ya Tanzania inashuka na tutapiga kelele sana kama hakuna lugha maalum ya kufundishia. Sisi tunatumia lugha ya kigeni kufundishia, tunawaza fikra za kigeni, mimi nasema hata tupige kelele, hata tuite Malaika waje wafundishe hatuwezi kubadilisha elimu ya Tanzania kama hatutatumia lugha ya kwetu ya kujielewa ambayo ni lugha ya Kiswahili. Namwomba Waziri atamke hadharani ni lini nchi ya Tanzania itaanza kutumia lugha ya Kiswahili kama lugha rasmi ya kufundishia toka elimu ya msingi mpaka elimu ya vyuo vikuu?

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua ni uwezo mfinyu sana wa kifikra kumfundisha mtoto kwa kutumia lugha ya Kiswahili darasa la kwanza mpaka la saba halafu anapofika sekondari unamuanzishia elimu ya kigeni, hapo huo

mwendelezo siyo mzuri. Mimi napendekeza kwamba ni vizuri tukatumia lugha za kigeni katika kujifunza ili kufahamu mambo mengine ya dunia na tujifunze sana, tujifunze Kiingereza, Kichina, Kifaransa lakini elimu yetu tuitoe kwa lugha ya Kiswahili.

**MBUNGE FULANI:** Kweli.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Hapo tutafikiri fikra sahihi na ambazo zitatufanya elimu yetu itapanda zaidi. Namuomba Mheshimiwa Waziri alitolee ufafanuzi zaidi tusifuate fikra za Magharibi. Nchi ambazo zimeendelea, mimi ninafanya utafiti kwa mfano Zimbabwe wanafundishia lugha tatu, nilikuwa naongea na Mkurugenzi wa Shirika la Uchapishaji la Zimbabwe anaeleza kwamba wanapotumia lugha ya kigeni kama Kiingereza wale wanafunzi hawafaulu sana kama wanavyotumia zile lugha za kienyeji. Hali kadhalika Afrika ya Kusini wana lugha kama saba za kufundishia, wanaotumia lugha ya Kiingereza wanafeli vibaya sana lakini wanaotumia lugha za kienyeji wanafaulu vizuri sana. Ni kwa nini hapa Tanzania sisi tusitumie lugha ya Kiswahili katika kufundishia?

**MBUNGE FULANI:** Hamna anayekupigia makofi.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Najua hamtapiga makofi kwa sababu mmeathiriwa na athari za Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni vizuri kabisa tufahamu kwamba nchi yoyote ile usomaji wa vitabu ni jambo la msingi sana, kusoma vitabu vya taaluma mbalimbali viwe vya utalii, sayansi na vile vya shuleni. Tatizo katika nchi ya Tanzania hatuna Shirika la Uchapishaji wa Vitabu, tumelibinafsisha hali inayopelekea hata uchapishaji wa vitabu katika nchi yetu kujikita kwa watu binafsi kama Nyangwine na wengineo ambao wako kibiashara zaidi. Mimi naomba kama nchi tuamue kuanzisha Shirika la Uchapishaji wa vitabu ili tuweze kunyanyua kiwango chetu cha elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kwa haraka haraka ni ukubwa Wizara hii, kila siku huwa nasema kwamba ikiwezekana vile vyuo vya *VETA* ni kwa nini visihamie katika Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia? Kwa sababu *VETA* ile ni *application* ya Sayansi na Tekonojia sasa ni kwa nini inakuwa katika Wizara ya Elimu? Ni vizuri tukaangalia ni namna gani ya kupunguza ukubwa wa hii Wizara, vyuo vya *VETA* vyote viwe ndani ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la vyuo vya *VETA* katika Mkoa wa Kagera, watani zangu wamelalamika sana hapa, kama Mkoa mzima huna chuo cha *VETA* ni aibu. Hali kadhalika katika Wilaya yangu ya Tarime kila siku ninaahidiwa.

Mheshimiwa Naibu Waziri utakapokuja hapa uniambie ni lini mtajenga chuo cha *VETA* katika Wilaya ya Tarime? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ukaguzi limeongelea lakini la mwisho ninaomba kuongelea suala la Walimu wa Sayansi. Tumejitahidi sana kujenga shule zetu na tumejitahidi sana kusomesha Walimu katika fani mbalimbali lakini Walimu wa sayansi hawapo. Unakuta Wilaya nzima inaweza kuwa na Walimu wa Sayansi sita katika shule za sekondari. Kwa mfano, katika Wilaya yangu ya Tarime, nina shule karibia arobaini za sekondari lakini nina Walimu wa Sayansi wasiopungua kumi. Mimi ninaomba tuweke Sera na utaratibu wale wanafunzi wanaofaulu vizuri masomo ya sayansi kutoka kidato cha tano na cha sita tuwaingize kwanza wakasomee Ualimu baadaye watoe huduma ya kuelimisha jamii ndiyo uzalendo katika nchi. Hili tukilipanga vizuri litawezekana lakini kama hatutakuwa na dhamira ya dhati ya kuwaendeleza Walimu hawa wa Sayansi tutapiga kelele siku zote na hatutaweza kufanikisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wale wanafunzi ambao wanafaulu vizuri masomo ya sayansi waende kwanza wakasomee Ualimu, Bodi ya Mikopo iwalipie na wakishamaliza wafundishe hata miaka mitano kama watabadilisha kwenda kusomea fani nyingine itakuwa ni vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja lakini naomba kwamba tulitafakari zaidi suala hili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Chacha, Mheshimiwa Arfi.

**TAARIFA**

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa taarifa Msemaji wa mwisho kwamba mimi ni Baba na Babu na siyo Mama. Kwa hiyo, naomba anitake radhi na kama aliteleza tu ulimi namsamehe. *(Kicheko)*

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Samahani, mimi nilisema yule Baba, Mama nilisema Mwalimu Susan Lyimo, ahsante. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa kwa kuwa hoja imekuwa Mama, sasa twende kwa akina Mama nao wachangie. Mheshimiwa Magdalena Sakaya atafuatiwa na Mheshimiwa Muhonga Ruhwanya na Mheshimiwa Margareth Mkanga ajiandae.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi uliyonipa ya kuweza kuchangia Wizara kwa uchache sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nianze kwa kusema kwamba kiukweli wenzangu wamesema kwamba hali tunayoenda nayo kwenye nchi yetu, hali

ya elimu kama hatutakuja na *altenative* ya nini tufanye, Taifa hili tunaliangamiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia elimu inashuka siku baada ya siku na ziko sababu nyingi tumekuwa tunasema hapa Bungeni ukaguzi, Walimu wamekata tamaa, mazingira ya kusomea watoto wetu ni mabaya, miaka 50 ya Uhuru baadhi wanakaa chini kwenye mawe na kwenye udongo, shule zingine hazina maabara, kiukweli hali ni mbaya sana. Mimi nitashangaa Mbunge atakayesimama hapa aseme elimu inapanda, ina maana yeye sijui kazaliwa nchi gani sijui.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimeshangazwa sana na kitendo cha Wizara kushusha madaraja, hilo hamtudanganyi sisi siyo watoto tunaona. Zamani kuanzia 34 ilikuwa ni *division* sifuri leo hiyo ni *passmark* kwa upande wa sekondari, leo Wizara inatuambia madaraja yako palepale, nashangaa! Wizara imeshindwa kuwafundisha watoto vizuri kwa kuhakikisha inaweka mazingira mazuri, Walimu walipwe vizuri, kuwepo na vifaa madarasani, matokeo yake ni kama vile kocha ameshindwa kufundisha timu yake ifanye vizuri kwenye uwanja anapanua lile goli ili magoli yaingie kirahisi, huko sio kusaidia Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ina maana Mwalimu kashindwa la kufanya, kocha kazi imemshinda na mimi ni mkweli, kiukweli Waziri ambaye yuko kwenye Wizara hii, mwaka jana nimesema na mwaka huu nitasema na mwakani nitasema, ameshindwa kusaidia elimu Tanzania. Hiyo ni ukweli kabisa, ameshindwa kusaidia watoto wetu kuanzia chini, toka amekuwepo anazidi kubebwa, kwa nini tunambeba mtu ambaye ameshindwa kusaidia elimu Tanzania? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Ndugu yake Rais.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Nasikitika sana, nchi ambayo tuna misitu, tena tumeshamiri kwa misitu, tunasafirisha magogo kila kona, mbao kila kona, mtoto anakaa chini kwenye udongo, kiukweli ukianza kuzungumzia elimu ya Tanzania inaumiza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana Wizara imetuambia kwamba inajenga maabara, tumelia sana kuhusu shule za Kata, mazingira yake ni mabaya na wanaosoma kule ni watoto wa maskini. Serikali ikasema imekuja na mpango wa kujenga maabara, leo Wilaya yangu hakuna shule hata moja ambayo ina maabara na shule zingine za Kata. Tunawezaje kujenga shule, tunaiacha mazingira yaleyale tunakuja na mipango Bungeni, leo hakuna kinachofanyika halafu tunapiga makofi elimu inapanda, elimu inapandaje kwa mazingira haya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana leo hapa tujibiwe, kama Waziri huyu, Mheshimiwa Kawambwa, ameshindwa kusaidia elimu ya Tanzania matokeo yake ni kuendelea kushusha *grade* za watoto wetu, watoto wanamaliza sekondari hawawezi kujieleza hata kwenye masuala ya kawaida, watoto wanamaliza *primary school* hawawezi kusoma na kuandika, watoto wanamaliza chuo kikuu hata kuandika barua ya *application* wanashindwa, leo tunaendelea kumuacha, tunambeba elimu yetu inadorora wakati watoto wa wakubwa wako shule za maana. Mimi nasikitika kwa niaba ya Watanzania maskini, nimesoma katika hali ya shida lakini hatutendi haki kwa watoto maskini wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la *private school,* tunatambua mchango wa *private school* kwa watoto wetu wengi lakini shule za *private* zimeachwa *lose* sana, wamiliki wa shule zile wanapandisha gharama za ada wanavyopenda wao. Naiomba sana Serikali kwa kuwa mchango wa *private school* unajulikana lakini shule zile ada ziwe na *standard* ili watoto wengi waweze kwenda kule kwa sababu ndiyo kimbilio baada ya kuona shule zetu za Serikali hazifanyi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye masuala ya Walimu. Suala la kilio cha Walimu tutalia mpaka lini hapa Bungeni? Tutasema mpaka lini hapa Bungeni, haiwezekani kwa mazingira ya wale Walimu hata ningekuwa mimi ningekufa moyo wa kufundisha, kweli kabisa. Zaidi ya miaka minane wanalia madai yao, wanalia posho zao mbalimbali hawalipwi wameishia kupewa ahadi lakini hawapewi, wakitaka kugoma Serikali inakimbilia Mahakamani, hakuna kugoma, wakitaka kujieleza hawasikilizwi, ni kwa nini Serikali haitambui nini madhara ya Walimu kutokulipwa madai yao, kweli Serikali haitambui, wamekufa moyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine wanafundisha wanavyojisikia, anatoa *instruction* watoto waandike tu ubaoni ile kumfuata mtoto mmoja mmoja afundishe hawana huo muda kwa sababu Serikali yenyewe haiwajali. Naiomba Serikali atakavyokuwa ana-*wind up* Mheshimiwa Waziri atuambie kwa uhakika na iwe ni ahadi ya kweli ni lini madai ya Walimu wa Tanzania yatalipwa ili Walimu waweze kufanya kazi kwa moyo kwa manufaa ya watoto wetu na siyo kuendelea kudidimiza elimu kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Walimu hawasikilizwi na watoto na wenyewe hawasikilizwi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Ya pili?

**MBUNGE FULANI:** Endelea ya kwanza, kanyaga twende.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la ukaguzi wa shule. Wamesema wenzangu hapa, tatizo kubwa la watoto kufeli pamoja na matatizo mengine mengi ya mazingira na mengine niliyoyatajwa pia suala la ukaguzi halipo kwa uhakika. Wakaguzi hata wachache waliopo hakuna vitendea kazi. Tunawezaje kumtuma Mkaguzi akakague shule za Kata nzima na ukiangalia mazingira ya vijijini tumetoka huko tunajua lakini Mkaguzi hana vitendea kazi, hawezeshwi. Tumeweka ofisi pale hatuwawezeshi kuhakikisha kwa kuwa na fedha ya kutosha, hili ni tatizo. Naiomba sana Wizara watuambie kwamba ni lini watahakikisha kwamba vitengo vya Ukaguzi kwenye Halmashauri zetu vimewezeshwa kikamilifu kwa fedha na wale Wakaguzi wenyewe pia wapewe elimu mara kwa mara na waweze kuwezeshwa vizuri wafike kwenye vituo kwa muda kuhakikisha kwamba elimu inakuwa ni bora na siyo bora elimu kama elimu yetu ambapo ipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni la vyuo vyuo vya *VETA*. Serikali ilisema mwaka jana au mwaka juzi kuwa itahakikisha kila Wilaya imekuwa na chuo cha *VETA*. Ni kwa nini mpaka sasa hivi Wilaya nyingi hazina vyuo vya *VETA?* Wilaya ya Urambo haina Chuo cha *VETA*, Kaliua haina Chuo cha *VETA* na Wilaya nyingine nyingi. Baada ya kuwa elimu imeshuka watoto wanakokimbilia wale ambao wamefeli sana *division four* na *three* ambazo hazitambuliki na Serikali wanakimbilia *VETA* leo Halmashauri nyingi hazina vyuo vya *VETA*. Naiomba Serikali ihakikishe kila Wilaya imekuwa na chuo cha *VETA* kama kimbilio la watoto maskini lakini pia ni sehemu ya kutoa stadi za kazi waweze kujitegemea kwa sababu hata waliomaliza Vyuo Vikuu hawapati kazi kwa sababu viwanda vyetu mmebinafsisha, watoto wetu wanazurura mitaani na kazi hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Sakaya. Kuna Mheshimiwa mmoja ameniandikia hapa, ule mfano ulioutoa Mheshimiwa Sakaya wa kuogeza goli, wamesema Kiswahili kizuri siyo kupanua ni kutanua goli. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya atafuatia na Mheshimiwa Mwalimu Margareth Mkanga, Mheshimiwa Mhonga!

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi leo niweze kuchangia lakini pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema ili niweze kusimama hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba nitoe salamu za wanafunzi wa vyuo vikuu, wanalalamika kwamba pesa zao zinachelewa mno. Kwa hiyo, naomba pesa zao zisiwe zinachelewa. Baadhi wamesema wameziona kwenye akaunti zimeingizwa, baadhi wanasema hawajaona, kwa kweli wanafunzi wanahangaika. Nasisitiza *boom* lipelekwe mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niende kwenye suala la *Big Results Now*. Najua Wizara hii mpo katika huo mpango wa *Big Results Now* katika zile Wizara chache ambazo mmesaini lakini nyie mna malengo yenu tisa. Nataka kujua mmeoanisha vipi au mmewashirikisha vipi Walimu kwa sababu ni wadau wakubwa ambao watasababisha hayo matokeo yaonekane yakiwemo matokeo ya kuboresha kiwango cha elimu na wanafunzi kufaulu. Naomba kujua hilo kwamba mmewashirikisha vipi Walimu?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nina suala lingine dogo, sasa hivi wazazi wengi wanakimbilia shule za *private*, lakini tunajua kweli kwamba biashara ni huria bei ni kubwa mno. Tunaomba Serikali muangalie hili ili muweze ku-*regulate,* wanatoa elimu nzuri lakini bado bei ni kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nitaongelea suala la kitengo cha Ukaguzi wa Elimu. Elimu haiwezi kuwa bora kama haikaguliwi. Sehemu ambapo kuna Wakaguzi hakuna vifaa wala pesa. Je, hamuoni kwamba kutokukagua elimu inazidi kuwa duni? Naamini kabisa kama shule nyingi zingekuwa zinakaguliwa zingefungwa. Shule hazina vyoo, maji, madawati, *computer lab,* maabara za masomo ya sayansi ya kawaida, hazina sakafu, paa zimetoboka, nyumba za Walimu hakuna, Walimu hawatoshi. Kwa mfano, tu kwa Wilaya ya Kigoma Vijijini ambayo sasa hivi kuna Uvinza na Kigoma Kaskazini, kuna Majimbo mawili, tunahitaji Walimu mia sita wa shule za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano katika shule moja ya Mtanga kuna wanafunzi 502, ina Walimu sita tu, shule hii ni kongwe ilianza toka mwaka 1971. Shule hii imechakaa mno, madarasa mengine yamefungwa hayatumiki kwa sababu hakuna kabisa hata madirisha, sakafu chini watoto wanaweza kupata hata funza. Nawashukuru sana Gombe wametusaidia pale madarasa mawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba shule hizi zimechakaa sana hazivutii wanafunzi kwenda shuleni, mazingira ni mabaya na ndio maana

watoto wanazidi kufeli na Walimu vilevile tunasema ni wachache. Pamoja na hivyo hata kama kuna mpango huu wa kuendelea kujenga shule mpya, kuwepo na pesa za *maintance* za shule za zamani, ili ziendelee kuwasaidia wanafunzi kwa sababu watoto bado wanaendelea kuzaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu wanalalamika mabadiliko ya mitaala inapofanyika hawashirikishwi. Kwa hiyo, wanashindwa sasa kuendana na mabadiliko ambayo yanakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo linanisikitisha tunajua kabisa Vijiji vyetu vingi havina umeme. Tulianzisha somo la TEHAMA, lengo letu lilikuwa ni nini? Wanafunzi wanachorewa ubaoni *computer* hawaelewi ni kitu gani, wengine hata *TV* hawajawahi kuiona na umeme hakuna na hatutegemei lini baadhi ya Vijiji vitapata umeme. Tunajua kuna huu mpango wa *REA* lakini nao unasuasua kwa sababu pesa zenyewe sio za ndani maana pesa nyingi za maendeleo tunategemea kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna shule nyingine zipo Mjini lakini hazijaunganishwa na umeme. Kwa mfano, shule moja ya Kiheza pale Kigoma, nimewachangia umeme, namshukuru Mungu aliniwezesha, najua siku yoyote wataniambia kama wameweka umeme nitawafuatilia nijue. Wanasoma somo la TEHAMA, ni shule yangu ya msingi ambayo mimi nimesoma. Tunashukuru kuna Kanisa pale karibu ndio wanapoenda kujifunzia mara moja kwa mwezi au mara moja kwa miezi miwili. Hata hivyo, kile chuo ambacho wanaenda kujifunzia wanapokuwa *busy* hawapati hiyo nafasi, bora hawa ambao wapo Mjini, walioko vijini kwa kweli tunataka kujua Serikali ilianzisha somo hili kwa nini wakati wanajua hawajajiandaa vya kutosha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu yenyewe ndio inayotengeneza matabaka ya watoto, tunatengeneza watwana na wabwana ndani ya nchi yetu. Watoto wa maskini wataendelea kuwa na elimu duni na watoto wa watu wenye uwezo wataendelea kuwa na elimu ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia shule ambazo ni za *private*, watoto wanakula shuleni kwa hiyo, wanavutiwa kwenda shuleni, wana maabara, wanafundishwa vizuri *computer* tena zinafanya kazi, wana Walimu wengi wa kutosha. Sasa hebu angalieni tu matokeo haya yanaonekana wapi? Yanaonekana kwenye matokeo ya mwisho watoto wanapofanya mitihani, mitihani yao inafanana. Matokeo yake sasa wale watoto wanaosoma shule za msingi za kawaida na hizi shule za Kata ambazo hazina Walimu wala vifaa, matokeo yao ni ya chini mno. Ukiangalia matokeo mazuri ni ya watoto ambao wanaosoma shule za *private*. Naomba kujua, Serikali ina mkakati gani ya kuboresha shule zetu hizi za kawaida ili elimu ya Tanzania iwe *standard,* angalau

mtoto anayesoma *private* na shule za Serikali kuwepo na uwiano ambao unafanana wa matokeo ya mitihani na uelewa vilevile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni vitabu vinatofautiana, Walimu pia wanalalamika kila shule unakuta wanatumia vitabu wanavyotaka wao! Vimeruhusiwa ndio lakini vina wachanganya pia wanafunzi. Shule hii wanasoma hiki, shule hii wanasoma kitabu kingine na Mwalimu wa *tuition* anamfundisha kwa kitabu kingine! Kweli *syllabus* zinafanana lakini mabadiliko ya vile vitabu na hata utunzi pia ni tofautitofauti kwa hiyo, Walimu nao wanataka kulijua.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine kwa nini *multiple choice* bado inaendelea? Mnawafanya wanafunzi wanakuwa wana *guess* majibu. Bado tunaomba hili suala kama mlivyokubali suala la KKK, tunapigia kelele na hili suala la *multiple choice* lifutwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru kwamba maoni yetu yamesikilizwa yakiwemo maoni ya Wabunge wengine wa Kambi ya Upinzani kwamba sasa hivi wanafunzi wa darasa la kwanza na la pili wataanza kusoma KKK (Kusoma, Kuandika na Kuhesabu). Kuna bibi mmoja alimuuliza mjukuu wake sasa darasa la kwanza unabeba madaftari tisa, ukifika chuo kikuu si tutakukodishia toroli ubebe madaftari yako? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache naomba Serikali inipe majibu ya mambo yangu yote niliyouliza na vilevile siungi mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya. Mheshimiwa Mwalimu Margareth Mkanga, Mwalimu wa sekondari ya Kilakala kwa miaka mingi atafuatiwa na Mwalimu Profesa Peter Msolla. *(Makofi)*

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuzungumza. Nashukuru nimeona baadhi ya mambo niipongeze Wizara kwa hayo machache tu kwamba watarejesha utaratibu wa kusaili watu sawasawa na kupandisha ma-*grade* ya Walimu, kutoa ruzuku na kadhalika, kuna maboresho nimeyaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nasikitika sana kwamba nimesoma mara tatu hii hotuba ya Wizara hakuna mahali palipoandikwa angalau neno la wanachuo wenye ulemavu au wanafunzi wenye ulemavu au watoto wenye ulemavu. Haya Matokeo Makubwa Sasa kielimu, tukishakuwa na makundi makundi na kuyaacha makundi yenye mahitaji maalumu, mimi sijui hayo Matokeo Makubwa Sasa yanakuwa ya kibaguzi ama yanakuwa ya namna gani? Nimesikitishwa na hilo, sielewi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Wizara hata kama watasema yanaenda Halmashauri sijui huko lakini Wizara mama ndio inatoa maelekezo na sera. Sasa kama mtoa sera na maelekezo amesahau hivyo, hata kutaja haya maneno hawa watekelezaji watatekeleza kutoka wapi? Mimi siwaelewi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hilohilo, siku zote nimesema kwamba watoto wenye ulemavu wanahitaji Walimu, wenye taaluma ya elimu maalum. Hata hivyo, jinsi walivyosahauliwa hakuna cha Patandi kwamba ina nini, Walimu hawa wanaandaliwa wapi? Bila maandalizi yao hawa watoto wenye ulemavu watafundishwa na nani? Wakati wa Bunge la Katiba tuliona hapa, tukapewa hata maelekezo, sijui mguso, ile anasomea Mwalimu maalumu jamani kuweza kuwafundisha hawa watu, hakuna kilichosemwa kuhusu mambo kama hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa kweli ni kusikitika tu. Ama nadhani hawakutajwa hawa wa sababu kulikuwa na suala la elimu jumuishi, mimi nauliza elimu jumuishi hivi mpango ule umeishia wapi? Je, mnafikiri utafanikiwa kwa namna gani kama hata wafundishaji wenyewe hawajaandaliwa, mimi hili nalo silielewi. Elimu jumuishi hata kama ipo haiwezi kutatua changamoto zote za watoto na wanafunzi wenye ulemavu. Moja, mpaka sasa hivi nimeshasema, kuna uhaba, ushindikani wa watoto kufika mashuleni. Majengo bado hayakidhi haja ya kuweza watoto hawa kuingia madarasani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niliambiwa kuna ramani maalumu zipo kutoka Wizarani zinazoelekeza Halmashauri kujenga madarasa ya namna gani, ramani zile zimeishia wapi kwa sababu hata majengo yanayojengwa sasa mbona hali ni ileile? Halafu tunasema Matokeo Makubwa Sasa hiyo ni habari ya ajabu kabisa. Kwa sasa kwa wengine lakini kwa wanangu mimi na wa kundi langu mimi hakuna, tunarudi nyuma maskini kama zamani. Nawasikitikia sana wanangu kwa sababu mimi niliokotaokota chochote nikafika hapa nilipofika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna changamoto ya Walimu wanaosaidia watoto hawa wenye ulemavu kutopata posho ya mazingira magumu. Tumesema hapa mazingira magumu kwa Walimu wote lakini Walimu wanaohudumia watoto wenye ulemavu jamani ni kazi nzito na sio wengi. Tatizo ni nini Serikali kuwapa moyo watu hawa wanaofanya kazi ya Mungu! Hawa wengine wanaenda kulaki watoto majumbani mwao kwa sababu wazazi wengine ukishalemaa wanasema eeh mzigo gani huu, haangaiki hata kumsomesha lakini Mwalimu mpendwa ndio anaenda kumbeba anamleta shule, anamsomesha, mnawasaidiaje hawa? Unajua mambo mengine yanaweza yakaniliza kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vitengo vya watoto wenye ulemavu vinavyosomesha hivyo vichache huko, hela ya chakula hawapelekewi kwa wakati hata kidogo, Walimu wanachangia eti kuwapikia uji. Kwa sababu kuna ulemavu kwa mfano wale watoto wenye matatizo ya ubongo, wale bila ka-uji katikati hapo hawakai darasani, pesa haziendi mnazifanyia nini? Hata za hao watoto yatima maskini wa namna hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalo lingine, mimi ni changamoto, ni kulialia tu. Naomba sana watoto wenye ulemavu ama watu wenye ulemavu katika ngazi zote, hivi Serikali ikiwasomesha bure inaona kazi gani? Wazazi wamehangaika na hivi viumbe, wakavipeleka shule vikasogea, mnaona shida gani kuwasomesha bure kabisa, ikawa ndio haki yao? Sio wengi hawa kwamba Serikali inashindwa kulipa. Naomba hilo liangaliwe na sio kuangalia tu litimize. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Elimu Tanzania niliona angalau ndio chombo kinatuonaona hata wenye ulemavu. Wakikusanya vijisenti huko wanatoa vifaa kwa watoto wenye ulemavu kwa ngazi zote tu za elimu tangu msingi mpaka wapi! Nilikuwa naomba kufahamu mwaka jana tulibadilisha Sheria kwamba wao wachangiwe zaidi ya asilimia mbili ya mapato ya nchi ili kuweza kuimarisha chombo hiki…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mwalimu Mkanga samahani muda hauko upande wako.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, haya nitaunga mkono nikipata majibu ya haya yote. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Peter Msolla atafuatiwa na Mheshimiwa Masoud Abdallah Salum.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakumbuka kwamba katika Mpango wetu wa Maendeleo kufikia mwaka 2025, Tanzania imejiwekea lengo la kuwa ni nchi yenye uchumi wa kati, ionekane na kutegemea kilimo lakini itegemee zaidi viwanda. Hiyo hatua ya kwenda kwenye viwanda tunahitaji kuwekeza zaidi kwenye elimu ili tuweze kutoa wataalam wetu ambao wanaweza kutoa hiyo huduma kwa urahisi hapa nchini. Tunachohitaji ni ubora wa elimu inayotolewa. Tunahitaji *quality*, hatuhitaji uwingi kwa maana ya *quantity*. Kwa hiyo, katika

mtiririko wote wa elimu kutoka huko chini mpaka vyuo vikuu umuhimu wa ubora wa elimu upewe kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuwe nchi ambayo itafikia uchumi wa kati ambayo itategemea viwanda ni lazima tuwekeze sana kwa upande wa sayansi yaani tuwe na *critical mass of scientist*. Kwa bahati mbaya sana nchi yetu ina upungufu mkubwa sana wa wanasayansi na ni katika kila maeneo, ukienda kwa madaktari, ma-*engineer* ni hivyo hivyo na maeneo mengine mengi. Kwa hiyo, kuna haja ya kuwekeza katika upande wa sayansi. Mathalani mwaka 2013 Walimu wa sayansi waliokuwa wanahitajika walikuwa ni 29,000 lakini waliopatikana walikuwa ni 2000 sawa na asilimia 6.7. Mwaka huu mahitaji yameongezeka, Walimu wa sayansi wanaohitajika ni karibu 36,000 lakini ambao wanategemewa kupatikana ni chini ya 2000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya yangu ya Kilolo mwaka huu tumepata Walimu 122 wa sekondari lakini katika hao tumepata Walimu tisa tu wa sayansi na katika sayansi hizo hakukuwepo hata Mwalimu mmoja wa *physics*. Vilevile hata mgawanyo wa Walimu wachache wa sayansi, nafikiri Wizara iangalie kwa sababu kuna sehemu wanakwenda wengi na kuna sehemu nyingine tunapata wachache sana. Ili tuweze kuwa na maendeleo ambayo yanafanana ni vyema Wizara ikaangalia hata hao wachache tunaopata basi mgawanyo wake uende sawia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada ambazo Serikali inafanya za kujenga maabara na kujitahidi kuwezesha sayansi kwa vitendo, bado kuna umuhimu wa Serikali kuangalia uwezekano wa kutengeneza vifaa vya maabara na kemikali hapa nchini badala ya kuagiza kutoka nje. Vile vinavyotengenezwa hapa nchini na bahati nzuri tuna rasilimali nyingi na nzuri, mimi na hakika vile vitakuwa na bei nafuu zaidi kuliko kuendelea kuagiza kutoka nje. Hivi sasa tunaagiza vifaa vingi kutoka Kenya hapa jirani tu na sisi tuna rasilimali kwa maana ya madini, gesi vitu vyote vipo. Kwa hiyo, ni jitihada ya Serikali kuingia ubia na mashirika mengine tuweze kutengeneza hivi vifaa hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupunguza uchache wa Walimu wa sayansi tunajua kwamba kuna Walimu wengi waliostaafu, Walimu wengi hao wa sayansi wako vijijini, wale ambao bado wana afya nzuri na wanaweza kufanya kazi vizuri, nashauri Serikali ione uwezekano ya kuwaajiri hao watu kwa mkataba, pale tunapopata watu wetu wenyewe basi tuweze kuwaachisha lakini kwa sasa hivi tuwatumie vizuri ili kusudi ili *gap* lililopo liweze kupungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kurudia ushauri wangu niliotoa kwa Serikali mwaka jana kwamba Wizara hii ni Wizara kubwa, ina mzigo mkubwa kutoka shule za msingi, chekechea, sekondari kwenda mpaka vyuo vikuu

nenda VETA, Wizara moja. Nashauri ule utaratibu uliokuweko huko nyuma wa kutenganisha elimu ya kawaida na elimu ya juu urudishwe ili kusudi Wizara hii iweze kutilia maanani, elimu ya chini, ya msingi, ya sekondari ambayo ndio msingi mzuri wa kuwapeleka vijana katika shule za sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wamezungumza mambo mengi lakini jambo la *VETA* ambalo lilikuwa ni kupeleka vyuo hivyo katika kila Wilaya, tunaomba jambo hili lijulikane kamili tuone utaratibu kwa sababu hata katika Wilaya yangu ya Kilolo licha ya kudai kwa zaidi ya miaka saba mpaka leo hii hatujapewa chuo cha *VETA* ambayo iingetoa fursa ya kipekee kwa vijana wetu kuweza kujiajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongeze lile walilozungumza walio wengi, wengine wamesema ni kutanua magoli, upangaji wa madaraja ya ufaulu wa kidato cha nne, nilizungumza wakati nachangia hotuba ya Waziri Mkuu. Mimi naona hili ni jambo la msingi vinginevyo tutaendelea kusomesha mbumbumbu wengi. Tuombe Wizara iangalie kwa umakini ili kuona kwamba upangaji wa madaraja unaleta *quality* kuliko *quantity* kama inavyoonekana sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango wangu huu, napenda kutoa shukurani zangu kwa kunipa nafasi hii ili hayo machache niliyoeleza ikiwa ni pamoja na kunitajia ni lini Kilolo itapata chuo cha *VETA* ili wananchi waweze kunufika zaidi. Ahsanteni sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Profesa Msolla. Kwa wasiomfahamu Prof. Msolla kwa miaka mingi alikuwa ni *Vice Chancellor* wa *Sokoine University of Agriculture*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim atafuatiwa na Mheshimiwa Meshack Opulukwa na Mheshimiwa Mwalimu Benardetha Mushashu ajiandae.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Ulikosea kidogo tu ungesema na Mwalimu Masoud Abdallah Salim. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kilio cha muda mrefu cha Walimu katika sherehe ya siku ya Walimu Duniani iliyofanyika Mtwara miaka michache iliyopita, Serikali iliahidi kwa kipindi kile na mgeni rasmi alikuwa ni Kiongozi Mkubwa tu akasema Serikali imekubali kupokea kilio cha Walimu cha kuwapatia Posho ya Kufundishia (*Teaching Allowance)*, hadi leo hamjatekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana kutosema kweli au uwongo ni jambo la kawaida lakini kwa Walimu kwa hili ningeomba sana mfikirie kwamba ile ilikuwa ni ahadi kule Mtwara siku ya Walimu Duniani kwamba Walimu

mtawapatia Posho ya Kufundishia (*Teaching Allowance)*. Naomba sana Waziri anapofanya majumuisho atueleze ni kwa nini zile ahadi za Posho ya Kufundishia (*Teaching Allowance)* ziliyeyuka ni sababu zipi za msingi zilizopelekea ziyeyuke na ni lini fedha hizo Walimu watapatiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Walimu wanalalamika sana juu ya jambo hili la posho ya mazingira magumu. Katika miaka miwili iliyopita ilikubalika kwamba Walimu watapatiwa shilingi laki tano lakini baadaye Serikali ikaja na hoja kwamba zile shilingi laki tano ni kwa baadhi ya Walimu wapya tu na siyo wale Walimu wengine, Walimu wapya waliokusudiwa kuajiriwa wale Walimu wakongwe hawakuwemo, fedha zile hazikutolewa na kukawa na malalamiko ya muda mrefu. Tuambiwe sasa juu ya fedha hizi za posho za mazingira magumu, Serikali mmejianga vipi kuweza kuwapatia Walimu ili iwe ni motisha kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Wizara ya Afya miaka michache iliyopita kulikuwa na posho ya mazingira magumu na ndiyo maana baadhi ya Madaktari na baadhi ya Wauguzi wengine waliokuwa wana hamu ya kwenda vijijini. Sasa hamuoni mkitoa fedha za posho za mazingira magumu itaweka motisha kwa Walimu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Ualimu, Naibu Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Jenista Mhagama wewe ni Mwalimu, herufi ya kwanza maana yake ni usumbufu, herufi ya pili maana yake ni adha, herufi ya tatu maana yake ni lawama, herufi ya nne inda, kila mwalimu ana jina na wewe Mwalimu Mhagama unalo jina, ya tano maana yake mahangaiko na mwisho ni uvumilivu na umaskini. Ninyi si Walimu na mimi Mwalimu mwenzenu? Huo ndiyo Ualimu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokaa hapa tusiwatendee haki Walimu, hili jambo halikubaliki. Posho ya nyumba hatuwapi, tuwapeni Walimu posho zao za nyumba ili wale ambao wamepanga fedha zao za mshahara wazitumie kwa matumizi mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, *transportation allowance*, (fedha za usafiri), jamani ni kawaida katika mataifa mengine fedha za usafiri au *bus fair* zinatolewa, kwetu hapa ni mshahara wake Mwalimu mwenyewe anaenda kazini anatoa mfukoni mwake ndiyo anapata nauli ya usafiri. Hili la posho ya usafiri kwa Walimu tuliangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu ajira mpya Mkoa wa Pwani waliajiriwa tarehe 1 Machi, 2013, waliripoti kazini, wakajaza mikataba lakini hadi leo hawajalipwa. Madai yao ni ya muda mrefu, Walimu hawa ni zaidi ya 100 kutoka

Mkoa wa Pwani. Waziri Shukuru Jumanne Kawambwa na Naibu wake Mwalimu Jenista Mhagama watuambie Walimu wale ambao waliajiriwa mwaka jana tarehe 1 Machi, 2013 ambao hamkuwapa mshahara wao wa mwezi ule na ni mwezi mmoja kamili, tatizo ni nini na kwa nini fedha zao msiwape? Malalamiko yamekuwa ni mengi. Nadhani Waziri atakapofanya majumuisho atawapa hamasa Walimu wale ionekane kwamba fedha zao zinapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za kupanda madaraja nazo hazitolewi, hata zikitolewa malimbikizo *(arreas)* zao vilevile nazo hazipatikani. Leo hii wanapanda madaraja Walimu fedha zao hazikutolewa, kesho kutwa wanapanda tena madaraja, zile fedha ambazo zimepita kwa kipindi kile hazitolewi, hili nalo ni tatizo, kuna malalamiko kweli. Kule Shinyanga nako kuna matatizo hayo ni mengi kwelikweli, ukienda kule Chato nako mengi kwelikweli, wanapanda madaraja Walimu fedha zao hazitolewi, hata zikitolewa *arreas* zao hazipatikani, wakipanda tena madaraja zile za nyuma zinasahauliwa. Suala hili limeleta malalamiko makubwa na hizo ni *Bad Results Now* (Matokeo Mabaya Sasa). Malalamiko ya Walimu yamekuwa ni makubwa, mjitahidi sana. Natumia lugha leo nyembamba kabisa ya kuwapendeni sana Walimu wenzangu, nawaheshimu sana lakini suala zima la fedha hizi za Walimu, za kupanda madaraja, madeni ya Walimu, kwa kweli inatia uchungu na elimu yetu ndiyo maana kila tukienda inaendelea kushuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule hazikaguliwi kwa wakati, shule hazina vyoo, shule zinafungwa, sijui kwa Jenista Mhagama kwao hakuna shule iliyofungwa? Nako tetesi zipo kwamba huko Peramiho kuna baadhi ya shule zimefungwa, hakuna vyoo, hazivutii. Kama hakuna bahati yako njema kweli lakini kuna shule vyoo vimeharibika tumeona kwenye runinga, havivutii na ndiyo maana wanafunzi katika hali kama hiyo wanashindwa kusoma. Naomba sana suala zima la vyoo liweze kupewa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pesa za kujikimu kwa vyuo vikuu hazitolewi …

*(Hapa kengele ililia kuashiria*
*kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Tena Mheshimiwa Masoud ile shule walisema iko karibu kabisa na kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama. *(Kicheko)*

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Ni hatari kweli, usikatae Mheshimiwa Jenista ndiyo mambo hayo.

**NAIBU SPIKA:** Lakini siyo Jimboni kwake ni Jimboni kwa Mheshimiwa Nchimbi. *(Kicheko)*

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo mambo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pesa za kujikimu kwa wanafunzi wa vyuo vikuu hazitolewi, maisha yamekuwa magumu, wanafunzi hawa jamani wanahangaika, wanatangatanga. Wanafunzi hawa wengine ni wa kike jamani hata wa kiume wafanye nini? Suala hili jamani mliangalie kweli, ni jambo moja kubwa sana. Wanafunzi hawa wa kike wanavyopata shida wanasema Serikali inataka tufanye nini? Kuna wengine wana Wabunge wao wanawapigia simu, wengine wanakutana nao angalau wanawasaidia, wengine maskini Wabunge wao pengine bahati mbaya hawapo inakuwa ni tatizo. Naomba sana Waziri na Naibu wake na yule wa TAMISEMI, Mheshimiwa Kasssim Majaliwa, naomba suala hili la fedha za kujikimu wanafunzi wa vyuo vikuu kwa wale ambao hawajapata waweze kupatiwa, nasikia wanaziita kwa jina la *boom*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nimalizie juu ya madeni ya Walimu. Madeni ya Walimu kama nilivyoongelea mapema ni vema liangaliwe kwa wakati wake, Walimu wapate fedha zao kwa wakati angalau na wao wajisikie, isiwe kila siku madeni ya Walimu yanaongezeka na Walimu pale ambapo wanataka kuchukua hatua mnakwenda Mahakamani. Kwenda Mahakamani siyo suluhisho, suluhisho ni kuwapatia fedha zao Walimu kwa wakati, wapate fedha za motisha, posho ya kufundishia mliahidi kule Mtwara miaka mitatu iliyopita na ilikuwa ni uongozi wa juu wa Serikali lakini hadi leo mliwadanganya Walimu wanalalamika na fedha za kupandishwa madaraja wapatiwe na fedha zao za nauli nazo pale ambapo wanadai waweze kupatiwa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na nadhani Waziri na Naibu wake kwa sababu nao ni Walimu na Mwalimu Kassim Majaliwa na yeye amefanya kazi zaidi ya miaka 20, nafikiri mkifanya majumuisho mtatoa majibu yaliyo mazuri, ya ufasaha na ya kuwatia moyo Walimu. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mwalimu Masoud Abdalla Salim, sikujua kama na wewe ni Mwalimu. Sasa anafuata Mheshimwa Meshack Opulukwa na Mheshimiwa Mwalimu Benardetha Mushashu.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami leo niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Waziri Mkuu anatoa hotuba yake kwenye ofisi yake, napenda kunukuu kwenye hotuba yake ukurasa wa 65

alisema, kutokana na kuwepo kwa malalamiko mengi kuhusu vyuo vikuu nchini kutoza ada tofauti kwa mafunzo ya aina moja, Serikali imekamilisha mwongozo wa gharama halisi ya kumsomesha mwanafunzi wa elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyuo vyetu vimekuwa na gharama kubwa sana kusomesha mwanafunzi anapokwenda kupata digrii iwe ya kwanza, ya pili au ya tatu. Upandishwaji holela huu umewafanya wazazi au wanaolipia gharama hii ya elimu ya juu kushindwa kuimudu hivyo kuishia njiani au kwa kuahirisha masomo kwa sababu gharama imekuwa ni kubwa sana na hawawezi kuimudu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kwamba pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu kuwa imeshakamilisha mwongozo kama hotuba yake ambavyo imesema kuhusu gharama za elimu ya juu za kumsomesha mwanafunzi lakini pia ingeenda mpaka chini ili kuweza kupata pia gharama halisi za mwanafunzi kuanzia kindergarten, *primary school* kwa sababu gharama ni kubwa sana na wenye shule hawa wamekuwa wakijipandishia ada kiholela na kuwafanya wazazi kuwa na mzigo mkubwa sana kuweza kumudu gharama za kusomesha watoto kwenye shule za *private*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la ukaguzi wa shule ambalo limeongelewa na wachangiaji walio wengi. Mwaka 2011 mwezi wa Februari nilipokuwa nikiuliza swali kwa Waziri wa Elimu kwamba ni lini sasa Halmashauri zetu zitapewa magari kwa ajili ya Idara ya Ukaguzi. Aliyekuwa Naibu Waziri wakati ule ambaye sasa si Naibu Waziri tena alisema kwamba Serikali ilikuwa imeshaandaa mpango na ilikuwa ipo kwenye mkakati wa kununua magari 19 kwa ajili ya ukaguzi nchi nzima. Pia Halmashauri ya Wilaya ya Meatu ilikuwa imeahidiwa gari wakati ule. Napenda kujua lile gari limefikia wapi kuanzia mwaka 2011 mpaka leo kwa sababu ili angalau shule zetu ziweze kukaguliwa tunahitaji haya magari ili yaweze kufanya kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya Walimu kwenye Halmashauri zetu, mimi naamini mengi yanachangiwa na watendaji wetu wa Halmashauri. Hivi karibuni Naibu Waziri Mwanri alikuja kwenye Halmashauri yangu na akawa anaongea na Baraza la Madiwani pamoja na watumishi wengine wakiwemo Walimu. Kilichokuja kujitokeza ni kwamba Walimu walikuwa wanadai haki zao au stahili zao ambazo ni za muda mrefu lakini Watendaji wa Halmashauri wakamwambia Naibu Waziri kwamba fedha zile zilikuwa tayari zimekwishalipwa na yale karatasi za madai zilikuwa zimeshapigwa muhuri wa *paid*. Naibu Waziri alishangaa kuhusiana na suala hili na akatoa maelekezo kwamba anadhani huo utaratibu siyo mzuri kama Walimu wanakuwa na matatizo ya kutokulipwa fedha zao au mapunjo ama vinginevyo ilikuwa ni vizuri wanafikisha matatizo yao kwa mamlaka inayohusika ili angalau tatizo la Walimu kutokulipwa fedha zao kwa wakati liweze kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongelea suala la *capitation*, suala la *capitation* limekuwa tatizo kubwa sana, kwanza ni fedha ndogo inakuja na haji kwa wakati. Napenda tu kutolea mfano kwenye shule mojawapo kwenye Halmashauri yangu. Shule hii ipo pale Mjini Mwanhuzi kwenye Halmashauri yangu kwa mwaka huu wa fedha ambayo ni kuanzia Julai 2013, mtoto alikuwa anaingiziwa na Serikali Sh.599.60 na shule hii ina watoto takribani 1070. Ukiangalia ule mgawanyo ambao Serikali imetoa kwenye fedha za *capitation* kwamba asilimia 30 fedha za ukarabati, asilimia 30 fedha za madaftari pamoja na zoezi la UMISHUMTA ambalo limeanza hivi sasa, asilimia 20 mitihani pamoja na mambo mengine, kumekuwa na mkanganyiko mkubwa kuhusiana na fedha hizi za *capitation* na hasa ile asilimia 30 ambayo ilikuwa inakwenda kwenye mitihani pamoja na madaftari.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakuwa na michezo ya UMITASHUMTA ambayo inategemewa kuanza hivi karibuni na kutokana na mwongozo sasa ambao umetolewa na ofisi ya Mkurugenzi ambao wameandikiwa Waratibu Elimu Kata na Walimu wa Shule za Msingi kwenye Wilaya ya Meatu ambayo nitapenda kuiwasilisha kwenye meza yako, inasema kwamba shule zinatakiwa zichangie fedha hizi na iandikwe *cheque*, inapoandikwa hii *cheque* aandikiwe Mwalimu mmoja ili aziwasilishe fedha hizi kwenye mamlaka inayohusika. Mimi naamini hapa ndipo wizi wa fedha hizi utakapoanza kujitokeza, kama anaandikiwa cheki Mwalimu ili aweze kuiwasilisha, haisemi aiwasilishe wapi, inasema aiwasilishe kwenye mamlaka inayohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichukulia kwa mfano shule hii ambayo ina wanafunzi 1070 kama nilivyosema ya Mwanhuzi shule ya msingi, ukichukua asilimia 30 ya ile fedha ambayo ni ya ukarabati pamoja na mambo mengine iliyokuja ni Sh.57,000 tu. Katika Sh.57,000 na ile asilimia 30 ambayo ni fedha ya madaftari pamoja na mitihani na chaki na kila kitu, kwenye Sh.57,000 iliyopatikana kwenye kipindi cha mwaka huu ugawanye utoe mambo ya mipira kwa ajili ya UMITASHUMTA, mpira wa miguu, mpira wa pete, mpira wa kikapu na mambo mengine, ambapo fedha hii kimsingi inanunua mpira mmoja tu labda mpira wa miguu au mpira wa pete. Kwa hiyo, fedha hii ni ndogo sana. Kama Serikali ilikuwa haijajiandaa kwa mambo ya michezo kwa watoto wa shule za misingi, suala hili napendekeza liweze kusitishwa kuliko fedha hii ambayo ni kidogo sana iendelee tena kutumika kwenye masuala ya michezo na kuweza kuwafanya Walimu Wakuu wa shule washindwe kutimiza majukumu yao jinsi inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ninayoyasema yameandikwa katika barua niliyonayo hapa ningependa pia kuiwasilisha katika meza yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tatizo la Maafisa Elimu mbalimbali katika shule zetu. Napenda kuongelea katika Halmashauri yangu kuna Afisa Elimu mmoja ambaye ni Afisa Elimu Sekondari. Afisa Elimu huyu wa Sekondari ambaye kwa jina anajulikana kama Charles Nkonde amekuwa akifanya *deal* na Wakuu wa shule kwa ajili ya kuweza kufuja mali ya shule na hasa fedha za matumizi ya shule zinapoingia katika shule zinazohusika. Amekuwa akifanya hivyo kama Walimu wa kawaida wanaendelea kuwa wanafuatilia matumizi ya shule kama yanakwenda vibaya, Mwalimu huyu amekuwa akitumia utaratibu aidha wa kuwahamisha au kuwaita kwenye ofisi yake kwa ajili ya kuwapa onyo kali au adhabu nyingine yoyote ambayo amekuwa akiona inafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kuna Mwalimu mmoja ambaye alikuwa anafundisha shule ya Sekondari ya Meatu. Baada ya kufuatilia mapato na matumizi ya shule ambayo yamekuwa yakija pale kwa muda mrefu na yanatumika isivyo na ile Kamati ya Shule ambayo kwa bahati mbaya sana Kamati ya shule hii Mwenyekiti a Kamati ya shule ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi wa Wilaya ya Meatu na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi wa Wilaya ya Meatu amekuwa ndiye Mzabuni wa kuleta chakula, kujenga hayo majengo, kuleta kuni pamoja na mambo mengine, hii ni *conflict of interest*. Ni vizuri sasa Afisa Elimu huyu ambaye sasa anatumia nafasi yake hii akishirikiana na Wakuu wa Shule kuwanyanyasa Walimu wengine, ndiyo maana hata elimu inashuka kwa sababu Walimu wanakosa ile *morale* ya kuweza kufundisha kutokana na matatizo yaliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wizi huu unaofanywa katika shule hii na Walimu ambavyo wamekosa ile *morale* ya kuweza kufanya kazi na kwa sababu Walimu wanahamishwa bila utaratibu. Kuna Mwalimu ambaye amehamishwa mwezi wa kwanza. Mimi nilikuwa sijui, utaratibu unasema kwamba ili Mwalimu aweze kwenda katika eneo lingine ni lazima awe ameshalipwa hela yake kabla. Sasa Mwalimu amehamishwa tangu mwezi wa kwanza, hajaingia darasani hata huko alikoenda kwa sababu hajapewa stahili yake ya uhamisho na leo hii shule ile haina Mwalimu tena ni Mwalimu wa Sayansi, Mwalimu wa *biology* lakini lengo ni kumkomoa tu huyu Mwalimu kwa sababu tu anafuatilia mapato na matumizi ya shule. Napenda katika majumuisho ya Waziri atakapokuwa analiongelea suala hili aweze kutoa tamko kwa Watumishi wa Halmashauri na hasa Maafisa Elimu wanaotumia nafasi zao vibaya kuwanyanyasa na kuwagandamiza Walimu wa ngazi za chini.

Mheshimi Naibu Spika, kuna suala la Walimu kutokulipwa fedha zao za malimbikizo. Kuna Walimu ambao walipanda madaraja mwaka 2010 katika

Halmashauri yangu ya Meatu lakini hawajawahi kulipwa hizo fedha zao mpaka hivi tunavyoongea. Wamenituma na wameniomba sana Waziri mwenye dhamana ya Elimu uweze kusaidia kutatua suala hili kwa sababu limekuwa ni la muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kutokulipwa fedha hizi, pia wana matatizo ya fedha zao za likizo ambazo ni za muda mrefu sana. Waliokwenda likizo mwaka juzi, mwaka jana hawajalipwa, kuna baadhi waliolipwa nusu lakini hata wale wanaoanza likizo kuanzia mwezi wa saba mwaka huu wana wasiwasi kwamba inawezekana hata fedha zao zisilipwe tena kwa sababu kumekuwa na ubabaishaji katika malipo na stahili za Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwalimu Benardetha Mushashu atafuatiwa na Mheshimiwa Lekule Laizer.

**MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze na mimi kuchangia. Kwanza kabisa, nampongeza Waziri na Naibu Waziri kwa hotuba nzuri na Watendaji wote nawapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, malalamiko ya Walimu yamekuwa ya muda mrefu sana. Hawalipwi mishahara yao na stahili zao kama za likizo, matibabu na malimbikizo ya nyongeza za mishahara. Mnajijengea uhusiano mbaya sana na Walimu pasipo na sababu. Sijasikia kada nyingine ya wafanyakazi ambao wanafanyiwa hivyo. Serikali mnajitahidi, mnalipa malimbikizo lakini mwaka unaofuata tunasikia bado kuna malimbikizo ya Walimu. Je, ni nani anasababisha kuendelee kuwa na malimbikizo ya Walimu? Kwa nini asichukuliwe hatua. Napenda kujua ni lini mishahara ya kutosha na stahili za Walimu zitalipwa na hayo malalamiko yaweze kwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoani Kagera tuna wanafunzi wengi ambao wamehitimu darasa la saba, waliohitimu kidato cha nne lakini hawakuweza kuendelea. Wanapenda shule, wanapenda kujiendeleza kwa kupitia ufundi. Mkoa wa Kagera hauna Chuo cha *VETA*. Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri ni lini mtatupa Chuo cha *VETA* cha Mkoa wa Kagera? Hapa nitawaomba Waheshimiwa muweze kutupa jibu linaloridhisha mtakapokuja kujibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Elimu iliyopo inahamasisha sekta binafsi waweze ku-*invest* katika elimu na kweli waliwashawishi na wamejenga shule mengi sana. Sasa hivi kila unapopita unakuta kwamba kuna malalamiko, wanasema kodi zimekuwa kubwa. Mimi najiuliza je, bila sekta binafsi Wizara ya Elimu au Serikali peke yake wataweza kumudu idadi kubwa ya wanafunzi waliopo? Ni lini sasa Serikali itachukua hatua iwaite watu wa shule binafsi, mkae pamoja, mjadili yale matatizo yao na muangalie namna ya kuwapunguzia hizo kodi kusudi waweze kuendelea kutoa elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa mambo mawili. Kwanza, umebahatika umepata majembe mawili katika Wizara yako, wa kwanza ni mama mahiri sana, mchapa kazi, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Naibu Waziri wako lakini wa pili ni Katibu Mkuu wako Profesa Mchome. Mtu mwenye *vision* ya hali ya juu na ambaye anafanya kazi bila kuchoka. Kwa hiyo, najua hii mipango mizuri niliyoiona humu ikitekelezeka, najua Wizara hii ina changamoto nyingi lakini mambo yataendelea kuwa mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niwapongeze vilevile kwa jinsi mnavyozidi kuongeza Walimu, mwaka huu inaonekana kwamba mtaajiri Walimu 36 lakini nasema bado haitoshi. Hizo jitihada inabidi ziendelee kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu wa ngazi ya cheti hadi mwaka 2013 walikuwa wanajifunza masomo 13 kwenye vyuo vya ualimu. Wakitegemewa kwamba watakaporudi shuleni waweze kufundisha masomo 13. Hata nyie hapa hata kama una akili namna gani huwezi kujifunza masomo 13 yote ukayaelewa vizuri na ukaenda ukayafundisha huko shuleni. Ndiyo maana watoto hawa-*perform* kwa sababu Walimu wenyewe wanakuwa hawajaelewa masomo vizuri, wanapokwenda kufundisha kule hawafundishi. Sioni kwa nini umlazimishe Mwalimu asome masomo 13 akiwa kwenye Chuo cha Ualimu. Ukiangalia wanaosoma diploma au digrii wanasoma kati ya masomo mawili mpaka manne. Kwa nini hata hawa Walimu wa cheti wasipunguziwe masomo wakawa wanasoma masomo matatu au manne kusudi wakayaelewa vizuri wakitoka hapo waende kufundisha vizuri huko shuleni, ni lini mtabadilisha hali hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Wizara ya Elimu kuendelea kuajiri Walimu kama nilivyosema, lakini hadi mwaka juzi kulikuwa na matatizo makubwa sana ya Walimu kwa sababu shule nne katika Tanzania zilikuwa na Mwalimu mmoja mmoja. Tulikuwa na shule 17 zilikuwa na Walimu wawili wawili tu katika shule hizo. Tulikuwa na shule 56 zilizokuwa na Walimu watatu watatu na tulikuwa na shule 104 zilizokuwa na Walimu wanne wanne. Hii ina maana gani? Ina maana kwamba watoto walio katika shule hizi walikuwa wanashinda

tu shuleni, wanapiga kelele, wanacheza, wanaenda kufanya kazi nyingine badala ya kusoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoani Kagera shule nyingi bado zina Walimu wachache ambao hawakidhi mahitaji ya kila somo. Kuna upungufu mkubwa sana katika masomo ya *science, physics, chemistry, biology* na *mathematics.* Serikali ina mpango gani wa kumaliza tatizo la Walimu wa sayansi nchini na kuwapnga katika shule ili waweze kufundisha hisabati na masomo ya sayansi ipasavyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa *TSD,* wapo Walimu nchini ambao hawajaajiriwa lakini wapo shule wanafundisha kwa takribani miaka 10, 15 mpaka 20. Walimu hawa walitokana na mfumo ambapo wakimaliza vyuo kabla ya matokeo ya mitihani wakapangiwa shuleni. Matokeo yalipotoka wakajikuta labda hawakuweza kufaulu somo moja au mawili katika yale waliyokuwa wanasoma lakini Walimu hawa wameendelea kuwa shuleni, wanafundisha, wanalipwa mishahara japokuwa hawajaajiriwa rasmi na hii inakiuka utaratibu wa masharti ya utumishi wa umma. Napendekeza hawa Walimu watambuliwe haraka iwezekanavyo, warudie mitihani ile ambayo hawakuweza kufaulu na ajira zao lakini zianze pale pale walipoanza kazi kwa sababu siyo kosa lao. Yeye anajua ni mwajiriwa kwa sababu anaona anaendelea kulipwa mshahara kumbe akija kustaafu anashtukia hana mafao. Kwa hiyo, naomba muwatambue, wafanye hiyo mitihani, wasafishe vyeti vyao kusudi waweze kuendelea kuajiriwa na watakapostaafu waweze kulipwa mafao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa la Walimu kuhudumiwa na chombo zaidi ya kimoja. Walimu wanaajiriwa na kulipwa mishahara na TAMISEMI ambayo ni Halmashauri lakini mambo ya nidhamu, usajili, upandishwaji wa madaraja, wanashughulikiwa na *TSD*. *TSD* iko kwenye Ofisi ya Rais, Manejimenti ya Utumishi wa Umma. Kwa hiyo, unakuta ni vigumu, mimi nakuajiri, nakupa mshahara lakini kwenye nidhamu ni mtu mwingine na huyu ambaye anaangalia nidhamu yako siye anayekupa mshahara. Inakuwa ni tatizo ndiyo maana unaona matatizo ya Walimu hayaishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile *TSD* ya sasa hivi haiwezi kutatua changamoto zilizopo za sasa, shule zimekuwa nyingi sana na wanafunzi na Walimu wamekuwa wengi sana na hasa ukizingatia kwamba *TSD* haina ofisi katika Mikoa mipya minne na katika Halmashauri zaidi ya 37. Sasa huko ambako hakuna ofisi nani anashughulikia nidhamu za Walimu? Vilevile mpaka mwaka jana kulikuwa na kesi zaidi ya 1,000 za nidhamu za Walimu ambazo zimeshindwa kushughulikiwa na kulikuwa na Walimu zaidi ya 31,687 ambao wameshindikana kupandishwa madaraja kwa sababu ya *TSD* kukosa kukosa

fedha za kuitisha vikao. Nachosema ni kwamba wakati umefika sasa tuwe na chombo kimoja ambacho kitakuwa kinashughulikia matatizo ya Walimu. Waziri anapohitimisha aniambie ni lini Serikali itakubali kuanzisha hicho chombo cha kushughulikia matatizo ya Walimu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wazazi wamejivua wajibu wao wa msingi wa kulea watoto wao. Mtoto akishindwa mitihani inasemekana ni Mwalimu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mwalimu Benardetha Mushashu.

**MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana. Mheshimiwa Michael Lekule Laizer.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ambayo nimeikosa kwa muda mrefu, nimejinyamazia.

**MBUNGE FULANI:** Pole sana.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Kwa hiyo, nakushukuru sana kunipa nafasi hii niseme machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka kuzungumzia ukosefu wa elimu kwa wanafunzi walioko vijijini ambayo imeonyesha tabaka kubwa sana kati ya watoto wa viongozi, kati ya watoto wa matajiri na watoto wa wazazi walioko vijijini ambao hawana uwezo. Nadhani viongozi wengi walioko hapa na Wabunge watoto wao hawapo katika shule tunazozungumzia, wako *international schools,* wao ndiyo wamejaa vyuo vikuu, watoto wa wazazi tunaowazungumzia hapa wa vijijini, hawana elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashindwa kuunga mkono Wizara hii. Mimi nitaungaje mkono Wizara hii na watoto wa Jimbo langu walioko katika shule za Kata wote wamefeli? Hivi nikiunga mkono watanionaje, wananiona kwamba mimi ni mnafiki na siwezi kuunga mkono kwa sababu kuna matatizo mengi sana ambayo tunayasema kila siku. Hawana maabara, hawana *library*, hawana Walimu, Walimu wawili, watatu ndiyo wanafundisha shule. Hivi hawa wanafunzi kwa miujiza gani watafaulu waende chuo kikuu. Ukitaka uthibitisho nenda katika vyuo vikuu vyote vilivyoko nchini kuna baadhi ya makabila ambayo hayapo. Sasa haya makabila ambayo hayapo hata vyuo vikuu na ni

Watanzania na sisi ndiyo viongozi tunaowawakilisha, hivi tunaweza kweli tukasema tuko katika elimu ya Tanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu nenda uangalie wingi wa Wamasai walioko katika vyuo vikuu, wingi wa Wabarbaig walioko katika vyuo vikuu. Sasa limetokea tabaka kubwa sana la watu wenye elimu na watu ambao hawana elimu, wamejazana vijijini, ni Watanzania, ndiyo hao wanafunzi ambao hawajui kusoma na kuandika, wamemaliza darasa la saba, wote wanaomaliza *form four* wanarudi nyumbani, hivi hawa Watanzania wote watafanya nini? Baadaye wataongozwa na watoto wa wakubwa na watoto wa matajiri, ndiyo nchi hii tunavyoipeleka. Hivi tunawazungumzia watoto ambao huko vijijini ndiyo wamewapa kura na ndiyo baadaye watawapa kura lakini wenu wako katika shule zenye nafuu hata hawasomi katika vyuo vikuu vilivyoko nchini wako nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo jambo limeniuma mimi mpaka nikakataa kumpeleka mtoto wangu hata mmoja katika *international schools* pamoja na kwamba nina uwezo. Nimeshindwa kuwatenga na watoto wa wazazi wengine ambao nawaongoza mimi. Watoto wangu wote wamesoma katika shule za Kata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuangalie jambo hili kwa sababu ni la hatari. Ni afadhali sasa katika bajeti hii ziara zote zifutwe za Mawaziri na Wabunge, hakuna tena kusafiri kwenda nje, bajeti hiyo irudi katika shule za Kata. Pamoja na matumizi mengine ambayo hayafai, yote yarudi katika shule za Kata tuimarishe wawe na maabara, wapate Walimu, wawe na *library* ndiyo tunaweza tukanyanyua hili tabaka ambalo tumeliacha nyuma. Hata ukienda Kongwa kuna shule ambazo hazina maabara pamoja na kwamba chuo kikuu kiko hapa, inawezekana Wagogo wengi hawapo. Ni wachache, Wagogo waliopo ni Wagogo wa matajiri, Wagogo ambao ni watoto wa viongozi. Kwa hiyo, naomba tuangalie jambo hilo kwa sababu ni hatari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni suala la vyuo vya *VETA*. Mimi tangu mwaka 2000 Mheshimiwa Kapuya alipokuwa Waziri wa Elimu, naahidiwa kwamba *VETA* itajengwa, tulikuwa katika shule 28, akiingia Waziri mwingine anaiondoa Longido, kwa hiyo, kila Waziri anayeingia anaiondoa Longido. Mheshimiwa Waziri uliniahidi mwaka uliopita na aliyekuwa Naibu wako alijibu hapa kwamba ni lazima Longido mwaka huu itakuwa katika shule tano. Hizo shule tano zilizokuja kipindi hiki Longido imeondolewa imewekwa shule zingine ambazo hazikuwepo. Huu upendeleo jamani angalieni kwa sababu ni hatari sana.

Mwisho, tuna shule ya Longido ya wasichana, niliomba kwa muda mrefu shule hii ipatiwe gari. Shule ipo mbali sana kilomita 100 kutoka Longido.

Wakiugua hakuna gari ya kuwapeleka hospitalini na hospitali haipo katika kijiji hicho na ni moja kati ya shule za Kata. Tulisema hebu tuwapeleke wasichana wakae wenyewe tuangalie kama wasichana wa Kimasai wataendelea. Naomba kwa upendeleo huo jamani mnisaidie hiyo shule ipate gari.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kukushukuru sana kwa kunipa nafasi lakini naomba shule za Kata, kipindi hiki Serikali iondoe fedha zote za usafiri wa viongozi wasiende nje hizo shule za Kata zipate *library* na maabara. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kufuatana na muda wetu mtaona muda hauko upande wetu. Niwashukuru kwa uchangiaji, kwa kweli mnaotaka kuchangia Wizara hii bado mko wengi.

Ni kazi kweli hata jinsi gani jioni tutafanya lakini naomba wale ambao wako kwenye orodha yangu basi muwahi kufika saa 10 ile. Maana mkifika tu mimi nita-*tick* wale ambao wako tayari na nitawapa kipaumbele. Asubuhi hii wamechangia watu kama 16 na tutapata kama watu 10, 13, 14 jioni kadri muda utakavyoruhusu.

Baada ya hapo tutakuwa na dakika 10 kwa Mheshimiwa Naibu Waziri (TAMISEMI), dakika 10 Waziri wa TAMISEMI, dakika 20 Mheshimiwa Naibu Waziri Elimu, dakika 30 Mheshimiwa Waziri. Itakuwa jumla kama dakika 70 kwa ujumla wenu wote.

Mheshimiwa Waziri katika kumalizia na mimi niseme tu kwamba tumeshakaa wadau wa elimu Mkoa wa Dodoma tukajadiliana sana kwa nini Mkoa wetu haufanyi vizuri. Moja ya mambo ambayo tuliyaona ni ukaguzi kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge nakusisitiza sana. *(Makofi)*

Ushauri wetu sisi ulikuwa ni kwamba Wizara ikubali kwamba Idara ya Ukaguzi iende TAMISEMI. Ukiipeleka Idara ya Ukaguzi TAMISEMI asilimia 80 ya matatizo yake yanaisha lakini mkiendelea kusisitiza ibaki huku iliko itakuwa kila mwaka tukija hapa tunaongelea habari ya ukaguzi, ukaguzi, ukaguzi. Basi nimeona na mimi nifikishe fikra hizo za wadau wa elimu Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Baada ya maelezo hayo, naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi hadi saa 10.00 jioni ya leo.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyoahidi asubuhi, nitaangalia kwenye orodha yangu hapa, wale mliowahi mtapata kipaumbele. Nimwite Mheshimiwa Abdallah Njwayo. Mheshimiwa Njwayo hayupo? *Okay!* Kachelewa huyu! Mheshimiwa Said Mtanda anza, niangalie wale waliowahi.

**MHE. SAID M. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha tena kuchangia Hotuba hii ya Wizara ya Elimu. Nitumie fursa hii pia kuwapongeza Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari kwenye Jimbo la Mchinga, kwa kazi kubwa wanayoifanya katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, nimpongeze Mheshimiwa Mama Salma Kikwete, kwa kazi kubwa anayoifanya katika Sekta ya Elimu na hasa katika Mkoa wa Lindi. Tunapongeza kwa juhudi zake za kuanza mchakato na hatimaye ujenzi wa shule kubwa ya kisasa ya wasichana pale Lindi. Sisi tutamuunga mkono na nina imani Wapiga Kura wangu wa Jimbo la Mchinga, wasichana, watapata fursa ya kusoma katika shule hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nijipongeze mimi mwenyewe kwa sababu pia nimekuwa mchango mkubwa katika Jimbo langu, hasa katika kuboresha Sekta ya Elimu katika Jimbo la Mchinga. Kwa kushirikiana na Wananchi wa Jimbo la Mchinga, mwaka huu nimetafuta madawati 300 ambayo tutayagawa kwenye Shule za Msingi na Sekondari. Ningependa Mheshimiwa Waziri akubali kuja Jimbo la Mchinga kujionea changamoto za elimu, lakini pia kuweka Jiwe la Msingi katika Shule ya Awali Uleka na Kipunga na Shule ya Awali Kitohavi, ambazo tumeziboresha sana kwa juhudi kubwa za Mbunge na Wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea na Bajeti hii ya Wizara ya Elimu, kwanza, niwapongeze Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Waziri, Dkt. Kawambwa, kwa kazi kubwa wanayoifanya. Tunatambua mazingira magumu yaliyoko katika Wizara hii ya Elimu na changamoto nyingi ziliziko katika Sekta ya Elimu. Ninawataka wasife moyo, waendelee kufanya kazi zao kwa uadilifu na umakini mkubwa, kwa sababu changamoto za elimu ni nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia Bajeti ya mwaka jana, mtakubaliana na mimi kwamba, fedha ambazo tuliziomba kwa ajili ya Wizara hii nyingi hazikufika, hususan fedha za Miradi ya Maendeleo. Wamepata shilingi bilioni sita tu fedha za ndani, kati ya bilioni 18 zilizoombwa, lakini pia fedha za nje wamepata bilioni nane kati ya bilioni 53 zilizoombwa; utafanya nini? Utekelezaji wa MMEM II hauwezi kufanyika katika mazingira ya namna hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, bado tunayo haja kubwa ya kuhakikisha bajeti ya Wizara inapanda badala ya kushuka mwaka hadi mwaka, jambo ambalo linasababisha kudidimiza kabisa elimu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie pia kuhusu vipaumbele vilivyowekwa. Ukisoma Hotuba ya Waziri, ukurasa wa 49, utaona vipaumbele vya Wizara vilivyowekwa katika awamu hii ni kuinua ubora wa elimu, kuongeza upatikanaji elimu kwa usawa, yaani wanawake, wanaume, waweze kupata haki sawa katika elimu. Ninajiuliza kwamba, yako mambo na matatizo makubwa na changamoto kubwa sana katika mfumo wetu wa elimu; ni kwa nini Wizara haijaamua kuja na vipaumbele hasa vinavyolenga kuboresha mazingira wezeshi kwa Walimu kuweza kutekeleza wajibu wao?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, ukienda ukurasa wa 45 wa Hotuba hii ya Bajeti, kuna upungufu mkubwa sana wa Walimu wa Sayansi. Kwa hiyo, nilifikiri miongoni mwa vipaumbele ambavyo Wizara hii ingeweka kwa mwaka huu ni kuangalia ni kwa namna gani tunaweza kuongeza idadi ya Walimu wa Sayansi na masomo mengine, ili wanafunzi katika Shule mbalimbali za Msingi na Sekondari wapate fursa ya kujifunza na kufundishwa, hatimaye waweze kufanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma ukurasa wa 45 wa hii Bajeti, utaona mfano, Somo la *Agriculture* kwenye mahitaji ya Walimu wa Sayansi, mahitaji halisi ni Walimu 905, waliopo Walimu 300, upungufu Walimu 605, sawa na asilimia 66. Kwa hiyo, unaweza ukaona hali ilivyo. Ninajaribu kutoa mifano michache tu, ukiipitia Hotuba utaona mifano mingi; Somo la *Physics* mahitaji ya Walimu ni 10,203 waliopo ni Walimu 3,748, upungufu ni Walimu 6,455.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mazingira haya, ninajiuliza ni kwa vipi na kwa namna gani tunahitaji watoto wetu waweze kufanya vizuri kwenye masomo ya sayansi? Maeneo ya Shule za Sekondari kama vile Kitomanga, kuna Mwalimu mmoja wa Sayansi, Shule ya Sekondari Mipingo kuna Mwalimu mmoja wa Sayansi, Shule ya Sekondari Matimba, Shule ya Sekondari Mvuleni, Milola na hata kule Rutamba, zina upungufu mkubwa wa Walimu wa Sayansi. Kwa hiyo, ninaomba suala la kuandaa na Mpango Mkakati wa kuwezesha upatikanaji wa Walimu wa kutosha uwepo, ili shule zetu ziweze kuwa na idadi kubwa ya Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukaguzi wa shule; mwaka jana Shule za Msingi zilizotarajiwa kukaguliwa ni 7,200, lakini zilizokaguliwa ni 3,835 tu. Shule za Sekondari 4,000 zililengwa kukaguliwa, lakini hadi mwaka unakwisha shule 1,577 ndizo zilizoweza kukaguliwa. Ofisi ya Elimu pale Lindi, Mkaguzi na Afisa Elimu Msingi hawana vitendea kazi, hawana pikipiki, hawana magari, kwa hiyo,

naomba Wizara hii ihakikishe vitendea kazi vinapatikana. Mkaguzi pale Lindi apate pikipiki na Afisa Elimu Msingi, ili waweze kusimamia shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Shule ya Msingi Dimba, nyumba za Walimu zinakaribia kudondoka, mazingira ni magumu sana. Shule ya Msingi Namkongo, shule ambayo nyumba ya Mwalimu imeezekwa kwa nyasi, shule ile nyumba ya Mwalimu imejengwa kwa matope. Unamhitaji Mwalimu afanye kazi kwa moyo, itawezekana vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko shule nyingine kwa sababu ya kutokaguliwa, tumeweza kujionea wenyewe wanafunzi wanakaa kwenye madarasa hakuna sakafu. Kwa hiyo, ningependa kuiomba Wizara hii ihakikishe kwamba, suala la ukaguzi linapewa kipaumbele kwa sababu ndilo litakalotuwezesha kubaini matatizo na changamoto zilizopo, ili tuweze kulipatia ufumbuzi suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kwa kuomba sana utekelezaji wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM). Matokeo yanaonesha dhahiri kwamba, kwa mwaka 2007/2008 malengo yalikuwa kujenga madarasa 45,000, yaliyojengwa ni 6,000. Nyumba za Walimu 2008/2009, malengo yalikuwa ni kujenga nyumba 89,000, zilizojengwa ni 4,700 tu. Vyoo, mwaka 2010/2011 ilitarajiwa vijengwe vyoo 127,950, lakini hadi mwisho vilivyojengwa ni 3,200. Kwa hiyo, tunapoachana na Mpango huu wa MMEM II, sasa hivi tunajiuliza tunaelekea Mpango mwingine wa MMEM III; utekelezaji katika MMEM II haukufanyika, umefanyika chini ya asilimia 50, tunaendaje sasa kuibua na kupanga Mpango mpya wa MMEM III? Tutekeleze lipi wakati haya ya nyuma tumeshindwa kuyatekeleza?

Kutokana na kutojengwa nyumba hizi za Walimu, ndiyo maana maeneo mbalimbali ya Jimbo langu niliyoyataja yamekumbwa na upungufu mkubwa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. SAID M. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja, lakini pia ningependa kupata maelezo ya kina katika haya niliyoyasema. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Said Mtanda, tunakushukuru. Mheshimiwa Al-Shaymaa Kwegyir, atafuatiwa na Mheshimiwa Margaret Sitta!

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema, kwa kuweza kusimama tena katika Bunge lako Tukufu. Sikuwepo kwa muda wa

kama miaka miwili hivi, leo nimesimama; Mwenyezi Mungu ni Mkubwa, nashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa na mikakati mbalimbali ya kutoa elimu kwa watu wenye ulemavu, lakini changamoto nyingi bado zipo kwenye kundi hili la watu wenye ulemavu. Kikubwa kilichonistua ni kwamba, kwenye Hotuba hakuna sehemu niyoona imezungumzia masuala haya ya watu wenye ulemavu, labda sentensi moja au mbili, sidhani, nimetafuta sana sikuona. Kwa kweli, nimeshituka sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa la uhaba wa nyenzo za kufundishia na za kujifunza kwa watu wenye ulemavu. Tatizo hili linatokana na Serikali kutotoa fedha. Ninakumbuka fedha za kununulia nyenzo hizo hazijatolewa kwa muda wa miaka minne mfululizo. Bajeti ya mwaka jana ya Elimu, zilitengwa milioni 750 kununulia vifaa vya kugharamia elimu kwa ajili ya watu wenye ulemavu, lakini zilizotolewa ni milioni 150 kati ya hizo. Cha ajabu ni kwamba, hizi nyingine zimekwenda wapi? Hilo linasikitisha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni ukosefu wa nyenzo, vifaa vya kuwaandaa Walimu wa Elimu Maalum. Hili nalo ni tatizo, kuna chuo pekee Mama Margareth Mkanga amekitaja, Chuo cha Patandi ambacho kipo Arusha. Hakuna fedha yoyote inayopelekwa kwenye chuo hiki na matokeo yake Walimu wanaomaliza katika Chuo hicho wanakuwa hawana uwezo wa kuwafundisha watu wenye ulemavu, hawa-*qualify,* wanababaisha babaisha tu. Sasa matokeo yake, kwenye shule za watu wenye ulemavu kunakuwa hakuna Walimu na ndivyo ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutopkuwepo kwa usalama wa kutosha katika shule; kuna shule za vitengo kwa mfano Shule ya Tanga Jiji, kuna Shule pale Pongwe ina watoto wenye ulemavu wapatao 71. Sasa katika hawa watoto 71, kuna watoto 42 wenye ulemavu wa ngozi, shule ile haijazungushiwa uzio ipo tu wazi na mnajua tatizo lililopo kwa watu wenye ngozi kama ya kwangu. Tatizo linajulikana tunawindwa kwa ajili ya kuuawa. Pale hakuna uzio kinachofuata ni nini? Ni wale watoto kuvamiwa kwenda kuchinjwa na kukatwakatwa. Kwa hiyo, ninaomba shule ile iwekewe *fence* ya uhakika kwa ajili ya usalama wa wale watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni uhaba wa Walimu niliousema wenye uwezo wa kufundisha watoto wenye ulemavu. Tatizo hilo lipo na mfano ni uwezo wa kutumia lugha ya alama. Walimu wa lugha ya alama hatuna, wapo wachache sana. Kwa hiyo, hili ni tatizo kubwa na ni kutokana na hizo shule zenyewe hazipatiwi fedha; kwa hiyo, hakuna Walimu wanaokwenda kwenye zile shule, elimu inayopatikana pale si ya kutosha, matokeo yake hakuna Walimu wa Elimu Maalum. Hilo Mheshimiwa Waziri analijua, nimeshamfuata

mara kadhaa, nashukuru nawaona mkienda kwenye hizi shule. Nimemwona Mheshimiwa Naibu Waziri, alipoteuliwa tu, alienda kwenye shule za watu wenye ulemavu. Nashukuru kwa hilo, umejali, lakini tunaomba ziongezeke nguvu zaidi; pesa hizi zinakwenda wapi? Zinachomekwa sehemu nyingine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ina maana suala la watu wenye ulemavu halijapewa kipaumbele kama yanavyopewa kipaumbele masuala mengine. Tunaomba masuala ya watu wenye ulemavu yapewe kipaumbele pia. Chuo cha Patandi kama nilivyosema, tunaomba kiboreshwe; hilo ni pendekezo ambalo ninaomba Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri mlifanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninaloomba, Vyuo vyote vya Ualimu vya hapa nchini vijumuishe Somo la Elimu Jumuishi. Elimu Jumuishi ni elimu ambayo inachanganya watu wenye ulemavu na ambao hawana ulemvu, wanachanganywa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, lakini siyo mwisho kwa umuhimu, naomba nirudi kwenye eneo langu nililozaliwa, Muheza. Muheza tuna tatizo, hatuna Walimu, tunaomba maabara. Niseme haraka haraka, Walimu bado wanadai madeni yao Muheza. Tunaomba Mheshimiwa Waziri, alisikie hilo. Kama nilivyosema, madawati ni tatizo nchi nzima na sisi Muheza pia hilo tatizo tunalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi uliyonipatia, sina mengi, sipendi kengele inigongee. Kwa hayo, machache naomba Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, suala la watu wenye ulemavu mwone umuhimu wake. Katika vipaumbele vya Wizara na masuala ya watu wenye ulemavu yapewe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana. Mheshimiwa Mama Margaret Sitta, atafuatiwa na Mheshimiwa Ramo Makani!

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Naishukuru Kamati ya Huduma za Jamii, kwa ushirikiano wao, mimi nikiwa Mwenyekiti. Namshukuru pia Makamu Mwenyekiti, aliyesoma Taarifa kwa niaba yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mengi ambayo ningezungumzia, lakini Kamati yetu imeyaweka. Kwa sababu ya muda, nitaongelea masuala machache sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu iliona umuhimu kwanza wa kuipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa kuja na Mpango Maalum unaoitwa Matokeo Makubwa Sasa; tunawapongeza sana. Wakati huo huo tunaamini kwamba, yako mengine muhimu ambayo yanatakiwa yafanyiwe kazi, ili huu mpango uweze kufanikiwa.

La kwanza, ni kuangalia Walimu wenyewe ambao wanafundisha darasani.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapozungumzia shule, unaanza na Walimu na Wanafunzi, ndiyo maana ya elimu, mengine yote yanafuata. Walimu ndiyo watu wa kwanza kabisa kuwaangalia katika kufanikisha Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu hawawezi kufundisha vizuri kama wanakwenda kudai madai yao Halmashauri; wanaacha kufundisha wanakwenda Halmashauri kudai mishahara imechelewa, kudai fedha zao mishahara yao haijarekebishwa au kwenda kudai hawajapandishwa madaraja. Yote haya yanatokana na mfumo wa kuhudumia Walimu ulivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naamini Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi ina masikio na inaelewa, wasikivu wanaelewa; ninaamini kwa hili watanielewa. Bahati nzuri mimi mwenyewe ni Mwalimu, nimefundisha zaidi ya miaka 20, lakini pia nilikuwa Afisa Elimu wa Wilaya, naelewa Walimu wanavyopata matatizo. Niwahi pia kuwa Rais wa Chama cha Walimu kwa karibu miaka kumi. Mimi mwenyewe nikiwa Rais wa Chama cha Walimu, niliongoza msafara au kundi la Walimu, wakati huo Mheshimiwa Mary Nagu, akiwa Waziri wa Ofisi ya Rais (Utumishi), tulikwenda kupinga kuondolewa Tume ya Utumishi kwa Walimu au Tume ya Ajira ya Walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matatizo makubwa Walimu waliyonayo; wanahudumiwa na vyombo vingi. Hivi tutumie maneno gani ili Serikali isikie?

Namshukuru sana Mheshimiwa Celina Kombani, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, ambaye nilipochangia Bajeti yake, alikubali kwamba, atawaita wadau tuongee. Nami mategemeo yangu ni kwamba, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi pamoja na Naibu wake, kwa kuwa wao ndiyo wanaosimamia Sera za Elimu, kufanikiwa kwa Sera za Walimu ni pale ambapo Walimu watapata haki zao kwa wakati, ndipo watapata motisha. Motisha ya fedha hii wanayopewa, sijui kupewa suti au nini haisaidii. Motisha ya kwanza kabisa ni Mwalimu kupata haki zake kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipata bahati, naomba nirudie tena, tulipata bahati tulikwenda Kenya, tumeangalia wanavyofanya kazi wenzetu. Mimi mwenyewe nikiwa Waziri wa Elimu, niliunda Tume pia ikashirikisha Wadau

wakaenda Kenya wakaiona ile Tume. Wajumbe walioko kwenye Kamati ya Huduma za Jamii wangepata nafasi ya kuongea wangesema; tuliona ni kitu kizuri, Mwalimu anahudumiwa katika siku 14.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mkataba wa huduma hapa nilionao, wanasema hivi, naomba kwa ruhusa yako; wamewapa waajiriwa katika Tume ya Kuajiri Walimu wamewapa mkataba wa huduma ambao unasema, Tume itashughulikia ombi lolote la usajili na kumtumia mwombaji cheti chake kwa kusajiliwa katika muda usiozidi siku 14. Kujibu barua yoyote inayotoka kwa mwalimu siku 14. Watakaofanikiwa kupata nafasi za kazi watatumwa shuleni au chuoni katika muda usiozidi siku 14. Wanaorudi baada ya likizo ya masomo, watatumwa katika shule au chuo katika muda usiozidi siku 14. Mkataba huu hapa wa huduma ambao walimu wanashughulikiwa katika Tume ya Ajira ya Walimu Kenya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi naamini kwamba, pengine sisi tuna mazingira yetu tofauti, siyo lazima tuchukue kila kitu kutoka Kenya, lakini tukikaa, naamini Tume ya Ajira ya Walimu ndani ya Tanzania, itafuata mazingira yetu, lakini kuwa na chombo kimoja, mimi naona na ninaamini na ninaongea kwa niaba ya Kamati yangu, kwamba; chombo kimoja cha kuhudumia Walimu ndiyo jawabu kuliko mfumo uliopo sasa hivi ambao una urasimu mwingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu mimi kwa niaba ya Kamati ya Huduma za Jamii, tulete azimio. Nitawaomba Waheshimiwa Wabunge wote mniunge mkono, kiundwe Chombo cha Walimu kama ufumbuzi wa matatizo yao hapa nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tuseme nini kuhusu hili suala? Naamini siku ya leo, Mheshimiwa Waziri atakapokuwa akijibu pale mbele atatueleza. Mtu ukipewa ushauri, sisi kama Kamati tumekwenda mpaka kumshauri Waziri Mkuu, kwa masuala haya haya ya Chombo cha Walimu, ni vizuri basi mkasema tumeshindwa kwa kitu gani, lakini kimya tu sisi hatuelewi. Sisi tunaomba Chombo cha Walimu kiundwe. Nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Eng. Ramo Makani, atafuatiwa na Mheshimiwa Susan Lyimo!

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kwa namna ya pekee kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu, Mungu wa Mbinguni, kwa kuniwezesha kusimama mahali hapa wakati huu ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika hoja iliyoko Mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, mimi nakubaliana kabisa na ukweli kwamba, tunazo changamoto nyingi na kubwa katika Sekta ya Elimu. Changamoto ambazo ni kweli kabisa kama hatutachukua hatua basi hata

mipango yetu yote ya maendeleo ikiwemo Dira ya Mwaka 2025, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na hata Mipango yetu ya kila mwaka kamwe haiwezi kufanikiwa bila kufanya jitihada za makusudi kabisa katika kuboresha elimu katika maeneo mbalimbali ambayo yana changamoto mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo moja ambalo napenda kwa maoni yangu niliseme kwa uwazi kabisa, Tanzania siyo kisiwa, sisi ni sehemu ya maeneo mengine yote ya Dunia na changamoto tunazozipata zinaweza pia zikawa zinatokea mahali pengine Duniani; ni vizuri katika kujipima tukajipima kwa kujilinganisha na wengine. Tunaweza tukajipima pia kwa kuangalia vigezo tulivyojiwekea wenyewe, kabla hatujaanza kuzungumza lugha za kukata tamaa na kuanza kusema kwamba, tumeshindwa na kwamba sasa tumefika mahali ambapo kamwe hatuwezi kusimama tena. Lugha za kukata tamaa mimi naomba nisiwe mmoja wa maneno hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mmoja ni kwamba, pengine nafikiri umefika wakati sasa katika yale maeneo ambayo tunafanya vizuri tujipongeze basi au tuyaainishe tu kwamba, hapa tumefanya vizuri. Mimi nimesoma taarifa hii ambayo ni taarifa iliyowasilishwa kama Hotuba ya Bajeti, ukurasa wa 13, nimeona kwamba, kwa upande wa uzalishaji wa walimu, ukurasa huu unasema katika mwaka huu tunaouzungumzia jumla ya walimu 36,338 wameweza kupatikana na kuingia sokoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda kuwa mfupi, niseme tu kwa ufupi kwamba, hili ni zaidi ya lengo tulilojiwekea la kuzalisha walimu kwa mwaka katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Watu wanaweza kupitia Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na wakajiridhisha kwamba, idadi hii ni kubwa zaidi ya mara mbili ya lengo tulilojiwekea la kuzalisha walimu. *(Makofi)*

Niseme tu kwamba, pengine changamoto hapa itakuwa sasa; moja, ni ubora wa Walimu tuliowazalisha zaidi ya idadi; ya pili, itakuwa zaidi ya ubora ni namna ya kuwa-*retain,* kuwafanya wabakie kuwa Walimu; na hii ndiyo unaweka yale yote yanayohusiana na mishahara, yanayohusiana na madeni wanayodai na mambo mengine yote ambayo unaweza ukayahesabu kama mambo ambayo yanaweza kuwafanya watu wengine zaidi wapende kusoma ualimu na wale waliosoma ualimu wapende kubakia kuwa Walimu. Hayo nayo pia yako mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa eneo moja ambalo pia napenda kuchangia ni kwamba, ukiangalia michango yetu yote, pamoja na haya niliyoyasema mimi, mengi ni yale ambayo tunatakiwa tukumbuke kwamba, Wizara imepewa *instrument,* kwenye *instrument* ile wamepewa majukumu

mbalimbali ambayo sasa yanatafsiriwa kwenye Sera ambazo zinatunga Sheria zitakazoletwa hapa. Kwa mtindo ambao siyo wa kawaida, Sera ya Mafunzo ya Elimu ya Mwaka 2004 ililetwa hapa Bungeni kipindi kilichopita, mtakumbuka, kwa namna ambayo ilikuwa ni matokeo ya mjadala kwenye Bunge hili. Tukalazimisha Sera ile iletwe hapa kwa sababu ya kutaka ku-*address* changamoto zote hizi tunazozizungumzia na huo ulikuwa ni mfano bora wa kuisimamia Serikali. Kwa namna ile nalipongeza Bunge kwa sababu pale tulisema kwamba, ile Sera iletwe ili tuone kama ndani yake kweli tumeweza ku-*address* yale matatizo yote yaliyotajwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kwamba, baada ya Sera ile kupitiwa, asubuhi ya leo na wengine wamechangia wamesema kwamba, sasa iko kwenye hatua ya Baraza la Mawaziri. Hapa nitakachosema ni kwamba, kwa kweli Sera ile sasa ifike mwisho kusema kwamba, bado ipo kwenye hatua za kushughulikiwa. Sera ile ikamilike na baada ya pale ziletwe Sheria mbalimbali za utekelezaji wa yale yaliyomo ndani ya Sera ile, kwa sababu yote tunayoyazungumza hapa watu waende wakasome ile ile Rasimu ya Sera, yote yapo mle tuanze sasa kutekeleza sera ile baada ya kuwa imepitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sayansi na teknolojia; kwenye vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo, tumeweka kipaumbele cha kwanza kama miundombinu *(infrastructure),* lakini ndani yake kuna sayansi na teknolojia. Kwa kweli tumefika wakati sasa tuwe tunarudi kwenye Mpango wa Maendeleo, tuwe tunarudi kwenye mipango yetu ya mwaka na kujipima kwamba ni namna gani tunatekeleza yale tuliyojiwekea kama malengo, kila mwaka katika miaka yote mitano. Miaka mitano inaisha mwaka kesho, sasa kwa kuwa inaisha mwaka kesho tunatakiwa kujipima je, kwenye kipengele cha sayansi na teknoloji hasa kuhusiana na suala la kuandaa Walimu kwa idadi, ile ya *quality* itafuata baadaye, lakini kwa idadi kwanza tumefikia wapi. Kwa sababu hata hawa niliosema tumefikia lengo, wengi wao siyo Walimu wa sayansi na teknolojia, wakati tumesema changamoto kubwa ni sayansi na teknolojia.

Kwa hiyo, tuna haja sasa ya kupeleka nguvu zaidi kwa Walimu wa sayansi na teknolojia. Sikulisema lile siyo kwamba tumevuka tu lengo la mwaka, lakini kwa idadi ya Walimu tuliotakiwa kuwa nao mpaka kufikia mwaka kesho, baada ya miaka mitano, pia tumevuka lengo tulilokuwa tumejiwekea. Kwa hiyo, sasa unaweza kusema kwamba, kwa maana ya idadi ya Walimu kwa idadi wameshatosha, kwa maana ya Walimu wa masomo mengine mengi yaliyobaki, lakini kwa sayansi bado tuna changamoto kwa hiyo tujielekeze kule zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nirudi kwenye Jimbo langu kule Tunduru. Kwa ufupi kabisa, kwa sababu muda umeshaisha, nataka kusema tu kwamba,

upo mpango wa ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi katika ngazi ya Wilaya nchi nzima. Utekelezaji wa hili ni lazima uzingatie yale yaliyokwishawekwa tayari, maana huku tumesema kwamba, tutazingatia vigezo fulani, mojawapo ya kigezo ni mahali penyewe na umbali kufikia Chuo cha karibu kilichopo cha aina hiyo, iwe cha ufundi stadi kwa maana ya Chuo cha *VETA* ama *FDCs.* Sijaona kwenye mpango cha *FDC* Nandembo kule Tunduru, hakimo kabisa kwenye mpango wa kuboreshwa ili nacho kiweze kutoa wanafunzi au wahitimu watakaokuwa wamehitimu katika kada hizo.

Kuhusu *VETA,* hakuna kabisa kama walivyosema wengine, lakini sasa kwa sababu ni kilio cha nchi nzima, ukifuata vigezo Tunduru haiwezi kukosekana. Kwa sababu yenyewe kwa muda mrefu imekuwa iko nyuma, lakini pia kutokana na kukosekana kwa miundombinu na kutofikika na umbali wa kutoka Tunduru kwenda kukifikia Chuo kimoja chochote kile cha *VETA,* ni umbali mkubwa sana. Kwa hiyo, nilitegemea Serikali ingeweza kuweka kipaumbele. Kwa hiyo, katika hili naomba sana wakati wa utekelezaji wa mpango wa ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi katika ngazi ya Wilaya, basi Chuo cha Tunduru kiwepo kwenye mpango kwa sababu ya hilo nililolieleza hapo awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna dhana ya kwamba, elimu ya nje ndiyo bora zaidi. Nafikiri suala hili tuliangalie kwa ukaribu. Mimi kuanzia darasa la kwanza na shahada zangu zote mbili, nimesoma hapa hapa. Juzi tu nimetoka Maputo kwenda kuwa-*address* Wahandisi wote wa Afrika, Ma-*consultant* na sikuona kama kuna shida yoyote katika hilo, isipokuwa …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha*
*kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ramo Makani, dakika saba ni chache sana, tulipenda kusikia uliyotaka kutuambia. Mheshimiwa Susan Lyimo, atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Kisangi!

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii ili niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu. Nashukuru kwamba, Wabunge wengi au wote wanaelewa matatizo makubwa na changamoto nyingi zinazoikumba Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza na Matokeo Makubwa Sasa. Wiki iliyopita Wizara hii ilikuwa inaadhimisha Wiki ya Elimu, pamoja na masuala mengi iliyofanya, ilitoa tuzo kwa wanafunzi waliofanya vizuri sana Tanzania. Hili ni

jambo muhimu sana, lakini jambo ambalo linanifanya nichangie ni jinsi ambavyo tuzo hizo zilitolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kwamba, katika watoto kumi bora, walikuwa wasichana saba na wavulana watatu. Jambo la kusikitisha ni kwamba, Wizara iliamua kutoa tuzo hizo kufuatana na suala zima la jinsia; kwamba, mtoto aliyekuwa wa tisa na wa kumi wasichana wawili wale, hawakupata tuzo yoyote, wakati wavulana wa kumi na moja na kumi na mbili walipata nafasi.

Suala la kujiuliza; kama suala ni akili na siyo jinsia ilikuwaje watoto hawa wa kike hawakupata. Sisi akina mama na hata wanaume naamini tunatambua jinsi gani watoto wa kike wanavyopata matatizo makubwa katika suala la elimu. Nilitegemea kwamba, hawa watoto wawili ndiyo walipaswa vilevile kupata motisha hiyo, kwa sababu suala la kumshika Makamu wa Rais mkono, *psychologically* linamfanya mtoto afanye vizuri zaidi. Kwa hiyo, nilitaka maelezo, Waziri au Naibu Waziri watueleze ni kwa nini waliwaengua wasichana waliofanya vizuri waliokuwa katika *top ten* wakawaingiza wavulana ambao hawakuwa kwenye *top ten? (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nilitaka kujua hizo zawadi ambazo walipaswa kupata wamepata au hawakupata? Taarifa nilizonazo, walipewa bahasha zisizokuwa na pesa, lakini baadaye ndiyo wakaja kupewa laki mbili, wakati walitakiwa wapewe laki mbili na nusu, wapewe na vocha ya shilingi laki tano. Naomba maelezo ya kina. Nataka niseme tu kwamba, kama Matokeo Makubwa Sasa ni kumotisha watoto halafu wameshaanza kwa kutowamotisha, hili ni jambo ambalo linatia wasiwasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee na suala zima la Vyuo vya Elimu ya Juu. Naelewa kwamba, kuna walimu au *lecturers* katika Vyuo Vikuu ambao wanastahili kupewa kitu kinachoitwa *housing allowance*. Ninge-*declare* kwamba, mimi ni Mjumbe katika Baraza la Chuo Kikuu cha Ardhi, lakini vilevile natambua kwamba, siyo Chuo cha Ardhi tu ambao wanapata matatizo. Hizi fedha kwa ajili ya *housing allowances* zimekuwa zikichukua muda mrefu sana na ieleweke kwamba, walipoleta utaratibu huu, Walimu wengi waliokuwa wanaishi katika nyumba za Vyuo Vikuu ilibidi waondoke wakatafute nyumba, wale wanaostahili, ili waweze kulipwa. Matokeo yake, hawapati fedha hizi kwa wakati na hivyo inawaletea matatizo makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye suala la bajeti. Ni wazi kwamba, wenzangu wameshazungumzia suala zima la bajeti, lakini nilitaka kuzungumzia suala zima la ubaguzi ulioko katika Wizara. Sheria inasema wazi wazi kwamba, mtu anapotaka kujenga shule ni lazima awe na vigezo maalum, iwe ni Shule ya Serikali au iwe ni shule binafsi. Mojawapo ni pamoja na kuwa na matundu ya

vyoo. Kinachosikitisha ni kwamba, tunakuwa na matatizo makubwa ya matundu ya vyoo kwenye Shule za Kata, kwa sababu Wizara hii hii haisimamii. Hii ndiyo sababu tunasema ni lazima Wizara iwe na chombo maalum cha usimamizi. Haiwezekani Wizara hiyo hiyo iwe ndiyo mchezaji, iwe kocha, iwe *referee,* ndiyo sababu tunapata matatizo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, katika MMEM II walitegemea kuwa na madarasa elfu arobaini na tano, lakini wameweza kuwa na madarasa elfu sita mia nane tu. Hii ikiwa ni asilimia kumi na tano. Vilevile nyumba za Walimu, walipanga kuwa na nyumba za Walimu themanini na tisa elfu mia tisa, wameweza kujenga nyumba elfu nne mia saba, sawa na asilimia tano. Matundu ya vyoo, walipanga kuwa na matundu mia moja ishirini na saba elfu mia tisa arobaini na tano, lakini mpaka mpango umekamilika wamekuwa na matundu elfu tatu mia mbili, sawa na asilimia 2.5. Sasa tukisema hawa watu ni wababaishaji tunakosea?

Kwa hiyo, ukiangalia unaona wazi kwamba, haya ni matatizo makubwa sana ya kiutendaji. Tukiangalia hata kwenye MMEM II, matatizo ni hayohayo, fedha za ruzuku tumeeleza, wakisoma vizuri na nashukuru Waziri ameniambia kwamba wamepitia Hotuba ya Kambi ya Upinzani; kwa sababu walikuwa na siku nzima ya jana, ninaamini mtakuja na majibu ya kuridhisha.

Jambo la kushangaza, katika bajeti ya maendeleo, mwaka jana waliomba bilioni 53.7, wahisani wakatoa bilioni 8.3 tu. Mwaka huu wanaomba bilioni 71 kwa wahisani hao hao! Sasa unajiuliza kwa akili ya kawaida haingii akilini, unawezaje kuwa 8.3 halafu leo unaomba bilioni 71? Kwa hiyo, naona haya ni matatizo makubwa na tunapaswa kuyaangalia vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na madaraja mapya na ufaulu. Najua ina changamoto kubwa, kuna walio-*support* na namshukuru sana Profesa Msolla na wale wengine. Kama mtu una akili timamu, umeenda shule vizuri, utaelewa kwamba huu ni uchakachuaji. Ninachotaka kusema, ni ukweli ulio dhahiri kwamba, ufaulu au elimu yetu inaporomoka.

Ukiangalia wenzetu wa shule binafsi, hebu watuambie kwa nini wanafanya vizuri kiasi hicho. Mwaka jana, *top twenty* kulikuwa na shule mbili tu za Serikali tena zile za Vipaji Maalum, Shule ya Mzumbe ikiwa ya kumi na saba na Shule ya Kibaha ikiwa ya kumi na nane, halafu tunasema tunafanya vizuri! Mwaka huu matokeo, hakuna shule hata moja ya Serikali ambayo ipo kwenye *top ten,* kwa hiyo ni lazima tujiulize; Serikali kulikoni kwa nini wenzetu wa *private* wanafanya vizuri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Wizara ina haja kubwa sana ya kuona inafanya nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni suala la ukaguzi. Ubora wa elimu ni lazima uendane sambamba na ukaguzi. Tumeeleza kwenye kwenye Hotuba yangu kwamba, ni asilimia karibu ishirini tu ya Shule za Sekondari zinakaguliwa na asilimia kumi na nane tu ya Shule za Msingi. Sasa kama hawakaguliwi watafanya nini Wanafunzi na Walimu? Hii ndiyo sababu unakuta wastani wa Mwalimu kufundisha darasani ni saa tano na dakika ishirini na nne, lakini sasa hivi katika utafiti uliofanyika, Walimu wa shule za mijini, wanafundisha chini ya saa mbili kwa siku, wakati wale wa vijijini wanafundisha kati ya saa mbili na saa mbili na nusu.

Kwa hiyo, kama hamna Wakaguzi na niseme tu, kama Wilaya moja, kwa mfano Wilaya ya Kinondoni ninakotoka, ina shule 238 za msingi halafu wanapewa shilingi laki tano kwa mwaka kukagua; wanakagua kitu gani? Kikubwa zaidi hawana vitendea kazi vya kuweza kwenda kufanya kazi. Kama Kanda inapewa milioni moja na laki tano kwa mwaka wanafanyaje kwenda kukagua Vyuo na Shule za Sekondari?

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema tu kwamba, hili ni tatizo kubwa na tunaomba sana, tuliambiwa na wakati Mheshimiwa Rais anaongea na Wakuu wa Shule Binafsi kule Mbeya mwaka jana, alisema kwamba, kutakuwa na wakala, lakini mpaka leo hakuna jambo hilo. Naomba nikiri kwamba, kwa kweli elimu kama walivyosema wenzangu ni jambo la msingi sana na hata tukifanya mambo gani kwenye mambo mengine, kama hatuboreshi elimu tunajichimbia kaburi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Susan Lyimo. Mheshimiwa Marim Kissangi, atafuatiwa na Mheshimiwa Wenje!

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa, napenda nimpongeze Rais wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kumteua Mheshimiwa Jenista Mhagama, kuwa Naibu Waziri katika Wizara hii ya Elimu. Sisi kama Walimu, tumepata matumaini makubwa kwamba, sasa Mheshimiwa utawasaidia Walimu wenzako. *(Makofi)*

Baada ya kumpongeza Mheshimiwa Rais, nampongeza Mama Salma Kikwete, kwa kutuwekea Shule ya WAMA katika Mkoa wa Pwani, Wilaya ya Rufiji. Nampongeza sana kwa juhudi zake, kwanza, amechukua watoto wasio na uwezo mikoa yote akawaunganisha pamoja, kuwapa elimu iliyo bora. Pili, ametuletea changamoto kwa sisi tunaotoka katika Mikoa ya Rufiji, ambayo kidogo elimu kwetu ilikuwa shida kidogo, kwa sababu pale tunapata fursa ya kwenda kubadilishana uzoefu na wale wanafunzi wanaosoma pale WAMA. Mimi nimpongeze Mheshimiwa Mama Salma Kikwete, kwa juhudi zake.

Unapotenda Duniani mambo, usitegemee kupata mema, wewe utayakuta kesho kwa Mwenyezi Mungu, rehema zake utazikuta huko; wewe fanya kazi mama yangu usikate tamaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kuhusu kiwango cha ufaulu. Watoto wangu wa Shule ya Mbagala St. Anthony, wamefanya mahafali yao Jumamosi, wameondoka na masikitiko makubwa sana baada ya kupata taarifa zisizo sahihi na ambazo hazina ukweli. Wameambiwa kwamba, viwango vya ufaulu vimekuwa vina tofauti kubwa, kwa hiyo, ninyi mtakuja kufeli *Form Six* na maneno mengi tu ya ushawishi. Mimi niwaambie wanafunzi wote waliomaliza *Form Six* ikiwemo na wale wanaotoka kwenye Shule ya Mbagala St. Anthony, kwamba, viwango vya ufaulu havijabadilishwa, wewe kama unafanya vizuri darasani utafaulu tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, viwango vilivyobadilika ni kwamba, napenda wanisikilize leo na wanielewe, Daraja la A, litakuwa *marks* 75 – 100, yaani hiyo ni bora sana *Excellent,* Daraja $B^+$ 80 – 74 Vizuri sana; Daraja la B 50 - 59 Vizuri; Daraja C 40 – 49 Wastani; Daraja D 30 – 39 inaridhisha; Daraja E 20 – 29 hairidhishi, ina maana umefeli na F umefeli 0 – 19; lipi la ajabu?

Kilichobadilika hapo ni mchanganuo wa madaraja. Tulikuwa tunatumia Daraja A, B, C, D, imeongezwa B+ na hiyo ina sababu. Sababu ni kwamba, kama A, anachukua *marks* 75 – 100, sasa mtoto wako kama alipata 74 si anaingia kwenye B+. Hiyo inakusaidia mzazi kutafakari kujua mwanangu kwa Daraja la B alipata *marks* fulani. Hivi ni halali mtu aliyepata B ya 74 akaungana na mwenye B ya 50 wote wakapata B. Je, hili daraja tusome hapo tuangalie lina manufaa; maana watu wanafanya mambo ya kizushi huko mitaani! Jamani tuambizane ukweli, lakini pia niwaulize Walimu, Walimu wote wa Sekondari wamepewa hivi vitabu, watoe elimu. Wazazi hawajui, Watoto hawajui wanahangaika, wanakuwa *discouraged* na masomo, kumbe jambo ni lile isipokuwa tumeongeza makundi.

Meshmiwa Naibu Spika, lililofanyika Tanzania si geni, Uganda wao wanafaulu makundi tisa, Nigeria wana makundi tisa, South Africa wana makundi tisa, Kenya wana makundi 12, Tanzania ndiyo tumetoka kwenye tano kwenda saba; lipi geni? *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tufike mahali tuelewane, tusiwe tunazusha. Sisi tumesomeshwa, tumesoma vizuri, leo tunawaambia watoto wetu kwamba elimu haifai! *No,* elimu inafaa tena elimu nzuri. Mimi nasema tulivyosoma sisi siyo mlivyosoma ninyi leo akina John. Wanafunzi wanaosoma sasa hivi ni wazuri, wana-*confidence* nzuri kama Mheshimiwa John Mnyika,

anaongea, ulisoma wapi kama hukusoma Tanzania? Mheshimiwa Serukamba ulisoma wapi kama hukusoma Tanzania?

Mimi nataka niwaambie kuwa msiwakatishe tamaa wenzenu, waacheni na wao wasome. Tunatambua changamoto zipo nyingi tu na hakuna nchi ambayo inatoa elimu ambayo haina changamoto.

Ya kwanza ni hiyo ya Walimu. Jamani matatizo ya Walimu yamezidi. Huyu Mwalimu nataka niulize leo mwajiri wake ni nani? Nielezeni mwajiri wa Mwalimu; akienda Halmashauri anaambiwa Serikali Kuu sijui haijafanya nini, akienda huku anaambiwa Halmashauri sijui nini, akienda huku Utumishi sijui nini!

Nasema leo naunga na Mheshimiwa Sitta, Walimu waundiwe Chombo chao, tumechoka sasa kusikia. Huyu Mwalimu jamani ni mtu wa aina gani? Ukimwuliza Afisa Elimu anakwambia mimi siyo kamwulize Mkurugenzi, ukimwuliza Mkurugenzi anakwambia mimi siyo kamwulize *DC,* ukimwuliza *DC* anakwambia mimi sihusiki nenda kwa *RC, RC* siyo nenda Wizarani! *No,* tumechoka, tunataka sasa masilahi ya Mwalimu yawe wazi na iundwe Tume ambayo itakuwa Chombo cha kusimamia masilahi ya Walimu. *(Makofi)*

Mwalimu akikaa vizuri ndiyo ataweza kufundisha vizuri. Mwalimu anapopewa masilahi mazuri ataweza kufudisha vizuri. Kuna mtu hapa alisema mtu anamaliza shule hajui Kiingereza, hiyo si kweli, mtu haendi kusomea Kiingereza. Unatakiwa kujengewa maarifa shuleni, ukijengewa maarifa wewe utakuwa mzuri, kwa sababu Kiingereza siyo *issue;* kuna nchi kama China, wanaongea Kichina lakini wana Madaktari wa Kichina; kuna Wahindi tunaenda hospitalini, hawajui Kiswahili wala Kiingereza, lakini wanatupasua kila siku na tunapona. Kiingereza siyo kipimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mdharau kwao mtumwa, lazima tujivunie Utanzania wetu, hata kama kuna udhaifu tuurekebishe sasa, lakini tusiwakatishe tamaa wenzetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, tunakushukuru sana Mwalimu.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja, naomba uniongeze dakika mbili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, tunakushukuru sana. Baadhi yetu hatukujua na wewe kama ni Mwalimu pia na umetoa darasa hapa.

Mheshimiwa Ezekiah Wenje, atafuatiwa na Mheshimiwa Assumpter Mshama.

**MHE. EZEKIAH D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, kuna matatizo makubwa mawili kwenye mfumo wetu wa elimu. Tuna tatizo kwenye mfumo, lakini pia kuna tatizo kwenye miundombinu, kwa maana ya *education infrastructures.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ieleweke kwamba, mtu anaposema tuna tatizo kwenye mfumo wa elimu, kusema ukweli siyo ku-*discourage* watu na siyo kuwakatisha watu tamaa. Naomba nianze kwa kusema kwamba, mimi natoka kwenye Kamati ya Huduma za Jamii, kuna kipindi tulienda Nairobi kama alivyosema Mama Sitta, tukakutana na Kamati ya Bunge ya Kenya inayoshughulikia Wizara ya Elimu. Wakatuambia kwamba, wao kwenye nchi yao, Serikali yao ilipitisha kwenye uchaguzi, ilikuwa ni ajenda ya uchaguzi kwamba, kila shule, wana shule 24,000, kila mtoto Kenya wana mpango sasa wa kuwapa *laptop;* yaani mtoto anapewa *laptop* shuleni, wamefika huko. Wakatuambia kwamba, mpaka sasa *almost* shule 18,000 wameshapeleka umeme ili wapeleke hizo *laptop.*

Sisi huku mwanafunzi bado anakaa kwenye jiwe, sasa najiuliza; kama sisi bado tupo kwenye zama za mawe shuleni, halafu Kenya wako kwenye *ICT*, yaani wako kwenye zama za kompyuta shuleni, halafu tuko kwenye *East African Community,* hivi hawa wanafunzi watashindana vipi katika Soko la Ajira la Afrika Mashariki? *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunaposema ukweli kwamba tuna matatizo, siyo kwamba tunakatisha watu tama, kinachosemwa hapa ni ukweli. Kuanzia Dar es Salaam mpaka Mwanza, mpaka Bukoba, mpaka Ruvuma, kote huko wanafunzi wanakaa chini, Miaka 50 ya Uhuru kwenye nchi ambayo ina mbao! Madawati tu tunataka tutumie miaka mia mbili ili wanafunzi wapate viti vya kukalia. Mimi nimesoma *Michile Primary School* huko Rorya, nilikaa kwenye mawe, wadogo zangu leo miaka kama 20 baadaye wanakaa kwenye mawe, watakaokuja tena miaka 30 ijayo watakaa kwenye mawe. Hizi zama za mawe mpaka lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nielewe; kuna fedha za wizi wa rada, tuliambiwa kwamba hizo chenji za wizi zinaenda kununua madawati shuleni pamoja na kutengeneza vitabu. Sasa naomba Waziri wa Elimu atupe takwimu kwamba, madawati mangapi yamenunuliwa na yalipelekwa wapi, kwa sababu Bunge lilipitisha hapa na likaridhia kwamba, hizi fedha ziende kununua madawati na vitabu. Sasa tunataka kwenye majumuisho yake atupe mchanganuo wa madawati ambayo yamenunuliwa na hizi fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ninachotaka kukizungumzia; juzi nimeenda Mwanza, kila shule ukienda Walimu wanalalamika kwamba,

wanajiendeleza kama walikuwa na cheti wanapata *degree,* wanachofanyiwa wanasema wanabadilishiwa Muundo wa Utumishi *(re-categorization)*; hawapandishwi mshahara wala hawapandishwi daraja na wameshajiendeleza wametoka kwenye cheti wamepata *degree*. Walimu wengi wanalalamika, Wilaya ya Ilemela, Wilaya ya Nyamagana na si huku kwetu tu, tatizo la nchi nzima Walimu wanalalamika kila sehemu. Sasa tunataka tupate maelezo kutoka kwa Waziri, kwa nini inachukua muda mrefu mtu anapomaliza kusoma hapandishwi mshahara na cheo ili kuwa-*motivate* Walimu wengi zaidi waende shule?

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ninachotaka kuzungumzia ni suala la ujenzi wa viwango vya chini kwenye shule zetu. Hizi Shule za Kata zimejengwa, ukienda leo dukani kununua simu ya nokia ya shilingi 60,000 unapewa *guarantee*. Simu ya 60,000, sisi tunawapa wakandarasi wanajenga madarasa ya milioni 80, darasa halina *guarantee,* linaharibika ndani ya miaka miwili hakuna *floor* kwenye darasa na hao makandarasi wapo tu. Wanapewa kazi kila siku, unakuta shule imejengwa ndani ya miaka mitano, unaenda leo unakuta imezeeka utafikiri ilijengwa miaka 50 iliyopita, wakati shule zilizojengwa zamani; Bwiru Boys, Bwiru Girls, nenda Tabora Boys, Tabora Girls, Pugu na Mzumbe, zilijengwa na watu waadilifu zipo mpaka leo, *floor* iliyowekwa miaka hamsini iliyopita ipo mpaka leo. Leo sisi tunajenga *disposable classes*, darasa ambalo linajengwa linaisha ndani ya miaka miwili; ni ubadhirifu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ninachotaka kukizungumzia ni hii kitu kinachoitwa *Big Results Now (BRN),* kwenye Wizara ya Elimu. Siku Wizara ya Elimu inafanya *BRN* niliona, *commitment* waliyokuwa wanatoa Kamishna wa Elimu, Waziri wa Elimu, kila mtu anatoa *commitment* ya kuongeza ufaulu, siyo *commitment* ya kuboresha *quality* ya elimu inayotolewa. Hiyo ndiyo *commitment* waliyotoa. Kwa hiyo, hii *BRN* ya Wizara ya Elimu ni janja tu, ni namna ya kuongeza ufaulu wa wanafunzi na ndiyo maana mara unasikia wanaofanya Mtihani wa *Form Two* wanaswagwa wote wanaenda bila hata kuchujwa ili wafike kwenye yale malengo waliyosema ya kuongeza idadi ya ufaulu, bila kuangalia *quality* ya elimu inayotolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba leo tupate tamko la Serikali hapa; hivi nani anayedanganya ndani ya nchi hii, Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwenye Sera yenu mnasema kwamba elimu ya msingi bure; hebu tuambieni kama kweli elimu ya msingi ni bure nchi hii?

Mwanafunzi anapoenda kuanza darasa la kwanza anatakiwa atoe hela ya dawati shilingi 60,000, mchango wa maji shilingi 12,000 kwa mwaka, kuna rimu ya karatasi shilingi 12,000, kuna mchango wa mlinzi shilingi 12,000 kwa mwaka, kuna nembo shilingi 10,000 kwa mwaka. Hizi gharama zote ukiziunganisha inakimbilia shilingi 100,000 kwa mwaka halafu mnadanganya

watu kwamba elimu ni bure! Elimu ipi ni bure hapa? Hebu leo tuambieni; ukienda sekondari mnasema shule ya kutwa ni shilingi 20,000 kwa mwaka. Huyo mwanafunzi anatakiwa apeleke dawati shilingi 70,000, ndoo shilingi 5,000, jembe shilingi 5,000, fyekeo, awe na sweta, awe na *tshirt,* hizo zote ukijumlisha inakimbilia shilingi 200,000. Hivi nani anamdanganya nani? Waambieni Wananchi ukweli, kama hamna uwezo wa kutoa elimu bure, semeni hii kitu hamuwezi kutoa bure waambieni ukweli msiwadanganye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri tuambieni leo; hivi elimu ya msingi ni bure au siyo bure?

Leo nimepigiwa simu hapa kutoka Mkolani Shule ya Msingi Mwanza kwamba, Walimu wanarudisha mpaka wanafunzi nyumbani kisa eti hawajatoa shilingi 5,000 ya *mock; mock* ipi hiyo? Kama mnapeleka mtihani, pelekeni mtihani wafanye, mwanafunzi anapofukuzwa kwamba hajalipa shilingi 5,000; kama baba yake hana sasa afanye nini aache shule kwa sababu hana 5,000 na ameshasoma mpaka darasa la saba?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kusema kwamba, wanafunzi wanaoingia *Form One* kwa mwaka ni kati ya wanafunzi 450,000, *average enrolment*. Kati yao ni asilimia 80 ndiyo wanaosoma wanafika mpaka *Form Four,* wakishafika *Form Four* ni asilimia 20 tu ndiyo wanaofaulu sasa kwenda *Form Five* na *Six*. *(Makofi)*

Sasa hebu angalia hiyo *trend,* wanafunzi 420,000 asilimia 80 wanafika *Form Four …*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzugumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. EZEKIAH D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Wenje. Mheshimiwa Assumpter Mshama, atafuatiwa na Mheshimiwa Christina Mughwai na Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, ajiandae!

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika suala la elimu. Kwanza, napenda nimshukuru Mungu, kwa kunipatia uhai na kunipatia nafasi kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu niweze kuchangia.

Kwanza kabisa, naipongeza Wizara ya Elimu, mahali ambapo tumefikia kusema kweli tupo mahali ambapo huwezi ukadhalilisha. Tunaonekana tunaenda, japo hatukimbii, lakini kwa kumwongeza Mheshimiwa Jenista Mhagama katika duru hilo, naamini kwamba, sasa tutaanza kukimbia. Kwa kweli ninavyokujua Mheshimiwa Mhagama, kwa bidii zako na kwa namna ambavyo unajituma, tumepata mtu katika Wizara ya Elimu; Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwapongeze Walimu wangu wa Jimbo la Nkenge, kwa namna wanavyofanya kazi katika mazingira magumu, wanadai mishahara yao mpaka leo hawajapewa, wanafundisha wako kule pembeni, hawana umeme, hawana nyumba za kukaa, wana maisha magumu, lakini bado wanachapa kazi, tunayaona matokeo yao. Kwa hiyo, nilichokuwa naomba kwa Wizara hii, naomba muwafikirie Walimu hasa wanaofundisha vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mungu anasema hivi, ukisoma Biblia inasema; mshike sana elimu usimwache akaenda zake. Nilikuwa najiuliza ni mtu; maana usimwache akaenda zake nani?

Ukiangalia katika nchi yetu unaweza ukaona kama tumemwacha ameenda zake, kwa sababu ukitazama namna ya mifumo tunavyoiendesha, nianze kwa kusema, mtoto anapokuwa anaingia shule ya awali, tuna aina mbili; kuna watoto wa wenye uwezo wanaanza na Kiingereza kuanzia shule ya awali na kuna watoto wa wasio na uwezo wanaanza na Kiswahili kuanzia awali. Hawa watu wanaanza pamoja, wanafika mpaka darasa la saba, *all over the sudden,* siku moja Jumatatu moja, wanaingia Kidato cha Kwanza wote wanatakiwa kuongea Kiingereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watoto watakapotahiniwa, *by all means* kwa mara ya kwanza ya *form one*, lazima yule mtoto ambaye amejifunza kupitia *nursery* ya *montessory* na kuendelea na shule ya *international,* hawezi kufanana na mtoto ambaye amejifunza katika shule za kata. Kwa nini tunatengeneza mfumo ambao haueleweki? Kwa nini tusiamue kama lugha ya kufundishia ni Kiingereza watoto wote wajifunze kwa Kiingereza na kama tunaamua ni Kiswahili tupeleke watoto wetu wote kwenye mfumo wa Kiswahili? Huwezi kuwa na nchi moja, yenye mifumo miwili na watoto wa aina tofauti na matokeo yake, wale watoto wa watu maskini hata kama wako *intelligent*, hawawezi kufanana na mtoto anayeongea Kiingereza tangu vidudu mpaka Darasa la Saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali tuamue aidha Kiswahili, tumeshakijua wote ni *mother tongue,* ni kama lugha ya kila mmoja, tukiache Kiswahili kiwe cha kuongea na kiwe na darasa au tuamue watoto wote

wajifunze kwa Kiswahili; lakini watoto wa wakulima wanajifunza kwa Kiswahili, watoto wa watu fulani wanajifunza kwa Kiingereza, mwisho wa habari yote wanaopata *opportunity* ya kuendelea mbele ni watoto wa watu walio na uwezo.

Kwa mfano, sasa hivi tuko katika Soko la East Africa, tunashindana katika lugha. Unapochukua mtoto wa Kihaya aliyetoka Bukoba, ukamuweka na mtoto aliyetoka Nairobi pale au aliyetoka Nakuru, ambaye tangu amezaliwa anajifunza kwa Kiingereza na wote unataka kuwapa umeneja katika hoteli fulani, lazima mtoto wa Kihaya hataweza kufanikiwa. Anafikiri kwa Kiswahili, anaongea kwa Kiingereza, yule wa Nairobi au wa Tanzania Dar es Salaam, aliyejifunza *international school, straight* anakwenda kwenye Kiingereza; *by all means* yule mtoto ambaye ulimwacha kule nyuma hawezi kufanikiwa. Tuamue elimu yetu tuwe na kitu gani, hapo nitakuwa nimeridhika. Kwa sababu kinachoniuma kuna watoto wana akili sana, ukiwasikiliza wana akili sana lakini wanashindwa lugha. Kwa hiyo, ninashindwa kuelewa tunachagua mfumo gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, tatizo lingine ambalo ninaliona katika nchi yetu ya Tanzania ni Walimu kukosa *morale*. Ukiangalia nchi zingine, nitaomba nikusomee hapa, nchi zingine walipogundua kwamba elimu imeshuka walifanya nini. Ukiangalia Malawi, waliamua kuwapatia nyumba Walimu wanaofundisha kutoka vijijini. Kwa hiyo, Mwalimu akitoka hapa akaenda Bukoba kule Nkenge Misenyi, anakuta nyumba ipo, ni vigumu kurudi mjini, kwa sababu anajua atapata mahali pa kulala, anakuwa *motivated.*

Ukiangalia Uganda, wao waliamua kuongeza asilimia 30, yaani katika mshahara wake wanamwongezea asilimia 30 yule ambaye anafundisha katika mazingira magumu. Mozambique, waliamua kufanya *double,* kama unapokea laki mbili wanakupatia laki nne. Kwa hiyo, Mwalimu yeyote ambaye anaanza maisha atatamani kwenda kufundisha Misenyi kule Mtukula. *(Makofi)*

Ukienda Lesotho, wao waliongeza kama 60 kila mshahara wa mtu wanamwongezea 60,000 kwa ajili ya mazingira magumu. Tukifanya hivyo, nina uhakika watu wa kutoka maeneo ya vijijini hawataacha kazi; Mwalimu ukimwongezea 60,000 ni hela. Mwalimu anayefundisha Dar es Salaam na yule wa Misenyi wakawa *at par,* haiwezekani mtu akaenda Misenyi, watu wataamua wote kukaa mjini.

Kwa hiyo, hebu tuangalie, kuna wataalam walishauri kuwa labda tuongeze posho ya usafiri au tupandishe mishahara, *promotion* zao ziwe zinapanda haraka na wapewe vipaumbele kwenda masomoni kuongeza kozi. Ukimwambia Mwalimu aende Misenyi, atajisikia vizuri kwamba, atapanda haraka; ita-*motivate* kwenda kufundisha Misenyi. Wapewe fursa za kozi

mbalimbali, Mwalimu ajue nikiwa Bukoba kule nitapewa nafasi, kwa hiyo, watakimbilia kwenda kufundisha na hakutakuwa na *gap*.

Watu wapandishwe vyeo, kwa mfano, mimi leo nimetumiwa *message*, mtu anakuwa na kidato, yaani vipande vyao vinaenda kwa vidato, lakini kidato amepanda mwaka huu atakuja kupata mshahara wake mwaka 2016. Hiyo siyo sawa sawa, kwa hiyo, Walimu walioko kwenye maeneo ya mazingira magumu, ningeomba waangaliwe na ndipo tutaweza kuona kwamba, hatuna pengo kubwa katika nafasi za vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine ambalo limeongelewa na watu wengi; kwa mfano, katika Wizara ya Elimu, kuna vyombo vitatu vinamshughulikia Mwalimu. Ukiangalia Wizara ya Utumishi inaajiri, TAMISEMI inapeleka utekelezaji na utendaji, Wizara ya Elimu Sera na Mwongozo, Wizara ya Fedha mishahara na mambo ya fedha. Hivi kweli huyu Mwalimu siku ya siku anajulikana yuko upande gani?

Mimi naungana na Mama Sitta, hebu tuunde chombo ambacho kitamshughulikia Mwalimu. Anapoenda kuchukua mishahara anaenda kwingine, anapoendea ajira anaenda kwingine, anapoendea mambo ya mwongozo anaenda kwingine; huyu Mwalimu anajikuta hana baba wala mama, anayumba. Kwa hiyo, mimi nakubaliana tuunde chombo ambacho kitawashughulikia Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mshama. Mheshimiwa Christina Mughwai Lissu, atafuatiwa na Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo!

**MHE. CHRISTINA M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kuchangia katika Bunge hili, naomba nitoe pole sana kwa Wananchi wa Wilaya ya Ikungi, kutokana na ajali mbaya kabisa iliyotokea katika Kijiji cha Utaho, ambapo Wananchi wengi wa Kijiji cha Puma, Utaho yenyewe na Kijiji cha Ninyinga, takribani Wananchi 15 na Askari Polisi walifariki hapo hapo. Pamoja na hilo, naiomba sasa Serikali pamoja na neema ya barabara hii kuu, inapopita katika maeneo ya vijiji, waweke matuta ili magari yaweze kupunguza mwendo katika maeneo ya watu, kwa sababu barabara hii imeleta janga katika maeneo ya vijiji tunakotoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Elimu ya Tanzania iko *ICU*. Nashindwa kuelewa Waheshimiwa Wabunge wanaosimama hapa wakisema kwamba, tunafanya vizuri na ufaulu wa umepanda. Hivi ufaulu utapanda vipi katika mazingira ambapo darasa ni la nyasi na mtoto amekalia mawe? Ufaulu utapanda vipi mahali ambapo Mwalimu mmoja kwa shule moja? Ufaulu

utapanda vipi mahali ambapo Mwalimu mmoja tena mwenye madai lukuki akifundisha darasa la watoto 80 mpaka 100? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ufaulu utapanda vipi wakati mtoto akihisi kwenda chooni hakuna matundu ya kutosha wanapanga foleni? Imefika wakati tukubali kwamba, Elimu ya Tanzania iko *ICU* na mimi niseme zamani tulisoma zama za kale za mawe. Leo hii ukistaajabu ya zama za kale za mawe, utaziona zama za siku hizi za mawe za Serikali ya CCM. Watoto wanakalia mawe shuleni halafu mnasema kiwango cha ufaulu kimeongezeka! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, samahani, tangu mimi nimekuwa Mbunge nimeshuhudia kalele na kilio cha Walimu. Madai ya madeni ya walimu. Karibu *term* yangu ya kwanza ya Ubunge inaisha, bado madai ya Walimu yapo. Hakika kero za madai ya Walimu na kero za mazingira magumu zimegonga kwenye sikio la Chama cha Mapinduzi na Serikali yake lililokufa. Walimu poleni, kelele zenu zimeingia kwenye masikio yaliyoziba yasiyosikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la shule binafsi. Kwanza, niwapongeze na ninatambua mchango mkubwa ambao unafanywa na Sekta Binafsi katika Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo; kwa kweli wana mchango mkubwa.

Nizungumzie ada, hivi ni nani anayekagua viwango vya ada vinavyotozwa na shule binafsi? Leo hii ni mzingo mkubwa, wazazi wengi wanashindwa kumudu. Tunaiomba Serikali ipunguze mzigo kwa wazazi wanaopeleka watoto kwenye shule binafsi. Wazazi hawana jinsi, kwa sababu kwenye Shule za Serikali ni shida tupu, wanajifunga mkanda waende *private,* lakini kule nako wanakutana na ada ambazo ni kubwa kuliko uwezo wao. Pamoja na ada hizo kubwa, shule binafsi zinaandamana na michango mingi; mwanafunzi baada ya kulipa ada ataambiwa changia jengo, changia dawati, changia maabara, changia uwanja wa michezo.

Sasa mimi nashangaa, mzazi aliyepeleka mtoto shule ya *private* anapochangia majengo, maabara, mabweni, kitanda; hivi hiyo shule imekuwa ya umma au ni *private*; kwa sababu mwisho wa siku mtoto ataondoka mmiliki wa shule ataendelea na shule yake?

Naomba ufafanuzi iwapo ni halali kwa wazazi kutozwa michango katika shule za *private* hasa michango inayoendana na kutengeneza miundombinu ya shule hizo ilhali hizo shule siyo za umma?

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee suala zima la bajeti ya Wizara hii. Takribani asilimia 80 ya bajeti yake ya maendeleo kama ilivyoelezwa kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Naibu Waziri, inaenda kwenye mikopo ya elimu ya juu. Sasa mimi sijui kama huo ndiyo mpango wa mradi wa maendeleo; hii asilimia 20 inayobaki kweli itatosha kero hizi zilizoko kwenye Sekta ya Elimu? Ndiyo maana katika Hotuba yake Mheshimiwa Waziri, vipaumbele vyake haviko wazi, wanasema tu wataboresha hivi, watainua hali hii, lakini pia bajeti yake ni ndogo, asilimia 20 itaenda kufanya kazi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, nawashukuru Watanzania, wanafuatilia mjadala huu, uliponitaja kwamba nitakuwa mchangiaji ninayefuata, nimepokea *message* kutoka kwa Walimu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wanasema Mheshimiwa zungumzia na *housing allowance*. Walimu wa Vyuo Vikuu, *housing allowance* imekuwa ni madeni matupu. Hivi Mwalimu atafundishaje, jamani tuwajali hawa Walimu wa vyuo, mishahara yao kwanza ni midogo, sasa wanapokuwa tena hawana uhakika na makazi yao kweli huyo atakaa afundishe *economics* watoto waelewe? Tafadhali, Wizara inayohusika angalieni suala la *allowances* za Walimu wa Vyuo Vikuu. Sikilizeni kilio chao, waboresheeni mazingira ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi wa shule umekuwa ni tatizo kubwa, kwa sababu ukiangalia kwa hali ya kawaida, mwanafunzi anayesoma kama hakuna mtihani hatafanya jitihada za kutosha. Vivyo hivyo hata Walimu wetu, kama hawakaguliwi watafundisha *at leisure*. Kwa hiyo, naiomba Wizara, kwa sababu suala la ukaguzi wa shule limekuwa gumu kwa Wizara kufanya, basi niunge mkono hoja ya kuweka Wakala wa Ukaguzi. Afadhali uweke mtu ambaye atakuwa *independent,* ambaye ndiyo kazi yake, kukicha ni ukaguzi wa shule, kukicha ni ukaguzi wa shule. Tutaweza kuinua kiwango cha elimu na hapo ndiyo tutaanza kuongea habari ya kuongezeka kwa ufaulu.

Sasa hivi unaposema ufaulu umeongezeka, bila kuonesha ufaulu huo umeongezeka kwa jitihada gani zilizofanyika, tunakuwa tunajidanganya. Siyo kwamba, ufaulu umeongezeka, ila ni vigezo vya ufaulu vimefanyiwa marekebisho ili ionekane watoto wamefaulu. Hali halisi, Elimu ya Tanzania iko *ICU,* inatakiwa ifumuliwe na kupangwa upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Christina Mughwai. Kwa wasiofahamu, nimesoma Shule ya Msingi kwenye kijiji chao, yeye na Mheshimiwa Tundu Lissu.

Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Njwayo na Mheshimiwa Charles Mwijange ajiandae!

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia Wizara ya Elimu. Napenda niseme kwamba, Wizara hii ina tanzu mbili; ina sehemu ambayo inahusiana na elimu kwa upande wa Tanganyika, Tanzania Bara; na ina sehemu ambayo inahusiana na Elimu ya Juu ambayo ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano. Sasa na mimi ningependa Elimu ya Juu irudi katika mfumo wa zamani; kwa hiyo, kuwe na Waziri ambaye atashughulikia Elimu ya Juu, ambayo ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano.

Toka asubuhi watu wanachangia, lakini wanachangia kwa sababu ya upande mmoja tu wa Tanzania Bara. Sasa niseme kwamba, Elimu ya Juu kwa sababu ni suala la Muungano ni lazima irudishwe vilevile kwamba iwe ni sehemu ya Elimu ya Juu itakayoshughulikiwa na Waziri atakayeshughulikia Masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, niseme kwamba, katika utoaji wa mikopo, katika kujiunga na masomo ya elimu ya juu; kuna *ratio* gani ambayo wanapatiwa Wazanzibari?

Si hilo tu, katika *scholarship* ambazo zinapatikana, Wazanzibari wanapata kiasi gani?

Nataka nijue kwa kipindi cha miaka kumi, ni wanafunzi wangapi kutoka Zanzibar ambao wamepatiwa mikopo ya kujiunga na Elimu ya Juu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kauli au taarifa ambazo zinasema kwamba, vijana ambao walikuwa na ufaulu wa masomo ya dini, hawapatiwi mikopo. Sasa naomba Waziri athibitishe hili ni kweli au akanushe? Kama ni kweli, kwa nini wasipatiwe mikopo vijana ambao wana ufaulu wa masomo ya dini?

Tatu, tuseme kwamba, wanaofaulu masomo ya dini kama hawapatiwi mikopo leo, ni hawa hawa watu wa dini ambao mpaka kwenye Bunge Maalum tuliwashirikisha, ni hawa hawa watu wa dini ambao panapotokea lolote lile la kuhitilafiana, tunawaita wao wawe wasuluhishi wetu. Leo tunawabagua, lakini kwenye maridhiano tunawataka; ni kwa misingi ipi leo tuwabague?

Mheshimwia Naibu Spika, jambo lingine niseme kwa hili, baniani mbaya kiatu chake dawa. Kwamba, tunapokuwa na hitilafu tunawataka, lakini pale ambapo hapana hitilafu tunasema hawa wasipewe mikopo. Kwa hiyo, naomba Waziri athibitishe kama hili lipo au halipo na kama lipo ni kwa sababu zipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, kuna baadhi ya shule, Mwalimu mmoja anafundisha madarasa kumi. Hivi kweli tunadai kiwango cha elimu kimepanda, Mwalimu mmoja anafundisha madarsa kumi elimu hiyo inapandaje?

Lingine, mimi sielewi Serikali ya CCM ambayo ipo madarakani kwa nusu karne, miaka hamsini, kuna Mheshimiwa mmoja pale tumeambiwa ana karibu shule 12, anaajiri Walimu anawalipa. Serikali ambayo ina miaka 50 inashindwa kuwashughulikia Walimu na kuwalipa mishahara yao! Si hilo tu, kuna Chuo cha St. Mary ya Tabata, pale wamemaliza mafunzo yao ya ualimu, tuna upungufu wa Walimu na siyo Chuo hicho tu kuna vyuo vingi; kwa nini Serikali haichukui hatua ya kuwaajiri wafundishe watoto wetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niseme kuwa, bado suala la elimu hatujalipa kipaumbele kinachostahili. Kadiri tunavyokwenda, basi elimu yetu bado inadidimia. Tunaweza tukamlaumu Waziri, lakini Waziri peke yake halaumiki, ni Serikali ndiyo yenye dhamana ya kuweza kuajiri Walimu kwa ujumla wake. Kwa hiyo, nasema kwamba, Serikali ichukue hatua ya kuwaajiri Walimu ili vijana wetu waweze kupata elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna taarifa kwamba, Somo la Kiarabu katika Chuo cha *UDOM* limeondolewa. Naomba Waziri athibitishe hili ni kweli au akanushe na kwa nini liondolewe Somo la Kiarabu au kwa sababu kuna watu wanasema kwamba Uarabu ni ugaidi? *(Makofi)*

Lugha ni lugha tu na Mtume kasema nendeni mkatafute elimu popote, someni lugha yoyote, hata uende China basi tafuteni elimu. Leo tunasikia Somo la Kiaribu limeondolewa ni kwa sababu zipi? Hivi ninyi hamhitaji kufanya biashara na Waarabu? Hatuhitaji sisi kufanya biashara na Nchi za Kiarabu? Kwa nini tunakwenda kwao?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kombo, nakushukuru sana, Mheshimiwa Njwayo na Mheshimiwa Charles Mwijage, jiandae!

**MHE. JUMA ABDALLAH NJWAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, samahani, nilikuwa hospitali kidogo, maana naambiwa awali uliniita na sasa umeniita tena, lakini nina ndwele kidogo kwa hiyo nilikuwa ninajiganga.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme ahsante kwa kunipa nafasi hii ili niungane na Wabunge wenzangu, kutoa mchango wangu kwenye Hotuba hii ya Bajeti iliyoko mbele yetu. Awali ya yote, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu - Profesa Mchome na Watendaji wengine

mbalimbali. Ninataka niwaambie kuwa, hakuna kazi rahisi Duniani, kila kazi ina changamoto, jibidiisheni, pateni ushauri mbalimbali tusonge mbele. Msiwe na wasiwasi, kupigwa mawe ni kitu cha kawaida, unachofanya unajirekebisha unasonga mbele. Hilo liwe muhimu kwenu na kwamba, msipate shida ya kutopata ushauri, mkiona mmekwama tafuteni ushauri kwenye maeneo mbalimbali, tutasogea tu. *(Makofi)*

Jambo lingine, naomba kuipongeza Wizara hii na TAMISEMI, kwa kupeleka mpango wa kompyuta kwneye Shule za Msingi za Mkoa wote wa Mtwara. Maana nasikiasikia watu hapa wanasema, eee, hakuna hata kompyuta, Kenya kuna kompyuta na sisi tumeshaanza. Tanzania ni kubwa, ina mikoa zaidi ya 25, lazima tupate pa kuanzia na tupate pa kuishia. *(Makofi)*

Naomba pia kuipongeza Wizara kwa namna ilivyofanya, safari hii imeleta Walimu wa kutosha Jimboni kwangu, haijapata kutokea. *(Makofi)*

Katika Walimu 312 waliopangiwa Tandahimba, Walimu 300, asilimia 96 wameripoti. Wale wa Shule za Sekondari, katika walimu 86, walimu 71, asilimia 83 tayari wamesharipoti; haijapata kutokea kwa kweli. Nawapongeza na nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoomba basi, yafuatayo; la kwanza, Walimu wale hawakupata mishahara, kwa sababu walikuwa wanaripoti polepole na wametoka mbali. Kwa hiyo, sasa huu mshahara wa mwezi wa tano uwe *automatically* na wa mwezi wa nne, uwekwe pamoja pamoja ili tuondoe matatizo. Kwa sababu wamekopa, inaeleweka, katika kuripoti, mambo hayakuwa sawasawa, hawawezi kuripoti pamoja na kwa hiyo wameachwa, lakini kwa sababu wameishi kwa shida na madeni, basi tuwasaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepata meseji hapa sasa hivi inasema, Mheshimiwa Mbunge wetu, vijana wako hatujapata fedha za mkopo wa chakula hapa *SUA*. Hali ni mbaya sana, tunahangaika tu. Naomba hilo tulimalize, malizeni, si jambo hili lipo, la kawaida linajulikana, tusiwacheleweshee watoto, wasipate adha bila sababu. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, naomba niseme machache yafuatayo:-

La kwanza, tumekuwa na matatizo na manung'uniko makubwa kwa Walimu wetu wa Shule za Msingi na sekondari. Nina ripoti hapa, taarifa mbalimbali kuhusu ufaulu wa watahiniwa katika mitihani ya Kidato cha Nne na Shule za Msingi. Kumeonesha *improvement* fulani, lakini kuna mambo yanaonekana hapa kuna changamoto, hasa kwa Walimu. Nilichojifunza na kubaini ni kwamba, Walimu wamekuwa hawapati motisha hasa wa Shule za

Msingi na Sekondari. Tuamue sasa kama Serikali, kutengeneza aina ya motisha ya kutosha kwa Walimu wetu.

Mimi kwa muda mrefu sana, sijasikia Walimu wa Shule ya Msingi wakienda semina, hata hili jambo la mshahara kung'ang'ania tu mshahara peke yake halitatatua tatizo. Wakati tukiwapa mishahara na motisha ya aina nyingine, wafanye semina, ndani ya kazi pale wapate *training*. Nimepata kigugumizi tu, nilichokuwa nataka kusema, ni mafunzo kazini! *(Kicheko/Makofi)*

Ndugu zangu, lazima wapate mafunzo kazini ya mara kwa mara kama watu wengine wanavyopata. Haiwezekani, haiwezekani, wakati wengine wanapata haya mafunzo, lakini wao wapo, kwa vyovyote vile, watakuwa *demoralized*. Kwa kukosa motisha, hawata-*perform* vizuri.

Kwa hiyo, mimi nashauri, Serikali itafute kila namna ya kuhakikisha motisha na aina nyingine ya *incentives* kwa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari. Wapate tena kwa wakati, ikiwemo mafunzo ya mara kwa mara na semina za mara kwa mara ili kuboresha utendaji wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kusema kidogo kuhusu tatizo la gharama kubwa za ada kwa shule zetu za *private*. Tumekuwa tukilalamika muda mrefu kwamba, shule zetu za *private* zina gharama kubwa ya ada na kwamba, shule hizo hizo zinatofautiana kati ya shule moja kwenda shule nyingine. Jambo hili ndugu zangu Serikalini halikubaliki, ni lazima tutengeneze utaratibu wa ku-*harmonize* hizi ada zetu, ili zifanane na vilevile ziwe zinazofaa, *affordable* kwa Wananchi wetu. Ikiwezekana, Serikali tuweke *subsidy,* ruzuku fulani kwa shule za *private*, ili tuwakomboe Wananchi, Wazazi na Walezi wa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huko nyuma niliwahi kuuliza swali Bungeni, linalohusu suala la ujenzi wa Chuo cha *VETA* Wilayani Tandahimba. Nikaahidiwa hapa kwamba, liko kwenye awamu ya pili na kaka yangu, Dokta Kawambwa, ndiyo alisimama kwenye *podium* akajibu lile swali. Awamu ya pili, hakuna shida, eneo lipo tutafanya, lakini hakuna ninachoona kinafanywa, hakuna maendeleo yoyote Wizara inafanya; lini sasa?

Mimi naomba sana, jambo hili tulimalize, maana katika shule zile 26 na nne ninazotegemea kupata mwakani, zitakuwa 30, wale watoto wakimaliza wapate mahali pa kukimbilia. Isiwe *form five* tu na vyuo vingine na *VETA*, kama zinavyojulikana hizo *VETA*, zimekuwa msaada sana; kwa hiyo, naomba jambo la *VETA* lile tumalize, maana eneo lipo, kinachongojwa ni Wizara kukamilisha tu jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kuzungumzia kidogo kuhusu Chuo cha Ualimu cha Kitangari kilichoko Newala, Mkoani Mtwara. Chuo kile kwa muda mrefu, hakijafanyiwa ukarabati wa miundombinu iliyopo, kinakatisha tamaa. Wakati umefika sasa mkisaidie, paboreke pale, miundombinu ya kila kitu, maji, umeme na mambo mengine, pamoja na majengo yale, yawe yanayofanana na kuwa Chuo!

Wanakuwa *demoralized* Walimu pale, hata wanafunzi wanapofika pale, wanaona kama Chuo cha ajabu kidogo. Natambua Chuo hiki kipo Jimboni kwa kaka yangu, Mheshimiwa George Huruma Mkuchika, lakini yeye kama Waziri, hana nafasi ya kusema kama mimi niliyeko huku. Naomba jamani, tafadhali, tukiangalie Chuo kile. Kamati ya Bunge ilitembelea kule, waliona hali halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Njwayo, ahsante sana. Mheshimiwa Charles Mwijage, atafuatiwa na Mheshimiwa Ritta Kabati na Mheshimiwa Mwalimu Marombwa, atakuwa wa mwisho!

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Hii ni mara ya nne mfululizo ninachangia Wizara hii. Mara tatu nilizochangia, ushauri wangu kwa kiasi kikubwa umezingatiwa, kasoro jambo moja la msingi na katika hili sitabadilika; matatizo makubwa yanayoipata Sekta ya Elimu Tanzania, ni kwa sababu ya kutokuwa na baba, mara iko TAMISEMI, mara iko wapi!

Wizara ya Elimu, Sekta ya Elimu, iwe chini ya mamlaka moja. Mtaalam wa Uvuvi, Mkurugenzi wa Uvuvi, hawezi kumjali Mwalimu. Mtu aliyejifunza uvuvi au uwindaji au vitu vingine hawezi kujali hilo. Ukiiacha kasoro hiyo, mambo mengine Wizara ya Elimu mmeyajibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuwapongeza Wananchi wa Wilaya ya Muleba, hasa Jimbo langu la Muleba Kaskazini. Kwa miaka mitatu ambayo nilikuwa kwenye jahazi la uongozi, tumejenga vyumba 130 vya madarasa. Mkuu wa Wilaya, Bwana Lembrisi Kipuyo, baada ya kufika, tunashirikiana tunajenga maabara saba. Viongozi wenzangu naomba niwaambie jambo moja, ni mwiko Kiongozi kulalamika, usilalamike, wape Wananchi majawabu. *(Makofi)*

Msiwadanganye Watanzania kwa kuwaambia Serikali itakuja kuwajali watoto wenu. Serikali huwa haizai, Serikali haiendi *clinic*. Ukizaa mtoto wako, lazima ujue utamfanya nini, Serikali itakupa *lift* ukishaanza safari. *(Makofi)*

Ndugu zangu maneno tunayosema yanawapotosha watu ambao wanatuamini. Mimi Wananchi wa Muleba wamenikubalia na nimejenga vyumba 130. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, uje ufungue shule hazijafunguiliwa, uje ufungue maabara saba na maabara zote saba msingi nimegharimia mwenyewe. Nawashukuru rafiki zangu, ambao wameniunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia marekebisho kwenye elimu hii, Serikali hii, nikiwa nazingatia upungufu ambao sikubaliani nao. Jambo la kwanza, mmefanya vizuri, mmetengeneza Vyuo vya *VETA*. Kosa moja mmlilofanya, mmetenga Vyuo vinne vya *VETA* kwenye mikoa minne mipya, Mkoa wa Kagera siyo mpya ni wa zamani kwa nini mmetunyima? Sikubaliani na sitaki kuwaaminisha watu wa Kagera kwamba, wanaendelea kutengwa, tumetoka kwenye kutengwa, tunadai Chuo cha *VETA* ngazi ya Mkoa katika bajeti hii. Nina imani tutaelewana Bwana Kawambwa.

Mambo mengine yanakwenda vizuri, nawapa angalizo, mnatengeneza Sera mpya ya Elimu na mnakuja na kitu kinaitwa Elimu Msingi, Elimu Msingi ina mashaka yake. Elimu Msingi ni kuongeza muda wa wanafunzi kukaa shuleni, iwe miaka minane, tisa au kumi. Kabla hamjakwenda huko, tupitishane kwenye kipindi cha mpito, tusirudi kwenye kimbiakimbia, tuliyokwenda kwenye sekondari za kata. Hakikisha kabla ya kuongeza muda wa kuishi shuleni, kila Shule ya Msingi imekuwa na madarasa ya kutosha, imekuwa na Walimu wa kutosha, imekuwa na vitabu vya kutosha, tutengeneze wataalam ambao wameiva vizuri.

Niwapongeze Wizara kwa kuja na Bodi ya Wataalam wa Elimu. Katika Taarifa ya Waziri anasema, itakuja Bodi ya Wataalam wa Sekta ya Elimu, itakayoangalia maadili, itakayoangalia nidhamu na weledi. Nasema, ongezeni na kuangalia masilahi yao, ukitaka kuangalia nidhamu ya mtu, umpe masilahi mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuja na wazo kwamba, kwenye rika husika, sisi vijana wanaokwenda elimu ya juu ni asilimia 2.7, mnalenga kutupeleka asilimia tano. Chonde chonde, pamoja na haja ya kusajili Wanafunzi wa Chuo Kikuu kufikia laki tatu, hakikisheni mnafanya mahusiano, mnafanya *linkage* na Sekta nyingine, kusudi vijana wanaotoka kwenye vyuo, waweze kupata fursa za kufanya. Siyo lazima waajiriwe, lakini waweze kuwa *absolved* kwenye Sekta nyingine. Kinyume chake, tutatengeneza jeshi ambalo tutakuja kushindwa kuelewana nalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie usajili wa shule. Nimewaeleza kwamba, Muleba Kaskazini tunajenga shule kwa kasi sana. Kamati yenu ya Usajili au Idara yenu ya Usajili ina upungufu. Serikali imewataka Wananchi wajenge shule, anakuja mtu anaitwa Afisa wa Usajili kutoka Kanda Kigoma, anamwambia mtu hii shule siwezi kuisajili, haina nyumba ya Mkuu wa Shule, haina sijui jumba la utawala, haina maabara; Shule za Tanzania zina jumba la utawala! Kwa hiyo, ondoeni huu upungufu unaotufanya sisi tuonekane watu ambao hatuelewi hali halisi. Kama Wananchi wamejenga shule yao, Serikali umekuta kuna upungufu, ni wajibu wako kuboresha pale ambapo Wananchi wamefikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie hiki kinachoitwa Shule Binafsi. Ninachoomba mimi, ile Idara ya Ukaguzi, ambayo inakagua Shule za Serikali na Shule Binafsi izikague sawia. Kuna upotofu wa kitu kimoja, watu wanadhani Shule Binafsi zote zinafanya vizuri, kuna Shule Binafsi ambazo watoto wanakwenda kupoteza muda na wanakwenda kupoteza fedha za wazazi wao.

Nawaomba chondechonde, hakikisheni zote zinakaguliwa, kusudi ile fedha ambayo wazazi wanajinyima kwenda kule irudi. Upungufu mwingine wa Sera ya Serikali, mpango wenu Serikali angalieni, umekuwepo utaratibu wa watoto ambao walisomea kwenye shule hizi za binafsi, wanapokwenda kuomba *sponsorship* Chuo Kikuu, wanakataliwa. Ukweli ni kwamba, wazazi wanaosomesha kwenye shule binafsi wanajinyima na wazazi wengine ambao hawasomeshi shule binafsi, fedha zao wanafanyia vitu ambavyo havina tija; mwingine anajenga nyumba, mwingine anakwneda kusomesha mtoto.

Sasa usimpe adhabu huyu ambaye aliamua kuwekeza ndani ya mtoto, ukampa *bonus* mtu ambaye aliamua kununua magari au kununua mifugo. Hilo suala linaleta changamoto. Mheshimiwa Kawambwa wakati bado upo kwenye Wizara hii ambayo haina mfumo, haina muundo, kabla ya kutengenezewa Wizara yako, hili suala uliangalie. Kwa kweli mimi sitaridhika kama tutaendelea kuwa namna hii.

Kuna suala la mazingira magumu ya Walimu. Ukizungumza mazingira magumu ya Walimu, huwezi kuelewa. Mtu ukienda kwetu sisi, ukaenda Bumbile, ukaenda Gosba, ukaenda Rutoro, ukaenda Ngenge, ndiyo utaelewa nini maana ya mazingira magumu.

Nachukua fursa hii, kuwashukuru Walimu wote ambao wamekubali kuingia Wilaya ya Muleba na kufanya kazi. Ninawashukuru Wananchi wote wa

Muleba, ambao wameamua kuwapatia Walimu wote wanaokuja kwetu, nyumba za kuishi kwa malipo nafuu au bila malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naomba kushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Charles Mwijage, kwa mchango wako. Mheshimiwa Ritta Kabati, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Kahigi, Mheshimiwa Marombwa utafunga ukurasa. Mheshimiwa Ritta Kabati!

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba nianze na kumpongeza dada yetu, Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwa nafasi aliyoipata ya Unaibu Waziri wa Wizara hii. *(Makofi)*

Ninaamini kwamba, hatatuangusha kama Mawaziri wengine Wanawake ambavyo wamekuwa wakichapa kazi. *(Makofi)*

Wizara hii ni muhimu sana, lakini inasikitisha kuona Serikali haijaweza kutoa kipaumbele, kwa sababu pamoja na bajeti ambayo tumekuwa tukiipitisha hapa Bungeni, tunaona bado bajeti yenyewe haifiki kwa wakati. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie, zile fedha ambazo tunazitenga kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, basi angalau iweze kufikishwa yote na kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu wanafanya kazi kwenye mazingira magumu. Nafikiri Wabunge wote leo hii tumeongea lugha moja, kulalamikia mazingira magumu wanayofanyia kazi. Kwanza, hawana nyumba za kuishi, urasimu wa kupandishwa madaraja bado upo, hawalipwi posho za mazingira magumu, halafu mishahara yao pia ni duni sana na madeni yao hayalipwi kwa wakati. *(Makofi)*

Mimi niongelee kuhusiana na kutolipwa madeni yao, tatizo hili linalalamikiwa karibu nchi nzima. Hata Tabora na Iringa; mimi nichukulie mfano katika Manispaa yetu ya Iringa, Walimu wanadai zaidi ya milioni 130, lakini kila siku hatujui lini watalipwa. Sasa labda leo Serikali ituambie, tatizo ni nini na ukomo wa hayo madeni ni lini? Kwa sababu hii inapunguza hata *morale* yao ya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kuhusu Kitengo cha Ukaguzi. Niungane kabisa na ushauri ulitolewa na Kamati hii kwamba. Serikali iiwezeshe Idara ya Ukaguzi wa Elimu nchini kuwa Wakala unaojitegemea, ili kutekeleza majukumu yao na ipewe fedha za kutosha. *(Makofi)*

Wakaguzi wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, hawana vyombo vya usafiri. Kwa mfano, katika Mkoa wetu wa Iringa, utaona shule zilizoko pembezoni kama Kilolo, Mufindi na Iringa Vijijini, zina miundombinu migumu sana kuweza kufikiwa na hawa Wakaguzi. Kwa hiyo, utakuta wanafanya kazi kwenye mazingira magumu.

Ukija kwenye Manispaa yetu ya pale Iringa, kuna Shule 49 za Msingi na za Sekondari 16. Pamoja na kazi nzuri wanayofanya Kitengo kile, lakini hawana usafiri. Utakuta hawa Wakaguzi wanatumia magari yao wenyewe. Sasa labda tungeangalia hata Serikali iwasaidie angalau iwalipie tu mafuta waweze kufanya kazi zao, maana wanatumia fedha zao za mfukoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba pia Serikali iangalie changamoto nyingi zilizopo katika Vyuo vyetu Vikuu nchini. Kwanza kabisa, kuna ucheleweshaji wa fedha za mikopo, kucheleweshwa kuanza ratiba ya masomo pindi chuo kinapofunguliwa, ucheleweshwaji wa wahitimu ngazi ya stashahada, ukosefu wa masomo katika baadhi ya kozi, kukosekana kwa programu mbalimbali juu ya mafunzo ya ujasiriamali, uhaba wa nyenzo za kujifunzia, upungufu wa Walimu vyuoni, ulinzi na usalama vyuoni. *(Makofi)*

Mengi sana nimeyachangia maandishi, kwa hiyo, mtayaona na nimetoa na ushauri wangu.

Naomba nizungumzie kuhusu ukarabati wa shule kongwe. Serikali imeanza sasa kuzikarabati shule kongwe. Katika Mkoa wetu wa Iringa, kuna Shule Kongwe, Shule ya Malangali, Shule ya Tosamaganga na Shule ya Wasichana ya Iringa. Vilevile kuna Shule ya Wasichana ya Tabora na kuna Shule ya Lugalo.

Mimi nimesoma Shule ya Sekondari Lugalo. Mara nyingi sana nimekuwa nikiitembelea Shule ile, pamoja na kuwa kuna watoto wenye uhitaji maalum, lakini imekuwa haitengewi fedha kabisa. *(Makofi)*

Pale kuna watoto wasiiona, kuna watoto wenye ulemavu wa ngozi, lakini shule ile haina haitengewi fedha kabisa. Isitoshe vifaa vingi sana havipo katika ile shule vya kujifunzia na kufundishia na hata Walimu pia ni matatizo kwenye ile Shule. *(Makofi)*

Mimi ningeomba, safari hii waliletewa wale watoto wenye ulemavu wa viungo bila kuwa na taarifa, matokeo yake watoto wamepata *UTI* kwa sababu wanatumia vyoo na wale wanafunzi wa kawaida. Kwa hiyo, ningeomba iangaliwe. Vilevile Shule ya Lugalo, imewekewa programu ya kompyuta, lakini sasa na hawa watoto wengine nao wapewe hiyo programu ili wasijione kwamba wao wanatengwa na wenye ulemavu pia wanaweza kutumia kompyuta.

Kwa hiyo, mimi naomba iangaliwe kwa ukaribu sana ili wale watoto wenye ulemavu wasijisikie kwamba wanatengwa na jamii.

Ninataka nizungumzie kuhusu utaratibu wa Hamlamshauri zetu, kutenga fedha kwa ajili ya kulipia watoto yatima.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa na watoto yatima wengi, na huu utaratibu Halmashauri nyingi zimekuwa zikilipia hawa watoto kuanzia *form one* mpaka *form four.* Lakini watoto hawa wanapofaulu kwenda *form five, form six* na chuo kikuu hawalipiwi tena, wamekuwa wakipata shida sana katika vyuo vikuu, unaona mara nyingi wanakwenda kwa Wakuu wa Wilaya wanapewa zile *form*, lakini wanapata matatizo, walio wengi sasa wanaacha kusoma shule. Mimi naomba Serikali iweke mpango maalum endelevu wa kuwasaidia watoto yatima, ndiyo tutakuwa tumewasaidia kweli hata uyatima wao utakuwa umesaidiwa inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba shule za sekondari zilizo mbali zinawekewa mabweni? Kwa sababu utakuta watoto wengi sana wanapata shida, wanachukua nyumba mtaani, wanapata mimba sasa huko kwenye shule za mtaani. Ningeomba sana kwa kweli hili pia liangaliwe, shule za Kata zisizokuwa na mabweni sasa hivi ziwekewe mabweni ili watoto wa kike wapate haki ya kusoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niipongeze sana Serikali yetu kwa kujenga shule nyingi sana za Kata na vyuo vikuu katika Mkoa wetu wa Iringa. Lakini naomba niweke angalizo, kwa wale madalali, kumekuwa na tabia mbaya sana, madalali wanakuja kwenye Mkoa wetu, wanawarubuni watoto ambao wamefaulu na kwenda kuwafanyisha kazi za nyumbani.

Sasa mimi naomba niseme kwamba sasa hivi lazima uwepo mkakati, na niombe wale madalali wanaokuja kuchukua watoto wetu wa kike sasa ifike kikomo, wasije tena kuchukua watoto wa kike. Niseme kwamba Iringa hakuna shamba la watoto wa *house girls*, na sisi tutapambana nao. Basi naomba niunge mkono hotuba hii na niwatakie mafanikio mema katika utekelezaji wake. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Asante sana, nakushukuru sana Mheshimiwa Ritta Kabati. Mheshimiwa Prof. Kahigi, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwalimu Marombwa kuwa mchangiaji wa mwisho. Mheshimiwa Kanalwanda!

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii nami nizungumze kidogo kuhusu Wizara hii ambayo ina Changamoto nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nianze kwa kuungana na Wabunge wenzangu pamoja na Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Huduma za Jamii kuzungumzia uundwaji wa chombo kimoja cha kumhudumia mwalimu. Jambo hili limezungumziwa sana na Kamati toka tuanze Bunge hili.

La kushangaza sana ni kwamba, Wizara haijatusikiliza kabisa kabisa, na Mwenyekiti wetu tumekuwa tukimtuma kwenda kule kuwakumbusha lakini haijatusikiliza kuhusu jambo hili na badala yake inakuja na mipango ambayo wala haijapitishwa kwenye Kamati wala kukubaliwa na Kamati. Kwa mfano ukurasa wa 7 wa hotuba ya Waziri, imeaandaa Muswada wa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Kitaalam ya Waalimu Tanzania.

Halafu ukurasa unaofuata ina kitu ambacho inakiita Muswada wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Ithibati na Udhibiti wa Ubora wa Elimu ya Msingi. Tulipokwenda Kenya, Tume ya huduma za Waalimu Kenya inashulika na haya yote. Kwa hiyo naomba nisisitize ambayo yamesemwa na Mwenyekiti wa Kamati yetu na Wabunge wengine kwamba tunataka Wizara ianzishe chombo kimoja cha kumhudumia mwalimu ili haya malalamiko haya yote yashughulikiwe na chombo kimoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika,tumezungumza hapa, Wabunge wengi sana wamesema kwamba elimu imeporomoka, ubora wake umeshuka. Mimi ningependa tu kuonesha mifano miwili ya viashiria vya kushuka huku. Wale ambao walisoma zamani, kina Mheshimiwa Wasira, Mheshimiwa Mkuchika na wengine, mnafahamu kwamba zama hizo Tanzania ilikuwa juu sana kuhusiana na utamaduni wa kusoma, kusoma vitabu tu, na vitabu vilikuwepo na watu walikuwa wanaandika vitabu. Lakini siku hizi utamaduni wa kusoma umeporomoka. Hivi hata humu Bungeni, wangapi ambao wanasoma vitabu! Lakini mnaposafiri kwenye ndege kwenda huko ng'ambo wengine si mnawaona na vitabu wanasoma kwenye viti vyao? Mnawaona wanasoma lakini sisi wenyewe tukiende huko tumekaa kwenye viti tu, unaona. Kwa hiyo utamaduni wa kusoma umeporomoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha pili, utamaduni wa uandishi umeporomoka, watu hawaandiki. Hivi hata hawa maprofesa waliomo humu wangapi

wameandika vitabu? Mwaka wa jana afadhali Prof. Mwandosya alituonesha kitabu ambacho ameandika akiwa Mbunge hapa. Mimi ninavyo vitatu vinatoka hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo ni viashiria kwamba elimu yetu ina matatizo, wanafunzi hawafundishwi kusoma vizuri, hawafundishwi kupenda kusoma toka wakiwa wadogo. Hakuna maktaba katika shule zetu. Ni kweli kwamba Dkt. Mcharazo anasambaza vitabu kwenye maktaba, anafanya kazi nzuri sana, lakini sisi watu wazima tunazitembelea hizo maktaba za Wilaya au za Mikoa? Hatuendi huko, sana sana utakuta watoto wa shule wanajisomea labda kwa ajili ya mitihani yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, uandishi wa vitabu umeporomoka, vitabu haviandikwi kama zamani. Kwa hiyo ni viashiria viwili vya kuoesha kwamba jamani elimu hii imeporomoka inahitaji mkakati mzito kabisa wa programu za usomaji na uandishi kwenye ngazi zote za shule za msingi na sekondari ili uwaandae watu wakifika kwenye vyuo vikuu waweze kuandika vizuri, waweze kuandika kwa mantiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku hizi mkisoma tasnifu zinazoandikwa na wanafunzi wa vyuo vikuu wa shahada ya pili, mtashangaa sana zimejaa mambo ya ajabu, mwalimu lazima ukae pale ujaribu kuelewa huyu mwanafunzi anasema nini, haya ni matokeo ya kuporomoka kwa utamaduni wa kusoma na kuandika. Kwa hiyo naomba Wizara labda itueleze masuala haya itayashughulikiaje, kwa sababu hata kwenye vyuo vikuu si salama. Kwenye ukurasa wa 42 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri anazungumzia *Literacy and Numeracy Education Support Programme* ambayo kwa kifupi inaitwa *LENS* kwa kifupi ambao umelenga kuboresha KKK kwenye darasa la kwanza na la pili. Mimi nilikuwa napenda kufahamu, mna mradi wa kuboresha kusoma, kuandika na kuhesabu kwenye darasa la kwanza na la pili tu, sasa baada ya hapo kuwe nini, yaani programu za baada ya hapo zitakuwaje? Kwa sababu fedha yote mmeiweka kwenye darasa la kwanza na la pili, Je, hapo tu ndipo kwenye matatizo, baada ya hapo hakuna matatizo?

Naomba niende kwenye vyuo vikuu: Vyuo vikuu OC haziendi. Naomba hilo lishughulikiwe. Posho za nyumba za waaalimu haziendi. Na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mabweni yake yaani yamechakaa, mengine nadhani karibu yataanguka. *(Makofi)*

Halafu, kuna wahitimu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wa Saikolojia hawapati ajira, eti sababu inayotolewa kwamba wana somo moja tu, sasa kama ni somo moja kwa nini mtaala uliundwa hivyo? *(Makofi)*

Halafu kuna tatizo lingine la Chuo Kikuu, wengine wanadhani kwamba kuporomoka kwa elimu kupo kwenye ngazi za chini tu, hapana, hata kwenye vyuo vikuu, kuna upungufu mkubwa sana wa walimu. Leo hii asubuhi Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari anasema kwamba mimi nafundisha UDOM, mimi sifundishi, sijaajiriwa kule, nasaidia tu kama tunavyosaidia tunapohitajika, lakini kwa sababu kuna upungufu wa waalimu. Kwa hiyo hilo suala pia naomba majibu; je, Serikali inafanyaje kuwa-*train* hawa waalimu wa vyuo vikuu?

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kwamba labda kungefanyika tathmini. Wizara iandae kufanya tathmini kwenye vyuo vikuu vyote, hasa kuhusiana na ubora wa elimu inayotolewa kwenye vyuo vikuu, kwa sababu ni muhimu sana. Najua kwamba Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinafanya jambo hili, lakini vyuo vikuu sasa hivi hapa nchini ni vingi sana na kunahitajika kufanyika tathmini ya kiwango cha elimu kinachotolewa na ubora wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye Jimbo langu Bukombe. Wizara imetuahidi Bukombe kwamba tutapata Chuo cha Ufundi, tulikuwa miongoni mwa Wilaya 28, sasa tutapata lini chuo cha ufundi?

**NAIBU SPIKA:** Asante Profesa!

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Asante sana.

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana sana. Mchangiaji wetu wa mwisho Mwalimu Marombwa atatufungia kipindi chetu cha uachangiaji cha Waheshimiwa Wabunge.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangi katika bajeti hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Kwanza nianze kwa kumshukuru sana Rais kwa kuweka safu mpya katika Wizara hii. Mimi naamini *composition* hii iliyopo kwenye Wizara hii, mafanikio makubwa sana yanaweza kupatikana kwa muda mfupi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, wenzangu wamesema hapa sasa hivi watoto wetu wanakaa kwenye mawe, wako kwenye enzi ya mawe: Mimi nadhani iwe ni aibu kwa Mbunge kusema kwamba mimi katika jimbo langu watoto wanakaa kwenye mawe, wapo kwenye enzi ya mawe. Wewe kama Mbunge jukumu lako ni nini? Unafanya kazi gani huko jimboni, kwa sababu wewe ni Mjumbe wa Halmashauri ya Wilaya? Kaa utafakari uone kwamba kuna

matatizo moja, mbili tatu katika jimbo langu, tunafanya nini kuweza kuyatatua matatizo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nikueleze tu, kwenye jimbo langu nimeshatumia fedha nyingi sana kwa ajili ya kuimarisha shule za msingi kuwapatia maji, na juzi tu Wabunge wa Wilaya ya Rufiji tumetoa tani 50 za *cement* kwa ajili ya kujenga maabara katika shule zetu za sekondari, juzi tu. Sasa watu watakaokuja hapa na kusema watoto sasa hivi wako enzi ya mawe tujiulize, wewe una sifa gani ya ubunge, unafanya nini? Pambana kuhakikisha kwamba hilo jimbo lako na Wilaya yako inakwenda mbele, kazi yako ni kutatua matatizo, kazi yako si kuelezea hata tatizo la madawati, litatue! *(Makofi)*

Mheshimiwa NaibuSpika, mimi nizungumzie…

**NAIBU SPIKA:** Mwalimu naona ujumbe huo Waheshimiwa wanataka urudie kidogo sijui, hebu! *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wameusikia. Wameusikia, kwa sababu dakika ni chache.

Mheshimiwa Naibu Spika nizungumzie maendeleo ya elimu yetu…

**TAARIFA**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Marombwa naona Mheshimiwa Cecilia Pareso!

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumpa taarifa, kazi za Mbunge zinajulikana, kazi ya Mbunge si kwenda kutengeneza dawati, kutafuta *cement*. Kwa mujibu wa Katiba kazi ya Mbunge ni kuisimamia na kuishauri Serikali ndiyo maana tunasema hapa.

**MBUNGE FULANI:** Na kutengeneza madawati pia!

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Ni Afisa Mahusiano pia!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Marombwa, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, huo ni upungufu, jua wajibu wako wa Mbunge ni nini. Huo ni uipungufu. Wewe kazi yako pamoja na kuisimamia lakini na kuhangaika, kila kona ya nchi yetu, kila kona ya dunia hii kuhakikisha kuwa unasaidia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya jimbo lako, hiyo ndiyo kazi yako. *(Makofi/Kelele)*

Mheshimiwa Naibu Spika,…

**TAARIFA**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa hebu tuache kelele, tusikilizane tafadhali, *order*. Mheshimiwa nani, jitambulishe! Mheshimiwa unahama hama. Mheshimiwa wenje, huko si kwako, haya sema.

**MBUNGE FULANI:** Aondoke! Arudi kwake!

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe huyu mzee taarifa, Mheshimiwa Marombwa.

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Hamna mzee humu ndani!

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba Mbunge hakusanyi kodi, pamoja na kwamba kazi ya Mbunge siyo kutengeneza madawati na Mbunge hakusanyi kodi, jimboni kwangu mimi Wenje naweza nikawa Mbunge wa kwanza kutengeneza madawati mengi Tanzania. *(Kicheko/Makofi)*

Mwaka 2011 nimetengeza madawati…

**MBUNGE FULANI:** Waambie CHADEMA wenzio hao!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Wenje,…

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mwaka 2012 nimetengeneza madawati 400 jimboni. Kwa hiyo pamoja na kwamba sikusanyi kodi, lakini hayo yote nimefanya. Naomba nimpe huyu mzee taarifa aelewe. Na yeye jimboni kwake wanafunzi wanakaa chini, ni aibu, halafu anakuja hapa kujisifia sifia wakati wanafunzi wanakaa chini jimboni kwake.

**MBUNGE FULANI:** Wamesikia CHADEMA wenzio hao!

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Taarifa kwa Pareso hiyo!

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa naomba tusikilizane. Kwa kweli Mheshimiwa Wenje hukuwa unatoa taarifa, ulikuwa unachangia na nilishakupa nafasi ya kuchangia. Mheshimiwa Marombwa na yeye ana *right of opinion*, kabisa, lazima Kiti kimlinde mawazo yake. Tunaruhusiwa kuwa na uhuru wa mawazo humu ndani. Mheshimwia Marombwa pokea taarifa hiyo endelea kuchangia. Naombwa asiguswe tena baada ya hapo. Mheshimiwa Marombwa changia.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Wenje, kumbe lile ambalo nilikuwa nalizungumza mimi linawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, dakika zangu unilinde. Mimi nizungumzie masuala ya ufaulu wa wanafunzi katika shule zetu. Kwa muda mrefu shule zetu, hasa za Sekondari, zilikuwa na upungufu mkubwa sana wa waalimu, na matokeo yake, kutokana na upungufu huo ufauli wa watoto wetu ulikuwa ni mdogo sana. Lakini mimi niishukuru Serikali, kwa miaka hii minne/mitano kwa kweli waalimu wengi wameandaliwa na wamepelekwa katika shule zetu za sekondari. Kwa mfano mwaka huu katika Wilaya yangu ya Rufiji sina shule ya sekondari iliyo na walimu chini ya kumi, haipo. Sasa naamini kwa idadi hii kubwa ya waalimu itaweza kwa kiasi kikubwa sana kupandisha matokeo ya wanafunzi wetu wa shule za sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na ufaulu huo, kuna changamoto nyingi ambazo zinasababisha watoto hawa washindwe kufaulu vizuri. Ukichukua Kitabu cha Taarifa Kuhusu Mtihani wa Kumaliza elimu ya Msingi Mwaka 2013 kilichoandaliwa na Baraza la Mitihani, na kitabu kingine cha Taarifa Kuhusu Ufaulu wa Watahiniwa katika Mtihani wa Kidato cha Nne Mwaka 2013, kuna changamoto nyingi sana. Changamoto kubwa ambayo inaoneshwa katika taarifa hizi ni kwamba karibuni mada zote zinazofundishwa katika shule za sekondari na shule zetu za msingi, kwa kweli wanafunzi wengi wanafaulu chini ya wastani.

Kwa mfano ukichukua katika elimu hii ya sekondari, masomo yote kasoro somo la Kiswahili mada zote zilizotolewa katika mtihani wa kumaliza elimu ya sekondari, kule mwishoni maoni yake ni kwamba watoto hawa matokeo yao ni hafifu, hafifu, hafifu, hafifu, hafifu kwa masomo yote na kwa mada zote.

Mheshimiwa Naibu, hii inatufundisha nini? Mimi ninaamini kwamba inawezekana kukawa kuna tatizo na tatizo hili linawezekana kwa kiasi kikubwa sana linachangiwa na maeneo mengi. Lakini mimi niliangalie eneo la walimu; ukiangalia matokeo haya yanaonesha wazi, kwamba kwa nini matokeo yanakuwa hafifu. Ukipita katika kila mada matokeo ni hafifu hafifu hafifu! Je, walimu wetu wana uwezo wa kutosha wa kufundisha mada hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninafikiri ifikie hatua sasa Serikali, wenzangu wamezungumzia kwanza kuwepo na *in service training. In service training* inasaidia sana. Mwalimu toka anapoanza kazi mpaka anamaliza kazi, hajaenda kozi yoyote, mafunzo yoyote kazini kwa miaka yote hata mara moja. Huyu mwalimu atafanya kazi namna gani. Kweli ana uwezo wa kufundisha mada hizi vizuri, kwa sababu mitaala inabadilika, mada mbalimbali zinabadilika,

lakini mwalimu ni yuleyule aliyejifunza miaka 20 iliyopita ndiye anaendelea kufundisha katika shule zetu hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nilikuwa napendekeza kwa wenzetu Wizara ya Elimu, ikae ijiipange. Matokeo haya kila mwaka hayaendi mbele, kwa nini yamekuwa *stagnant* hapa hapa, kwa nini hayaendi mbele? Hebu tuchukue. Siyo kwamba walimu wana mgomo, hapana. Mimi nina imani mafunzo kazini ni ya muhimu. Ninaomba sana mafunzo yatolewa kwa walimu wetu ili yaweze kusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa hivi kuna mpango ulioanzishwa wa kuanzisha *Diploma in Primary Education*. *Diploma* hii ni nzuri sana, inamfanya mwalimu huyu wa shule ya msingi, aliyemaliza darasa la kumi na mbili, asomee masomo yale yale ya elimu ya msingi ili akirudi baada ya miaka miwili ya *Diploma*, aweze kufanya vizuri.

Naishukuru Serikali hili imekubali kulishughulikia na imeanza mwaka huu. Lakini ombi langu, ada ni kubwa. Walimu hawa wanajilipia wenyewe, Halmashauri zetu hazitoi pesa. Mimi nilikuwa ninaomba ada ile ni kubwa, na ni vizuri kwa walimu hawa…

**NAIBU SPIKA:** Asante sana Mwalimu Marombwa, najua unayo mengi. Lakini nakushukuru sana kwa mchango wako. Umechangamsha Bunge kidogo. Sisi watu wa Dodoma hapa tuna msemo, nikiutafsiri kwa Kiswahili wanasema "mbwa aliyekonda ni aibu ya mwenye mbwa". Kwa hiyo kama watoto wako wanakaa juu ya mawe, aibu ya Mbunge. *(Makofi/Kicheko)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. RACHEL R. MASHISHANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Matokeo Makubwa Sasa huku walimu ni kipaumbele cha mwisho tena namba tisa, Serikali inategemea nini? Walimu wanafanya kazi katika mazingira magumu hawana posho za kufundishia, mazingira si rafiki ya kufundishia hakika Matokeo Makubwa Sasa itakuwa ni ndoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejaliwa kuwa na shule nyingi sana, lakini shule bila vitendea kazi, bila walimu ni kazi bure. Nyumba za walimu hakuna, hii Serikali ina mkakati gani kuhakikisha mazingira ya wanafunzi na mwalimu yanakuwa rafiki?

Mheshimiwa Naibu Spika, wingi wa shule za misingi na sekondari uendelee na ajira zinazotolewa kila mwaka, walimu tunao wengi sana lakini Serikali imekuwa ikiajiri mafungu mafungu na kuacha wengine wakihangaika

mtaani, kuna tatizo gani Serikali kama ipo *serious* kuajiri walimu wote wanaotoka vyuoni?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo gani Serikali kukosa fedha ya kuchapisha vitabu ili visambazwe mashuleni, shule zingine hazina vitabu, mnategemea Matokeo Makubwa Sasa (BRN) ita-*work,* bajeti yenyewe ni ndogo na kibaya zaidi fedha zaidi ya nusu inatoka kwa wahisani, mnapanga mipango wakati fedha hamna mkononi hapa hakuna Matokeo Makubwa Sasa ni madogo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya ukosefu wa walimu wa sayansi sasa imekuwa kero hapa nchini, mfano mkoa wa Shinyanga hauna kabisa walimu na kama wapo hawazidi 50; hili ni jambo la kusikitisha sana, tunategemea kupata wahandisi kweli hapa?

Naomba Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza walimu na sayansi pengine kwa kupunguza ada kwa masomo ya sayansi ili wanafunzi wengi kusoma na kufundisha wenzao watakapomaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, maabara zimekuwa ni kiini macho tu. Shule zinajengwa lakini hazina maabara, sasa haya Matokeo Makubwa Sasa yatapatikanaje au ni ndoto za alinacha? Serikali naomba iwekee msukumo suala la maabara ili liendane na utitiri wa shule zetu zinazojengwa kila kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwepo kwa shule nyingi bado ukaguzi umekuwa hauridhishi kwani wakaguzi wamekuwa hawana vitendea kazi na kibaya sasa ofisi zimekuwepo lakini hazina wakaguzi. Naomba Serikali iongeze wakaguzi, shule zetu hazikaguliwi. Manispaa ya Shinyanga haina sekondari kidato cha sita yaani *A-Level,* ni lini sasa Serikali itaanzisha sekondari kwa ajili ya kidato cha tano na sita?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa machache haya naomba kumalizia kwamba mzigo mzito wa masomo yanayosomwa na wanafunzi wa darasa la kwanza upunguzwe, mbona sisi tulisoma masomo matatu? Kuna faida gani au Serikali imeona kiwango cha elimu kinakuwa au kinashuka?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ZAYNAB M. VULLU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote niunge hoja mkono hoja ya Wizara ya Elimu.

Pamoja na kuboresha elimu katika viwango mbalimbali, naomba Serikali ichukue maoni na mapendekezo au ushauri wa kuboresha elimu katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa la walimu wa masomo ya sayansi, ni juhudi zipi ambazo Serikali imeweka ili kuhakikisha walimu wa masomo ya sayansi yanaongezeka sambamba na walimu wa shule wanayofundisha masomo ya sayansi za kisayansi katika shule zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi wa shule unasaidia kuleta ufanisi kwa wanafunzi wote wa shule pia kujua walimu nao wanawajibikaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua shida zote wanazopata walimu wetu, ni vipi Serikali imejipanga kwenye kupunguza makali ya hayo matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda kumpongeza Mheshimiwa Mama Salma Kikwete kwa juhudi na mchango wake kwa jamii katika kuhakikisha shule ambayo ameianzisha wanapata elimu bora na ya kiwango cha kitaifa, kwani shule hiyo imeonyesha mfano wa kufaulisha watoto wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya.

Pamoja na kazi nzuri inayofanya ukweli uliopo ni kuwa kuna matatizo mengi ya kisera na kimfumo, matatizo ambayo yanaporomosha elimu katika nchi hii. Baadhi ya matatizo yanahitaji ufumbuzi haraka ni haya yafuatayo:-

Kwanza, ni upungufu wa walimu hasa shule za vijijini walimu wanapangwa wengi mijini na wakati mwingine walimu wa vijijini wanahamishiwa mijini hasa walimu wa kike. Baadhi ya walimu ni watoro na wengine walevi kiasi kwamba ufundishaji unathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ukaguzi ni muhimu sana lakini halipewi uzito unaostahili na hivyo shule nyingi hazikaguliwi jambo ambalo linasababisha walimu wajisahau kwa kuendeleza ulevi na uzembe, nasisitiza wakaguzi wapatiwe usafiri wa uhakika hata ikibidi usafiri wa pikipiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu wamekufa moyo kutokana na kutolipwa haki zao na stahili zao mbalimbali madai ya walimu yatatatuliwa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala la madeni ya walimu litaisha lini? Tatizo ni Serikali au walimu wenyewe kwani Serikali inadai madeni yanalipwa lakini

walimu wanaendelea kudai madeni yao. Nani mkweli Serikali au walimu? Naomba jibu.

Pili ni upungufu mkubwa wa walimu wa sayansni nalo ni tatizo ambalo linahitaji kupewa kipaumbele aidha kutokuwepo kwa maabara kunazidisha tatizo la ubora wa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ufundishaji mashuleni uwe wa kutumia lugha ya Kiswahili, tuondokane na kasumba ya kimagharibi ya kudhani kiingereza kitaboresha elimu. Nchi nyingi duniani zinatumia lugha zao kufundishia mashuleni kwa mfano, Urusi, China, Vietnam, nchi za Kiarabu na baadhi ya nchi za Kiafrika kama Afrika Kusini, Zimbabwe na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri tufanye uamuzi sasa kutumia lugha ya kiswahili kufundihsia mashuleni.

Suala la chakula cha mchana kwa wanafunzi ni muhimu na linasaidia kuimarisha mahudhurio shuleni na kuwafanya wanafunzi wazingatie masomo.

Mheshimiwa Naibu pika, yote haya na mengine yatafanikiwa kama Wizara hii itapatiwa bajeti ya kuridhisha na kwamba fedha zinazotengwa basi zipelekwe Wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. NAMELOK E. M. SOKOINE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara ya Elimu irejeshe muundo uliokuwepo awali, tuwe na Wizara ya Elimu inayoshughulikia masuala ya elimu ya awali, msingi, sekondari, vyuo vya elimu na vyuo vya ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Elimu ya Juu itakayoshughulikia Vyuo vya Elimu ya Juu vyote na utafiti, hivi sasa Vyuo vya Elimu ya Juu vimetawanyika na vingine vipo Wizara ya Mawasiliano vingine vipo Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, hivyo kukosa usimamizi thabiti kwa sababu elimu siyo *co-business* za Wizara hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Monduli ni moja ya Wilaya yenye mahitaji ya Chuo cha *VETA*. Je, ni lini Wizara ya Elimu itajenga Chuo cha VETA katika Wilaya hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARGARET A. MKANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nyongeza ya niliyochangia kwa kusema ni kama ifuatavyo:-

Naunga mkono ushauri wa Kamati kuwa Serikali ione uwezekano wa kuanzisha Tume ya Utumishi wa Walimu ili waweze kuhudumiwa ipasavyo na kuwezesha Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa kufanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Wizara au Serikali kwa ujumla ipandishe hadhi Kitengo cha Elimu Maalum pale Wizara kuwa Idara ya Elimu Maalum au Kurugenzi iweze kujitegemea na kuweza kushauri vizuri masuala ya wenye ulemavu yanavyopaswa kuwa ndani ya Taifa zima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa walimu wa taaluma ya elimu maalum ni wachache nchini kuweza kuwahudumia watoto/wanachuo wenye ulemavu, napendekeza somo la elimu maalum lifundishwe kwa wanachuo wote wanaosomea ualimu katika vyuo na ngazi zote za elimu ili wenye ulemavu wasikose kupata elimu bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia ni sababu ya Wizara mama ya Elimu kusahau kabisa angalau maneno "wenye ulemavu" ndani ya hotuba nzima. Kwa msingi huo siungo mkono hoja mpaka nitakapopata majibu ya kuridhisha kwa vipengele vyote katika hotuba hii.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii na mimi niweze kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara hii. Napenda niishauri Serikali iangalie sana shule za watu binafsi, shule hizi zinapandisha ada bila ya mpangilio hivyo basi kila mwaka utaona ada zao zinaongezeka jambo ambalo limekuwa ni kero kwa wazazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya shule wanafunzi wanashindwa kwenda shule kwa sababu ya kukosa vyoo. Jambo hili linasikitisha sana kuwa shule zinafungwa kwa sababu ya kukosa vyoo. Jambo hili linafanya watoto kupata shida sana kiasi cha kuweza kuacha shule. Naiomba Serikali jambo hili ilione kuwa ni kikwazo kikubwa cha kusababisha kuporomoka kwa elimu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nizungumzie kuhusu mishahara ya walimu. Walimu wa nchi hii wanaishi katika mazingira magumu sana, mishahara ni midogo kukidhi haja na wanapokuwa katika hali hii ngumu ya kufikiria ugumu wa maisha waliyonayo wanshindwa kufundisha vizuri. Watakapoongezewa mishahara wakapungukiwa na ugumu wa maisha basi ni dhahiri kuwa wataweza kufundisha vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia kuhusu upungufu wa walimu wa sayansi, hata wanafunzi wengi sana wanasoma masomo ya *art* na wanafanya hivi kwa kukosa misingi mizuri ya mafunzo ya elimu ya sayansi wakiwa shule, hivyo naomba Serikali iwapembue wanafunzi walio na vipaji

mapema na kuweka pamoja na kuwapatia walimu wazuri wa sayansi ili tuweze kuwatayarisha vizuri.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri kwa hotuba nzuri, pia Naibu Waziri kwa jitihada zake katika kuboresha elimu hapa nchini. Niwapongeze watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na utendaji wao mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ndiyo ufunguo wa maisha. Mimi ningeanza mchango wangu kwa kuzungumzia suala la ukaguzi wa shule katika Halmashauri zetu umekumbwa na changamoto kubwa sana ya kukosa vitendea kazi. Kwa kuwa shule ya nyingi za msingi na kata zipo vijijini sana ni vema Idara ya Ukaguzi wakapewa usafiri wa uhakika na bajeti za mafuta ziwe za kutosha ili kuwezesha kazi ya ukaguzi kufanyika.

Katika Wilaya ya Geita ipo changamoto kubwa sana katika idara hii na katika mkutano wa mwaka na Chama cha Walimu Wilaya ya Geita walizungumzia hili tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ielekeze nguvu zake katika Idara ya Ukaguzi na hii itasaidia kuboresha utendaji kazi kutoka shule zetu. Kwa kuwa Wizara ya Elimu ipo katika mpango wa BRN ninaamini mafungu yapo hivyo tuboreshe Idara za Ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, idara nyingine ambayo ipo nyuma sana ni Idara ya TSD. Idara hii ipo na changamoto kubwa sana, ninaomba Serikali Kuu iiangalie idara hii kwa uzito kwani ndiyo inayoshughulikia masuala ya nidhamu ya walimu.

Jambo la pili linahusu Vyuo vya Elimu ya Ufundi, katika hotuba ya Waziri ukurasa wa 60 inazungumzia kuanzia ujenzi wa vyuo vinne inazungumzia kuanza ujenzi wa vyuo vinne vya VETA katika Mikoa mipya ikiwepo Mkoa wa Geita. Jambo hili ni jema na ninapenda kushukuru kwa mpango huu. Mkoa wa Geita, umeundwa kwa Wilaya ya Geita, Nyang'wale, Mbogwe, Chato na Wilaya ya Bukombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya zote nilizozitaja hazina Chuo cha VETA na hii inapelekea uhitaji mkubwa sana wa kuwa na Vyuo vya VETA. Sera ya Taifa ni kila Wilaya kuwa na Chuo cha VETA. Pamoja na kuwepo kwa mpango wa ujenzi wa Chuo cha VETA Mkoa lakini napenda kujua tu ni lini sasa Serikali itajenga Chuo cha VETA katika Wilaya zote tano za Mkoa wa Geita ikiwemo Wilaya ya Geita?

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kutokana na uhitaji mkubwa wa vijana wetu wanaohitimu kidato cha nne wanahitaji kupata ufundi stadi ili kuweza kumudu maisha yao.

Mheshimiwa Spika, ninahitaji nipate ufafanuzi juu ya haya wakati wa majumuisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache naunga mkono hoja.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii inabebeshwa lawama kubwa kuhusu kushuka kwa elimu na ni kweli. Bila kujenga msingi mzuri wa mfumo wa utoaji elimu na kujenga motisha kwa walimu hali haitabadilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa maelezo, ushauri na maombi katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, msingi urekebishwe kwa kupunguza idadi ya masomo kwa wanafunzi, pili, jitihada za kuongeza idadi ya wanafunzi ifanyike na hasa shule za vijijini ambapo huduma za jamii ni duni na tatu, motisha kwa walimu ikiwa pia ni mishahara posho na malipo ya awali kuwezesha walimu kuenda katika maeneo waliyopangiwa na malipo ya kustaafu yafanyike kwa wakati na kwa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, mafunzo kwa walimu yaendeshwe kuongeza upeo na mabadiliko ya kitaifa na dunia, tano, uhamisho wa walimu ufanyike kwa msingi wa busara badala ya kukomoana na chuki miongoni mwa watendaji na wasimamizi katika sekta na sita, ukaguzi wa shule ufanyike kwa usimamizi wa Wizara ya Elimu badala ya kuachia jukumu hilo kwa Halmashauri za Wilaya ambapo magari na mafuta hayatolewi, kiwepo kitengo maalum cha ukaguzi ndani ya Wizara yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo nimetumia fedha za Mfuko wa Jimbo Wilayani Muheza kufanya yafuatayo:-

(a) Nimenunua *mobile laboratories* tano kwa shule tano za sekondari miongoni mwa shule zisizokuwa na maabara.

(b) Kutokana na mkakati mpya wa Wilaya ya Muheza wa kuhamasisha ujenzi wa maabara katika shule zote za sekondari Wilayani kwa mwaka huu wa fedha nimetoa mabati 100 kwa shule 17 za sekondari na jumla mabati 1700, geji 28 – wastani shilingi 40,800,000/=. Mkakati ni kuendelea kutumia fedha za Mfuko wa Jimbo kusaidia mabati katika shule nyingine saba za sekondari ambazo hazijapata msaada huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Mfuko wa Elimu, UNESCO na Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu watasaidia vipi jitihada za Halmashauri ya Wilaya ya Muheza na Mfuko Wa Jimbo katika mkakati wa ujenzi wa maabara kwa shule zote za sekondari mwaka 2014/2017?

Mwisho nashauri pia Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu uwe karibu sana na Bodi za Shule za Sekondari kuona matatizo.

Ushauri na mapendekezo yanayojitokeza katika shule na ambapo ushauri unatolewa na haufanyiwi kazi hivyo kudhoofisha uwezo wa vikao vya Bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kutokana na umuhimu wa elimu Kitaifa na kwa watoto wa Tanzania.

**MHE. DKT. HAJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono na napongeza Wizara kwa mpango wa Serikali wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN). Lakini naiomba Serikali iongeze jitihada ya kutatua matatizo ya walimu ambayo kila mwaka yanazidi kuongezeka. Mfano madeni na upungufu wa nyumba za kusihi hasa wale wanaoishi vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Ulanga Magharibi lina shule ya sekondari kata *(form one* mpaka *four)* zipatazo 14 lakini hatuna sekondari ya juu *(high school),* mabweni katika shule ya sekondari ya Kipingo - Malinyi na Igota ili sekondari hizo zianze kutumika kwa kusajili na kutoa mafunzo ya *high school (form five – six)*. Ahsante sana.

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kwanza nimshukuru Mungu kwa kunijalia afya njema kiasi cha kufikia kuchangia bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na Kamati ya Huduma za Jamii ambayo kwa pamoja wameungana na Wizara na kuweza kufanikisha bajeti/hotuba na taarifa yenye mwelekeo mzuri na wenye matumaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa shule nyingi za Kata hazipati masomo yote kikamilifu hasa somo la sayansi ambalo linakosa walimu na vitendea kazi pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikwazo kikubwa kinachosababisha hasa kwa sayansi ni ukosefu wa umeme, hivi sasa kwa vijiji vilivyo kando ya barabara kuu kutoka Mtwara hadi Masasi, vimebahatika kupata umeme. Lakini kwa bahati mbaya umeme huu haujafikishwa mashuleni. Hivyo naiomba Serikali ihakikishe shule hizo zinapata umeme ili somo hili la sayansi lifundishwe ipasavyo yaani kwa nadharia na vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia niongelee mambo ambayo kwao yanaweza kuwa sababisho la matokeo yasiyoridhisha kwa wanafunzi moja inawezekana kuwa walimu kutopewa mishahara ya kuridhisha, pili walimu kutopewa motisha kwa kazi za ziada, kutopata mahitaji muhimu kama vile nyumba, vitendea kazi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile hawapewei nafasi za masomo ili kuinua viwango vya elimu, baadhi yao waliishia kwenye shule za msingi na kwamba wanahitaji kupata diploma baada ya sekondari.

Vilevile kwa upande wa wanafunzi kuwa wanatoka katika familia duni ambapo wanakosa mahitaji muhimu kama vile sare, lishe duni na kadhalika. Hivyo ni budi Serikali ifanye juhudi ya kurekebisha haya. Ahsante  sana.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupatiwa majibu ni lini Serikali italipa madeni ya walimu shilingi milioni 60?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali isisubiri mgomo wa walimu ndipo ishtuke suala hili linafukuta sana, naomba majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu wanaoishi na kufundisha katika mazingira magumu Serikali katika bajeti iliyopita ilipitishwa hapa Bungeni kuwa watalipwa posho kwa walimu hao shilingi 500,000/=. Fedha hizo hazilipwi na malalamiko ni mengi naomba maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu wengi wanapandishwa madaraja, mishahara yao hailipwi sambamba na kupanda madaraja yao, naomba maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, malipo ya uhamisho wa walimu yalipwe kwa wakati bila kuchelewesha ikiwa ni pamoja na fedha za malimbikizo yao fedha ya likizo, pia naomba maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchache wa walimu wa sayansi katika shule za sekondari za kata na hasa Mkoa wa Rukwa hii ni kutokana na kuwa pembezoni mwa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya walimu waliopo katika vyuo vya kutopatiwa ajira wakati wamefaulu vizuri na ukilinganisha watumishi wengi wanapangiwa Mkoa/Mikoa kwa nini sasa wanafunzi wanaotoka katika Mkoa Rukwa na wamesoma na kumaliza Vyuo vya Ualimu kwa nini wakose ajira

wakati tuna upungufu wa walimu? Naomba maelezo au ukitaka nikuletee majina, nipo tayari kuleta.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakaguzi wapewe zana za kuwawezesha wafanye ukaguzi wao kama vile pikipiki, mafuta na posho, vilevile ofisi na makazi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Sumbawanga haina hata Chuo kimoja cha Ufundi - VETA. Nilishaomba majengo ya wakufunzi wa barabara naomba nijibiwe kwa nini Serikali isiyatumie majengo hayo kuanzisha? Chuo kimoja cha VETA.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu kwani Mkoa wa Rukwa upo nyuma sana kielimu, hii ni kutokana na ukosefu wa mkuu wa walimu wa kutosha na hasa walimu wa sayansi, tunaomba Serikali kuweka kipaumbele kwa Mikoa iliyopo nyuma kiuchumi na hasa Jimbo langu la Wilaya ya Sumbawanga Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ufafanuzi wa maelezo kwa yale niliyoyatolea kero.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuchangia kwenye maeneo yafuatayo:-

Kwanza ninaomba kuleta kilio cha wanafunzi wa elimu ya juu kuhusu mpango wa kutoa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu kwa kuweka madaraja ambapo kwamba wapo wanaopatiwa mikopo kwa 100% wapo wanaokopeshwa 80% au zaidi ya 50% lakini wapo pia wenye 0% yaani ambao hawapewi kabisa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishwaji wa kutoa mikopo kwa madaraja ulikuwa na nia njema. Hata hivyo utekelezaji wake umekuwa hauendani na hali halisi kuna kipimo gani kinachotumika kutoa mikopo ya 100% kwa baadhi ya watoto wa vigogo ili hali kuna watoto waliotoka kwenye maisha duni hawakopeshwi kabisa?

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe Wizara hii ifanye juhudi za makusudi na hiyo ni kama Bodi hii ya Mikopo wanadhani kwamba jambo hili halipo waende Chuo Kikuu cha Mzumbe ili kujiridhisha na jambo hili. Ni hdhiri kwamba Bodi ya Mikopo imeendelea kuwa na mfumo mbovu wa kutoa mikopo kwa wanafunzi maana inalenga kubagua na kuleta chuki miongoni wa wanafunzi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuiomba Serikali na kuishauri kwamba kama Bodi ya Mikopo imeshindwa kuwatendea haki wanafunzi wa elimu ya juu ni vizuri huu mfumo ukabadilishwa ili wanafunzi wote wapewe mikopo hata kama italazimika kutoa asilimia 50 kwa kila mwanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya Wizara hii imeanzisha kuwepo kwa changamoto ya upatikanaji wa wataalam wa Kitanzania katika fani za gesi, mafuta, chuma, urari, makaa ya mawe na madini mengine. Hii inadhihirisha kwamba nchi yetu inahitaji kuongeza kasi zaidi kuwekeza kwenye elimu ya kisayansi zaidi ni vizuri kama Serikali itatumia walimu waliostaafu iwape ajira ya mkataba hadi hapo wanafunzi mbalimbali wa sekta hiyo ya sayansi watakapofuzu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwatetee walimu. Ni dhahiri kwamba changamoto ya upatikanaji wa walimu inaenda sambamba na changamoto zinazowakabili walimu hao katika mazingira ya kazi.

Walimu wamekuwa na malalamiko yasiyopungua dhidi ya mwajiri wao, yaani Serikali kutolipa posho za hali ngumu, kupandishwa cheo bila kulipwa nyongeza ya mishahara yao kwa wakati, mishahara midogo, makazi duni kwenye maeneo wanayoishi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tumeshindwa kuwaweka walimu ambao ndiyo mashine ya kuzalisha wanasayansi basi ni dhahiri kwamba Taifa letu haliwezi kuendelea. Ninaomba sasa ifike mahali kero hizi za walimu zitatuliwe ili kuleta tija kwenye elimu yetu kwani ni ukweli kabisa kwamba nchi yoyote ile inapiga hatua kutokana na mchango mkubwa wa kuwepo kwa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu inapunguza umaskini, ninaomba kuhitimisha kwa kuomba pia Watanzania hususani wanafunzi wapende kuwa na utamaduni wa kujisomea vijitabu na hata kuandika masuala mbalimbali, hii pia ni njia nzuri kwa wao kuongeza *quality* ya uelewa. Wasiendelee kungoja mfumo kama nyenzo ya wao kupata elimu kwani hilo ni sawasawa na bora elimu kuliko elimu bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti nzuri hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwa darasa la kwanza wawe na *syllabus* ya kusoma kuandika na kuhesabu tu. Wasiwe na masomo mengine na katika kusoma mengine ya a e i o u – a b c d… wasianze na kusoma sentensi ndefu ndiyo maana watoto hawawezi k.k.k. tuangalie *syllabus* yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukaguzi watengewe ofisi zao wasiwe chini ya Halmashauri ya Wilaya au *Town Council* wakiwa chini ya hao wanakuwa hawafanyi kazi kwani Mkurugenzi wa Mji au Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya hawatatekeleza maagizo ya wakaguzi kwani

Wakurugenzi hao ni mabosi ndiyo wanatoa magari, mafuta kwani Idara hii ya Ukaguzi haina nyenzo za kufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, siasa mashuleni si sawa, sheria ya mwaka 1992 imekataza kufanya siasa mashuleni pia *University Act No. 7* ya mwaka 2005 zinakataza kwa hiyo tusifanye siasa mashuleni, ndiyo chanzo cha maandamano mashuleni na uvunjifu wa amani mashuleni. Migomo na migogoro yote sababu ya siasa tuache, siasa shuleni ifutwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba tuongeze idadi ya shule na vyuo vya ualimu Lindi kwani tumesahau sana Mkoa wa Lindi na Mikoa mingine. Ukilinganisha utaona Lindi hawana shule za kutosha za chekechea, shule za msingi, shule za sekondari na vyuo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna sababu sita za kuwa wa mwisho kielimu Lindi, moja ni tatizo la ukombozi wa Afrika, Lindi kulikuwa ni maeneo ya mafunzo ya kivita, pili, sera za elimu za mkoloni kutaifisha shule kuwa kila mtoto aende akasome popote ili mradi ana fedha, shule za Kusini zikaja na watoto wa mikoa wenye fedha hii ilituacha hoi, sababau zipo sita. Sasa tunaiomba kwa makusudi tuongezewe shule za aina zote mkoa wa Lindi.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kumpongeza Mheshimiwa Mhagama, Naibu Waziri baada ya hapo naunga mkono hoja na Waheshimiwa Wabunge waliolalamikia mabweni na ubora wa elimu. Aidha napenda kusisitiza yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza shule za binafsi kuanzia shule za awali, msingi na sekondari zinazotozwa kodi za *Corporate Tax, VAT, Skill Development Levy* ya Serikali za Mitaa wakati shule kama hizi zinazomilikiwa na mashirika ya dini zinapewa *exemption* ya kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, athari za haya shule hizi zinatoza karo ya juu. Nashauri shule binafsi zote zipate *tax exemption.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na ukosefu wa walimu wa sayansi katika shule za sekondari kwa sababau wasomi hawa wamekuwa wachache. Nashauri wanafunzi wengi wasome masomo haya na kuwe na posho maalum kwenye *profession* au masomo hayo. Kwa mfano Wilaya ya Mbulu yenye sekondari 29 na mbili zinazotarajiwa kuanzishwa kama walimu wa sayansi 147 na upungufu wa walimu 328.

Mheshimiwa Naibu Spika, waraka wa Wizara wa mwaka 2012 unaohitaji maabara, madarasa 16 ya chuo na nyumba mbili za walimu, ofisi na maktaba ni masharti magumu sana, nashauri kuwe na *exceptional cases.*

Mheshimiwa Naibu Spika, madaraja ya ufaulu wa kidato cha nne tunachohitaji ni *quality* siyo *quantity* kuwa na wanafunzi waliofaulu ambao hawajaelimika ni bure, bora kuwe na waliofeli *division zero* lakini wameelimika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mgogoro wa shule ya sekondari ya Nambi naomba Wizara imuagize Katibu Tawala wa Mkoa wa Manyara (RAS) atatue mgogoro wa mahali pa kujenga sekondari hiyo ambayo inasababisha sekondari ya Meinrag iwe *over croweded* tangu mwaka 2011 inakuwa na wanafunzi 1300 badala ya 640.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kipo kilio kibukwa nchini cha wanafunzi kufeli masomo ya sayansi yaani hisabati, fizikia na kemia. Lakini pia upo uhaba mkubwa wa walimu wa masomo hayo nchini. Mkoa wa Kilimanjaro una uhaba wa walimu 898 ambao ni 45% ya mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, masomo ya sayansi yanaendelea, sambamba na maabara 541. Ninaitaka Serikali iwaambie wazazi na wanafunzi Kilimanjaro ni lini walimu wa sayansi watapelekwa na ni lini maabara zitajengwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kufeli katika masomo ya sayansi kunatokana na mambo mengi, mojawapo na kubwa zaidi ni ukaguzi usiokidhi au kutokuwepo ukaguzi, ukosefu wa vituo vya walimu vya mafunzo kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi ni kama chombo cha kusaidia Serikali yoyote kujua utendaji kazi wa shule zake yaani *school performance,* matokeo ya ukaguzi hata hivyo yanategemea sana namna ukaguzi utakavyofanywa na dhamira ya ukaguzi. Tegemeo ni ukaguzi uwe na lengo la kuongeza na kuchochea mabadiliko chanya katika ufanisi wa utendaji wa shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ukaguzi hautafanyika kwa umakini na kama matokeo ya ukaguzi hayatarejeshwa kwa wahusika na kama hakuna ufuatiliaji wa mapendekezo *(recommendation)* yaliyotolewa na wale waliofanya ukaguzi na kama hakuna tathimini *(monitoring and evaluation)* ya kujua kama ukaguzi unaleta mabadiliko katika *perfomance* za shule au la, ukaguzi unakuwa hauna maana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ripoti ya CAG ya mwaka 2004 katika shule 1734 zilikaguliwa shule 406 sawa na 23%. Mwaka 2006/2007 katika shule 2567 zilikaguliwa 678 sawa na 26% na mwaka 2008/2009 katika shule 3798 zilikaguliwa 346 sawa na 9%.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo shule zinakaa bila kukaguliwa kwa miaka mitano. Kanuni na sheria za ukaguzi zinaitaka Idara ya Ukaguzi kukagua shule kila mwaka. Ingawa idara hii ina upungufu wa vifaa, ofisi na wafanyakazi, lakini pia utendaji kazi wa Idara ya Ukaguzi kutokana na taarifa ya CAG, idara inaonyesha upungufu katika utendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika *handbook* ya idara hii yapo mambo 148 ambayo wakati wa ukaguzi yanatakiwa yazingatiwe.Katika mambo hayo, hakuna hata moja linalolenga mkaguzi aweke kipaumbele utendaji mbovu wa wanafunzi *(poor performance students* na *school and student performance issues)* wakaguzi wanaweka kipaumbele katika maeneo mengine mfano mahudhurio, fedha, uongozi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la matokeo mabaya ya wanafunzi katika masomo muhimu halipewi kipaumbele katika mpango kazi wa Idara ya Ukaguzi, mambo muhimu kama shule zilizofanya vibaya katika mtihani wa mwisho *(form five* mpaka *six)*. Shule ambazo hazijakaguliwa muda mrefu matatizo yaliyopo katika shule husika, wakati muafaka wa ukaguzi, wakati muafaka wa ukaguzi, wakati muafaka kufanya mtihani na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, yangetiliwa mkazo wanafunzi wangeweza kufanya vizuri zaidi. Katika *special audit* iliyofanyika mwaka 2004 na 2006 katika shule 110, hakuna hata ripoti moja ya ukaguzi uliyoonyesha tatizo la wanafunzi kuacha shule *(drop points)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ripoti za ukaguzi zinatakiwa zitolewe kwa walimu wakiwa wa shule zilizokaguliwa, kwa Bodi za Shule, kwa wazazi kupitia Bodi za Shule, kwa umma, kupatia waandishi katika redio, magazeti, mitandao ya kijamii na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuficha matokeo ya kaguzi za shule, kuzuia umma kupitia waandishi wasioone inakosesha idara mchango wa maoni mazuri ya Watanzania waliopo nje ya shule zilizokaguliwa kutokana na haya uwezo wa Idara ya Ukaguzi kusaidia Serikali katika kuweka sera na mipango ya kuboresha utendaji mbovu wa wanafunzi mashuleni ni mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia shule Serikali inaweza kutekeleza mipango yake ya afya (mfano chanjo tofauti) na stadi za maisha kwa wanafunzi, mpango wa wanafunzi kupata chakula cha mchana mashuleni imeonyesha mafanikio makubwa ya kuongeza mahudhurio kupunguza utoro, kuongeza afya za watoto na hata kupunguza athari za utapiamlo kwa familia maskini. Ripoti ya *Word Bank* na *World Food* ya mwaka 2009 – 2013 inasema kila siku watoto milioni 66 wa shule za msingi wanakaa na njaa na 23% ya watoto hao wapo Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto milioni 75 wenye umri wa kwenda shule hawaendi shule na 55% ya watoto hao ni wasichana na 47% wanaishi Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara. Kulisha watoto shuleni tutakuwa tumetimiza mojawapo ya malengo ya milenia inayotaka nchi washirika wapunguze njaa kwa kiwango cha nusu ya njaa iliyopo duniani, kila mtoto kupata elimu ya msingi na kuhakikisha nafasi sawa ya elimu kwa mtoto wa kike.

Mheshimiwa Naibu Spika, ripoti zinasema kumlisha mtoto wa kike shuleni kunamondolea muda wa kukaa nyumbani kwa kazi za nyumbani, kumfanya awe na miaka mingi shuleni na hivyo kupata uhalali kufanya maamuzi kuhusu kuolewa, kupanga idadi ya watoto anayotaka kuzaa na kubwa ni uchumi kwake na familia yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali ifuatailie namna ukaguzi wa shule unavyofanyika na kuhakikisha mapendekezo yaliyotolewa na wakaguzi yanafanyiwa kazi na idara hivyo ifanyiwe tathmini kuona kama ukaguzi unaleta mabadiliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi siungi mkono hoja ya bajeti ya Wizara hii kwa sababu elimu imeshuka na kupelekea watoto wengi kutojua kusoma na kuandika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tatizo la ukaguzi hili ni tatizo sugu na ndilo linalofanya kuwa na matokeo mabaya kwani wanafunzi bila ya kukaguliwa kiasi kwamba walimu wanafanya wanavyotaka na kupelekea walimu wengi kujiingiza kwenye vitendo vya ulevi jamabo ambalo halileti maslahi kwa Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mfumo wa elimu kuwa katika Ofisi ya Waziri Mkuu, kuendelea kuwepo Wizara hii na maamuzi sahihi juu ya Wizara hii kwani Wizara sasa haina sauti na shule pamoja na walimu kwa ujumla. Ni ngumu sana kupata matokeo mazuri ya shule na walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri mfumo wa zamani urudiwe ili uweze kuwezesha Wizara kuwajibika moja kwa moja kwa Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna uhaba mkubwa wa walimu katika Mkoa wa Katavi hususani katika Jimbo langu la Mpanda Vijijini. Kuna tatizo la uhaba wa walimu katika shule za sekondari za Mishamo, Ikola, Katuma, Mpandandogo, Karema, Kabungu na Mwese. Shule hizi zimekuwa na matatizo makubwa ya uhaba wa walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili ndiyo eneo ambalo kama sijapata maelezo ya kutosha juu ya uhaba wa walimu katika shule hizo mimi sitaungi mkono hoja ya Wizara hii, naomba Mheshimiwa Waziri aje na kujibu juu ya kupelekea walimu katika shule hizo ambazo nimeziorodhesha.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la makazi ya watumishi na shule kwa ujumla kuna hali mbaya sana, kuonekana kuwa mwalimu ni sehemu ya adhabu. Ninazo shule za msingi zifuatazo kama Waziri angefika na kuona hali ya majengo yalivyochakaa hawezi amini. Shule hizo ni Ikola, Kabungu, Mwese na Milala. Shule hizi zimejengwa miaka ya sabini na kuwa chakavu zaidi, naomba Serikali kupitia Wizara hii izitembelee na kuzikarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la malalamiko ya walimu juu ya madai mbalimbali kuhusu stahili zao kama malimbikizo ya likizo, kupandishwa vyeo, matibabu na kadhalika, walimu wanaidai Serikali, naomba Serikali iwalipe walimu madeni yote wanayodai.

Mwisho, naomba sana muangalie juu kupandisha mishahara kwa watumishi wa Idara ya Elimu hasa walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaunga mkono hoja hii nikipata majibu haya.

**MHE. ABDALLAH HAJI ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu muweza wa yote kwa kunijaalia afya nzuri na pili, nakupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Spika kwa kumudu vyema majukumu yako ya kuliongoza Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kuchangia kuhusiana na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, ni utaratibu nzuri uliowekwa na Serikali ili kuwawezesha wanafunzi kumudu kupata elimu, ila kuna changamoto nyingi katika upatikanaji wa fedha hizi. Moja ni wingi wa waombaji kwamba wanafunzi ni wengi na kasma itolewayo ni ndogo kwamba haikidhi kwa waombaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali itenge fungu kubwa kulingana na wingi waombaji angalau kupata asilimia 75 ya waombaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine ni jinsi ya fedha hizi zinavyotolewa au zinavyogawiwa kwamba viwango hutolewa tofauti kwa waombaji bila hata kufanya utafiti kwa wanafunzi hao. Wapo wapewao viwango vikubwa, vya kati wa vya daraja la chini kabisa ambalo huwa ni mzingo kwa baadhi ya wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Seikali katika kukuza bajeti na iweze kuwapa wanafunzi viwango sawa bila kuzidiana kwa sababu hakuna utafiti unaothibitisha mahitaji halisi ya wanafunzi hao na hii itaondoa utata na lawama

miongoni mwa wanafunzi na Bodi. Pia ikizingatiwa kwamba mwisho wa siku fedha hizi wanahitajika kuzilipa hivyo ni busara viwango vitolewe sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine ni ucheweleshaji wa mikopo. Hiyo ni kweli kwamba mikopo inacheleweshwa vyuoni kiasi kwamba wanafunzi hupata usumbufu mkubwa katika kujikimu kimaisha na kimasomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi wa elimu ya juu hujiunga vyuo mbalimbali katika kila pembe ya nchi yetu mfano wanafunzi kutoka Mwanza, Arusha, Mbeya na maeneo mengine hujiunga na Vyuo Vikuu Zanzibar kwa hali ambayo hujikuta hawana mjomba wala shangazi, wanachongalia ni fedha ya mkopo kwa ajili ya kujikumu kimaisha na masomo, ila zinapochelewa huwa ni tatizo kubwa linalowakumba wanafunzi hata kufikia kudhalilika hususan wanafunzi wa kike.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo naishauri Serikali kuharakisha kupeleka mikopo hiyo kwa wakati kwamba inapocheleweshwa athari zake ni kubwa zikiwemo kushuka kwa matokeo ya wanafunzi badala ya kushughulikia masomo hubaki kufikiria vipi wanaweza kuishi vyuoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mungu akuongezee busara.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la ukosefu wa nyumba za walimu ni kubwa sana. Mwaka 2013/2014 fedha zilizotengwa ni shilingi 617,083,004,000/=, mwaka 2014/2015 fedha zilizotengwa ni shilingi 799,020,389,000/= kutokana na ukubwa wa Wizara yenyewe fedha zilizotengwa ni chache na hazitoshi. Kwa maana hiyo ujenzi wa nyumba za walimu utekelezaji wake hautakuwa na ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujua ni lini Serikali itatimiza ujenzi wa nyumba Wilayani Mbarali katika bajeti hii, je, Wilaya ya Mbarali ni miongoni mwa Halmashauri 40 zitakazopewa fedha za ujenzi wa nyumba za walimu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile elimu ya Tanzania inaonekana kutokidhi mahitaji ya wahitimu kwa maana ya kuwawezesha kujiajiri na hivyo kutegemea ajira kutoka Serikalini, kwa vile elimu inayotolewa ya msingi, sekondari hadi vyuo vikuu ndiyo hasa kiini cha upungufu niliotaja hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu ya Serikali sasa kupitia Wizara ya Elimu ipo tayari kuleta mabadiliko ya elimu inayotolewa ili iweze kutoa ajira kwa wahitimu kwa kufundisha masomo ya ufundi, kilimo bora, ufugaji, biashara, kuanzia darasa la kwanza hadi vyuo vikuu ili wahitimu waweze kujiajiri wanapohitimu masomo yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo ya vyuo vikuu imekuwa na matatizo makubwa na hivyo kutokuwa na mpango mzuri na wa wazi katika kutoa

mikopo, naomba Mheshimiwa Waziri utakapokuwa unajibu utoe maelekezo jinsi mkopo inavyotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu watoto yatima na watoto wa mitaani, Serikali ina utaratibu gani wa kuhakikisha watoto hawa hawakosi haki yao ya msingi ya kupata elimu? Naomba kujibiwa kuhusu jitihada za Wizara katika kunusuru kizazi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, posho ya mazingira magumu kwa walimu utekelezaji wake unaanza lini? Je, Serikali haioni umuhimu wa kutoa motisha hiyo kwa walimu ili walimu wasiyakimbie mazingira hayo?

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Wizara, Katibu Mkuu na watendaji wake naomba Wizara izingatie yafuatayo:-

Kwanza, kutokana na takwimu za Baraza la Mitihani matokeo ya mitihani yameonyesha udhaifu mkubwa katika ufundishaji maana *perfomance* ni dhaifu. Naomba Wizara iziangalie takwimu hizi na kuweka mkakati thabiti wa kuondoa udhaifu huu. Nampongeza sana Mtendaji Mkuu wa Baraza la Mitihani kwa kuandaa takwimu hizi na pili ni kuhusu Wilaya ya Mbinga ambayo ina shule nyingi za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ni kwamba walimu wa shule za msingi na sekondari hawatoshi. Naomba tuangaliwe na kuongezewa idadi ya walimu na mgao wa walimu naomba uzingatie uwiano wa idadi ya shule na wanafunzi.

Pia tumeanzisha shule ya sekondari ya sayansi ya wasichana. Tunaomba nyongeza ya walimu wa masomo ya sayansi, shule hii inahitaji mabweni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba pia tufikiriwe katika mgawo wa fedha za ujenzi wa maabara, ujenzi wa nyumba za walimu pamoja na ununuzi wa vifaa vya maabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia maombi yetu haya Serikali itakuwa inaiwezesha Mbinga kukamilisha mipango yake ya elimu. Mungu awabariki.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Wizara kwa kufufua Kitengo cha Ukaguzi nchini. Ni kitengo muhimu sana na mchango wake katika kuboresha elimu ni mkubwa sana. Naiomba Serikali iendelee kukiimarisha kitengo hiki na kukiwezesha kwa rasilimali watu na vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu wanaokaa katika mikoa ya pembezoni wanapata taabu sana kufuata mishahara mahali kwenye mabenki. Naiomba Serikali iboreshe mpango wa huduma za kibenki kwa kutumia simu za mikononi. Mpango huu unawaletea nafuu sana walimu hawa kupata huduma za kibenki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iendelee kuboresha na kuhimiza masomo ya sayansi katika mashule yote. Zamani kulikuwa na *combination* ya P.M.M ambayo pamoja na zingine za sayansi zilichangia sana kuwa na wahandisi nchini, *combinantion* hii inaweza kurudishwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana katika bajeti ya Mheshimiwa Waziri alitoa taarifa kuhusiana na mpango wa Serikali kusaidia ujenzi kikamilifu kuna sekondari mbili kila Wilaya kama ilivyokuwa awali, lakini katika taarifa yake ya mgao wa sekondari hizo mbili uliowekwa zipo baadhi ya Wilaya zilipewa migao ya ujenzi wa sekondari hizo kwa zaidi ya mbili hadi tisa huku Wilaya zingine zikiachwa na idadi ile ile ya sekondari mbili kama Wilaya yangu ya Bahi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo baada ya Waheshimiwa Wabunge kugomea mgao huo aliahidi hapa Bungeni kuwa angerekebisha mgao huo ili kuleta usawa wa mgao kwa kila Wilaya, lakini nimesikiliza katika hotuba yake ya bajeti ya mwaka 2014/2015 jambo hili hakulizungumzia kabisa wala hajatoa taarifa ya mgao mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ili nisitoe shilingi tafadhali Mheshimiwa Waziri atupe taarifa juu ya jambo hili wakati anajibu hoja mbalimbali za Wabunge. Ahsante.

**MHE. MWANAMRISHO T. ABAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nyumba za walimu je, kwa nini Serikali haijiwekei mipango madhubuti ya kujenga nyumba za walimu kupitia mashirika ya NSSF na LAPF, NHC kwa kodi nafuu ili walimu waweze kuishi vizuri na kufanya kazi zao kwa moyo na ufanisi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mikopo ya elimu ya juu, kumekuwepo na malalamiko mengi kuhusu mikopo hii inavyotolewa kwamba wanaopata mikopo ni watoto wa wenye uwezo na watoto wa wakubwa tofauti na walengwa ambao ni makundi maalum kama walemavu na watoto wa wazee wasio na uwezo na wa kaya maskini. Je, Serikali inaboreshaje kuondoa tatizo hili na malalamiko haya?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wanafunzi wanaopata mimba mashuleni, elimu ni haki ya kila mtoto anapofikia umri wa kusoma au kupelekwa shule, naiomba Serikali iandae utaratibu wa kuwarejesha shuleni wanafunzi wanaopata mimba shuleni pale tu wanapojifungua, kwani elimu ni haki yake na ni msingi wa maisha yake. Adhabu anayopewa mtoto wa kike anapobeba mimba ya kumfukuza shule inaumiza na inamuathiri kisaikolojia ikizingatiwa kwamba adhabu hiyo inamkumba peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iyazingatie kwani ukimuelimisha mwanamke mmoja sawa na Taifa zima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imalize madai ya walimu ya stahili zao ambazo Serikali hazijawalipa ili kuondoa migomo na maandamano yasiyokuwa na maana kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa nakupongezeni hasa Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri katika Wizara hii ya Elimu, hongera sana mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba kuwasilisha.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata fursa hii ili nami niweze kutoa maoni yangu katika Wizara hii. Ni nani anayesimamia viwango vya ada katika shule binafsi?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mchango mkubwa wa elimu unaotolewa na shule binafsi, ada zinatozwa na shule hizi ni kubwa mno na zinatofautiana kwa shule na shule. Ada hizi kubwa zimekuwa ni mzigo mkubwa kwa wazazi na wazazi wengi hawawezi kumudu na hivyo kuleta matabaka ya kielimu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ada hizo kubwa, shule za binafsi zimekuwa zikichangisha michango mingi sana mfano majengo, vifaa, madawati na kadhalika ili hali shule hizi si za umma. Hii inaonyesha kuna tatizo la kuzingatiwa kwa vigezo vya usajili wa shule ambapo shule zisizokamilisha vigezo husajiliwa na kuwafanya wamiliki wa shule hizo kubebesha wazazi mzigo wa ukamilishaji wa shule hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwa kawaida kabisa kuona shule isiyo na vyoo, maabara, viwanja vya michezo, zenye walimu wawili au mmoja na matatizo mengine mengi, swali la kujiuliza ni kuwa ni nani anayekagua shule hizi? Ni nani anyethibitisha viwango ama vigezo vya usafi vya shule hizi? Je, Wizara imeshindwa kusimamia suala la elimu katika nchi yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, vifaa vya maabara kwa masomo ya sayansi pamoja na kuwa ni pungufu kwa karibu shule zote waagizaji wa vifaa hivyo wengi huagiza kutoka nchini Kenya na hivyo vikiletwa hapa nchini huwa ghali sana. Ni kwa nini waagizaji hawa wasinunue vifaa hivi moja kwa moja huko ambako wenzao Kenya hununua ili kupunguza bei za vifaa hivi vikifika hapa nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, madai ya walimu na mazingira magumu ya kazi yamekuwa ni wimbo wa Taifa, ni lini Serikali hii ya CCM itathamini kazi hii ya ualimu kwa kuwatimizia walimu madai yao ya msingi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa na Naibu Waziri Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa kukubali kusimamia Wizara hii ngumu yenye changamoto nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itafute mfumo mzuri wa ajira za walimu na utaratibu mzuri wa kuwasimamia walimu, mfumo wa sasa haueleweki. Mwalimu huhudumiwa na Wizara nne, (TAMISEMI, Wizara ya Fedha, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Ofisi ya Rais - Utumishi wa Umma). Mkanganyiko huu huleta lawama hasa katika suala la upandishwaji vyeo, malipo mbalimbali na kaadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Ukaguzi imesahaulika kabisa na Wizara hii na ndiyo maana baadhi ya walimu wanafanya wanavyotaka wakijua kwamba hakuna anayewakagua. Kwa nini Idara ya Ukaguzi isiwe wakala ili iweze kufanya kazi ipasavyo? Hili ni pendekezo langu kwamba Idara ya Ukaguzi iwe Wakala - Ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri wanafunzi wanaomaliza kidato cha nne na kidato cha sita na kushindwa kuendelea na masomo ya elimu ya juu aidha kwa kukosa nafasi, wapelekwe Vyuo vya *VETA* ili wakajifunze ufundi utakaowawezesha kujitegemea, kwa sasa utaratibu huo haupo kwa sasa na wanafunzi hao hubaki mitaani wakizurura na wengine hujiingiza kwenye vitendo viovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitabu cha hotuba ya Wizara ukurasa wa 45 jedwali namba moja imeonesha mahitaji makubwa sana ya walimu wa masomo mbalimbali na hasa masomo ya sayansi, Mheshimiwa Waziri amelalamika bila kuonesha mkakati wa Serikali wa kuwahamasisha vijana kusoma masomo hayo ili kuziba nafasi zilizo wazi au kukidhi mahitaji ya Serikali. Nasikitika kwamba fedha za maendeleo hazipelekwi kwa wakati katika

Halmashauri zetu, mpaka mwezi Machi 2014 ni 21% ya fedha za maendeleo zilipokelewa. Je, kwa hali hiyo tutaweza kufikia malengo ya *BRN?*

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa mfano kwa Wilaya ya Bahi kwa shule za msingi 34 shilingi 273,029,699/= fedha za maendeleo hazijapokelewa mpaka sasa, shule za sekondari 24 shilingi 242,743,234/= hazijapokelewa. Nadhani BRN kwa Wizara hii ni ndoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema BRN ni ndoto kwa Wizara hii kwa sababu changamoto za Wizara hii ni nyingi mno na Mheshimiwa Waziri mwenyewe amezitaja kwenye hotuba yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya awali ni muhimu sana kwa watoto wanaoanza kujifunza kusoma kuandika na kuhesabu. Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba kuna upungufu mkubwa wa walimu wa awali wa darasa la kwanza na la pili, nashauri Wizara ifanye mkakati maalum ya kuwafunza walimu wa darasa la awali, vijana wapo wengi wanaoweza kujifunza na kuziba nafasi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. WARIDE BAKARI JABU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza kwa kuwasilisha bajeti hii vizuri na naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itupatie jibu kwa nini hamtaki kumaliza Chuo cha Sayansi Baharini *(Institute of Marine Science)* kule Zanzibar eneo la Buyu-Kiembesamaki. Inaleta aibu kubwa sana tawi la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam limechukuwa muda mrefu toka kuanza kujengwa inakaribia mwaka wa kumi sasa na pengine labda chuo hiki kimejengwa upande wa pili wa Muungano, kila mwaka fedha zinatengwa lakini hampeleki kuna nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, wahadhiri wanapata taabu wanapofanyia kazi na mazingira yaliyokuwepo chuo hiki pale Bandarini Zanzibar ambapo shughuli zote za usafiri na usafirishaji abiria zinafanyika kwenye eneo la chuo. Naomba sana Wizara hii iipe kipaumbele cha umalizaji wa ujenzi wa chuo hiki au chuo kikabidhiwe kwa mashirika kama NSSF wamalize ujenzi wa chuo hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu waangaliwe upya katika maslahi yao kwenye Chama cha Walimu (CWT) wasilazimishwe kujiunga kwani chama hiki hakiwapatii walimu mafao hao baada ya kustaafu. Walimu hawanufaiki, mwisho wake hivyo wasilazimishwe kukatwa fedha katika chama hiki. Nashauri iwe hiyari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naunga mkono hoja tena.

**MHE. MKIWA A. KIMWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuwapongeza Waziri Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa na Naibu Waziri Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa kuongoza Wizara hii, kwani ni Wizara ngumu sana tena sana. Inabidi mkaze buti ili elimu yetu iendane na wakati tulio nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kujua maombi yetu ya Chuo cha Kilimo Ukiriguru kuwa Chuo Kikuu cha Mkoa wa Mwanza, hili ombi lilikuja huko kwenu, ni vyema sana ombi hilo likakubaliwa kwa kukiendeleza chuo hiki, pia kiweze kuwasaidia wanafunzi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nilitamani sana malimbikizo ya walimu au madai ya walimu yahakikiwe na kama yapo yalipwe basi ili kuondokana na matatizo yetu. Kama Serikali haina fedha basi nashauri shule zetu turudie kulipa ada kama zamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba Mheshimiwa Waziri anifahamishe, Mwalimua wa Diploma anakuwa Mwalimu Mkuu lakini Mwalimu mwenye Shahada ya Uzamili anakuwa mwalimu wa kawaida kwenye shule hiyo hiyo, napenda kujua hili ili niweze kupata majibu ya kuwaeleza wapiga kura wangu ambao ni walimu na ndiyo walionituma haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kushauri kuwa Matokeo Makubwa Sasa bila wakaguzi wa elimu ni kujidanganya, hivyo ni lazima tukague shule na elimu pia, tuwanunulie usafiri, tuwape posho na maslahi yao wakaguzi, ni vema tuwekeze kwenye elimu ili tufundishe watu wetu ndipo tutakapojikomboa katika hali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusikubali tena kusimamisha mabasi yetu na kupakia watoto kuwapeleka Uganda na Kenya kusoma. Tuone aibu kwa hili na ni muhimu kuboresha elimu yetu.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya juu ni suala la Muungano. Naiomba Serikali ieleze Bunge hili Zanzibar ikiwa ni mdau husika wa pande mbili za Muungano huu katika Wizara hii ambayo elimu ya juu ni suala la Muungano wana asilimia ngapi wanayoipata kutoka katika Bodi ya Mikopo kwa wanafunzi wanaojiunga na elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ijibu ni *ratio* gani inayotumika ya kutoa nafasi na fursa ya wanafunzi kutoka Zanzibar juu ya kujiunga na elimu ya juu na kwa kipindi cha miaka kumi hadi kufikia Disemba, 2013 ni wanafunzi wangapi kutoka Zanzibar wamepata mikopo ya kujiunga na elimu ya juu na ni wangapi ambao wamekidhi vigezo lakini hawajapatiwa mikopo na kwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, *scholarship* zinapotokea Wazanzibar wanafaidika vipi na nafasi hizo? Je, Serikali inaweza kulijibu Bunge hili kwamba kwa kipindi cha miaka kumi hadi kumalizika kwa mwaka 2013 ni *scholarship* ngapi zimetokea Tanzania, Bara imepata nafasi ngapi na Zanzibar kama mdau wa Muungano imepata nafasi ngapi na je, nafasi hizo zinapotokea Zanzibar inapewa kama nchi iliyoungana na Tanganyika au inapewa nafasi hizo kama Mkoa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna taarifa kwamba Serikali imeondoa mikopo kwa wafaulu wa masomo ya dini. Serikali inaweza ikatueleza ni kwa nini imeondoa mikopo kwa wanafunzi ambao ni wafaulu wa mitihani ya dini?

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni mgogoro mwingine ambao una lengo la kudumaza elimu ya dini nchini. Kuna dhamira za makusudi ya kudhoofisha elimu ya dini nchini, inasikitisha kuona kuwa Mkapa aliweza kufungua Chuo cha Kiislam Morogoro lakini leo uhai wa Rais Kikwete ambaye ni muislam na Waziri Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawamba wote wanaridhia ubaguzi huu ambao una lengo la kuua elimu ya dini.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kutoa mikopo kwa wanafunzi wanaofaulu masomo ya dini kumefutwa lakini panapotokea tatizo lolote viongozi wa dini wanahitajika kutatua matatizo yaliyopo (baniani mbaya kiatu chake dawa). Tunaomba wafaulu wa masomo ya dini zote wapatiwe mikopo na masomo haya yarejeshwe mara moja na vijana wapewe haki zao za mikopo na kujiunga na elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna taarifa vilevile kwamba somo la lugha ya kiarabu UDOM limefutwa, hivyo kwa nini lifutwe au kwa sababu kuna watu wanatafsiri kuwa uarabu ni ugaidi. Kiarabu ni lugha kama lugha nyingine, kwa nini mnaruhusu kusoma kifaransa, kiingereza, *chinese* na lugha nyingine nyingi ubaguzi umekuja kwa lugha ya kiarabu na masomo ya dini tu au ni ile kauli inayosemwa mpaka makanisani kwamba Wazanzibar asilimia 95 ni waislamu ikiwa Wazanzibar tunawatesa kwa hili la elimu ya juu jambo ambalo linakutieni dhiki sana kutokana na dini yetu, kwa nini hamuachii hii Wizara Zanzibar ikawa na Wizara yake ya Elimu ya Juu?

**MH. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu yetu kwa ujumla, sio jambo la ubishi kuwa elimu yetu hapa nchini imeporomoka hadi kufikia asilimia 50.4 mwaka 2010 kwa kidato cha nne. Lazima tutambue ili nyumba iwe imara lazima msingi wake ujengwe imara. Shule za awali misingi sio mizuri tumekuwa

tukihimiza masomo ya KKK (Kusoma, Kuandika na Kuhesabu) kuanzia 1 – 3 ni muhimu kuliko ilivyo sasa mtoto huyu mdogo anabeba zaidi ya madaftari 10 hawezi kufuatilia masomo, yanakuwa ni mengi mno na cha pili kila shule ya msingi iweze kuwa na shule ya awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule nyingi za msingi hazina miundombinu muhimu kama vyoo ambavyo vinapelekea wanafunzi hasa wa kike kukosa masomo, tumeona kuna baadhi ya shule hazina madawati wanasomea chini, sehemu nyingine hakuna madarasa hata walimu unakuta mwalimu mmoja anafundisha darasa la kwanza mpaka darasa la saba masomo yote. Hii haiwezekani, huyu mwalimu akiugua inamaana shule inafungwa, mwanafunzi atafaulu kwa vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maslahi ya walimu, kwa sasa hivi madai haya ya walimu yamekuwa kama wimbo wa Taifa. Chama cha Walimu katika *report* yake ya mwaka 2013 madai ya walimu yamefikia shilingi bilioni 61. Bila walimu hawa kupata maslahi yao hawawezi fanya kazi vizuri.

Je, bajeti ya mwaka huu madeni haya yatalipwa? Je, posho ya walimu ya *teaching allowance* itarudishwa? Hii itawafanya walimu wafaye kazi kwa moyo mmoja. Tukumbuke walimu hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukaguzi wa shule na taasisi za elimu, bado ukaguzi katika mashule yetu hali siyo nzuri bila shule kukaguliwa Serikali wanajuaje kama kuna malengo na dira yanafanikiwa? Shule nyingi za Kata hazitimizi vigezo lakini zinafunguliwa, hazina walimu, hakuna maabara, hamna nyumba za walimu, vitabu, hakuna matundu ya choo ya kutosha na kadhalika. Je, ni kigezo gani kinatumika kuruhusu shule kufunguliwa?

**MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na elimu ya msingi na sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu kwa Tanzania yetu bado ina changamoto sana kama mazingira duni ya kujifunzia na kufundishia, madai ya walimu kama vile nauli na malimbikizo mengine, uhaba wa madawati na vitabu, mazingira magumu ya kazi hasa kwa walimu vijijini na maabara kwa shule za Kata hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kubwa zaidi ni kuondolewa kwa mafunzo ya walimu kazini. Ikumbukwe zamani walimu walikuwa wakitoka shuleni wanakwenda vyuoni miezi mitatu mitatu, lakini sasa hivi hakuna, hali hii inadumaza taaluma kwa walimu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kweli Serikali ina nia njema ya kuboresha elimu nchini, basi ishughulikie kuondoa kero zote hizo nilizotaja kama:-

(a) Madeni ya walimu ili wawe na moyo wa kufanya kazi;

(b) Mazingira duni ya kujifunza na kufundishia;
(c) Uhaba wa madawati na miti tunayo nchi nzima;

(d) Mazingira magumu ya kazi hasa kwa walimu vijijini; na

(e) Maabara kwa shule za kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ikishughulikia kero hizi walimu wataipenda kazi yao na kufundisha kwa moyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ili elimu iwe bora inahitaji kusimamiwa na kukaguliwa. Hivyo Kitengo cha Ukaguzi ni kitengo muhimu katika sekta hii ya elimu. Lakini kitengo hiki kinafanya kazi katika mazingira magumu na kufanya elimu kama mtoto asiye na wazazi wa kumshauri na kumuongoza. Kitengo hiki cha Ukaguzi hakina magari ya kuzungukia ukaguzi, hakuna majengo mazuri ya ofisi za ukaguzi, hakuna vitendea kazi kama thamani za ofisini, hivyo elimu bora inapatikanaje? Maadili ya walimu yanasimamiwa na kukaguliwa vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba na kuishauri Serikali kupitia Wizara Kitengo cha Ukaguzi kiwe ni taasisi inayojitegemea ili iweze kufanya kazi yake ipasavyo bila kuminywa na kusababisha elimu kudorola.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Bodi hii ina nia nzuri ya kutoa mikopo kwa wanafunzi ambao ni raia wa Tanzania lakini mikopo hii imekuwa ikitolewa kwa ubaguzi badala ya kupewa walengwa wanapewa watoto wa wazazi wenye uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa namuomba Waziri mwenye dhamana afafanue wakati wa majumuisho ni mwanafunzi gani anastahili kupata mkopo na asipopata alalamike kwa nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa Wizara ya Elimu ina jukumu la kutoa mafunzo kwa watu wazima lakini katika hali halisi, idadi kubwa ya watu wazima waishio mijini na vijijini hawajui kusoma wala kuandika, Serikali inasemaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, mgawanyo ya lengo la maendeleo ya milenia ni kutoa elimu kwa wote ifikapo mwaka 2015. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ilisema kwamba Tanzania inang'ara kwa kutekeleza malengo ya maendeleo ya milenia kwa ufanisi. Lakini je, watu wasiojua kusoma na kuandika, tatizo hili Serikali inalichukuliaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi wa vyuo vikuu hapa nchini wanaotakiwa kupewa mikopo wengi wao ni watoto kutoka familia zisizokuwa na uwezo. Kwa takribani miezi mitatu iliyopita wanafunzi wa vyuo vikuu na nikitoa mfano wa *Arusha University,* wameshindwa kuendelea na masomo yao kwa ufanisi kwa kutolipwa fedha zao za kujikimu. Mheshimiwa Waziri wa Elimu afuatilie jambo hilo kwani wanafunzi wengi wanaumia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wizara ya Elimu ya Ufundi naomba kujua ni kwa nini Wizara haijapeleka Vunjo vyeti vya kuhitimu elimu ya sekondari *(leaving)* tangu mwaka 2013? Vijana wanaotoka kwenda Jeshi la Kujenga Taifa, Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Jeshi la Polisi na maeneo mengine watakwenda kama hawana vyeti vya kumaliza elimu ya sekondari?

Mheshimiwa Naibu Spika, Vunjo kuna upungufu wa walimu wa sayansi 140 wataletwa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, vifaa vya sayansi ni ghali, shule haziwezi kumudu gharama zake, vifaa na dawa za maabara za sayansi ni ghali na shule haziwezi, shule zote za Vunjo hazina wataalam wa maabara za sayansi ni ghali shule haziwezi, shule za Vunjo hazina wataalam wa maabara za sayansi, shule za Vunjo mabweni yana upungufu mkubwa wa walinzi, wapishi mfano Ashira wapishi wawili tu, Mwika wapishi wawili hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maelezo ya Wizara.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naunga mkono bajeti hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo *with my few observations/comments below:-*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza elimu ndiyo ufunguo wa maisha, bila elimu katika kila jambo ni bure tu, pili, ukaguzi wa elimu haufanyiki kwa muda mrefu sasa tunatarajia nini katika elimu? Serikali ifufue, iwezeshe kitengo hiki muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, tatizo la ajira ni kubwa, lakini ajabu wanafunzi wanaomaliza elimu vyuo vya juu, bado wanaranda randa mitaani na kuwa *frustrated*, kwa nini wasiende kufundishwa? Je, wanasoma kweli kwa malengo?

Nne, walimu wanafanya kazi katika mazingira magumu sana hivyo kusababisha wengi kukimbilia mijini tu ambako hakuna haja ya *hardship allowance*, wale wanaofanya kwenye mazingira magumu wapewe *incentives*!

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, Bodi ya Mikopo ipo? Inamnufaisha nani na kivipi? *Initially* Bodi hii ililenga kumnufaisha mwanafunzi wa Kitanzania aliyefanya vizuri lakini hana uwezo ama wazazi uwezo wa kumsomesha hakuna. Lakini cha kushangaza Bodi hii ya Mikopo imekuwa na ukiritimba wa ajabu.

Watoto wenye uwezo (wazazi wao) ndiyo wanaopata mikopo, watoto wa walalahoi waliofanya vizuri hawana mikopo hiyo, *where are we heading*? *Criteria* zinazotumika haziridhisha na hazipo *fair*. Utumike utaratibu utakaokidhi *pass marks* na uwezo wa kiuchumi ili kuondoa sintofahamu hii ya ubaguzi bila kujali ni kwenye masomo gani, kwani yote ni muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla hali ya elimu nchini inasikitisha, mikakati thabiti ifanyike yenye kuleta tija, muwe *innovative*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, *with the above caution.*

**MHE. DKT. GOODLUCK J. OLE- MEDEYE**: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la miundombunu ya kufundishia Vyuo Vikuu, nimetembelea baadhi ya vyuo hapa nchini na kubaini yafuatayo:-

Kwanza ni kuhusu Chuo Kikuu Dodoma, Shule ya *Information* haina *computer* za kutosha na hivyo kufanya mafunzo kutolewa kwa nadharia. Hali hiyo hufanya maandalizi ya wataalam na wahandisi wa *computer* kuwa na mapungufu makubwa kwani mwanafunzi hawezi kuwa mhandisi kama hajapata mafunzo ya vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nahimiza Serikali itoe fedha kwa shule hiyo ili inunue *computer* na kufungwa kwenye maabara yale pamoja na kutoa *laptop* kwa wanafunzi ili iwawezesha kujifunza na kufanya mazoezi ya kutosha.

Pia *School of Humanities* haina vitabu vya kutosha wala maabara ya *computer* ambayo ingewezesha wanafunzi kupata vitabu kwenye mtandao *(online library).* Serikali ihakikishe kuwa shule zote kwenye chuo hicho na vyuo vingine vinapatiwa fedha za kutosha ili wapate vifaa vya kutosha vya kufundishia na kujifunzia ili tupate wataalam wenye ujuzi wa kutosha.

Pili, ni kuhusu Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu cha Mkwawa (MUCE), naipongeza sana Serikali kwa kujenga majengo ya kisasa ya mihadhara *(lecture theatres)* kwenye chuo hicho. Hata hivyo inasikitisha kuona kuwa kumbi hizo hazijatiwa samani ili ziweze kutumika, nahimiza Serikali ihakikishe kuwa kumbi hizo zinatengewa fedha za kutosha ili samani zinunuliwe na kumbi kuanza kutumika ili kupunguza msongamano kwenye kumbi chache zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mikopo ya elimu ya juu hadi sasa wanafunzi wengi wanaotoka kwenye familia maskini bado wanaendelea kukosa elimu ya Chuo Kikuu kwa sababu ya masharti magumu ya utoaji mikopo iliyowekwa na kanuni za mikopo hiyo. Ili wanafunzi wote waweze kupata mikopo nashauri yafuatayo yafanyike:-

(a) Kiwango kinachotengwa kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu kiongezwe.

(b) Kwa vile Taifa linahitaji wataalam wa fani zote zinazofundishwa kwenye vyuo vya elimu ya juu, ubaguzi unaozingatia aina kozi anayosoma mwanafunzi uondolewe.

(c) Serikali iangalie uwezekano wa kuhamisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na waajiri mbalimbali kutoa mikopo kwa masharti ya mhusika kulipa kupitia ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafundi stadi ni msingi wa utekelezaji wa ubunifu na usanifu unaofanywa na wahandisi wa fani mbalimbali. Aidha, ufundi stadi unawezesha vijana kupata ujuzi utakaowawezesha ama kujiajiri au kuajiriwa katika sekta rasmi. Kwa kuzingatia umuhimu huo nashauri Serikali itenge fedha za kutosha kwa Mamlaka ya Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) ili iweze kuongeza idadi ya vyuo nchini na kupanua vyuo vilivyopo ili kuongeza udahili. Halmashauri ya Wilaya ya Arusha inaomba kujengewa Chuo cha Ufundi Stadi kitakachoanza na stadi za ujenzi, utengenezaji wa matofali na vigae vya udongo, uashi, ufundi umeme, ufundi bomba na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha na narudia kusema na kuthibitisha kuwa naunga mkono hoja hii.

**MHE. JOHN J. MNYIKA**: Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini/mapitio ya utekelezaji kwa mwaka 2013/2014 yanaonyesha kwamba malengo ya msingi ya kuinua ubora wa elimu na kujenga stadi stahiki katika ngazi zote za elimu na

mafunzo bado hayajafuatiliwa kwa ukamilifu. Aidha, bado kuna vikwazo dhidi ya fursa sawa kwa wote katika ngazi zote za elimu na mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo katika majumuisho ya majibu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi iwasilishe vizuri ripoti ya Kamati iliyoundwa na Waziri Mkuu kufuatia kuporomoka kwa matokeo ya kidato cha nne. Aidha, ripoti hiyo iambatane na taarifa ya Serikali yenye kueleza mpaka sasa mapendekezo ya ripoti hiyo yametekelezwa kwa kiwango gani. Iwapo Wizara haitatoa kauli juu ya utekelezaji wa mapendekezo ya ripoti hiyo ambayo itasaida sio tu elimu ya sekondari bali pia ngazi nyingine za elimu, nitawasilisha hoja Bungeni ya kutaka ripoti hiyo iletwe, ijadiliwe na Bunge lipitishe maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika katika hotuba ya Waziri hata baada ya kuhoji mwaka 2012/2013 na 2013/2014 bado kuna wanavyuo 15 kwa upande wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hawajarudishwa masomoni. Wizara katika majumuisho inapaswa kueleza sababu za wanafunzi hao kutorudishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, toka wanafunzi hao wasimamishwe wapo wadau wa elimu waliotaka kuandaa maandamano kwa Rais na wengine walitaka kwenda Mahakamani. Katika hatua zote nimekuwa nikitumia njia ya usuluhishi ambayo imewezesha wanafunzi 45 kati ya 50 kurejeshwa. Kwa hivyo, kumekuwa na malalamiko ya ubaguzi juu ya urejeshaji wa kutozingatiwa kwa haki za msingi. Kwa hali hiyo, iwapo Wizara haitaeleza sababu za kueleweka, nitaunga mkono hatua za ziada ambazo wadau wa elimu wataamua kuchukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nyakati mbalimbali kati ya mwaka 2005 mpaka 2013, Rais Jakaya Kikwete ametoa ahadi mahususi juu ya matengenezo ya miundombinu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kuongeza hosteli zingine. Hata hivyo sehemu kubwa ya ahadi hazijatekelezwa. Kwa kuwa ahadi hizo ni za miaka mingi, naomba maelezo toka kwa Serikali sababu za ahadi hizo kutokutekelezwa na lini hasa zitatekelezwa. Aidha, hatua gani imefikiwa katika utekelezaji wa ahadi ya Rais ya kuongeza fedha kutoka kwenye bajeti ya ujenzi wa kituo cha wanafunzi *(student centre)* katika aya ya 48 na 49 ya hotuba ya Waziri juu ya UDSM, masuala hayo yote hayajatolewa majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 17, aya ya 22, kipengele (e); aya ya 63 kipengele (b) katika ukurasa wa 38 na aya ya 103 (b) katika ukurasa wa 70 wa hotuba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imezungumzia uzinduzi na kuendelea kwa ujenzi wa hospitali ya kufundishia ya Kampasi ya Mlongazila. Nilishiriki uzinduzi huo kwa dhamira ya kuunga mkono kuendelea kwa ujenzi kwa matarajio kwamba Serikali itaweka kipaumbele katika kupatia ufumbuzi wa mgogoro wa madai ya fidia ya ardhi ya wananchi waliondolewa katika eneo la mradi.

Hivyo, katika uzinduzi huo ili kuepusha vurugu kati ya askari waliokuwa wameletwa kwa wingi katika uzinduzi na wananchi wenye madai waliofika katika eneo hilo wakiwa na mabango, nilimwandikia ujumbe Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete kumkumbusha kutoa kauli katika hotuba yake juu ya mgogoro huo ili wananchi waweze kujua hatma yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimkumbusha Rais kwamba wananchi wa eneo husika walimwandikia barua Rais kwa nyakati mbalimbali kati ya mwaka 2012 na 2013 bila kupata majibu. Wananchi walifikia hatua ya kumwandikia Rais baada ya mgogoro huo kutopatiwa ufumbuzi na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Ofisi ya Waziri Mkuu akiwemo Waziri Mkuu mwenyewe.

Nashukuru Mheshimiwa Rais alijibu ujumbe na kueleza kwamba barua hizi hazijafikishwa kwake. Rais aliagiza kwamba niwape wasaidizi wake barua hiyo na nilimpatia na kumbukumbu zote siku hiyo hiyo Msaidizi wa Rais aliyejitambulisha kwangu kwa jina la Fyataga.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri na Elimu na Mafunzo ya Ufundi ambaye alikuwepo siku hiyo, awasiliane na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais anayehusika ili kutolea majumuisho na Serikali itoe majibu ya barua hizo za wananchi, hali hii itaepusha uwezekano wa kutokea migogoro au mapingamizi yenye kukwamisha mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine katika utekelezaji wa ujenzi kwa mwaka 2014/2015 Wizara ihakikishe kwa kushirikiana na Wizara ya Maji na Mamkala ya Maji Safi na Maji Taka (DAWASA) ili bomba linalokwenda chuoni liwe kubwa na liwe na mchepuo/mchepuko kwa ajili ya wananchi wanaoishi katika maeneo jirani ya Kwembe na Mlonganzila. Aidha, ufumbuzi upatikane wa mgogoro wa mpaka kati ya Manispaa ya Kinondoni na Halmashauri ya Kisarawe katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika majumuisho naomba Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi atoe majibu kuhusu masuala yafuatayo ambayo nilifuatilia kwa nyakati mbalimbali kati ya miaka ya fedha 2011/2012, 2012/2013 na 2013/2014 wakati wa mijadala ya Makadirio ya Mapato na Matumzi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Elimu) na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mosi, utekelezaji wa sera ya sekondari kwa kila Kata. Pamoja na kuwa masuala haya katika hatua za awali ni ya kujadiliwa kwenye Halmshauri ya Manispaa ya Kinondoni, nilihoji Bungeni kwa kuwa mahitaji ya utekelezaji wa sera hii katika baadhi ya maeneo ya Jiji la Dar es Salaam yanazidi uwezo wa Manispaa na nguvu za wananchi hali inayohitaji hatua za Serikali. Changamoto kubwa kwa upande wa Jiji la Dar es salaam

katika maeneo ambayo tayari kuna makazi na vitega uchumi ni kupata viwanja kwa ajili ya ujenzi wa shule ya sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Jimbo la Ubungo, kata zinazokabiliwa na tatizo hilo ni Ubungo, Mburahati na Kimara. Manispaa ya Kinondoni ipo tayari na itaanza kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa shule, tatizo ni kupata ardhi. Hivyo, naomba majibu kwa masuala yafuatayo ambayo niliomba Wizara ya Elimu ishirikiane na Wizara ya TAMISEMI na Manispaa ya Kinondoni kuwezesha hatua za haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kata ya Ubungo, Wizara imefikia wapi katika kufuatilia ombi langu kwa Serikali kukutana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) ili katika eneo la jirani na shule ya msingi Mlimani pajengwe shule ya sekondari. Sekondari hii itaweza kuhudumia watoto wa wahadhiri wa UDSM na wananchi wa jamii inayozunguka Chuo Kikuu. Aidha, itakuwa vilevile eneo la wanachuo kufanya utafiti na mafunzo kwa vitendo katika sekta ya elimu, sayansi na hisabati. Kama hilo halitawezekana UDSM itoe eneo katika sehemu ya Msewe kuwezesha ujenzi wa sekondari ya Kata ya Ubungo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kata ya Kimara eneo lililopatikana halitoshi, hata hivyo, Serikali Kuu iliwahi kulipa fidia ya shilingi bilioni tatu kwa *Twiga Chemicals* kurejesha kwa Serikali kiwanja cha ekari nane eneo la Baruti. Kiwanja hicho Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi iombe kitolewe kwa Manispaa ya Kinondoni kujenga sekondari.
Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Mburahati ina shule nyingi za msingi. Hivyo, Wizara ikubali shule moja ya msingi Mburahati iwe ya sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Fungu 46 yafuatayo yatolewe majibu na kama Wizara haina majibu basi bajeti irudishwe ifanyiwe maboresho, Programu 50, kifungu 5001 juu ya elimu kwa walimu/ama elimu ya walimu. Viwango vya fedha za vyuo vya ualimu, shule za mazoezi, posho za wanavyuo vya walimu za chakula na hata wa ufuatiliaji/mkaguzi zimeshuka, hali hii haikubaliki.

Aidha, kwa kuwa katika bajeti za Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) majibu stahiki hayakutolewa juu ya madai ya madeni ya walimu na uboreshaji wa maslahi ya walimu, Waziri Mkuu atoe kauli wakati wa majumuisho ya mjadala wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi juu ya mpango maalum wa kupunguza matatizo ya walimu na ualimu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Programu 10, Kifungu cha 1001, Kasma 270500 Bodi ya Maktaba Tanzania, naomba nyongeza ya rukuzu itumike pia katika

kutekeleza ahadi ambayo Wizara ilitoa Bungeni. Ahadi hiyo ni ile ya Maktaba Kuu ya Taifa Jijini Dar es Salaam kuwa na maabara ya mzunguko *(mobile library)* ili iweze kutoa huduma ya kiada na ziada katika Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam na jirani katika mashule, vyuo na maeneo ya jumuiya yaliyokuwa na maktaba au yenye uhaba wa vitabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Programu 30, Kifungu cha 3001 Elimu ya Msingi na Programu 40, Kifungu cha 4001 Elimu ya Sekondari. Natambua kwamba sehemu kubwa ya bajeti ya utekelezaji na utendaji sasa ipo katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, hata hivyo kwenye kitabu cha maendeleo *(Vol. IV)* Kifungu 3001 na Kifungu cha 4001 kwa ngazi hizo za elimu, utegemezi wa fedha za nje kwenye miradi ya maendeleo ni mkubwa sana. Hali hii ni hatari kwa maendeleo ya elimu. Fedha za ndani katika vifungu husika hasa kwa maendeleo zinapaswa kuongezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Programu 30, Kifugu 3002 kuhusu *Adult Education and Non Forma Education*, tofauti na wakati wa Mwalimu Nyerere mfumo huu wa elimu kwa sasa haupewi kipaumbele wakati ambapo kiwango cha kutojua kusoma na kuandika kwa watu wazima *(adult illetary rate)* kinaongezeka. Aidha, katika kutekeleza miradi iliyotajwa kwenye kitabu cha maendeleo Kifungu 2001 Kasma 4320 na 4370 ni ipi itagusa Jimbo la Ubungo? Katika kutoa majibu ya kuchukua hatua ya usimamizi wa kisera wa sekta ya elimu na mafunzo ya ufundi nchini naomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi izingatie yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini wahitimu wa Stashada ya Ualimu katika saikolojia *(BA Ed. Phychology)* watapewa ajira Serikalini? Ni hatua gani Serikali imechukua kufuatilia malalamiko ya wanachuo wa Chuo Kikuu cha Teknolojia cha *St. Joseph* – Kibamba waliyoyatoa kwa barua zao kwa mamlaka mbalimbali za Serikali mwaka 2012 na 2013?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imeweka utaratibu gani wa kusimamia ubora na kutatua migogoro katika vyuo vilivyopo chini ya Wizara nyingine mfano Vyuo vya Ardhi Tabora na Morogogo - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Chuo cha Madini - Wizara ya Nishati na Madini.

Aidha, katika kuongeza ufanisi wa ufuatiliaji na ukaguzi wa vyuo vilivyopo chini ya Wizara nyingine naomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ifuatilie vyuo mbalimbali vilivyopo katika Jimbo la Ubungo ikiwemo Chuo cha Usafirishaji Mabibo - Wizara ya Uchukuzi na Taasisi ya Maendeleo ya Maji - Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mikopo ya elimu ya juu, pamoja na fedha za mikopo ya elimu juu ya kuhamishiwa katika kitabu cha nne cha maendeleo, Wizara ieleze sababu ya kiwango kilichotengwa mwaka huu kupungua. Pia hatua gani imefikiwa katika utekelezaji na ahadi ya kufanya mabadiliko makubwa ya muundo na mfumo mzima wa Bodi ya Mikopo, utoaji mikopo na ugharamiaji wa elimu ya juu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuendelea kwa matatizo ya mikopo na malalamiko ya wanavyuo, Serikali iwasilishe Bungeni ripoti ya Tume iliyoundwa na Rais kufanya uchunguzi kuhusu matatizo hayo. Kwa minajili ya kupunguza gharama na kuhakikisha ubora wa elimu katika shule na vyuo binafsi, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ishirikiane na Wizara ya Fedha kupunguza au kuondoa kodi katika bidhaa na huduma zenye kuongeza gharama za elimu nchini. Aidha, uundwaji wa Mamlaka ya Hisabati na Ithibiti kabla ya elimu uharakishwe kuhakikisha ubora.

**MHE. CELINE O. KOMBANI**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza Waziri na Naibu Waziri kwa hotuba yao nzuri yenye ufafanuzi wa kina. Naomba kuchangia ukurasa 59 na 60 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, niliomba Wizara ya Elimu kutujengea Chuo cha VETA katika Wilaya ya Ulanga, Tarafa ya Mwaya. Nilitoa maelezo kwa maandishi Wizarani kwamba Wilaya iliandaa ekari 100 kwa ajili ya Ujenzi wa Chuo cha VETA, aidha wananchi wamefyatua matofali zaidi ya laki moja kama nguvu zao. Kwa bahati nzuri suala hili Mkurugenzi wa VETA *Engineer* Mosha alituma timu ya wataalamu kwenda kukagua eneo husika na kuahidi kwamba ataliangalia suala hili ili liingizwe kwenye mpango wa bajeti ya mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma kwa makini hotuba ya Mheshimiwa Waziri na kubaini kwamba Wilaya yangu haipo kwenye taarifa ya mpango na bajeti ya mwaka 2014/2015 ukurasa 59 – 60.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitawaeleza nini wale wananchi ambao wametoa ardhi yao na wamekwishafyatua matofali kwa mategemeo kwamba Wizara itawaunga mkono. Nilijenga hoja kwa umakini mkubwa nikiwa na matumaini kwamba hoja yangu ina mantiki. Hoja ya msingi ni kwamba Wilaya ya Ulanga ilikuwa na vyuo vingi vya ufundi vilivyokuwa chini ya Kanisa la Katoliki. Uongozi wa kanisa uliamua kugeuza vyuo vyote kuwa shule za sekondari hata timu yako iliyokwenda kukagua ikiongozwa na Bwana Kibendera imeshuhudia vyuo hivyo viligeuzwa shule za sekondari. Naomba ombi langu lipatiwe majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ukarabati wa shule za sekondari za zamani (kongwe), shule ya sekondari ya Kwiro ni kongwe na imekuwa ikikarabatiwa kidogo kidogo mwaka hadi mwaka. Kwa mwaka 2013/2014 tuliomba jumla ya shilingi 400,000,000/= kwa ajili ya ukarabati. Nashukuru Wizara ilitupatia shilingi 70,000,000/= ili tuanze ukarabati na ukarabati umeanza. Naomba tupewe fedha zilizobakia kwa sababu tuliahidiwa kupewa fedha zilizobakia mwishoni mwa mwaka 2013/2014 na sasa ni mwezi Mei. Namwomba Mheshimiwa Waziri atupatie fedha zilizobakia.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI**: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naunga mkono hoja hii, pili nampongeza Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuendeleza elimu nchini, pamoja na changamoto zinazoikabili sekta hii hasa upungufu wa rasilimali fedha na watu hususan walimu na masomo ya sayansi. Pamoja na pongezi hizi napenda kutoa maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi la kutumia majengo ya Kambi ya Konoike yaliyopo Kata ya Chikuyu (Manyoni) kuwa Chuo cha VETA. Naishukuru hatua ya Wizara ya kuwatuma Maafisa wa VETA kuja kukagua majengo hayo na baadaye ilifuatia ziara ya Naibu Waziri, Mheshimiwa Jenista Mhagama. Ziara zote mbili zilionyesha uwezekano wa majengo hayo kutumika kutoa mafunzo ya VETA kwa kuanzia na fani chache, kisha zitaongezeka hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasisitiza kwamba mwaka 2014/2015 shughuli za maandalizi yaanze kwa VETA, Wizara na Halmashauri kushirikiana kuweka mazingira ya chuo hicho kuanzishwa ili kutekeleza sera ya Wizara kwamba kila Wilaya iwe na Chuo cha VETA.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia pia kuhusu suala la kurejesha shughuli za taasisi ya elimu ya watu wazima. Taasisi hii huko nyuma ilikuwa imeendesha masomo ya sekondari kwa watu wazima. Sura hiyo ilisaidia wananchi wengi kupata elimu ya sekondari japo shule za sekondari zilikuwa chache sana wakati huo. Hivi sasa sekondari zipo nyingi (kila kata) na kuna watu vijijini wanaotamani sana kusoma masomo ya sekondari, lakini mfumo/utaratibu haupo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara itazame suala hili kwa makini ili kurejesha utaratibu wa kuwezesha watu wazima vijijini wanaopenda kupata masomo ya sekondari saa za jioni na siku za mapumziko *(weekends)* ili kuinua kiwango cha elimu vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala linguini ni upungufu wa walimu wa masomo ya sayansi. Katika kila Wilaya kuna upungufu mkubwa sana wa walimu wa masomo ya sayansi pamoja na jitihada za Wizara kuhamasisha vijana

kupenda masomo ya sayansi ili hatimaye tupate walimu wa sayansi, mkakati wa haraka ni kuona uwezekano kupata walimu hao kutoka nchi jirani za Afrika Mashariki hadi hapo tutakapojitosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kupunguza karo za walimu, Serikali kupitia Wizara hii, Wizara ya Fedha na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa mwaka 2014/2015 ichukue hatua thabiti kuondoa kero za walimu hasa madeni yao, stahili zao mbalimbali za kiutumishi na posho ya mazingira magumu. Kero hizi zikipatiwa ufumbuzi zitaleta motisha kwa walimu na hiyo ni nyenzo muhimu katika kuboresha elimu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, suala la huduma ya nyumba kwa walimu hasa vijijini nalo lipewe msukumu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena kusema kwamba naunga mkono hoja hii.

**MHE. JUMA SURURU JUMA**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara na viongozi wake kwa kuweza kufanya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mfumo wa kuhudumia walimu nchini ambapo bado hadi leo unahudumiwa na chombo zaidi ya kimoja, ni kweli walimu hapa nchini wanapata shida sana kupata au kufuatilia masuala yao. Hivyo naomba Serikali ni vema ikaweka chombo kimoja au mfumo mzuri wa huduma za walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la ukaguzi wa elimu nchini, ni muda mrefu sasa ukaguzi umekuwa suala tete bado na huenda ndilo linalotaka kuleta athari ya kushuka wa elimu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kutilia mkazo suala hili na kutoa fedha nyingi katika suala la ukaguzi au vilevile ikiwa Serikali itaona taabu kuihudumia idara hii ni vyema suala ya ukaguzi lifanywe kuwa wakala ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

**MHE. RICHARD M. NDASSA**: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba ya Wizara ya Elimu. Naomba niiombe Wizara isadie mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni upatikanaji wa walimu wa sayansi katika jimbo langu hasa katika shule ya sekondari ya Sumve *Girls A-Level.*

Pili, Serikali ione umuhimu wa kumaliza upungufu wa madawati katika shule za msingi na sekondari, jamii imejitahidi kiasi cha kutosha.

Tatu, Serikali ione umuhimu wa kuwalipa wazabuni waliotoa huduma katika shule zetu za sekondari ili kuwawezesha kulipa madeni yao waliyokopa kwenye mabenki mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. ANTONY GERVASE MBASSA**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nielekeze mchango wangu kuhusu Vyuo vya Maendeleo ya Ufundi. Vyuo hivi ni muhimu sana katika kusimamia maendeleo ya wananchi. Lengo kuu ni kuwajengea vijana uwezo wa kujiajiri na kuhimiza suala zima la ujasiriamali.

Vyuo hivi vilivyoanzishwa vina uhaba mkubwa sana wa wakufunzi, vitendea kazi na vitendewa kazi kwa kiasi kikubwa sana. Vyuo hivi sasa vinategemewa na vijana wengi sana hapa nchini. Lakini kwa hali ilivyo sasa, inaonekana kazi ya kundaa wakufunzi na kuvipatia vyuo hivi vitendea kazi, kasi yake ni ndogo sana.

Naiomba Serikali kuwa mpango mkakati wa dhati wa kuokoa vyuo hivi ni wazi wananchi wanahitaji sana na ni muhimu katika kujenga na kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna suala la ukaguzi na usimamizi wa elimu inayotolewa na vyuo hivi, hakika ni vema kuwa na ukaguzi ili kuharakisha taaluma inayotolewa ina ubora na kiwango stahili. Vyuo vya VETA hakika kwa sasa vinatoa wataalamu bora. Isiwe sifa hii ni kwa ajili ya vyuo vichache vilivyopo mijini kama vile VETA - Chang'ombe au VETA - Dodoma. Ikiwezekana hata vyuo vyetu hivi vilivyopo pembezoni viwe na kiwango sawa cha ubora wa taaluma kama inavyostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa kuna suala la uanzishwaji wa vyuo mbalimbali mitaani. Vyuo hivi vinatoza ada bila utaratibu maalum, vyuo hivi havina usajili rasmi na vinaanzishwa katika mazingira yasiyo rasmi kiasi kwamba nyumba na mazingira mara nyingi hayafai.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kuliangalia suala hili kwa upana mkubwa sana. Kuwepo na chombo cha kufuatilia suala hili na kuweka utaratibu maalum kwa maana ya kuwa na kiwango cha ada zinazoeleweka ambazo hazimuumizi mzazi, pia usajili na ukaguzi wa mara kwa mara ili kuwa na vyuo vinavyoeleweka. Vyuo hivi vina wahadaa wananchi kuwa watoto hawa watakapohitimu watapewa ajira, wakati suala la ajira limekuwa gumu kutatuliwa. Sasa huu uendeshaji wa vyuo bandia mitaani bila kuwa na

wakufunzi mahiri na wenye sifa, pia hali ambayo inapelekea kutotambuliwa katika maeneo vilipo. Naiomba Serikali kufanya utaratibu wa kuhakiki vyuo hivyo ili vitoe taaluma inayotambuliwa na Baraza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa napenda kumpongeza kwa kutambua shule zilizofanya vizuri mwaka jana, hakika juma hili la elimu lilitoa nafasi ya walimu wa Halmashauri mbalimbali, mikoa kufanya tathmini ya kielimu. Lakini pamoja na mafanikio hayo, ukokotoaji wa alama kwa ajili ya kuwapatia washiriki ulikuwa na kasoro nyingi. Hakika Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo ilifanya vizuri na kushika nafasi ya pili kitaifa. Jambo la kushangaza ni pale ilipopata medali nne tu kati ya 11 zilizopaswa kutolewa. Hii ilipunguza morali na hata baadhi ya Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo naomba mara nyingine utaratibu mzuri ufanyike ili mapungufu yaliyojitokeza yasirudiwe.

**MHE. MARYAMU SALUM MSABAHA**: Mheshimiwa Naibu Spika, suala la elimu kwa Tanzania limekuwa ni tatizo sugu, kwani Serikali ina shule za sekondari za kutosha hasa vijijini. Asilimia kubwa ya watoto (wanafunzi) ambao wanafaulu wanaishi vijijini wanakata tamaa ya kuendelea na masomo. Shule za sekondari ambazo ni za kata zinakuwa zipo mbali na makazi yao, wanatumia kilomita nane hadi 10 kufika shule.

Nashauri Serikali ingejenga mabweni katika shule za vijijini kwani wanafunzi wanapata taabu hasa wa kike, kwa sababu wakiwa wanaenda shule njiani wanakutana na vishawishi, wengine wanaishi mageto kwa kukosa hosteli, kuishi mbali na kwao. Wanafunzi wengi hasa wa kike wanashindwa kumaliza masomo yao kwa kupata mimba kwa sababu shule zipo mbali, wanafunzi wanakata tamaa ya kusoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iwe inawapatia wanafunzi chakula shuleni na wanafunzi ambao wanasoma masomo ya sayansi wanakuwa hawawezi kusoma kwa vitendo kwa sababu wanakuwa hawa vitendea kazi (maabara). Kuhusu suala la elimu, shule za Serikali ni mzigo kwa Taifa kwani hazitoi elimu bora tofauti na nchi za wenzetu kwa mfano Uganda, Kenya, Malaysia na kadhalika wanazithamini shule za Serikali. Nchi yoyote ambayo imeendelea inawekeza kwenye elimu, kwani wanakuwa wanapata maendeleo kwa kupata elimu, tofauti na Tanzania kwani Watanzania wengi hawathamini elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Watanzania wengi wanathamini shule za watu binafsi *(private)* kwa sababu zinatoa elimu bora, Tanzania tupo nyuma kwa elimu tofauti na Kenya. Kwa mfano wanafunzi wa Kenya wakienda shule wanaeenda na *laptop,* tofauti na wanafunzi wa Tanzania wanaenda shule na

fagio, jembe, kibati cha taka na kadhalika. Naishauri Serikali tuwekeze katika suala la elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mshahara wa walimu wanaofanya kazi pembezoni, baadhi ya walimu wanaofundisha pembezoni wanasomesha wanafunzi katika mazingira magumu kwani hawana vitendea kazi, wanaishi katika mazingira magumu, wanacheleweshewa mishahara yao na hawana miundombinu. Hii inapelekea wanafunzi wengi kufeli kwani walimu wanakuwa hawawasomeshi wanafunzi hawa kwa wakati muafaka, badala yake walimu hawa wanashughulika na biashara zao, baadhi ya walimu huamua kwenda kufundisha shule za watu binafsi *(private)* ili wapate kujikimu kimaisha. Ni lini Serikali itawalipa walimu madeni yao na kuwaongezea mishahara?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu (vyuo), mikopo ya vyuo vikuu imekuwa ikitolewa kwa ubaguzi. Wale ambao wana uwezo ndiyo wanaopewa mikopo, watoto wa wakulima hawapati mikopo kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iwape kipaumbele kwa watoto ambao wanatoka familia duni na iwachukulie hatua za kisheria wale wote wanaochukua mikopo na kushindwa kurudisha kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la elimu ya watu wazima, kwa kuwa kuna Watanzania wengi ambao hawajui kusoma na kuandika, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha elimu hii ya watu wazima inafika vijijini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhsuu watoto (wanafunzi) wanaopata mimba wakiwa shuleni, kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi imefanikiwa kuwarudisha shuleni wanafunzi waliozaa katika umri mdogo ili wapate kujiendeleza kimasomo, ni lini Serikali Tanzania Bara itawajengea shule maalum wanafunzi ambao walipata mimba katika umri mdogo ili wapate kujiendeleza kimasomo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la mitaala ya elimu, mitaala hii ya elimu inasababisha wanafunzi kufeli mitihani. Naishauri Serikali isiwe inabadilisha mitaala ya elimu mara kwa mara.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa elimu ni msingi wa maendeleo kwa maisha ya binadamu, ili mtu aweze kuendelea anahitaji kupata elimu kuanzia elimu ya awali, ya msingi, sekondari hadi chuo kikuu. Tumeona nchi nyingi duniani zenye maendeleo zimefanikiwa kisayansi, kijamii, kisiasa na kiuchumi kutoka na kuwa na elimu kamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu Tanzania kwa miaka ya karibuni kuanzia miaka ya 1985 elimu ya msingi na sekondari tumeanza kupiga hatua

nzuri. Watanzania wengi sasa wana elimu ya msingi na sekondari. Naipongeza Serikali kwa kujenga shule za kata, hii imesaidia sana kuwa na Watanzania ambao angalau wamepata elimu ya sekondari na kufuta ujinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mazuri hayo zipo changamoto ambazo zinakabili sekta hii ya elimu:-

(a) Upungufu wa walimu wa sayansi kwa shule za sekondari.
(b) Ongezeko la watoto yatima na watoto wanaotoka katika mazingira magumu.

(c) Mazingira magumu ya walimu hasa vijijini, nyumba za walimu bado hazitoshi.

(d) Upungufu wa madawati mashuleni.

(e) Upungufu wa vifaa vya kufundishia mashuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naiomba Serikali kutoa ufafanuzi juu ya mikakati iliyopo ili kupunguza kero hizi ambazo nimetaja hapo juu.

Pia napendekeza ada kwa watoto yatima na wale wanaotoka katika mazingira magumu ifutwe ili watoto wengi waweze kupata elimu ya sekondari na elimu ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza walimu wanaosomea masomo ya sayansi Chuo Kikuu wapewe mkopo asilimia mia moja ili kuwavutia watoto wengi wachukue masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namuomba Waziri atoe ufafanuzi wa *grading* hasa kwa shule za sekondari kuanzia matokeo ya mwaka 2013/2014 yamewachanganya wazazi na watoto bado hawajaelewa vizuri sababu *division one* mpaka *four marks* hazieleweki kwa mfano A, $B^{\pm}$, B, C, D na E.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtoto ili ajiunge na Chuo cha Ualimu awe amepata alama gani au kuanzia *division* gani na mwisho *division* gani na *point* ngapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naunga mkono hoja.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO**: Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri wa Elimu na TAMISEMI, Katibu Mkuu na wataalam kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ni *investment* muhimu kwa maendeleo ya nchi na watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za kutosha ziwekwe kwenye ukaguzi ili kuthibitisha na kuhakiki kuwa kinachopaswa kufundishwa kinafundishwa. Aidha, kudhibiti ubora wa elimu na kwamba watoto wanapata taaluma na maarifa stahiki. Mazingira ya kufundishia na kujifunzia yaboreshwe kama madarasa, madawati, vitabu na vifaa vingine na Serikali iweke fedha zaidi katika eneo hili ili wanafunzi wapate mazingira wezeshi ya kujifunzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, uratibu na ukaguzi wa elimu uimarishwe katika ngazi ya kata na kuwa karibu na shule vijijini.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo kubwa la utekelezaji mipango ya maendeleo ya miaka mitano kutokana na ukosefu wa fedha zikipangiwa Wizara hii ya Elimu.

Suala la upungufu wa walimu ni kubwa kwa mujibu wa taarifa ya Waziri wa Elimu, asilimia 55 katika masomo ya sayansi na hisabati, hili ni pengo kubwa sana hivyo Mheshimiwa Waziri kutokana na kutekeleza mpango wa maendeleo wa miaka mitano je, ni kwa kipindi gani upungufu huu utazibwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, shule za binafsi zimetoa mchango mkubwa katika sekta ya elimu bora kwa jumla na hii inadhihirisha kwenye ufaulu tofauti na nchi za jirani ambazo shule za Serikali zinatoa ufaulu mkubwa kutokana na kutambua mchango wa sekta binafsi katika elimu, je, Serikali imejipanga vipi kuisaidia na kuzipa fursa sekta binafsi ili ziweze kutoa huduma na elimu bora zaidi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Wizara haianzishi taasisi ya kuratibu kusimamia hasa viwango vinavyotozwa na shule binafsi ili viwango, mazingira na ubora wa elimu iendane na malipo yanayotozwa na shule hizi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi zilizopiga maendeleo ziliweka lengo kuwa na idadi isiyopungua 60% ya wahitimu wa vyuo na taaluma ya sayansi na hisabati, Waziri naomba utueleze mkakati wa kujua katika kila fani ya mahitaji ya wataalamu wa sayansi kama tisa, walimu, wahandisi na madaktari.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimuulize Waziri vyuo vingapi vya huduma ya sayansi vimehitajika kukabiliana na upungufu huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia Waziri atueleze namna wanavyofanya kazi na Wizara ya TAMISEMI kupunguza malalamiko ya walimu.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia maandishi nichangie hotuba ya Wizara ya Elimu. Ni ukweli ulio wazi matokeo au utendaji wa Wizara hii yakipimwa kufuatia wahitimu si mazuri, tumekuwa tukishuhudia wahitimu ambao kimsingi wana upungufu mwingi au wanashindwa kukidhi matumaini ya wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni mara yangu ya nne nikichangia Wizara hii. Akili yangu yote na ujuzi nilionao katika utawala wa rasilimali watu, tatizo la elimu ya Taifa ni mfumo na muundo wa Wizara zinazosimamia au kuhusika na sekta ya elimu. Nimelisema hili na bado naamini hivyo. Ili kutatua sehemu kubwa ya sekta hii na hasa vikwazo vinavyotokana na rasilimali watu ni muhimu iundwe Wizara ya kipekee itakayosimamia sekta hii kuanzia shule za chekechea, awali, msingi mpaka sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiacha upungufu wa kimuundo na wa mfumo, Wizara imejipanga na kuja na hotuba ambayo ikitekelezwa tunaweza kusonga mbele kama Taifa. Hata hivyo yapo mambo ambayo yanapaswa kuangaliwa kwa makini katika kutekeleza mpango wa Wizara kama ilivyopendekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inalenga kufikia lengo la asilimia tano (5%) ya rika husika kwa kuona kuwa wanapata elimu ya juu. Hapa ushauri kwa Serikali ni kuwa iwapo *linkage* kati ya sekta ya elimu na sekta nyingine ambazo zitatoa fursa ya kuwapokea wahitimu hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo lengo la kuhamasisha elimu ya ufundi kupitia *VETA* kwa kuongeza usaili wa wanafunzi. Nashauri Serikali ichukue jitihada za ziada kuhakikisha shule za ufundi zinakuwa chaguo na wala si shule ili mradi. *VETA by choice not by chance*. Jamii ina mawazo potofu kuwa shule za ufundi ni kimbilio kwa wale walioshindwa au kupita katika mkondo wa kutoa elimu inayofahamika kwa watu wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo la kugawa rasilimali. Hapo nazungumzia ombi langu la miaka mitatu juu ya ukarabati wa Chuo cha Elimu Katoke hasa katika ujenzi wa vyoo na mabweni. Jamii kama inavyofanya kwa sekondari nipo tayari kusaidiana na Serikali kwa kuleta tofari, mchanga na mawe ili tuokoe chuo hiki ambacho kipo katika hali mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna neema ya ujio wa sera ya elimu ambayo inabidi iangaliwe kwa makini mpango wa elimu msingi unaweza kuwa mzuri iwapo kutatengwa kipindi cha mpito. Kipindi cha mpito kitumike kuhakikisha kuwa rasilimali zote zimepatikana kabla ya kuanza hiyo sera ya elimu msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nieleze masikitiko ya wananchi wa Mkoa wa Kagera juu ya mahitaji ya chuo cha ufundi, hoja hapa ni *VETA* ngazi ya Mkoa. Maamuzi ya Wizara kujenga vyuo vya ufundi ngazi ya Mkoa kwa Mikoa mipya ili

hali Kagera ni Mkoa wa zamani wenye matatizo ya kijiografia inabidi kuandaliwa upya. Tofauti na Mikoa mingine Mkoa huu kwa pande nne za dunia ni Kusini tu tunapakana na Mikoa mingine kwa usafiri rahisi na nafuu wa barabara. Eneo lililotengwa ilikuwa ni busara na nashauri wapewe fursa ya kujengewa Chuo cha *VETA* ngazi ya Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la usajili wa shule. Tatizo la idara hii ni kuwa wanabidi kuwasiliana na mamlaka zinazohusika na uhamasishaji wa ujenzi wa shule jambo ambalo hawafanyi. Tumeshuhudia idara hii ikiwakatisha tamaa wananchi kwa kukataa kusajili shule zao (shule za vijiji na kata) au na kuwapa masharti magumu kutekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wamehamasika kujenga shule, wajibu wa Serikali ikiwemo Idara ya Usajili kuwasaidia wananchi pale wanapokwama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupata kauli ya Serikali kuhusu michango mingi inayochangishwa na kupelekea wanafunzi mara kwa mara kurudishwa nyumbani kwa sababu hawana fedha. Kumbuka Serikali mara kwa mara ilikuwa ikitoa kauli kuwa elimu shule za msingi ni bure, lakini kiuhalisia ni gharama kubwa, ni bora sasa Serikali itangaze ada rasmi za shule za msingi ili wazazi wajiandae na siyo kama ilivyo sasa kushitukizwa. Zipo shule kila mwanafunzi anatakiwa kila siku shilingi 300/=, kila Alhamisi shilingi 1000/= na kila Jumamosi shilingi 2,000/= na mara kwa mara walimu huanzia ziara za wanafunzi kwa kila mwanafunzi kuchangia kuanzia shilingi 7,500/= hadi shilingi 10,000/=. Hayo siyo majanga kwa wazazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali italipa mishahara ya walimu wanaojitolea katika shule za Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, lini Serikali italipa walimu wapya stahiki zao na walimu wanaodai madeni yao ya muda mrefu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara/Serikali iboreshe elimu ya awali, msingi ili kupata msingi bora wa elimu kwa kuimarisha ukaguzi ngazi zote, kwani bila wakaguzi Wizara haiwezi kujua matatizo halisi na bajeti sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna tatizo kubwa la shule za sekondari za kata kutokuwa na bweni na kusababisha wanafunzi kupanga mitaani na ni madhara makubwa kwa afya na ufaulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka mingi sasa kuna wanafunzi wengi wa kipato cha chini wanapohitimu *standard seven,* kidato cha nne hadi chuo kikuu wapo mitaani na hawana ajira, kibaya zaidi elimu waliyoipata haijawaandaa kujiajiri na waliobahatika kupata elimu ya ufundi wachache hawana vyuo vya ufundi vya kujiendeleza. Naishauri Serikali iwekeze kwenye vyuo vya ufundi na wanafunzi wanapomaliza mafunzo wakopeshwe vifaa vya fani zao na mitaji ili wajitegemee, hayo yafanyike ngazi zote za msingi, sekondari hadi chuo kikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna shule kadhaa za watoto wenye ulemavu ambazo hazina walimu, vifaa na kadhalika. Mfano, shule ya watoto wenye ulemavu iliyopo Lipangalala – Ifakara, Wilaya ya Kilombero, naomba Waziri aitembelee ili akaone hali ilivyo kweli utahuzunika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wanafunzi wenye ulemavu ambao humaliza shule za msingi na sekondari wamebaki mtaani/majumbani na Serikali halioni, upo umuhimu wa kuanzisha/kuimarisha shule za ufundi za watu wenye ulemavu na kupelekea baadhi ya wazazi wenye watoto wenye ulemavu hupeleka watoto wao nchini Kenya na hata hivyo kutokana na hali tete ya usalama nchini huko inakuwa ni vigumu kuendelea kupeleka watoto wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ndogo ya walimu na hata baadhi ya walimu wanajitolea je, ni kwa kiasi gani walimu hao wanajaliwa kwa hata kuwapa posho? Kwa kweli walimu hao hujitolea na huchangiwa na wazazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati umefika sasa kuboresha elimu kwa kuanzisha mfuko wa elimu kwa watoto wa Tanzania kwa kutenga 2% ya mapato ya rasilimali za asili za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyuo vikuu vya Serikali na binafsi vipo kwenye hali ngumu kwa wanafunzi kukosa ada, vifaa kubadilishiwa, kupandishiwa ada kiholela.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Serikali haitaki kutoa mikopo kwa wanafunzi waliomaliza ama *form iv/form vi* miaka mitatu iliyopita ambao wana sifa za kusomea ualimu na matokeo yake kuwanyima mikopo ili hali upo upungufu mkubwa wa walimu?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupata majibu ya Serikali kuhusu upangishaji wa Ofisi za Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kwa gharama kubwa iliyopo Mwenge – Dar es Salaam badala ya kujenga ofisi zao, huo sio ufisadi? Nataka ufafanuzi kuhusu hilo je, wamepanga kwa kodi ya shilingi ngapi kwa mwaka?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Chuo cha Ustawi wa Jamii kilichopo Sinza/ Kijitonyama Dar es Salaam je, kwa umiliki wake halisi eneo la chuo lina ukubwa gani kiwanja namba ngapi? Naomba nipate ramani ya eneo hilo na kimvuli cha hati.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono mawazo yaliyotolewa na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa James Mbatia, pia Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Nyambari Nyangwine na wengine ambao wanaishauri Serikali ifanye uamuzi mgumu wa kutenga rasilimali nyingi zaidi kuliko ilivyo sasa ili kuinua kiwango cha elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazo la Mheshimiwa James Mbatia kushauri Rais aunde Tume ya kuchunguza matatizo yanayoukabili mfumo wa elimu ni wazo muafaka. Ni bora kama Taifa tutafakari kwa sauti moja na tuishauri Serikali ichukue hatua kama Mheshimiwa James Mbatia alivyopendekeza. Nchi nyingine kama Marekani zimeshafanya hivyo siku za nyuma, hakuna sababu kwa nini tusijifunze kutoka kwa wengine. Hivi sasa changamoto zinazoikabili Wizara zimekuwa zikikusanyika na kujilimbikiza kiasi kwamba juhudi za Waziri/Naibu Waziri na wataalamu wa Wizara hazionekani kuonesha mafanikio mwaka hadi mwaka, juhudi za juu zaidi zinahitajika. Baada ya kuyasema hayo, ningependa sasa kujielekeza kwenye masuala ambayo hayajachangiwa na wenzangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utamaduni wa kusoma umeshuka sana Tanzania, Watanzania wengi hawapendi kusoma vitabu vya aina mbalimbali. Dkt. Mcharazo anafanya kazi nzuri sana ya kupeleka vitabu katika maktaba mbalimbali nchini lakini watu wangapi husoma vitabu hivyo? Mara nyingi ukienda kwenye maktaba utakuta watoto tu wakijisomea ambalo ni jambo zuri. Si rahisi kuwahamasisha watu wazima kuanza kupenda kusoma.

Ushauri wangu ni kuwa Serikali ielekeze juhudi zake kujenga utamaduni wa kusoma miongoni mwa wanafunzi katika shule za msingi na shule za sekondari. Hatua za kuchukua:-

(a) Wizara iandae progaramu ya usomaji ambao inahitaji walimu waliojifunza kufundisha kusoma ngazi zote za shule za msingi na shule za sekondari ili kuwa na programu nzuri ya usomaji, kunahitajika maktaba za shule zenye vitabu vya aina mbalimbali.

(b) Wizara iandae programu ya uandishi inayoenda sambamba na programu ya usomaji kwa ajili ya ngazi zote kwa shule za msingi na shule za sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, programu hizi zikitekelezwa ndizo zitakazokuza utamaduni wa kusoma miongoni mwa vijana wetu ili baadaye tuunde Taifa la watu wanaopenda kusoma na kuandika vitabu na maandiko ya aina mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mradi wa *Literacy and Namercy Education Support* mradi huu ni mzuri lakini utahusika tu na darasa la kwanza na la pili kuinua viwango vya KKK. Serikali ina mpango gani ili kuendeleza na kuupanua mradi huu hadi darasa la saba kwa nchi nzima?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mfumo wa alama na mkondo wa madaraja wa shule sekondari maelezo ya Kaimu Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani kwa Kamati ya Huduma za Jamii kuhusu jambo hili yalieleweka na yanakubalika kiasi kwa sasa. Napenda kushauri yafuatayo kuhusu jambo hili:-

(a) Mfumo wa alama nne utenganishwe na ule wa kidato cha sita.

(b) Baraza la Mitihani lifuatilie kwa ukaribu mfumo mpya wa alama na madaraja kwa ajili ya kuuboresha ili baadaye uwe ni mfumo/muundo bora Afrika Mashariki.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujua walimu waliomaliza mwaka 2013 *BED* pale *University of Dar es Salaam* hawajapata ajira kwa kisingizio cha kutoajirika. Hili ni janga, kama hawaajiriki ni kwa nini *course* hii iwepo vyuoni? Ni kwa nini kati ya vijana 67 waliohitimu ni 21 tu wamepata ajira tena *secondary* na si vyuoni tofauti na alivyojibu Naibu Waziri, TAMISEMI kuwa hawaajiriki kwa kuwa walisomea *Ed. Psychology?*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara itueleze nini hatma ya vijana hawa? Ni kwa nini *course* hii isisitishwe kama haiajiriwi wakati *prospectus* inaeleza wazi kuwa wataajirika katika vyuo vya ualimu?

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama vituo vya mitihani hasa kwenye shule za msingi na shule zenyewe kwa nini katika Jimbo la Nkasi Kusini na Wilaya ya Nkasi kwa ujumla kuna shule 14 zilizopo mwambao mwa Ziwa Tanganyika hazina vituo vya kufanyia mitihani badala yake wanaenda shule zingine jambo ambalo linawaletea usumbufu sana watoto na pia inahatarisha maisha ya watoto walio wengi sana na hasa kwa vile ni maeneo yenye changamoto za usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, zile sababu zinazofanya watoto wajongee na wasimamizi wasiende kwenye shule hizi zinatosha pia kuwa na mashiko kwa watoto ambao ni wengi shule hizo kutoenda kwa sababu zilezile. Katika shule hizi hali ya usalama kwa usafiri unaotumiwa na shule kusogeza wanafunzi ni mbaya, shule hizo ni shule za msingi za Tundu, Izinga, Mwinza, Lyapinda na kadhalika. Hali hii nimeisema mara kwa mara hata sijafanikiwa. Naiomba Wizara iniambie leo ni lini shule hizi zilizopo Wilaya ya Nkasi zitapatiwa vituo vya kufanyia mitihani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Nkasi ina Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Chala na Serikali ilidhamiria kukiboresha chuo hicho kiwe kinatoa mafunzo ya VETA, leo hii walimu wapo wawili tu na Mkuu wa Chuo ni wa tatu, unategemea nini, usafiri wa chuo hiki ni pikipiki. Fedha ya kuendeshea walipewa tangu Januari mwaka jana mpaka sasa hawana kitu kabisa. Changamoto hii ipo wazi na ilishapelekwa kwa Katibu Mkuu na aliweza pia kutembelea chuo hicho. Mpaka sasa hakuna marekebisho yoyote kati ya changamoto alizozikuta. Naomba Serikali iboreshe chuo hiki haraka kwani ni muhimu kwa maendeleo ya vijana wetu nchini, "Mafunzo ya VETA ni muhimu kwa vijana hasa wanaomaliza katika shule zetu za kata."

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukosefu wa walimu katika maeneo mengi walimu hawatoshi na eneo la Jimbo langu ni mojawapo licha ya juhudi inayofanyika na Serikali lakini changamoto hii bado inakuwepo kutokana na mgawanyo usio na uwiano, maeneo yenye upungufu mkubwa na ambayo yapo chini kielimu yapewe rasilimali za kuinua elimu zaidi kidogo kuliko maeneo yenye nafuu, mgawanyo huu unatakiwa uwe katika sera za mgawanyo wa rasilimali za Taifa. Nkasi tunahitaji walimu zaidi tena wote wa shule za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu posho za walimu nashauri walimu wapewe posho zao wanazostahili bila kucheleweshwa ili waweze kufanya kazi vizuri. Wapewe pia posho ya mazingira magumu, kuanzia sasa hivi imekuwa ahadi isiyofikia utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu walimu wa sayansi upo upungufu mkubwa wa walimu wa sayansi, naitaka Serikali iwatafute nje na ndani au iwa-*recruite,* itafute namna ya kuwaandaa kwa mkakati maalum kabisa, haiwezi ikawa kilio, kilio cha kila siku kazi ya Wizara ni sasa? Tafuteni ufumbuzi tafadhali.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza na kuunga mkono hoja. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa utendaji wao wa kazi, wanafanya kazi nzuri sana kuiondoa Wizara kutoka ilipokuwa na kuelekea katika maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumza na baadhi ya walimu ambao shule zao zilikuwa zinaendeshwa na Serikali Kuu, wanataka kurudi Wizara ya Elimu, maoni yao wanasema kuwa toka wamepelekwa Halmashauri maendeleo ya shule hizo yameshuka sana na yanaendelea kushuka. Nimeongea na walimu wa shule hizo sina budi kuipongeza Wizara ya Elimu kama ni kweli Wizara ya Elimu ingekuwa inafanya vibaya je, leo walimu hawa wangedai kurudi Wizarani?

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya walimu yanatokana na madai yao walipwe sasa. Nasikitika kuwa walimu hao bado wanaenda likizo bila malipo, bila nauli, je, tunamaliza madeni au tunaongeza madeni?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Chuo cha VETA katika Wilaya ya Uyui, Jimbo la Igalula VETA haijajengwa, ni lini inajengwa? Vijana wengi wapo tayari kusomea masomo ya fani mbalimbali za ufundi, Wizara ya Nishati na Madini inaweka umeme kata 10 za Jimbo la Igalula, nyumba zaidi ya 1000 zinahitaji *wiring* na pia nguzo na waya za umeme, mafundi umeme wengi watahitajika. Chuo cha VETA, kijengwe haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Igalula halikupata shule mbili za mfano na maabara mbili. Zote zimejengwa Tabora Kaskazini, hivyo basi Wizara ishirikiane na TAMISEMI kunijengea na kuboresha sekondari za Goweko na Tura kwa maabara na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali za walimu na maslahi yaboreshwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Jenista Mhagama, Naibu Waziri kwa kuteuliwa kwake katika kazi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi yamechangiwa na Wabunge wengine hivyo napenda kutoa ushauri wangu mfupi kama ifuatavyo:-

Kwanza, walimu wanalalamika sana madai yao na wapo wengi wanatafuta shule za binafsi ili waweze kuhama Serikalini kwani wanadai

kwamba wamechoshwa na usumbufu wa Serikali. Hivyo naomba suala hili litazamwe kwa umakini mkubwa walimu wapewe haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule za binafsi za bweni zifuatiliwe kwa upande wa zahanati na chakula. Zipo shule ambazo zahanati zake ni za ubabaishaji na pia zipo shule ambazo hifadhi ya chakula si nzuri na hivyo kupelekea wanafunzi kupata maradhi ya kuhara.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ishughulikiwe na chombo kimoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SALOME D. MWAMBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni muhimu kwani ukimsomesha mtoto utakuwa umelisomesha Taifa lote.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia vifaa vya kufundishia na kujifunzia *(teaching and learning materials)*. Vifaa vya kufundishia na kujifunzia ni kero, wanafunzi hawafundishwi ipasavyo, wananchi wamehamasishwa kujenga maabara lakini zimejengwa maboma tu hakuna vifaa vya kufundishia, matatizo ya nyumba za walimu utakuta walimu watano hadi sita wanakaa nyumba moja. Mwalimu anahitaji mazingira mazuri na utulivu wa hali ya juu. Utakuta mwalimu anapanga uswahilini, atasoma na kujiandaa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, vifaa vya kufundishia hakuna mashuleni au zana za kufundishia madarasa yamejaa. Naomba Serikali ilitilie mkazo jambo hili. Vilevile Serikali itoe motisha kwa shule, wanafunzi na walimu wanaofundisha shule zitakazofanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu watengewe chombo kimoja kitakachowasaidia walimu kufuatilia maslahi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. PHILIPA G. MTURANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, walimu wamekuwa wakihangaishwa sana bila kufahamu ni Wizara ipi hasa inaowajibu wa kuwashughulikia, hili limesababisha wengi wao kukosa haki zao stahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba na kuishauri Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ianzishe chombo kimoja rasmi cha kuwahudumia walimu yaani *Teachers Service Commission Delivery*. Chombo hiki kitashughulikia mambo ya walimu tu. Mambo hayo ni kama vile ajue mishahara, kupandishwa madaraja, uhamisho, stahiki zote za walimu na ukaguzi. Serikali ianzishe ama iruhusu wakala binafsi atakayeshughulikia ukaguzi na wakala huyu atajitegemea na atasaidia ufanisi wa kazi, lakini pia wakala huyu atakuwa na

watu wake (wataalam), atakuwa na kasma yake, hii itafanya Wizara kuwasiliana na wakala huyo moja kwa moja badala ya kuwasumbua walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu posho, imefikia wapi posho ya kujikimu ya walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, elimu inaporomoka sana kwa kasi kwa sababu ya somo la muziki linalokuwa kichocheo kibaya katika ubongo wa watoto.

Pili elimu mbaya ya matambuzi ya via vya uzazi katika umri mdogo na kufanya ubongo wao uendelee kukua katika hali mbaya ya kufikiri mambo ya kikubwa na si hivyo tu mtoto kunyimwa mapigo na maonyo hawezi kuwa mtiifu na matokeo yake watoto hawana nidhamu kwa wazazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kemeo la walimu kutofuma vitambaa, kusukana, kufanya biashara wakati wa vipindi utiliwe mkazo. Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GREGORY G. TEU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu TAMISEMI kwa kazi nzuri ya kutimiza wajibu wao na kuendeleza uboreshaji wa elimu hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, namuunga mkono Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, kwa ushauri wake kwamba tuwe na azimio la kuunda chombo ndani ya Wizara kitakachohusika na masuala ya ualimu na usimamizi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara yetu ya Elimu iseme wazi kuhusu suala la kukifanya Chuo cha Ualimu kilichopo Wilaya ya Mpwapwa *(Mpwapwa Teacher's College)* ambacho ni chuo kikongwe kipatiwe hadhi ya kuwa Chuo Kikuu Kishiriki *(Affiliated University)* cha Chuo Kikuu cha UDOM, hatua hii tayari Mheshimiwa Rais alisharidhia je, utekelezaji wa ridhaa hii ya Rais itaanza lini?

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha mahali hapa nami niweze kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ya mwaka 2014/2015. Pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na wataalam wake kwa kuandaa hotuba nzuri yenye mkakati thabiti ya kukuza sekta ya elimu hapa nchini. Bajeti hii imelenga kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo inasisitiza katika kuinua elimu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu bora ni jambo la msingi sana ili kujenga Taifa lenye uwezo wa kustahimili ushindani wa kibiashara usiokuwa na mipaka. Hata hivyo katika Taifa changa kama Tanzania, kunahitaji mkakati wa kipekee wa kuboresha elimu kwa kushirikisha taasisi na mashirika yanayojihusisha na elimu, Serikali, wanafunzi na jamii kwa ujumla. Wanafunzi wana wajibu mkubwa katika kujenga maadili mema wakati wapo shuleni. Maadili yawe mazuri yaliyojikita katika taratibu zinazokubalika na jamii nzima kwa faida ya Taifa na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanafunzi bora mwenye maadili mema hana budi kujenga utamaduni wa kujitegemea hasa katika masomo, hili husaidia kujenga moyo wa kujituma na kufanya kazi kwa bidii. Kazi kubwa ya mwalimu ni kumwelekeza mwanafunzi kisha mwanafunzi anatakiwa kufuatilia kwa undani ili kupanua ufahamu wa jambo kwa kusoma vitabu. Hili ni jambo la msingi sana kwa sababu umejengewa utamaduni hasa miongoni mwa wanafunzi wa Tanzania wa shule za msingi hadi vyuo vikuu kusoma kwa ajili ya kufaulu mitihani tu, tena kwa njia rahisi maarufu vyuoni iitwayo kudesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi wana wajibu wa kuwapenda kuwaheshimu na kuwasikiliza walimu wao. Siri iliyopo katika hili ni kwamba kumheshimu mwalimu kunamfanya ajitoe zaidi na kuonesha njia iliyo bora zaidi. Huu ndiyo msingi wa maadili mema kwani husaidia wanafunzi kuwa na utamaduni wa kuiheshimu jamii wakatayoitumikia baada ya kuhitimu masomo. Aidha, ni muhimu kwa wanafunzi kushirikiana na jamii wanayoishi nayo ili kuyajua mahitaji na changamoto zinazoikumba jamii, mwanafunzi anapaswa kujenga utamaduni wa ushirikiano wa karibu sana na wenzake kuanzia nyumbani, shuleni kisha kushiriki shughuli za kitaifa ili jamiii ishuhuhudie umuhimu wa elimu anayoipata.

Vilevile kujikubali na kujitambua ni jambo la msingi katika kuinua elimu nchini. Wanafunzi wengi kwa sasa wanazidiwa na ushawishi wa nguvu za utamaduni wa nchi za Magharibi. Wanafunzi hawa wanatakiwa kujielewa kuwa wapo katika nchi ya ulimwengu wa tatu na ili kujikwamua hawana budi kuthamini utamaduni wa nchi yao. Ni wajibu wa mwanafunzi kuhoji na kuelewa ukweli wa nguvu za ubepari wa nchi za Magharibi kwani hata ukosefu wa maadili kutokana na ushawishi wa siasa za nchi za Magharibi. Ni ukweli usiopingika kuwa maadili ni nguzo ya utamaduni wa jamii na elimu bora ni ile inayoleta manufaa kwa jamii na si vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kueleza mambo yanayochangia wanafunzi kukosa elimu bora. Yapo mambo mengi sana yanayoikumba jamii kielimu hasa nikiangalia katika mazingira ya hapa vijijini kwetu kuna matatizo mengi ya kiuchumi vijijini ikiwa ni pamoja na ukosefu wa ajira na wazazi wengi

kuwa chini kiuchumi. Wazazi na walezi wamekuwa wakihangaika sana katika kuendeleza watoto shuleni kwa kutumia kipato kidogo kwa ajili ya malezi na malipo ya shule mfano mzazi anafanya kazi ya mama lishe, hapo hapo hana ushirikiano na mwenza wake, yaani baba ambaye anatakiwa kuwa mkuu wa familia hajishughulishi na kazi, mzigo wote wa utafutaji na malezi unamuangukia mama peke yake. Maisha haya duni yamekuwa yakiwakatisha tamaa watoto kuendelea mbele kimasomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, rushwa pia ni tatizo kubwa sana katika nchi yetu. Rushwa ni kikwazo cha maendeleo katika nchi. Shule nyingi zinakosa maendeleo kutokana na kukosa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, maabara, maktaba na kadhalika. Mabillioni ya fedha yamepotezwa kwa njia zisizoeleweka ambazo iwapo zingeingizwa katika akiba za shule hata kwa kusomesha wale wasiojiweza zingesaidia kuinua elimu nchini. Jamani inauma sana hasa kwa wanafunzi wanaonyanyasika kielimu, wanasoma kwa shida, wanaishi kwa shida hata kazi hawapati japo wanaelimu ya kutosha.

Vilevile wapo wazazi ambao hawapendi watoto wao wa kike wasome, kwa mfano mtoto anafaulu kwenda sekondari lakini mzazi anakataa shule kwa vile mtoto aliyefaulu ni wa kike, mzazi anaona huyo mtoto hana faida akisomeshwa, kitu hiki siyo kizuri kabisa, watoto wa kike wana haki ya kusoma kama wa kiume.

Mheshimiwa Naibu Spika, ubebaji wa mimba mashuleni pia ni chanzo cha ukosefu wa elimu bora. Sheria za shule haziruhusu mwanafunzi aliyebeba mimba kuendelea na masomo. Wazazi nao hawana uwezo wa kumuendeleza kimaisha. Matokeo yake ni kuwa mtoto huyu anaishia kutanga na njia.

Ushauri wangu ni kuwa Serikali pamoja na walimu waruhusu wanafunzi waliopata ujauzito kuendelea na masomo yao hadi watakapojifungua, vilevile ni vizuri jamii ijue nini maana ya elimu na iwe mstari wa mbele kuwasaidia watoto kupata elimu bora pia Serikali ijaribu kuangalia ni nini chimbuko la kukosa elimu bora na ni kitu gani kifanyike ili kuboresha elimu hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuzungumzia suala zima la maadili ya wanafunzi na elimu bora, kwa nini jamii imekaa mbali? Suala la maadili pia huhusisha wanafunzi kutowahi shuleni au kutokuwepo darasani hivyo kutoshiriki vipindi na masomo mbalimbali, wanafunzi kuvuta bangi, sigara na dawa nyingine za kulevya, kukutana na walimu na kutopeleka taarifa za maendeleo yao ya shule nyumbani na kadhalika. Wazazi, walimu, wanafunzi, Serikali na jamii nao wanahusika na kushuka kwa maadili miongoni mwa wanafunzi kwa mfano wazazi hawataki kufika shuleni kufuatilia maendeleo ya watoto wao na pia hawashiriki mikutano ya wazazi na uongozi wa shule. Baadhi ya walimu walituhumiwa kushiriki ngono na wanafunzi wa kike. Pia

baadhi ya walimu wa kike nao wana upungufu wa maadili kwa kuwatongoza wanafunzi wa kiume, wanafunzi walisemwa kwa kuiga tabia mbaya za nchi za Magharibi kupitia vyombo vya habari kama runinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, mitandao ya ngono, magazeti ya udaku na miradi ya asasi zisizokuwa za Kiserikali ambayo inahimiza mikusanyiko ya wanafunzi bila udhibiti wa mienendo yao. Hata tunaweza kuilaumu Serikali kwa kutokuwa na sheria inayotilia mkazo maadili ya vijana na kuwa kama upo usimamizi wake ni butu. Hakuna utaratibu wa kufuatilia wanafunzi wanatumiaje teknolojia ya mawasiliano yaani kompyuta, simu, kamera na vifaa vingine vya elektroniki vinavyoweza kubeba picha, kutuma ujumbe na kadhalika jamii inalaumiwa kutowakanya wanafunzi kufika katika klabu za pombe kutembelea maeneo ya starehe au kufumbia macho utoto wa wanafunzi katika hali hiyo, inaonekana kwamba upungufu wa maadili kwa wanafunzi unaathiri maendeleo yake kimasomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanafunzi mwenye msingi bora wa maadili huwa na maendeleo kimasomo na anafanikiwa kuvuka ngazi moja ya elimu kwenda nyingine. Maendeleo yake huwa chanya, mwanafunzi asiye na maadili huvutwa nyuma na matendo. Napenda kutoa wito kwa jamii kuwa ni jukumu la msingi la jamii kushiriki katika malezi ya vijana wetu na hasa wanafunzi katika ngazi zote za elimu. Jamii irudi katika utaratibu wa zamani wa kushiriki malezi ya watoto hata kama wao si wazazi wa kuwazaa jamii inaposhiriki kumlea mtoto inamjengea uzalendo na heshima ya juu ya uwajibikaji kwa jamii husika. Inamsaidia mtoto kuwa na akili ya utulivu katika kuzingatia elimu, pia kuwa mtiifu na anayejipokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia jamii isijitenge na kukaa mbali katika kushiriki katika malezi. Malezi haya yanaweza kufanyika kwa njia na mbinu nyingi tofauti tofauti, jamii ikatae watoto kuonekana barabarani wakati wa saa za shule na wakati hakuna likizo. Pia jamii itoe taarifa shuleni inapoona watoto wanazunguka zunguka mitaani au mjini bila sababu maalum.

Aidha, jamii ipige kelele kwa Serikali kutunga na kusimamia sheria zinazohimiza wanafunzi kutokuwepo, kutokufanya au kuangalia sinema, mitandao na mambo yote yanayohatarisha mmomonyoko wa maadili ikiwemo miziki, picha za ngono na mavazi yasiyofaa. Halikadhalika ziwepo kamati ndogo ndogo zinazofuatilia maendeleo na maadili ya watoto kila mara katika ngazi ya kata na kijiji ambako jamii husika huwafahamu hawa watoto/vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawezaje kushirikiana kukabili kushuka kwa maadili kwa nidhamu ya wanafunzi? Suala la kushuka kwa nidhamu ni suala ambalo linakuwa kwa kasi nchini Tanzania. Suala hili linachangiwa na mambo mengi sana. Hii husababisha kuanguka kwa nidhamu na kushuka kwa kiwango

cha taaluma. Kushuka huku kwa nidhamu kunasababishwa na mambo yafuatayo:-

Kwanza, kukua kwa utandawazi kwa kasi. Suala hili huleta muingiliano mkubwa wa utamaduni wa nchi mbalimbali. Vijana wengi huwa katika kipindi cha mpito ambacho ni rahisi kwao kuiga kila wanaloliona hasa yanayotoka kwa watu wenye mwito katika jamii kama vile wasanii.

Pili, kukua kwa mawasiliano ya simu. Pamoja na umuhimu mkubwa wa mawasiliano ya simu, kumekuwa na matumizi mabaya sana ya simu kwa vijana kwani wanazitumia kwa mambo ambayo si mazuri kwa jamii kuongezeka kwa familia za mzazi mmoja kwa kiasi hali hii husababisha kupungua au hata kukosa kabisa malezi ya kutosha hivyo kumfanya mtoto kuwa na uhuru kuamua lolote lile.

Suala la walimu kukosa mafunzo ya kutosha, hili linahusu Wizara husika moja kwa moja. Ni muhimu walimu wapewe mafunzo mara kwa mara ya saikolojia ili uwezo zaidi wa kutambua mabadiliko ya tabia kwa wanafunzi na kuchukua hatua haraka kabla mtoto hajaharibika kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mila na desturi potofu, suala hili pia linachangia kushuka kwa nidhamu ya wanafunzi pale inapotumika vibaya kwa mfano kuna mila za jando na unyago kwa makabila mengi ya Kusini ambayo pamoja na mambo mazuri mengi yanayofundishwa pia yapo ambayo hayafai kwani yanapotosha hususani suala la mahusiano ya mwanaume na mwanamke. Hivyo basi suala la kushuka kwa maadili ni suala mtambuka kwani halisababishwi na mtu wala taasisi moja bali ni suala linalogusa jamii kwa upana wake. Hivyo kuliondoa kwake linahitaji pia ushirikiano wa jamii nzima pamoja na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana nizungumzie kuhusu Jimboni kwangu Kibaha Vijijini. Jimbo la Kibaha Vijijini tumekuwa tunakabiliwa na matatizo mengi katika sekta nzima ya elimu, shule nyingi zimekuwa katika viwango vya chini sana hivyo kupelekea hata elimu yetu kushuka, tumekuwa na changamoto za madawati, matundu ya vyoo ni machache katika kila shule zetu, majengo ya madarasa hayatoshelezi na hata yaliyoanza kujengwa kwa nguvu za wananchi bado Serikali imekuwa na uungwaji mkono hafifu sana katika jitihada za wananchi. Kwa sasa tuna nyumba za walimu takribani 184 (137 kwa shule za msingi na 47 kwa shule za sekondari). Hivyo kutokana na takwimu hizi tuna upungufu wa nyumba za walimu 542 (325 kwa shule za msingi na 217 kwa shule za sekondari) sawa na 75%.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Kwala tunahitaji nyumba moja ambayo itagharimu kiasi cha shilingi 21,000,000/= utekelezaji wake bado fedha hazijapatikana. *Ruvu Station* pia tunahitaji kiasi cha shilingi 26,000,000/= ili

kukamilisha ujenzi wa nyumba hiyo, ila utekelezji wake bado kwani fedha hazijapatikana. Vivyo hivyo Dossa Azizi tunahitaji kiasi cha shilingi 24,000,000/= ili kukamilisha ujenzi huo, ila utekelezaji wake bado kwani fedha haijapatikana nyumba za *Ruvu Station* na Dossa Azizi zikikamilika zitafanya kwa upande wa shule za sekondari kuwa na nyumba 49.

Suala la shule zetu kukosa madawati limekuwa ni kero ya siku nyingi sana, watoto wetu wamekuwa wakikaa chini kipindi cha masomo na hivyo kuondoa hamasa kwa wazazi pamoja na watoto wenyewe kwenda shule. Nimekuwa nafanya jitihada nyingi sana katika kuchangia sekta hii ya elimu kwa nguvu zangu binafsi, kwa kuchangia madawati, mabati kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na wakati mwingine kutafuta wadhamini mbalimbali ili tu kufanya shule zetu ziwe katika kiwango kizuri lakini kutokana na jitihada zote hizo bado tunahitaji jitihada za Serikali katika jambo hili ili kuniunga mkono katika jambo hili.

Vilevile kumekuwa na tatizo la muda mrefu sana la kukosa madarasa ya awali katika Jimbo langu, imefika mahali watoto hawa wa darasa la awali wamekuwa wakitumia madarasa hayo hayo yanayotumiwa na wanafunzi wa shule za msingi na wakati mwingine wamekuwa wakichanganywa pamoja, hilo si jambo la kufikirika katika dunia ya leo. Madarasa ya awali ni muhimu sana kwani humuandaa mtoto kabla ya kujiunga na darasa la kwanza, bila madarasa ya awali watoto wetu hawatakuwa katika hali nzuri kimasomo pindi watakapojiunga na darasa la kwanza, Jimbo la Kibaha Vijiji tumefanya jitihada kubwa sana kwa kuanzisha madarasa haya ya awali lakini tumekuwa tukikosa walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi naiomba Serikali kuweka utaratibu wa kujenga madarasa ya awali ili kuwaandaa watoto wetu. Vilevile tumekuwa tuna kero ya upungufu wa walimu katika shule zetu, walimu wamekuwa wachache kiasi ambacho kuna baadhi ya masomo yamekuwa hayafundishwi kutokana na kukosekana kwa walimu wa masomo hayo mfano kama walimu wa somo la sayansi waliokuwepo ni 66 wakati mahitaji ni 93 kwa hiyo kuna ukosefu wa walimu 27 katika fani hiyo muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu. Vivyo hivyo hata upande wa walimu wa shule za awali tunao wachache sana na kufanya baadhi ya maeneo watoto hawa kukosa kabisa kujiunga kwa darasa la awali na kwenda moja kwa moja kujiunga na darasa la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali sasa kutuletea walimu katika Jimbo letu na kutatua kero hizi za muda mrefu zinazotukabili.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu wetu wamekuwa wakiishi katika mazingira magumu sana kiasi ambacho hujutia hata ni kwa nini walisomea fani hizo, walimu wamekuwa wakiidai Serikali fedha nyingi sana, madai hayo si ya

leo au ya jana, ni ya muda mrefu lakini mpaka leo hatujui hatima ya walimu wetu watalipwa lini haki zao. Ugumu wa maisha, madeni sugu wanayoidai Serikali ndiyo hupelekea pia na wao kukata tamaa na kutokufanya kazi kwa kujituma na hivyo kusababisha watoto wetu kufeli kila mwaka kiwango cha elimu yetu kushuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu ni watu muhimu sana katika Taifa lolote lile. Sasa mimi najiuliza kwa nini hapa nchini kwetu hatuwajali walimu wetu? Vilevile kuna suala la walimu pindi wanapopata ajira ya kwanza kulazimishwa kujiunga na hivi vyama vyao na pindi wanapojiunga hutakiwa kulipia ada ilihali hali zao ni duni na hivyo vyama vya walimu kwa upande mwingine vimekuwa vikishindwa kuwatetea walimu na maslahi yao, naweza kusema kuwa hakuna faida yoyote ya vyama vya walimu kama vinashindwa kutetea haki za wanachama wao. Naiomba Wizara kuweka mikakati ya kulisimamia hili ili walimu hawa wawe huru na isiwe lazima kujiunga na vyama hivi ambavyo havina utetezi wala maslahi ya aina yoyote kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala zima la vyuo vya ufundi kuanzishwa ni jambo la msingi sana kuviboresha na kuviongeza pia, ni jambo linalotakiwa kupewa kipaumbele, vyuo hivi vimekuwa vikisaidia sana kuwapa vijana wetu elimu mbalimbali na hivyo kupelekea vijana hawa kujiajiri wenyewe, nilikuwa naiomba Serikali kuongeza vyuo hivi ili kuwapa mwanya vijana wetu kujiunga navyo, waangalie pia tatizo la baadhi ya vijana wetu wengine kuwa wanaishi maeneo ya mbali sana hivyo huwawia vigumu kujiunga katika vyuo hivi kwa kuwa hawana uwezo wa kumudu gharama za malazi pindi wawapo katika masomo, vilevile uboreshaji ufanyike katika vyuo hivi kwa kuongeza walimu na vifaa vya kujifunza kwa vitendo ili kuwajenga vijana hawa pindi wamalizapo elimu zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya Chuo Kikuu ni muhimu sana kwa Taifa letu, napenda kuipongeza Serikali kwa jitihada ilizozifanya kwa kuongeza vyuo vya elimu ya juu na hivyo kupelekea idadi ya wahitimu kuongezeka ingawa kuna changamoto ya ajira, ila bado tunahitaji kuongeza vyuo hivi na ikiwezekana kila Mkoa ukawa japo una Chuo Kikuu kimoja ili tu kutoa nafasi za vijana wetu kujiunga na elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na changamoto mbalimbali katika sekta nzima ya elimu ya juu na changamoto hizi ni wanafunzi kutokujengewa uwezo kitaaluma pindi wamalizapo elimu hizo kwani tumejionea vijana wengi wamekuwa wanamaliza elimu zao katika vyuo hivyo ila wamekuwa wanakosa kazi kwa kufeli kwenye usaili yaani *interview* wameonekana kuwa na uwezo mdogo sana wa kuweza kujielezea, hivyo kuna sababu ya kuwajenga vijana wetu kitaaluma na kujiamini.

Pia kumekuwa na malalamiko mbalimbali katika Bodi ya Mkopo. Wananchi wenye sifa wamekuwa wakikosa nafasi hizi na wale wasiokuwa na sifa ndiyo wamekuwa wakipata nafasi hizo na hivyo kupoteza dhana nzima ya mikopo hii. Naiomba Wizara kufanya marekebisho katika kero hii ili kutoa usawa katika upatikanaji wa mikopo hiyo. Hata hivyo naishauri Serikali kupitisha sheria ambayo itawaruhusu wale wanafunzi ambao wapo mwaka wa mwisho na hawajamalizia ada zao na wanahitaji kufanya mitihani yao basi waruhusiwe kufanya mitihani hiyo ya mwisho bila kuwa na pingamizi lolote kwa chuo husika ila tu wazuie vyeti vyao kama mwanafunzi huyo atakuwa hajalipa deni hilo, lakini sio utaratibu unaotumika hivi sasa na vyuo vingi kuwazuia wanafunzi kufanya mitihani yao ya mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie chanzo kinachopelekea kuporomoka kwa nidhamu ya wanafunzi. Nidhamu ni jumla ya mambo anayofanya mtu katika mazingira mbalimbali ikiwa ni pamoja na uvaaji wa nguo, utumiaji wa lugha, salam, utanashati pamoja na tabia. Nidhamu bora ni yale matendo yote mema/mazuri anayofanya mtu katika mazingira yake kama kuvaa vizuri, lugha nzuri na njema ya kupenda kusalimia watu wakubwa au wadogo, wazazi na walimu, usafi na kutii sheria za shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, utovu wa nidhamu ni jumla ya mambo yote mabaya anayofanya mtu katika mazingira mbalimbali kama vile lugha chafu, uvaaji mbaya wa nguo, kuiba, utumiaji wa dawa za kulevya ikiwemo bangi na sigara, hali kadhalika kudharau wengine, kutosalimia watu na kuongea na simu darasani pamoja na kuvunja sheria za shule. Vyanzo vya utovu wa nidhamu shuleni, malezi mabaya kwa baadhi ya wazazi au walezi, baadhi ya wazazi hasa wenye vipato hupenda kuwaridhisha watoto wao kwa kuwapa kila kitu ambacho mtoto anahitaji, kwa mfano simu, fedha nyingi na kadhalika.

Kuhusu utandawazi baadhi ya watoto wetu hasa waishio mijini hupenda kuangalia picha zisizofaa katika tovuti pamoja na mabanda ya video, hii huwaharibu kisaikolojia na kimaadili.

Suala la utumiaji wa dawa za kulevya, baadhi ya watoto wetu hupenda kutumia dawa za kulevya zikiwemo bangi na sigara bila ya kutambua madhara yake, hatimaye watoto hawa huanza kuchanganyikiwa akili na kuanza kuwa na tabia mbaya ya kutukana hovyo na ugomvi pasipo sababu, kuiga mambo ya mataifa ya Magharibi, kwa kawaida mtoto hujifunza kutokana na vitu anavyoviona, kwa sababu ya sayansi na teknolojia hivi sasa, mtoto hufanya mambo kwa vile ameona huko Ulaya au Marekani, kwa mfano wavulana kuvaa "Kata K" na wasichana "vimini" wakidai wanakwenda na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tamaa na vishawishi, baadhi ya watoto wetu hasa wa kike hupenda kushindana kimavazi na kujiona huyu mrembo zaidi

kupita yule. Kutamani kula vizuri chipsi na kuku na kudandia *lift* ambazo matokeo yake ni kupata mimba zisizotarajiwa. Aidha, baadhi ya watoto wa kike ni rahisi kushawishiwa na kurubuniwa na wanaume. Nini kifanyike ili kuondokana na tatizo hili? Vikao vya mara kwa mara vya *school baraza* vitasaidia kutambua matatizo waliyonayo wanafunzi na kuwapa zawadi wanafunzi wenye nidhamu bora. Hii ingesaidia kuchochea wanafunzi wengine kuwa na nidhamu nzuri hapo shuleni. Elimu ya malezi itolewe kwa wazazi na wanafunzi juu ya madhara ya utumiaji wa dawa za kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kuwe kunafanyika *school baraza* mara kwa mara sambamba na utoaji wa zawadi kwa wanafunzi wenye nidhamu bora. Pia kutungwe sheria ndogo ndogo zitakazodhibiti watoto kuangalia picha za ngono kwenye tovuti na mabanda ya video na kuacha kuiga tamaduni za nje kiholela. Hatuwezi kuboresha elimu bila kuboresha nidhamu, kwa sababu mwanafunzi akiwa hana nidhamu shuleni basi mitaani na nyumbani ndiyo zaidi. Hali hii ni kweli ipo na imekuwa kero kubwa kwa walimu, inafikia mwalimu anakosa amani. Pia baadhi ya walimu kutaniana na kuwatania wanafunzi inachangia mwanafunzi kutokuwa na nidhamu.

Pia mawasiliano duni kati ya mzazi au mlezi na walimu ili kufuatilia mwanafunzi huyo shuleni huchangia kuporomoka kwa maadili, baadhi ya wazazi wamefikia hatua ya kugombana na mwalimu wanapowakemea wanafunzi wakati makosa ni ya wanafunzi. Wanafunzi wengi wamejiingiza katika makundi mabaya, kuvuta bangi na dawa za kulevya. Hivyo vyote vinachangia utovu wa nidhamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na faida za utandawazi ikiwa ni pamoja dunia kuwa kama kijiji kumekuwa na kuiga utamaduni wa nje kama Ulaya na Marekani. Hii huchangia watoto wetu kusahau mila na desturi za nyumbani. Walimu kupuuzia vipindi darasani na kutofundisha vingine kabisa huwafanya wanafunzi kupata muda mwingi kucheza nje ya eneo la shule na pia kutosikiliza wakubwa na walimu.

Uondoaji wa adhabu ya viboko mashuleni pia umesababisha kupungua kwa nidhamu kwa sababu mwanafunzi akifanya kosa lolote anajua hataadhibiwa kabisa. Naiomba Serikali kuyazingatia haya yote niliyoyasema hapa ili kuboresha sekta nzima ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Sasa tunaenda upande wa Serikali, tunaanza na Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Ghasia, Waziri wa Nchi, TAMISEMI, ili tuwe tumemaliza kwa upande huo dakika kumi kumi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimwia Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Naibu Waziri wa Elimu pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Elimu kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea nayo, na leo wametuletea bajeti hapa ambayo pia inaonesha mwelekeo wa namna ya kuboresha elimu.

Mheshimwia Naibu Spika, mimi nataka niwatoe mashaka Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote, kwamba pamoja na changamoto zilizopo kwenye sekta ye elimu tunaendelea kufanya kazi ya kupokea pia na ushauri wenu ili pia tuweze kuboresha kiwango hiki cha elimu kwa ubora wake, lakini pia na matokeo yake ya ufaulu ambao pia tunautarajia uweze kupatikana. Bajeti ni hii na tunawaomba sana mwishoni pale mtupitishie hii bajeti ili tuweze kufanya kazi ambayo tunaiomba kwenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ugatuaji limezungumzwa, na tumelieleza mara nyingi, mimi nimeishatoa maelezo, na Mheshimiwa Waziri wa Elimu ameeleza. Nataka niwape matumaini tu kwamba jambo hili limeandaliwa kwa lengo la kuhudumia kwa ukaribu zaidi sekta ya elimu na watendaji wake kwenye sekta ya elimu na kazi hiyo tunaendelea nayo, na yale yote ambayo yanapaswa kushughulikiwa kwenye ngazi za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kwa mfumo huu ni rahisi zaidi kuliko vinginevyo. Lakini jambo hili bado linaendelea na tunataka tuwahakikishie kwamba huduma hizi za watendaji wetu wa elimu zitaendelea kufanywa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mheshimwia Naibu Spika, kwa maana hii sasa lilijitokeza swali hapa, nani mwajiri wa walimu hawa? Kwa sasa mwajiri wa walimu ni Katibu Mkuu TAMISEMI, ndiko wanawajibika kwake Katibu Mkuu wa TAMISEMII. Kwa hiyo walimu wote pamoja na watendaji wengine, watumishi wote wa Halmashauri, mwajiri wao ni Katibu Mkuu TAMISEMI, na Katibu Mkuu TAMISEMNI amekasimu madaraka kwa Katibu Tawala wa Mkoa, lakini pia kule kwenye ngazi ya Halmashauri Mkurugenzi ndiye anayeratibu shughuli za kila siku na matatizo yao kwenye ngazi ya Halmashauri.

Wakati tunapopokea michango, Mheshimiwa Susan alitaka kujua kwa nini elimu Serikalini imedorora kuliko ile ya *private*. Nataka nimhakikishie kwamba huwezi kulinganisha *private school* na *Government school* kwa *performance* yake, kwa sababu *private* ni mtu mmoja ametenga fedha zake nyingi, kajenga madarasa yake, ameamua kuihudumia shule moja tu, tena anachukua wanafunzi kwa kuchuja na wakishindwa katikati hapo wanafukuzwa. Lakini Serikali ni wajibu wetu kuwapokea watoto wote wa Kitanzania bila kujali kama mototo huyo ni *fast learner* au *slow learner.* Ni jukumu letu sisi kumhakikishia kwamba anapata elimu na kwamba anakwenda anapata ufaulu, anapata mabadiliko ili kule mwishoni aweze kuwa na ufalu mzuri.

Kwa hiyo ukilinganisha shule binafsi na za Serikali, huwezi kupata mfanano huo kwa sababu hizo. Lakini ninachotaka kuwahakikishia ni kwamba tunaendelea kufanya jitihada za kuhakikisha kwamba watoto wetu wanaosoma kwenye shule zetu, wanakuwa na ufaulu mzuri na kweli wanafikia viwango ambavyo sisi tunavitarajia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo kubwa ambalo tunalifanya sasa ni kukabiiliana na changamoto. Hii mijadala ambayo imejitokeza hapa na ushauri ambao mmetupatia Waheshimiwa Wabunge, jukumu letu ni kuchukua na kufanyia kazi, nataka tuwahakikishie mapendekeezo yenu yote tutayachukua. Wizara ya Elimu ipo na inafanya kazi sambamba na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, wote kwa pamoja tutashughulikia elimu na tunataka tuwahakikshie kwamba tutapata mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka kusema kwamba tunazo changamoto kubwa sana kwa vijana wetu. Mmonyoko wa maadili, sijausikia hapa ukizungumzwa, ni jambo ambalo lazima tulizungumze. Suala la mmonyoko wa maadili ambalo pia linapelekea kuwa na matokeo mabaya kwenye shule zetu, hili lazima tulizungumze. Lakini pia uwingi wa watoto shuleni nao hatuuzungumzi, lakini ni moja kati ya mambo ambayo tunayoyafanyia kazi. Kwa hiyo changamoto hizi ni muhimu, na lazima sasa tujipange wote kwa pamoja, Serikali, jamii na watoto wenyewe wawe na uelewa kwamba sasa wanawajibika kwenda shuleni na kuingia darasani na kusoma na kupata matokeo mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo sisi Serikali, Wizara ya Elimu pamoja na TAMISEMI, tunachofanya sasa ni kutekeleza wajibu wetu. Katika kutekeleza wajibu wetu tunajua pamoja na changamoto ambayo mmeileza ya walimu wetu na stahili zao, nataka niwaondolee mashaka, suala la madeni ya walimu, ni kweli tunayo madeni. Tulipokuwa tumetamka madeni ya walimu shilingi bilioni 61, madeni haya siyo halisia. Lakini madeni yapo, tunachofanya sasa tunahakiki na kila tunapomaliza kuhakiki tunalipa. Tumeishanza kulipa kutoka mwezi Agosti, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeishawaambia pia hata nilipokuwa najibu swali katika majibu yangu ya msingi kwamba kufikia mwezi Februari, 2014, tumeishalipa shilingi bilioni 19 na tumeishalipa Mwezi Machi na Aprili, sikuja na takwimu kwa sababu ilikuwa ni lazima tuwasiliane na Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili la mishahara na malimbikizo ambayo sasa yanaendelea kulipwa tutaendelea kulipa na mkakati wetu ni kuhakikisha kwamba tunamaliza madeni yote katika mwaka huu wa fedha wa Serikali. Kwa hiyo mpaka Juni 30, tunaamini kama zoezi la uhakiki litakuwa limekamilika,

madeni haya ya upande wa mishahara ambayo yanalipwa moja kwa moja na Hazina yatakuwa yameishalipwa kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini yako madeni ambayo yanalipwa ndani ya Halmashauri kupitia OC zetu. Kwa mfano, likizo uhamisho wa ndani, matibabu, masomo. Meneo haya tunaendelea kuyalipa kupitia ruzuku ambayo tunaipeleka kwenye Halmashauri, na tumejitahidi kupunguza madeni haya kwa kiasi kikubwa na tutaendelea kufanya hivyo ili tusiwe na madeni katika sekta ya elimu na walimu hawa. Tunataka walimu wafanye kazi yao wakiwa wameishalipwa stahili zao za msingi ili wafanye kazi ambayo sisi tunaitarajia na matokeo tuweze kuyapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ni lazima nieleze pia; suala la mazingira maagumu ambalo limejitokeza sana kwenye mjadala huu. Ni kweli, lakini sisi tulishatafuta ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema asubuhi pia kwenye swali la msingi la Lolesia Bukwimba, kwamba sisi hatukutenga fedha kama ambavyo Mbunge wa Nkenge alivyosema kwamba Kenya wanatoa fedha, wengine wanalipa. Sisi tumeamua kuingia kwa kujenga nyumba. Ndiyo maana tulitenga mradi wa kujenga nyumba 1,200 na tumeisha kamilisha nyumba 264, sasa tunakuja nyumba 528 na tutaendelea na nyumba 408 ili kuhakikisha kwamba tunajenga nyumba kwenye maeneo ya walimu ili mwalimu anapokwenda kufanya kazi, apate nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mpango ule ambao tumetenga shilingi bilioni 20 na tumeanza kusambaza kwenye Halmashauri 40, na kila Halmashauri tumeitengea shilingi milioni 500, kazi hizo zinaendela kwenye Halmashauri zenu kwa sasa. Wakishakamilisha, tunapeleka shilingi bilioni 20 zingine kwa ajili ya kujenga nyumba hizo kwa awamu, tunataka tuimarishe kwenye eneo hili. Kwa hiyo walimu ambao tunao wawe na matumaini kwamba mkakati huu tulionao utasaidia kupunguza ugumu wa mazingira haya ambayo walimu wetu wanaishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulijitokeza suala la ajira mpya, lilikuwa na maeneo mengi. Kwanza mgawanyo: Mgawanyo huu sisi tuliupata kutoka kwenye Halmashauri baada ya kufanya sensa. Kila Halmashauri ilileta mahitaji yake, na sisi tumepeleka. Tulipoajiri walimu kwa iddi ile, tumewapeleka kule ili waweze kupunguza matatizo makubwa. Natambua yapo maeneo bado yana upungufu mkubwa wa walimu. Lakini nataka niwahakikishie Watanzania, kwamba tutaendelea kuwaajiri. Wakati natamka hili, tunao vijana ambao bado hawajaajiriwa, na hii ni kwa sababu ya kibali cha awali tulichokipata cha walimu 36,338, ambacho tayari, na wale wote tumewaorodhesha, tumeomba

kibali. Wakati wowote tukipata kibali, tutaendelea na ajira hiyo ya walimu, kwa sababu tunahitaji walimu wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mishahara na posho zao: Suala la posho ya siku saba walishalipwa maeneo yote. Mishahara wengine hawakupata mshahara mwezi Aprili kwa sababu ya taratibu. Taratibu ni kwamba mwalimu lazima aje na vyeti vyote halisia. Hana vyeti halisi, siyo rahisli kumlipa mshahara mpaka tuhakikishe kwamba aliyekuja ndiye mwenyewe na cheti alicholeta ndicho chenyewe, na wengine walichelewa ku-*report*. Kwa hiyo mwezi Mei watalipwa mshahara wao wa Mei pamoja na Aprili, na tayari kule Utumishi wameishaingiza *Data Base,* iko kamili na kwa hiyo walimu wawe na matumaini kwamba mwezi Mei watalipwa mshahara wao. *(Makofi)*

Mheshmiwa Naibu Spika, miundombinu tunaendelea nayo. Suala la nyumba, nimeeleza kwenye mkakati wetu wa nyumba. Suala la maabara tumeeleza mikakati ya nyumba 1,400. Moja kati ya *package* iliyoko kwenye nyumba 1,200 ni maabara. Lakini agizo la Mheshimiwa Rais kwa kila Mkoa, wanaendelea kila Wilaya kuhakikisha kwamba wanajenga maabara ili tuwe na maabara. Sisi Wizara tunapeleka fedha za vifaa vya maabara. Kwa hiyo tuna uhakika kwamba maabara zote za sayansi zitafanya kazi yake vizuri kwa muda mfupi na vifaa vitakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la vitabu na madawati limezungumzwa. Mheshimiwa Wenje alitaka kujua, fedha ya rada imefikia hatua gani. Nataka kumhakikishia kwamba zabuni inaendelea na utengenezaji unaendelea. Awamu ya kwanza tutapata madawati 93,988 na awamu ya pili tumeishatangaza zabuni kwa ajili ya kupata madawati mengine tena. Tuna uhakika kila Halmashauri awamu ya kwanza itapata madawati yasiyopugua 600 na awamu ya pili tuna uhakikia kila Halmashauri itapata madawati yasiyopungua 400. Kwa hiyo, zaidi ya madawati 1,000 kupitia mpango ule tutayapata. Lakini bado niendelee kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge ambao mmejitokeza kuunga mkono jambo hili la kupunguza tatizo la madawati kwenye maeneo yenu. Waheshimwia Wabunge ni wajibu wetu kuchangia pale ambapo tunaona kwamba tunahitaji pia kuboresha sekta ya elimu wote kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la elimu maalum limezungumzwa na limelalamikiwa sana. Ofisi ya Waziri Mkuu inalifanyia kazi eneo hili. Kwanza tulitenga shilingi bilioni mbili ambazo tumenunua vifaa mbalimbali, tumeishapeleka fedha kwenye Halmasharui zetu zaidi ya shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kuimarisha shule zile pamoja na…

**NAIBU SPIKA:** Asante sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Asante sana, ninakushuru. Majibu yako yametusaidia sana, kutupa mwanga katika maeneo uliyoyapitia. Sasa nimuombe Mheshimiwa Waziri, Tawala za Mikoa na Serkikali za Mitaa, Mheshimiwa Hawa Ghasia, dakika kumi!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Lakini kabla ya kuchangia, napenda kuchukua fursa hii ya pekee kumpongeza sana Mheshimiwa Mwijage na Mheshimiwa Marombwa kwa kushirikiana na kuhamasisha wananchi wao katika kuboresha elimu katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimwia Naibu Spika, ni aibu Mheshimiwa Mbunge unasimama, unalalama, unabeza kwamba kuna watoto wanakaa chini na mwingine anasema siyo kazi ya Mbunge kuhakikisha kwamba kuna kuwa na madawati. Siyo lazima ununue, kuwahamasisha wanachi. Kwa sababu wale watoto ni wetu, tumewazaa kwa raha zetu, ni lazima tushirikiane na Serikali kuhakikisha kwamba watoto wale wanapata elimu nzuri. *(Makofi)*

Hata huko tunakosema wameendelea, ili Serikali iweze kuwahudumia vizuri, watoto wanaozaliwa, wameweka *limit* ya kuzaa. Ukienda China, mtoto mmoja. Sisi hatukuweka kiwango, kila mtu anazaa anavyotaka. Sasa hao watoto tunowazaa hatuwezi wote kuiziria Serikali. Lazima wazazi na Serikali tushirikiane kuhakikisha elimu yetu inakuwa bora. *(Makofi)*

Tunaenda katika Shule za *private,* hizo tunazozisifia, tunatoa ada elimu ya msingi zaidi ya shilingi milioni 2/milioni 3, hatulalami. Tunachangia madawati, tunachangia ujenzi wa Shule. Unakuja katika shule za Serikali unaambiwa changia dawati, nongwa. Unaambiwa changia labda ada mlinzi, kelele. Halafu tunalinganisha elimu hiyo inayotoka shule za *private* na shule za Serikali, wakati shule za watu binafsi tunazichangia kwa ada kubwa, kwa michango mikubwa.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa! Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Na elimu ya Serikali hatutaki kuchangia.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Hatutaki kuchangia. Mheshimiswa Machali kaa chini, hujaruhusiwa kuongea!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Machali, nakuomba sana, kwa sababu tuna *votes* nyingi hapa, amalize dakika zake kumi. Tafadhali Mheshimiwa Machali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMSEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie tena ni aibu. Ni aibu kwa Mbunge kuja ndani kulalamikia wanafunzi wanakaa chini. Sisi kama Wabunge kazi yetu ni kuwahamasisha wananchi wetu, maeneo mengine tunakaa kuna mbao wazazi wachangie. Lakini sisi kama Wabunge tuna uwezo wa kwenda katika mashirika mbalimbali kwenda kuomba kwa niaba ya wananchi wetu. Na tunayo Mifuko yetu ya Jimbo ambayo pia tunaweza tukachangia katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kule kwangu nimefanya harambee, nimejenga sekodnari yenye mabweni, ina kila kitu pmoja na gari ya shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niseme kwamba Serikali ya Chama Cha Mapinduzi ni Serikali sikivu, ni sikivu sana. Tumeingia hapa Serikali ya awamu ya nne, kulikuwa na lugha inasemwa kwamba walimu wamerundikana katika cheo kimoja, kuna mrundikano. Serikali ya awamu ya nne, imelishughulikia suala la mrundikano sasa hivi hilo neno mrundikano ni hadithi.

Mheshishimiwa Naibu Spika, lakini siyo hivyo tu, walimu walikuwa wanaajiriwa wanakaa zaidi ya miezi sita hawajapata mishahara. Tukaangalia tatizo ni nini, tukaona ni mfumo wetu. Tukaboresha, tukaeweka *Low Zone Version* 9. Tukauchukua ule mfumo tumepeleka kila Halmashauri. Mwalimu akiripoti akiwa na kila kitu, akiwa na cheti na viambatanisho vinavyotakiwa, ndani ya dakika mbili anaingizwa kwenye Halmashauri yake na taarifa ile inaenda Utumishi, na ndiyo maana sasa hivi tunazungumzia mshahara wa mwezi Aprili, na ikifika mwezi Mei, ndani ya miezi miwili hakuna mwalimu atakayekuwa anapiga kelele kwamba hajapata mshahara. Huo ni usikivu wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi, imekuwa ikiboresha hiyo miundo, imekuwa ikishughulikia masuala ya walimu. *(Makofi)*

Mheshimkwa Naibu Spika, suala la walimu kuchelewa wale walio-*report* kwa muda wakiwa na viambatisho vyote wote walipata mishahara. Waliochelewa ndiyo hao ambao tuna uhakika, ukiacha walimu ambao bado mpaka sasa hivi, Tabora kuna walimu 10 ambao bado hawajakabidhi vyeti, Ulanga wako wawili. Kwa hiyo siyo ajabu na kwenye Halmashauri zenu mwezi huu wapo watakakosa mishahara kwa sababu hawana vyeti. Kwa sababu ule

mfumo ukishaweka huyu ni Hawa Ghasia kamaliza kozi ya ualimu, cheti chake daraja la III(A) lazima uweke na cheti u-*attach* pale, usipo-*attach*, mshahara hupati. Kwa hiyo wale ambao mpaka sasa hivi hawajakabidhi vyeti *original* kule bado watakosa mishahara.

Mheshimiswa Naibu Spika, pia katika suala hilo la usikivu wa Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, tulikuta walimu wote wa shule za sekondari na msingi wanawajibika kwa Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, na kipindi kile Mheshimiwa
Mama Margaret Sitta alikuwa Waziri wa Elimu, lakini alikuwa hajui wana walimu wangapi wa msingi, wana walimu wangapi wa sekondari. Ukiuliza asubuhi unatajiwa idadi hii, ukiuliza jioni unatajiwa idadi hii. Tulifanya uhakiki, na tukakuta watumishi hewa, na katika kuhakikisha kwamba tunaondokana na tatizo hilo, tukahakikisha kwamba tunawaotoa wale walimu, tunawapeleka kwenye Halmashauri ili tuweze kuwahudumia. Na katika kufanya hivyo walimu wa sekondari sasa hivi wanapanda vyeo kwa wakati ukilinganisha na kabla ya hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba twende katika majimbo yenu kawaulizeni walimu, hivi mlipokuwa kwa Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na sasa hivi mlivyo Halmashauri hali wapi ni nafuu? Watawaambia sasa hivi ni nafuu, kuliko ilivyokuwa zamani. Mfano hata hao walimu waliokosa mishahara, amekosa tu mshahara anakimbilia kwa Mkurugenzi, na wengi wa Wakurugenzi wamewakopesha mishahara ya kuwawezesha kuishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi mwenyewe wiki iliyopita wakati ninatoka Dar es Salaam, nilipitia Gairo, nikakuta walimu wa sekondari wale ambao hawajapata mshahara na Mkurugenzi akasema kesho nitawalipa tutatafuta kwenye vyanzo vyetu vya ndani tutawalipa, na Wakurugenzi wengi wamefanya hivyo. Lakini wangekuwa chini ya Wizara ya Elimu, mwalimu yupo Nanyumbu, yuko Misenyi, amekosa mshahara hivi angekimbilia kwa nani? Unakimbilia kwa Mkuu wa Wilaya? Unakimbilia kwa Mkuu wa Mkoa, ana uwezo wa kukuhudumia? Lakini sasa hivi wakiwa na matatizo wana mahali karibu wanakimbilia na wanaweza kutatuliwa matatizo yao.

Kwa hiyo, suala lingine niwaombe Waheshimiwa Wabunge kwamba tukisimama humu ndani tunawakatisha tamaa walimu, mishahara midogo, mnawanyanyasa. Jamani Serikali ya Chama Cha Mapinduzi inawahudumia walimu, madeni yanalipwa; na sasa hivi tumechelewa kulipa madeni ya walimu kwa sababu uchakachuaji ni mkubwa, madeni feki ni mengi. Tumefanya uhakiki tumeshirikisha mpaka Chama Cha Walimu, tumewaambia haiwezekani mwalimu mmoja anadai shilingi milioni 500; na tumewafuata mpaka mwalimu mmojammoja wanaulizwa wanasema mimi sina deni, mimi deni nimebambikiwa. Baadhi ya walimu wanalipwa, wanadai tena wanalipwa, wanadai tena, walimu wengine hawana hata *cheque number,* siyo walimu.

Tunasema safari hii wale walimu ambao wamedai madai feki, tutawachukulia hatua stahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, narejea tena, Serikali ya Chama Cha Mapinduzi ni sikivu. Narejea tena, ni aibu Mbunge kuona sifa hapa kulalama kwamba wanafunzi wanakaa chini. Lazima tushirikiane tuwahamasishe wananchi. Baadhi yenu humu ndani tunashawishi wananchi wasichangie maendeleo yao. Sasa nataka kusema tunawacheleweshwa na wananchi wajue kwamba wanacheleweshwa, hakuna nchi isiyochangia, hata hao wahisani wanaotuchangia wananchi wao wanachangia maendeleo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hawa Ghasia.

**TAARIFA**

**MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

**NAIBU SPIKA:** Waziri Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mheshimiwa Machali unasemaje?

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Nilisimama mwanzoni nilitaka kumpa taarifa mzungumzaji aliyemaliza muda wake kwamba kwa mujibu wa Katiba yetu Ibara ya 63 si wajibu wa Mbunge kukusanya kodi kwa wananchi ili kusudi kupeleka maendeleo kwa watu wake. *(Makofi)*

Kwa hiyo, anaposema kwamba Mbunge…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Machali, ni vizuri sana sisi Wabunge tukajielekeza kwenye ukweli na ukweli mtupu. Hakuna aliyesema hapa kwamba ni wajibu wa Mbunge kukusanya kodi. Kwa hiyo, hayo maneno yako yaweke tu vizuri vile ambavyo mtu alivyokosea. Endelea Mheshimiwa! *(Makofi)*

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ndiyo yenye wajibu wa kukusanya kodi kutoka kwa watu wake ili ipeleke maendeleo au huduma kwa wananchi, siyo Mbunge!

Kama kuna Mbunge ambaye ana vitabu vya kwenda kukusanya kodi ajitokeze mahali hapa ili aweze kuthibitisha hilo. Kwa hiyo, naomba waache kufanya propaganda, waeleze ukweli. Kama Mbunge atajitolea mwenyewe kwa hiari yake na wengi wanafanya, lakini siyo kwamba ni sehemu ya wajibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na ninaomba apokee taarifa!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Machali, taarifa yako inahusu nini hasa kimsingi?

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Mheshimiwa Waziri alikuwa anapotosha umma kwamba ni wajibu wa Mbunge kuhakikisha kwamba mambo mbalimbali yanatekelezwa nao. Ni wajibu wa Serikali kwa sababu Wabunge hatukusanyi kodi. Sasa hebu waache kufanya propaganda hizi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mimi ningewaomba tuwe na uvumilivu, hilo la kwanza. Lakini la pili, tuwe tunajua kabisa kwamba taifa lote linatuangalia na wanaotusikiliza wana akili timamu na wana uwezo wa kupima. Matatizo ya wananchi ni wajibu wetu sote, ni wajibu wa Serikali, ni wajibu wa Wabunge na viongozi wote kabisa. Tukianza hapa kusema kwamba ni wajibu wa upande mmoja tu, si sahihi hata kidogo, na kwa Waheshimiwa Wabunge niwahakikishieni kwamba ni wajibu wetu zaidi, wananchi wanatuangalia sisi na wanatutegemea sisi, ni wajibu wetu sisi kujuana na Serikali kuhakikisha kwamba matatizo yanatatuliwa. *(Makofi)*

Nimuite Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo. Dakika 20!

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu ili nami kwa mara ya kwanza niweze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge ambao wamezichangia kwa kiasi kikubwa na wametushauri mambo mengi kuhusiana na bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako tukufu na Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa ambaye ni Waziri mwenye dhamana ya Wizara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii pia kuwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Peramiho na hasa kwa ushirikiano wanaonipa. Ninaomba niwaambie hakuna kulala, CCM yatosha, hakuna kingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile napenda nikupongeze sana wewe mwenyewe binafsi, Mheshimiwa Spika wetu, Wenyeviti wa Bunge na Wenyeviti wa Kamati zote za Bunge na niwapongeze pia Wasemaji wa Kambi ya Upinzani na Waziri Kivuli aliyewasilisha hotuba ya makadirio ya Kambi ya Upinzani kwenye Wizara yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa namna ya pekee nimshukuru sana Waziri wangu Dkt. Shukuru Kawambwa, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi

na Watendaji wote wa Wizara wakiwemo viongozi ambao wanaongoza mashirika na taasisi mbalimbali ndani ya Wizara yetu kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa na hasa kunipa miongozo na taratibu mbalimbali za kufanya kazi ili kufanikisha sekta hii ya elimu. Ninawashukuru sana wote na ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee naomba niwapongeze na kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge hili na hasa wale ambao wamechangia mada hii ya leo na kutambua juhudi za Serikali ya Chama Cha Mapinduzi katika kusimamia sekta ya elimu. Lakini ninawapongeza na wale waliotushauri katika sekta ya elimu nini tufanye ili tuboreshe sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la elimu ni suala la Watanzania wote, panapofanyika mambo mema ni lazima tupongezane, pale panapoonesha upungufu, tushauriane na hiyo ndiyo hadhi ya Mtanzania katika kuendeleza maendeleo ya nchi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumza mengi lakini kwa kiasi kile ambacho muda wangu utaniruhuru. Lakini yale mambo yanayohusu sera nitamwachia Mheshimiwa Waziri wangu na mimi nitajikita katika maeneo kadhaa yanayohusu elimu ya msingi, sekondari, vyuo vya ualimu, ukaguzi, elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi, lakini vilevile nitakwenda kujibu baadhi ya hoja zilizosemwa na Wabunge lakini pia hoja zilizosemwa na Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa ninaomba nianze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge na hoja nyingine mbalimbali zilizoletwa mbele ya Bunge hili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru sana Msemaji wa Kambi ya Upinzani dada yangu Sussan Lyimo, na hasa nimshukuru sana kwenye hotuba yake ukurasa wa 26, amesema yafuatayo:- "Kambi Rasmi ya Upinzani inaunga mkono maendeleo yanayofanyika katika kuboresha elimu ya juu nchini".

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni uungwana, ukiona Kiongozi wa Kambi ya Upinzani anakubali kwamba kuna maendeleo katika sekta ya elimu, huo ni uungwana na ninampongeza sana.Na ninapompongeza, nataka kuwaambia Waheshimiwa Wabunge kwamba kwa maneno haya ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani wa Wizara hii inamaana basi Serikali ya Chama Cha Mapinduzi si kwamba imelala bali ni sikivu na ndiyo maana kuna maendeleo. Kwa hiyo, hiyo nataka kuisema bila woga kabisa na maneno haya siyo ya kwangu na ninaomba niwaambie Watanzania kwamba kama maneno haya

yameandikwa kwenye Taarifa ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani ina maana anatuunga mkono hata Wabunge wa CCM tuliosema maendeleo yapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo siyo maneno yangu bali nimenukuu hicho kifungu na kipo kama kilivyo na siyo cha kwangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaendelea kujibu hoja na hizo ndiyo hoja zilizoonekana. Naomba Wabunge wawe wavumilivu tu katika kujibu hoja ni lazima ueleze na uhalisia wa mambo.

Hoja ya kwanza hapa nyingine iliyosemwa na Kambi ya Upinzani ni kwamba mpango wa matokeo makubwa sasa kutilia mkazo kuongezeka kwa kiwango cha ufaulu utasababisha wanafunzi kukariri badala ya kuelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa; lengo lake, kwanza ilikuwa ni kutatua changamoto katika sekta yetu ya elimu. Lakini ilikuwa vilevile kupima na kutathmini maendeleo hayo ambayo yanapatikana katika sekta hii ya elimu. Sasa tunaposema kwamba mpango huu utawafanya watoto wakariri badala ya kuelewa, sasa ukiacha kuangalia mipango iliyoainishwa kwenye mpango huu wa matokeo makubwa sasa, tumesema katika matokeo makubwa sasa tutajikita katika stadi za kujua kusoma, kuandika na kuhesabu.

Sasa tukijikita kwenye stadi za kujua kuandika na kuhesabu, bado kweli mtu atasema kwamba mpango wetu huu wa matokeo makubwa sasa unajikita kwenye kukariri?! Unajikita kusaidia watoto wetu kuelewa! Kwa hiyo mimi naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba tumejipanga na siyo kwamba tunakwenda bila kujua tunachokifanya kupitia kwenye Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakupa mfano mmoja tu, katika matokeo ya ufaulu mwaka huu hata kama tunabeza kazi nzuri ya Serikali na shule za Serikali yetu, matokeo ya ufaulu mwaka huu ambayo yanapimwa na BRN, angalia tu mfano mdogo wa shule yetu ya sekondari ya Mzumbe yenye wanafunzi 108, kati ya wanafunzi hao 108, wanafunzi 57 wamefaulu vizuri kwa daraja la kwanza, wanafunzi 27 wamefaulu vizuri kwa daraja la pili, wanafunzi 15 wamefaulu vizuri kwa daraja la tatu, wanafunzi 9 wamefaulu vizuri kwa daraja la nne na hakuna *division zero*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa haya yote yanaonesha ni kwa kiasi gani hata sisi wenye shule za Serikali ambao ni Serikali tunajitahidi katika suala hili la BRN ili kuwafanya watoto wetu waende mbele.

Mheshimiwa Salome Mwambu yeye ameleta hoja yake hapa kwamba Wilaya mpya ya Mkarama haina gari wala ofisi ya ukaguzi. Wilaya hii ni mpya na ninampongeza sana Mheshimiwa Salome Mwambu kwa kutambua

umuhimu wa Idara hii ya Ukaguzi kwenye Wilaya yake mpya. Kwa kuanzia, tunawasiliana na Ofisi ya TAMISEMI ili kwanza waanze kuisaidia Wilaya hiyo ipate ofisi za kuwaweka wakaguzi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mheshimiwa Joseph Roman Selasini yeye ameuliza kwamba tuna mkakati gani sisi Serikali kuhakikisha hizo Wilaya zetu na hasa Wilaya zile zenye mazingira magumu wanapata magari kwa ajili ya Idara ya Ukaguzi. Nasimama hapa kifua mbele kwa niaba ya Serikali yangu ya Chama Cha Mapinduzi, katika bajeti ya mwaka huu Serikali hii sikivu imeelewa na Watanzania nawaambia, kwamba imepanga kununua jumla ya magari 45 na yatasambazwa katika Wilaya mbalimbali. Sasa atakayetaka bajeti hii leo isipitishwe, anataka pia na magari hayo 45 ya kuimarisha ukaguzi yasinunuliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumejipanga na tutanunua magari hayo na tutayapeleka kwenye Wilaya zinazohusika.

Mheshimiwa Ally Keissy amesema kwamba Idara ya Ukaguzi haipewi fedha za kutosha. Mheshimiwa Ally Keissy nakubaliana na wewe. Mwaka 2013/2014 Idara hii ya Ukaguzi ilipewa milioni 339,673,500/=. Serikali sikivu ya Chama Cha Mapinduzi mwaka huu wa fedha imetenga bilioni 2,064,520,360/= kutoka kwenye milioni 335. Sasa Serikali hii haisikii? Serikali hii imeziba masikio? Serikali imesikia na inajua umuhimu wa ukaguzi na fedha hizo bajeti ya mwaka huu tena zimetengwa fedha za ndani. Kwa hiyo, Serikali yetu ni sikivu na Serikali imeanza kuthamini mchango huu wa idara ya ukaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Huduma za Jamii, ikiongozwa na Mheshimiwa Margaret Sitta, walitupa maelekezo na tuliyafuata. Tupo imara na tutaendelea kuisikiliza Kamati yetu, Serikali itafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Sussan Lyimo alisema, "kuna mpango gani wa kuifanya Idara ya Ukaguzi kuwa wakala?" Waheshimiwa Wabunge, nakubaliana na Mheshimiwa Sussan Lyimo, ni lazima niseme hapa nakubaliana na Kamati ya Bunge, lazima hapa niseme upo umuhimu wa kuifanya Idara ya Ukaguzi iweze kusimama na kufanya shughuli zake vizuri. Hilo halina ubishi, na kwa kuwa halina ubishi sisi kupitia kwenye Wizara yetu tumeamua kuanzisha Mamlaka ya Ithibati na Udhibiti katika elimu ngazi ya elimu ya msingi. Na tumesema ili kuanza kuandaa Idara ya Ukaguzi kuwa mamlaka, itaanza kwanza kufanya kazi chini ya chombo hicho ili iweze kujitegemea na kusimamia shughuli zetu za ukaguzi. Tumesikiliza Waheshimiwa Wabunge na tumeshafanya hivyo. Kwa hiyo, naomba niwahakikishie kwamba Rasimu ya Waraka tayari tumeshaipeleka Baraza la Mawaziri na baada ya muda sheria hii ikishatungwa haya mambo yote yatakaa sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chiligati, Mheshimiwa Abuu Jumaa wao walizungumzia sana uhaba wa walimu wa sayansi. Waheshimiwa Wabunge, Serikali hii ya Chama Cha Mapinduzi imesikia na inakubali tuna upungufu wa walimu 24,000 wa masono ya Sayansi, lakini haijakaa kimya. Kwa sasa tumeanza kutoa ajira na kuruhusu vibali kwa ajira ya ualimu wa masomo haya ya sayansi kwa wageni ambao wanatoka nchi za nje kama ma-*volunteer*, tuna ma-*volunteer* kutoka *JICA, Peace Corps* na kwingineko kwingi tu, wamekuja wanatusaidia.

Lakini tumesema hiyo haitoshi, sisi wenyewe ndani ya mkakati wa Wizara, mmeona kwenye tangazo letu la udahiri wa walimu kwenye vyuo vyetu vya ualimu safari hivi, tumesema sasa basi, tunakwenda kudahiri wanafunzi wetu waliomaliza kidato cha nne na kupata *division one* tunawapeleka watakaotaka kusomea ualimu wa masomo ya sayansi, tunawapa ruzuku, watasoma kwa ruzuku. Ni kazi hiyo inafanywa na Serikali yetu. Na wale waliopata *grade* ya pili kwa maana ya *division two* na *division three* hao tutawapa mikopo.

Kumejengwa tena hoja nyingine na Kambi ya Upinzani kwamba Serikali itenge bajeti maalum ya kuwapa walimu mafunzo maalum ya lugha na hasa lugha ya Kingereza ili waweze kutoa mada kwa uelewa na kuwafundisha wanafunzi vizuri. Mheshimiwa Sussan Lyimo nakushukuru, jambo hili ni la msingi sana na hapa watu wameeleza umuhimu wa kuwafundisha walimu wetu, umuhimu wa kuhakikisha walimu wanaendelezwa.

Mheshimiwa Sussan Lyimo, naomba nikwambie tu, suala hili wewe unapotuambia leo, sisi tulishaanza kulitekeleza toka bajeti iliyopita, tulishaanza. Tumeishaanza kuwa-*train* walimu wa masomo yale muhimu katika sekondari zetu, tumechukua somo la Jiografia, Fizikia, Hesabu, lakini pia tumechukua masomo ya lugha kwa maana ya Kiswahili na Kingereza. Tumeanza na tunaendelea na walimu wananisikia, wamepata hayo mafunzo ya kuwaboresha ili wawaboreshe wanafunzi wetu. Kwa hiyo, haya mafunzo ya walimu tunaendelea nayo.

Mheshimiwa John Mnyika amezungumza jambo la muhimu sana. Mheshimiwa John Mnyika amesema leo hapatoshi kama hatatajua *report* ya Tume iliyoundwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika kufuatilia kuporomoka kwa matokeo ya kidato cha nne mwaka 2012. Mheshimiwa John Mnyika tunakubaliana na ushauri wako, tumekubali na tutaleta taarifa ile kwenye Bunge kupitia Ofisi ya Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika atapanga utaratibu wa kujua suala hilo sasa litajadiliwa namna gani kama ni kupitia kwenye Kamati yetu, kama ni kupitia kwenye Bunge hilo sasa siyo kazi yetu. Lakini huo ni ushauri mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la elimu kama nilivyosema toka mwanzo ni la Watanzania wote na sisi Wabunge tunawawakilisha Watanzania, kwa hiyo, kile ambacho ni kizuri inatakiwa tuungane pamoja ili wote tushauriane. Kwa hiyo, hilo halina mgogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Huduma za Jamii ilituagiza Serikali tuhakikishe tunajitahidi kuiomba TPDC iendeleze mradi wa kuimarisha ajira kule Mtwara, hilo tumelipokea. Kamati pia ilituagiza tuone umuhimu wa kuharakisha ujenzi wa vyuo na leo ndugu zangu wa Kagera wameniambia hapa hapatoshi kama Kagera hakutakuwa na chuo cha VETA cha mkoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme yafuatayo:- Chuo kimoja cha *VETA* katika taifa letu kinajengwa kwa fedha isiyopungua shilingi bilioni 5. Chuo cha Wilaya kinajengwa kwa fedha isiyopungua shilingi bilioni 3.

Sasa naomba niagize yafuatayo kwa Mkurugenzi wetu wa VETA; kwa kuwa, tayari tumefanya ukarabati wa kutosha wa vyuo kadhaa nchini kikiwemo chuo cha Kagera, ninaomba haraka sana wakipandishe chuo cha Kagera kiwe na hadhi ya chuo cha Mkoa ili kutekeleza azma ya Mkoa wa Kagera kuwa na chuo cha Mkoa. Baada ya hapo utaratibu wa kujenga vyuo vya Wilaya tutaendelea kuufuata kwa kadri ya utaratibu tuliojipangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kulikuwa na hoja kutoka Kambi ya Upinzani inayohusu Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Mheshimiwa Susan Lyimo, tunakubali, wakati mwingine tumekuwa tukichelewa kutoa fedha hizo, lakini zinapopatikana tumekuwa tukizitoa na wanafunzi wanapata. Kwa hiyo, hapa unachotusukuma ni kuendelea kuhakikisha tunaharakisha fedha hizo zinawafikia wanafunzi kwa wakati unaotakiwa. Ni jambo jema, wote tunawatakia watoto wetu maisha bora, tunawatakia waweze kuendelea vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja nyingine kutoka kwa Dkt. Goodluck Joseph Ole - Medeye, ambaye alikuwa anazungumzia upungufu wa vifaa vya kufundishia katika chuo chetu kikuu cha Dodoma, Chuo chetu Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa. Naomba nimthibitishie Mheshimiwa Medeye kwamba, katika mipango yetu ya maendeleo mwaka huu matatizo haya yote yatazingatiwa na hakuna tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo labda ningependa sana nilizungumzie, Mheshimiwa Susan Lyimo alizungumza sana suala la kuhakikisha hawa walimu wetu ambao wamesoma shahada ya *education* na *psychology* wanaajiriwa haraka sana. Naomba tu nimwambie Mheshimiwa Susan Lyimo kwamba, baada ya kuliangalia suala hili tumekubali tutafute njia ya kuona

tunaweza kulimalizaje na watoto wetu wa kitanzania waweze kunufaika. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalize kwa kukushukuru. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na naomba Wabunge mpitishe bajeti yetu ili tukatekeleze majukumu ya elimu katika nchi yetu ya Tanzania. Asante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa Jenista Mhagama, Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, tunakushukuru sana.

Sasa moja kwa moja nimuite mtoa hoja, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa. Mheshimiwa Waziri, *you have the floor*. Mheshimiwa Waziri, una nusu saa.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu ili niweze kutolea ufafanuzi hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge walizozitoa wakati wakijadilia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka 2014/15.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta na Wajumbe wa Kamati hiyo kwa kuchambua na kujadili kwa kina bajeti ya Wizara yangu. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo kwa kuwasilisha maoni ya Kamati hapa Bungeni.

Naomba pia kumpongeza Mheshimiwa Susan Lyimo, Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani katika sekta ya elimu kwa maoni, ushauri na mapendekezo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru wananchi wa jimbo la Bagamoyo kwa kunipa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yangu jimboni na kwa kunivumilia pale niliposhindwa kuwa nao kwa sababu ya dharura za majukumu mengine ya kitaifa. Lakini pia niishukuru kipekee familia yangu, mke wangu na watoto wetu, kwa kuwa karibu nami na kunitia moyo kila wakati na hivyo kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kwa kutolea maelezo baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Hata hivyo, hoja ni nyingi na muda tulionao hautoshi kuweza kuzitolea maelezo au ufafanuzi hoja zote. Kwa hivyo tutajitahidi kuhakikisha kwamba tunaleta majibu ya hoja hizo kwa maandishi kupitia ofisi ya Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa majadiliano ya hoja ya Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge 26 walitoa hoja zao kuhusiana na sekta ya elimu na mafunzo ya ufundi, lakini pia Waheshimiwa Wabunge 10 walitoa hoja zao wakati wakichangia hotuba za Wizara nyingine. Baada ya kuwasilisha hotuba ya Wizara yangu, Waheshimiwa Wabunge 35 wamechangia hoja yangu kwa kuongea na Waheshimiwa Wabunge 58 wamechangia kwa maandishi. Kwa sababu ya muda sitaweza kuwataja majina wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu itazingatia ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Nami napenda nitumie nafasi hii kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya maeneo yaliyojitokeza wakati wa majadiliano. Kwa sababu ya ufinyu wa muda naahidi kuwa hoja za kila Mbunge zitajibiwa na Wizara yangu kwa maandishi katika kabrasha ambalo tutaliwasilisha katika Ofisi ya Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kwa michango yao walioyoitoa kwa maandishi na kwa kuongea hapa Bungeni wakati wakijadili hoja ya Wizara yangu. Niwahakikishie tu kwamba, michango hii mizuri na iliyojaa busara itatusaidia sana katika kusimamia utekelezaji wa bajeti hii na kuboresha sekta ya elimu na mafunzo ya ufundi katika siku zijazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nianze kutoa ufafanuzi katika baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge. Nianze na hoja ambazo zilitolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii. Nishukuru kwamba kwa kiasi kikubwa Kamati yetu hii imepongeza kazi nzuri ambayo imefanywa na Wizara na imetoa ushauri mbalimbali ambao niihakikishie Kamati hii adhimu kwamba, Wizara yangu itahakikisha inazingatia ushauri huu uliotolewa na kuutekeleza ipasavyo ili tuweze kupata mafanikio mazuri katika sekta ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo mahsusi ambalo linahusiana na mikakati ya VETA na NACTE kudhibiti vyuo visivyosajiliwa. Niseme hapa kwamba, NACTE na VETA wanaendelea kuutangazia umma vyuo vilivyosajiliwa na vile visivyosajiliwa na madhara ya kusomesha wanafunzi kwenye vyuo ambavyo havikusajiliwa. Vyuo vya ufundi stadi vilivyosajiliwa hutolewa katika chapisho kila mwaka na katika tovuti za taasisi hizi. Kwa hiyo, wananchi wahakikishe kwamba, hawapeleki watoto wao katika vile vyuo ambavyo havikusajiliwa aidha na Baraza la Ufundi *(NACTE)* au na *VETA*. Aidha, *VETA* na *NACTE* wana mawasiliano ya karibu kuhusu vyuo vyenye utata katika usajili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilikuwa na maoni katika eneo la madeni ya walimu na posho ya mazingira magumu. Kamati imesema kwamba, imedhihirika kwamba upungufu wa Walimu hasa katika maeneo ya vijijini unasababishwa kwa kiasi kikubwa na uwepo wa mazingira magumu katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kutoa ufafanuzi ufuatao. Serikali inatambua kwamba, baadhi ya watumishi wanafanya kazi katika mazingira magumu wakiwemo walimu. Katika kushughulikia kero hiyo Serikali inaanda taratibu za motisha kwa watumishi wote wanaoishi katika mazingira magumu. Serikali ndiye baba wa watumishi wote wa umma, wakiwemo walimu.

Walimu tunawapenda sana, tutawapa nafasi kubwa katika mchakato huu ili kuhakikisha kwamba wao wanapata kipaumbele wakati tunawashughulikia watumishi wote wa umma. Hata hivyo hatuwezi tukashughulikia kundi moja na wengine tukawaacha kabisa katika Wilaya hizo hizo na katika mazingira hayo hayo magumu, kuna mkunga, daktari na kila mtumishi mwingine wa umma ambaye ni muhimu hata kwa mwalimu mwenyewe ambaye yuko kule katika Wilaya hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nifanye mapitio katika hoja za Kambi Rasmi ya Upinzani. Moja ni katika eneo la Matokeo Makubwa Sasa *(BRN)*. Kambi Rasmi ya Upinzani imesema kwamba Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa kutilia mkazo kuongeza kiwango cha ufaulu utasababisha wanafunzi kukariri badala ya kuelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kutoa ufafanuzi ufuatao:- Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa una lengo la kutatua changamoto katika sekta ya elimu ambazo zimeathiri utoaji wa elimu bora nchini mwetu. Ili kukabiliana na changamoto hizo Serikali ilianzisha mpango huo wenye mikakati tisa ambayo kwa pamoja inatekelezwa ili kuweza kuinua kiwango cha elimu nchini mwetu. Mikakati hii tisa ni vitu mbalimbali na ndani mle kuna motisha ya walimu na kuhakikisha kwamba madeni yote yanaondolewa. Ndani mle katika mikakati hii ya pili kuna ujenzi wa miundombinu katika shule zetu ili kuhakikisha kwamba, shule zote zinakuwa ni shule kamili ambazo zinaweza kutoa elimu bora.

Ndani mle tuna mpango wa ufundishaji wa walimu na wanafunzi ili kuwawezesha kumudu zile mada ambazo zimegundulika kwamba ni ngumu kwa wanafunzi na wanashindwa kuzielewa vizuri na ndiyo maana wanafeli mitihani yao, lakini pia ni mada ngumu hata kwa baadhi ya walimu wenyewe

wanashindwa kuzisomesha vizuri na ndiyo maana wanafunzi nao wanashindwa kuzielewa vizuri. Huu ni mkakati ambao kwa kifupi tunauita *STEP (Student Teacher Enhancement Progamme)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa haiwezekani kwamba mikakati hii eti inaongeza tu ufaulu, inaongeza ufaulu kwa sababu inaongeza uwezo wa wanafunzi kumudu stadi zile ambazo wamesomeshwa katika ngazi husika. Katika ngazi ya elimu ya msingi wameweza kuzimudu stadi zile ambazo tunategemea kwamba mwanafunzi wa elimu ya msingi atakuwa amezimudu.

Katika elimu ya Sekondari vilevile. Kwa hivyo, kama sasa atakuwa amezimudu stadi zile ambazo tulikuwa tunataka aziweze katika kiwango hicho cha elimu kwa nini asi-*pass* mtihani! Utajuwaje kwamba amezimudu kama atakuwa ame- feli mtihani ule? Ndiyo maana kiwango cha mwisho kabisa cha tathmini yetu imekuwa kwamba watafauli kiasi gani kwa maana ya kwamba watakuwa wamemudu stadi zile katika elimu ya msingi ama katika elimu ya sekondari kwa kiasi kile ambacho kinatakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna namna nyingine dunia nzima, nenda Marekani, China, nenda Finland nchi ya kwanza kwa kiwango cha elimu duniani, kitu ambacho kinaweza kikampima mwanafunzi ni mtihani ambao ameufanya na kuweza kujua kwamba amefikia sehemu gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja nyingine ambayo inasema Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa motisha kwa walimu ni kipaumbele namba 9 na mpaka sasa madai ya walimu yaliyosababisha mgomo hayajatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe ufafanuzi ufuatao: Kwanza vipaumbele vile au mikakati hii ya utekelezaji wa Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa havikuorodheshwa kwa umuhimu kwamba ya kwanza ndiyo ya kwanza kwa umuhimu na ya 9 ndiyo ya mwisho kwa umuhimu. Mikakati yote ile lazima itekelezwe kwa pamoja na tunavyofanya ni kwamba, tunaitekeleza yote kwa pamoja kwa sababu mpaka umeitekeleza kwa pamoja ndiyo unaweza kupata matokeo yale unayoyataka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitoa motisha kwa walimu lakini hukujenga miundombinu ya shule utapata kitu gani? Ukitoa motisha kwa walimu lakini hukutekeleza mafunzo kazini kwa walimu katika mada zile ngumu, utafanikiwa kitu gani? Kwa hiyo, siyo kwamba mkakati huu umeorodheshwa namba 9 kwamba ndiyo namba 9 kwa umuhimu. Naomba ieleweke hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia katika jitihada za Serikali kuongeza ufanisi katika ufundishaji, Serikali imekusanya madeni ya walimu yenye jumla ya shilingi bilioni 52 mpaka ilipofikia mwaka 2011, kati ya hayo shilingi bilioni 22

yalikuwa ni madeni yasiyo ya malimbikizo ya mishahara na shilingi bilioni 30 yalikuwa ni madai yanayotokana na malimbikizo ya mishahara.

Niseme tu kwamba madai haya yote yalikuwa yamelipwa na Serikali. Nirudie, kwa yale madeni ambayo yalikusanywa kwa ushirikiano na Chama cha Walimu Tanzania *(CWT)* hadi ilipofikia Novemba, 2011, lakini baada ya hapo madeni yameendelea kukusanywa, na taarifa ambazo zimetolewa ni kwamba jumla ya shilingi bilioni 61 zinadaiwa na walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nieleze hapa kwamba, mtiririko huu wa madeni haya Serikali imeendelea kuyalipa huku inayahakiki. Kwa hiyo, ile shilingi bilioni 61 haiko *stagnant*, kwamba iko palepale. Serikali imeendelea kuyalipa kadri inavyoyahakiki.

Mpaka hivi sasa, kupitia hotuba ya Mheshimiwa Hawa Ghasia ambayo ameitoa hapa wakati anawasilisha bajeti yake, ukurasa wa 30 ameonesha mlolongo wa mtiririko wa fedha ambazo zilikuwa zinatoka Hazina katika mwaka huu wa fedha ikianzia mwezi Agosti, 2013, Septemba, 2013, Desemba 2013, Januari 2014 hadi Februari mwaka 2014, jumla yake ikiwa shilingi 19,231, 665,470. 67.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hatuko palepale *(stagnant)* kwamba madeni haya ya shilingi bilioni 61 kwa maana kwamba hiyo namba imekuwa namba moja ya ajabu ambayo kila siku iko vilevile, Serikali haisikii wala haijali, wala haijui madhira ya walimu na kwamba haishughulikii madeni haya. Kwa hiyo, tunaendelea kuyashughulikia madeni haya na Mungu akijalia tunatarajia tutafikia ukomo wake ndani ya mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine ambalo linahusu kasi ya ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi. Ni kweli Serikali imeahidi kujenga vyuo vya ufundi stadi vya VETA katika Wilaya zote nchini. Kutokana na changamoto ya upatikanaji wa fedha za kujengea vyuo hivyo, mpaka sasa ni chuo kimoja tu cha Wilaya kilichokamilika nacho ni cha Wilaya ya Makete.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za ujenzi wa chuo kimoja cha ufundi stadi cha *VETA* cha Wilaya ni kati ya shilingi za kitanzania bilioni 3 hadi 4.5. Kwa hiyo, ujenzi wa vyuo 30 vilivyo katika awamu ya kwanza unahitaji takribani shilingi za kitanzania bilioni 135, hii ni fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa ujenzi wa vyuo vya *VETA* vya Wilaya umepangwa kufanyika hatua kwa hatua kwa ushirikiano na wananchi na wadau wengine pamoja na sekta binafsi kwa kutumia Sera ya Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ya Mwaka 2009.

Sera hii inaweka mazingira wezeshi ya kisera, kisheria na kitaasisi yenye lengo la kutoa fursa kwa sekta binafsi kushiriki katika ubia huu. Katika dhana ya ubia huu sekta binafsi inahusika na kukarabati, kujenga, kuendesha, kutunza na kusimamia mradi mzima au sehemu yake kulingana na vigezo maalum vya utendaji vilivyowekwa na sekta ya umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejitahidi sana kusaka fedha, moja kwa kutenga fedha za ndani, lakini namba mbili kutoka kwa wahisani wetu na benki. Tumetenga fedha ambazo zitatuwezesha kujenga vyuo vitano vya *VETA* vya Wilaya mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tumekopa fedha kutoka *African Development Bank* ambayo itatuwezesha kujenga vyuo vya ufundi vya Mikoa minne ambayo ni Mikoa mipya. Hizi ni fedha ambazo tumezikopa na niseme tu kwamba urasimu wa kupata fedha hizi kutoka kwenye benki siyo mfupi.

Tumeanza zamani sana utaratibu huu, na wala hatushughulika na Benki ya Maendeleo ya Afrika peke yao, tumehangaika na benki chungu nzima na wahisani wengine. Lakini, kutafuta au kuomba si kupata, hiki ndicho ambacho tumemudu kukipata na Serikali itaendelea na juhudi hizo ili kuhakikisha ahadi ambayo tumeitoa kwa kila Wilaya kuwa na chuo cha mafunzo ya ufundi stadi, inawezekana.

Najua ni changamoto kwetu mpaka kufikia mwaka 2015, lakini tutajitahidi kwa kadri inavyowezekana ili tuweze kuvifikia vyuo vingi.

Waheshimiwa Wabunge wengi wameniuliza, wewe mwenyewe Mheshimiwa Naibu Spika, Kongwa kule umeuliza na Kongwa iko katika awamu ya kwanza ya ujenzi, Vyuo 30 ambavyo tumevipangia kwamba hivi tuanze navyo katika Vyuo vya Wilaya zote, lakini hivi Vyuo 30 ambavyo tumevipanga tuanze navyo hatuwezi sasa hivi. Hatuna fedha za kuweza kujenga Vyuo vya Ufundi Stadi katika Wilaya zote 30 za awamu ya kwanza ikiwemo Kongwa na ikiwemo Longido ya Mheshimiwa Lekule Laizer.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika hivi vitano ambavyo tunaanza navyo, vimo ndani ya 30 vile ambavyo tunaanza navyo vya awamu ya kwanza. Sasa wanasema kwa nini umekichukua hiki, kwa nini hukukichukua kile, hiki ni kitendawili kikubwa, lakini tuliweka vigezo maalum ambavyo vimetusaidia kuweza kuvitoa hivyo vitano. Nitaomba tu Waheshimiwa Wabunge waweze kutuvumilia katika hili kwa sababu tatizo kubwa ni kwamba, uwezo ni mdogo na tungependa sana kufanya hili, ndiyo maana tumeliahidi katika Ilani lakini kinachogomba sasa ni uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo Kambi ya Upinzani imeitoa ni kuhusu mfumo wa elimu. Wanasema Serikali ione uwezekano wa kuboresha mfumo wa elimu wa kupanua wigo wa elimu ya msingi kuwa miaka tisa badala ya saba. Niseme tu Msemaji Mkuu wa Upinzani hapa alikuwa *Sharp,* kwa sababu hili ni jambo la kisera na limo katika Sera yetu mpya ya Elimu ambayo ililetwa hapa katika Bunge na kujadiliwa na Bunge mara nne wakati nikiwa Waziri mara mbili na kabla ya mimi, Mawaziri walionitangulia mara mbili. Hii ni Rasimu ya sera iliyoletwa Bungeni kwa mara nyingi zaidi kuliko sera yoyote nyingine ambayo imeshawahi kuasisiwa na nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili limo mle ndani, sasa leo linakuwa hoja ya Upinzani kwamba elimu hii ipanuliwe ili iweze kuwa na muda mwingi zaidi wa mwanafunzi kukaa katika elimu kuliko mwanafunzi kumalizia darasa la saba ambapo anakuwa na umri mdogo na anapomaliza pale akiwa na umri mdogo hata hiyo *VETA* yenyewe kwenda kufanya mafunzo nayo inakuwa mtihani kwa sababu kule mafunzo ya ufundi nayo sio mepesi kwa watu wenye umri mdogo. Kwa hiyo, katika Sera ambayo sasa hivi iko katika Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na Mungu ajaliapo katika mwaka huu huu wa kalenda bila shaka Sera hii itakuwa imetoka na kwa maana hiyo tutaanza kutekeleza ile sera mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna hoja ambayo imeletwa na hoja ya Upinzani wakisema kwamba Wizara irejeshe utaratibu wa kuwezesha watu wazima vijijini wanaopenda kupata masomo ya sekondari saa za jioni na siku za mapumziko ama *weekends* ili kuinua kiwango cha elimu vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa utoaji wa masomo ya sekondari nje ya mfumo rasmi wa shule, bado upo na unaendeshwa na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kupitia Wakufunzi Wakazi wa Mikoa ambao huweka vituo katika shule za sekondari za Serikali zilizoko katika maeneo yao kwa makubaliano na wakuu wa shule husika. Hata hivyo kusambaa kwa huduma hii katika ngazi za vijijini kumekuwa na changamoto kutokana na uhaba wa wataalam katika fani ya Elimu ya Watu Wazima pamoja na kukosekana mwamko wa watu wazima waliopo vijijini kujitokeza kwa wingi katika vituo hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni jambo kubwa na sio rahisi sana, hata vituo vichache na wataalam wachache, lakini bado unakuta kuna uhaba wa wananchi wale ambao wangependa kufanya masomo haya kwa wakati wa jioni na pengine kwa sababu ya changamoto pia za uzalishaji mali katika maeneo haya ya vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo limeletwa na Kambi ya Upinzani ni kuhusu ugatuaji kwamba katika bajeti ya maendeleo Wizara imetenga shilingi bilioni 15 kwa ajili ya utekelezaji wa elimu ya msingi na shilingi

bilioni 12 kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya sekondari wakati utaratibu wa kusimamia utekelezaji wa miradi hii upo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kutoa ufafanuzi ufuatao kwamba, shughuli zinazoonekana katika bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi katika Kitengo cha Msingi na Sekondari zinahusiana na usimamizi, zinahusiana na ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa sera, lakini kubwa zaidi na linaloongeza fedha ni mpango huu mpya wa uboreshaji wa stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu ambao mkataba wake Mheshimiwa Waziri wa Fedha amesaini hivi karibuni wenye jumla ya thamani ya shilingi milioni 94.8 za Kimarekani ama shilingi bilioni 151 fedha za Kitanzania. Mradi huu unaitwa *LENS* unasimamiwa na Wizara ya Elimu na vifungu hivi vimepokea fedha katika mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine, kwamba Serikali kuendelea kutoa misamaha mikubwa ya kodi ambapo kufikia Juni 30 ilitoa misamaha ya jumla ya shilingi trilioni 1.52 kwamba misamaha hiyo haifai, haina tija Serikali iisimamishe kwa sababu ingeweza kujenga shule 300, ingeweza kujenga nyumba za walimu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba ushauri huo umepokelewa na Wizara yangu itawasilisha ushauri huo Wizara husika na Serikalini ili tuweze kulishughulikia suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoka Kambi ya Upinzani pia kuna hoja inayohusu madaraja ya ufaulu wa wanafunzi na hoja inasema kwamba, mfumo wa sasa wa upangaji wa madaraja umepanuliwa sana hivyo kuchukua wanafunzi wasio na uwezo. Naomba niseme kwamba hili jambo nasikitika sana na nashukuru kwamba Waheshimiwa kadhaa walilitolea ufafanuzi jambo hili halina mashiko wala halina uthabiti katika kulisema kama ni jambo la changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Kambi ya Upinzani imeeleza kuwa, Serikali imeshusha viwango si kweli na walioweza kuchangia katika wale wachangiaji Waheshimiwa Wabunge wamelieleza kwa ufasaha zaidi na pengine sina haja ya kulisema sana. Naomba nilitolee ufafanuzi kidogo kama ifuatavyo:-

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ipo mifumo mbalimbali inayotumika duniani katika upangaji wa viwango vya ufaulu ambapo mfumo unaotumiwa viwango vya ufaulu vinavyobadilika ama *flexible grade range* na wengine wanatumia mfumo unaotumia viwango vya ufaulu visivyobadilika ama *fixed grade range*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ilikuwa ikitumia mfumo wa viwango vya ufaulu vinavyobadilika ama *flexible* kuanzia mwaka 1973 hadi 2011. Katika mfumo huu viwango vya ufaulu vilipangwa kutegemeana na ufaulu wa watahiniwa katika somo husika na hivyo kuwa na viwango vya ufaulu vinavyotofautiana kati ya somo moja na somo lingine na kati ya mwaka mmoja na mwaka mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya changamoto kubwa ya matumizi ya mfumo huu ilikuwa ni kutofahamika kwa viwango vya ufaulu kwa kuwa vilikuwa vinabadilika kutegemeana na ufaulu wa masomo na hata Baraza lilikuwa haliwatangazii kwa sababu inategemea na ufaulu mwaka huu ulikuwaje na Baraza lenyewe linaweza likabadilisha ili likawa na viwango ambavyo itavitangaza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Mitihani liliamua kutumia mfumo wa viwango vya ufaulu visivyobadilika kwa madhumuni ya kuwawezesha wadau wa elimu kujua viwango vya ufaulu vinavyotumika katika kutunuku matokeo ya mtihani wa Taifa. Baraza limeanza kutumia makundi saba ya *grade* za ufaulu ambayo ni (A), (B+), (B), (C), (D), (E) na (F) badala ya makundi matano yaliyokuwa yanatumika awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu umelenga kupunguza mrundikano mkubwa wa alama katika kundi moja. Mifano ya nchi zinazotumia makundi mengi kwa lengo la kupunguza mrundikano wa alama katika kundi moja ni pamoja na nchi ya Kenya, wao makundi ya *grade* za ufaulu yako 12 sio saba kama sisi wala sio matano yale tulioachana nayo. Uganda wanatumia makundi tisa, Afrika ya Kusini yanatumia makundi saba, nchi za Afrika Magharibi kama Nigeria, Liberia, Sierra Leone, Ghana na Gambia wanatumia makundi tisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hakuna kigugumizi chochote wala kitu kipya wala kitu cha ajabu, wala ukusanyaji wa watu wote wale ambao wamefeli katika kuwapeleka mbele kwa sababu tu umeondosha mrundikano wa alama katika kundi moja kwamba (B) hata yule aliyepata 50 ni (B), aliyepata maksi 74 (B) tumezigawa zile tumeweka (B) ya juu ambayo ni (B+) na (B) ya kawaida. Lakini *pass* ni maksi 30 kama ilivyokuwa miaka yoyote.

Kwa hiyo, wananchi, Waheshimiwa wanapokuja huko mitaani wakawaambia kwamba, viwango vimeteremshwa ni kwamba anakudanganya, Waziri mwenye dhamana ni mimi, anakubabaisha anadhani kwamba yeye anaweza kufanya kitu cha ajabu katika sekta ya elimu wakati changamoto za sekta za elimu ni za dunia nzima. Sasa hivi nenda Marekani leo, nenda Uingereza leo magazeti yamejaa changamoto za sekta ya elimu tangu

*page* ya kwanza mpaka *page* ya mwisho, Waziri wa Elimu pale halali, wala hapumziki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipofanya ziara Finland pamoja na Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Kudumu ya Huduma za Jamii, ujumbe tuliokuwa nao katika ndege moja kuanzia Zurich ulikuwa ujumbe kwa Marekani unakwenda kujifunza Finland na nilipoongea na Waziri akaniambia na sisi tuna matatizo kama dunia nyingine, tunakwenda Finland kujifunza. Nani anashangaa matatizo katika nchi ambayo inaendelea kama Tanzania ambayo tumefanya kazi kubwa kuhakikisha kwamba elimu yetu inaboreka na hakuna anayeweza kufuata mfano wa Tanzania katika hatua zile ambazo tumezimudu mpaka hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ni mengi sijui kama nitaweza kuyamaliza. Kambi ya Upinzani ilizungumzia machapisho katika vyuo vyetu vikuu. Hoja ikasema kwamba Tanzania ni miongoni mwa nchi za Afrika zinazotoa machapisho kidogo kuliko zote. Mwaka 2010 ilitoa machapisho 120 tu ikilinganishwa na Botswana ambayo ilitoa machapisho 347.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Susan Lyimo nadhani afanye utafiti pamoja na Kambi ya Upinzani. Anasema Botswana imetoa machapisho 347. Nimpe mfano, *University of Dar es Salaam* peke yake mwaka 2013, imetoa machapisho 318, *MUHAS* peke yake imetoa machapisho 362 yaani zaidi ya nchi nzima ya Botswana ambayo ameiona eti ndio imetoa machapisho mengi kushinda vyuo vyetu; *SUA* machapisho 130, Mzumbe machapisho 168, *UDOM* 187, *MUCCoBS* 20, *MUCE* 26. Naweza nikamworodheshea na tumekwenda machapisho ya 300,039. Kama hukufanya utafiti, bora usiongee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii tumefanya makubwa katika sekta ya elimu. Tumeanza na Chuo kimoja Kishiriki na sasa tuna Vyuo zaidi ya 66 katika nchi yetu, Upinzani itaweza kufanya kazi hii. Lazima tuseme ukweli katika hili, mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mengi ambayo yamezungumzwa na Kambi ya Upinzani, naomba kwa sababu muda umekwisha kuna suala la ujenzi wa Vyuo Vikuu na kadhalika niruke ili niweze angalau nifikie maeneo mengine, isionekane kwamba nimebana huko peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna moja ambalo la muhimu sana nadhani hili lazima niliseme nalo. Hili limebuniwa na Kambi ya Upinzani kuhusu mgogoro wa Chuo cha Mtakatifu Joseph, Songea kulikosababishwa na kushindwa na uongozi wa chuo kusimamia mfumo wa uendeshaji na usimamizi wa vyuo vikuu jambo ambalo limekuwa chanzo cha matatizo pale chuoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili tumelimaliza, tumelifanyia kazi kwa wakati, Mheshimiwa Naibu Waziri alikwenda mara moja akatembelea akaona mazingira ya pale, lakini mara moja Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania *(TCU)* ambayo ina dhamana ya kusimamia elimu ya juu nayo ikaingilia kati, ikakitembelea chuo, ikapokea malalamiko hayo na kutuma wataalam wake kwenda Songea kuchunguza kiini na chanzo cha tatizo kilichosababisha mgogoro huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wataalam hao waliongea na uongozi wa chuo, uongozi wa wanafunzi na kubaini kuwa chanzo cha tatizo kilikuwa ni chuo kubadili jina la program za masomo ambazo zilikuwa zimeshasajiliwa bila ya kufuata utaratibu. Aidha, tatizo la uongozi wa chuo kuingilia mambo ya Serikali ama uongozi wa wanafunzi, tatizo la vyoo, upatikananji wa *internet* na wanafunzi kutoendelea na muhula wa masomo unaofuata kwa matatizo ya ujauzito.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutatua mgogoro huo *TCU* ilikutana na uongozi wa chuo na kuwataka watekeleze mambo kadhaa, yote yale ambayo yangepelekea utatuzi wa jambo hili. Naomba niseme kwamba haya yametekelezwa na sasa hali ni shwari na chuo kile kinaendelea vizuri chini ya uangalizi wa karibu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema muda hautoshi kuweza kutoa ufafanuzi wa hoja zote, hivyo, naomba kwa heshima na taadhima niahidi tu kama nilivyosema awali tutazijibu hoja za kila Mbunge kwa maandishi katika jedwali ambalo tutaliwakilisha katika Ofisi ya Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa. Hoja imetolewa na imeungwa mkono nashukuru sana kwa kujaribu kupitia hoja za Waheshimiwa Wabunge katika kuhitimisha hoja yako.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 46 – Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi**

Kif. 1001 – *Administration and Human Resource Management… … ... ...* ...Tshs. 23,093,008,000/=

**MWENYEKITI:** Kuna walioletwa na Vyama isipokuwa CCM kwa sababu imeonekana ni wengi sana, lakini kwa vyama. Sasa mnaposimama wawili wawili maana yake mnanichanganya. Kwa hiyo, kila chama mjitazame msimame mmoja mmoja ili tujue ni yupi anayesimama kwa Chama gani.

Tuanze kwanza kama muda utaruhusu tutaongeza. Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed kwa *CUF*, Mheshimiwa Susan Lyimo kwa CHADEMA, Mheshimiwa Francis Mbatia kwa *NCCR*-MAGEUZI, Mheshimiwa Augustino Mrema wa *TLP*. Napata ushauri hapa UKAWA mmoja tu. Mheshimiwa Mama Margaret Sitta Mwenyekiti, Mheshimiwa Assumpter Mshama, Mheshimiwa Peter Serukamba, kabla yake ni nani? Mnakaa maeneo yasiyo yenu, mnatuchanganya kidogo, Mheshimiwa Josephat Kandege, Mheshimiwa Selemani Jafo, Mheshimiwa Margareth Mkanga. Hatutachukua wote huko CCM tutachukua kidogo tu. Mheshimiwa Mwanjelwa, Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Mheshimiwa Gosbert Blandes. Basi jamani, nachukua kiasi tu. Sasa tuanze na Mheshimiwa Rajab.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nataka kupata ufafanuzi na maelezo ya kina kutoka kwa Waziri juuya mchezo mchafu ambao unaathiri mfumo wetu wa elimu, lakini vile vile unaathiri uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuzagaa kwa vyeti feki ambavyo kunaifanya hadhi ya Baraza la Mitihani la Taifa kushuka na kukosa imani hata katika Jumuia za Kimataifa. Naomba nitangulize kusema kwamba iwapo Waziri au Serikali haitanipa majibu ya kina katika hili au maelezo ya kina, nina lengo la kuondoa shilingi ya Waziri katika mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vyeti feki ambavyo Baraza la Mitihani ndilo lenye dhamana na jukumu la kuhakikisha kwamba kitu hiki hakipo katika nchi yetu inaonekana kuwa sasa limekuwa ni suala la kawaida, vyeti feki vimekuwa ni vingi kiasi kwamba vyeti feki hivi vinasababisha sasa kupata au kuajiriwa kwa watendaji ambao ni feki, Mawaziri mizigo, hata wale ambao leo wanashindwa kutoa ufafanuzi kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano juu ya majukumu ya Wabunge, lakini vile vile inasababisha pia kupata Makatibu Wakuu mizigo na wataalam feki, kwa sababu tu ya kutolewa kwa vyeti hivi feki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hivi karibuni tu, katika Chuo cha Polisi, Moshi wamerejesha wadahiliwa 122 ambao walikuwa na vyeti feki. Magereza vile vile wamerejesha wadahiliwa wengi tu kwa sababu ya kwenda na vyeti feki. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa anipe maelezo ya kina ya namna gani na ni kwa nini mpaka leo Baraza la Mitihani linashindwa kuthibiti vyeti feki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na hayo wakati wa udadavuzi wangu, nimefanya udadavuzi katika mitandao, nimeangalia katika *Public Services Recruitment Secretariat,* kupitia kwa msemaji wake Bwana Kassim Nyaki ambaye ndiye *Information Officer,* anasema kwamba kati ya watu ambao wanaomba kazi 13,541; waombaji hao 816 yeye katumia lugha ya Kiingereza anasema ni *Bogus academic qualification,* katumia neno baya ni *bogus Academic Qualification*. Kwa hiyo, naomba maelezo ya Serikali, naomba maelezo ya Wizara na kama hayakuwa na ufafanuzi wa kutosha nitaondoa shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Niwakumbushe wale wote mtakaopata nafasi ni dakika tatu. Kwa hiyo, ni vizuri kuji-*tune* katika dakika hizo ili twende vizuri. Mheshimiwa Waziri ufafanuzi!

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi ufuatao kwa hoja ya Mheshimiwa Rajab kama ifuatavyo:-

Amelitaja Baraza la Mitihani, Baraza la Mitihani kwa niaba ya Serikali, baada ya kugundua tatizo hili la udanganyifu katika vyeti ambalo huko miaka ya nyuma halikuwepo, watu walikwenda na stahili zao kama ametimiza viwango vya daraja fulani anachukua cheti, hakina hata picha, kina jina lake tu na anakitumia hicho bila kumpa ndugu yake na bila ya kumpa mtu mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadaye ukatokea udanganyifu, lakini Serikali kupitia Baraza la Mitihani imechukua hatua ya kubadilisha namna ya kuchapa vyeti hivi na hivi sasa vyeti hivi ni lazima viwe na *serial number,* viwe na jina kamili la kijana ambaye anafanana na cheti chake cha kuzaliwa na vyeti hivi ni lazima viwe na picha ya yule ambaye anapewa hicho cheti. Ndiyo maana kwa kutumia utaratibu huu imekuwa ni rahisi sasa hivi kwa yeyote ambaye anaajiri hasa sisi kwa upande wa Serikali tumeamua kabisa kuwa hatutaki kuajiri watu ambao wana vyeti feki.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyeti vinapelekwa mara moja Baraza la Mitihani na kesho yake majibu yanarudi kuwa hiki ni feki na hiki ni kizuri na ndiyo maana juzi Polisi walifukuza watu, hakuna sasa hivi uwezekano Mheshimiwa Rajab

mtoto wako akagushi cheti, hata kozi zote zile ambazo tunapeleka ni lazima, kwa mfano, sasa hivi Walimu wanapokwenda kwenye ajira, sasa hivi wote ni lazima warudishe vyeti vyao kwa mwajiri na mwajiri anavipeleka pale vinathibitishwa haraka kabla hata hajakaa muda wowote. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rajab umeridhika?

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sijaridhika kwa sababu Waziri ameshindwa hata kuonesha ukubwa wa suala hili kama ambavyo nilivyosema sisi tulifanya udadavuzi katika mitandao na tukalikuta ukubwa wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa 6% ya wale ambao wanaomba kazi katika *Public Organizations* wana *fake Academic Certificates*. Sasa unaposema kwamba sasa hivi tunaanza kuleta picha, tunafanya na mambo kama haya, hiyo haijawa *solution* ya kuondoa hili tatizo. Tunataka kujua ni kwa namna gani sasa Serikali kupitia Waziri wa Elimu na hatua ambazo amezichukua hata za kinidhamu kwa sababu hili suala lilikuwepo, hata za kinidhamu, kwa wale ambao wanafanya makosa kama haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tatizo ni kubwa sana la vyeti feki, bado naondoa shilingi. Naomba uwape nafasi wengine wachangie katika hili katika kuunga hoja yangu mkono.

**MWENYEKITI:** Haya simameni mnaotaka kuchangia. Wanatosha nilionao, tuanze na Mheshimiwa Sakaya kwa kifupi sana, kwa kifupi sana, dakika mbili mbili.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Rajab, suala la vyeti feki ni tatizo kubwa na ninaendeleza pale nilipoanza kuchangia asubuhi kuwa inazidi kudidimiza elimu yetu hapa Tanzania. Mheshimiwa Waziri hapo anasema kwamba vyeti vinawekwa picha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyeti vimeanza kuwekwa picha toka tukiwa *University* toka mwaka 2012, vyeti vyetu vina picha, vina *sign* na vina *serials,* lakini tatizo bado liko palepale. Kwa hiyo, kuweka picha kwenye cheti siyo *solution*, kuweka *serial number* siyo *solution,* tunataka tujue ni nini mkakati wa kuondoa tatizo hili kwa sababu haya yalikuwepo *ten years back* ambapo mpaka sasa tatizo liko palepale. Naunga mkono kwamba, ni lazima alete mkakati maalum wa kuondoa tatizo la vyeti feki.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Rajab. Hili ni tatizo kubwa sana na ndiyo linasababisha

wanafunzi wengi wakimbilie kufaulu mitihani badala ya kujifunza kwa sababu elimu ni *process* na tatizo hili limekuwa kubwa. Naomba Serikali irejee hata kwenye kitabu cha Msemakweli, Toleo la pili la dharura, linaonesha kuna Mawaziri, kuna Wabunge wako humu humu ambao ni Madokta feki, wana vyeti feki na ndiyo maana inakuwa ni tatizo kuwasimamia wananchi huko nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili ni suala nyeti ambalo ni lazima Serikali yenye nia ya dhati ya kuwa na elimu bora ni lazima tulisimamie, hawa watu hawajakanusha wako humu ndani tuko nao na ndiyo maana tuna Mawaziri mizigo kwa sababu wana vyeti feki wamepata nyadhifa kwa vyeti feki. Tunaomba Serikali isiwe na kigugumizi, tunaomba hawa watu waonekane hapa hadharani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali kwa kifupi sana.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nafikiri kama tunataka kutenda haki juu ya suala hili la uwepo wa vyeti feki, ninyi kiti mna mamlaka makubwa sana. Msako huo ungeanzia hapa hapa ndani kwa sababu kama inafikia watu wanatajwa ambao ni Mawaziri, ni Wabunge wana *PhD* feki, halafu Bunge lako Tukufu bado linakaa kimya, tutegemee kuwa watu bado watakwenda kupiga *deal* huko, hivi vyeti feki, taaluma feki zitatolewa humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale ambao mngewataka katika suala la uwajibikaji tu wa kawaida wakanushe na wathibitishe ni kwa namna gani ambavyo hawana taaluma feki ambazo ni digrii feki watusaidie. Vinginevyo tutegemee kuwa tatizo hilo litaendelea ku-*exist* kama hatuwezi kuanza kuwajibishana sisi wenyewe humu ndani. Wale waliotajwa hebu watuambie, walieleze Bunge lako tuanze hapa hapa kuwa ni kweli kuwa wana *degree* feki au siyo feki?

**MBUNGE FULANI:** Wakamatwe, wanyongwe kabisa.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Rajab.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa kadri ya taarifa nilizonazo mezani hakuna mtu yeyote ametajwa. Mheshimiwa Celina Kombani!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vyeti feki huko lilikuwa ni kubwa zaidi ukilinganisha na sasa hivi baada ya teknolojia kukua. Sisi kwa mfano, katika kudhibiti vyeti feki kwa upande wa Serikali, ndiyo maana Mheshimiwa Rajab anasema tunafanya, *scrutiny* ya hali ya juu sana kuhakikisha kwamba tunawasiliana na Wizara ya elimu na Baraza la

Mitihani ili tusiajiri Watumishi ambao wana vyeti feki. Ndiyo maana huo utandawazi umefanya mpaka Mheshimiwa Rajab aone kuwa, kuna hilo tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo zamani tatizo lilikuwa ni kubwa zaidi. Kwa upande wa Serikali yaani wafanyakazi wa Serikali sasa hivi tumeshafanya *verification* ya wale ambao wana vyeti feki, kutokana na mfumo wetu tulioufunga sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana unakuta wakati mwingine, baadhi ya Walimu wanachelewa kupata mshahara kama alivyosema Mheshimiwa Hawa kwamba Walimu 12 wa Manispaa ya Tabora hawajapata mshahara wao, kama ana cheti feki kwenye *system* yetu, cheti kile kinakataa, ina-*reject*. Kwa hiyo, hiyo ni mikakati ya Serikali kama wewe cheti chako ni feki huwezi ukapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo mifano, ni kweli wapo ambao utakuta kwamba shule ya Sekondari ya wasichana, aliye na cheti ni mvulana. Kwa hiyo, huu ni utandawazi, tumejitahidi kiasi cha kutosha kuhakikisha kwamba tunawasiliana na *NACTE* na vyeti hivi havitengenezwi Baraza la Mitihani vinatengenezwa mitaani. Baraza la Mitihani wanajitahidi kwa kiasi kikubwa sana kuhakikisha kwamba, hawatengenezi vyeti feki, viko mitaani na Wabunge msioneshe vidole wenzenu na ninyi mmo. *(Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** Nani, mtaje.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Ghasia umalizie kwa kifupi sana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napinga hoja ya Mheshimiwa Rajab ya kuondoa shilingi kwa sababu ya vyeti feki, kwa sababu Baraza la Mitihani silo linalotengeneza vyeti feki, vyeti feki vinatengenezwa mtaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi za Baraza la Mitihani ni kuhakikisha linadhibiti vyeti feki, haviingii katika Mtandao wa Serikali na ndiyo kazi inayofanywa na ndiyo maana Mheshimiwa Rajab ameweza kusimama hapa akisema kuwa Jeshini wamewarudisha, Polisi wamewarudisha, Magereza wamewarudisha, Sekretarieti ya Ajira wamewarudisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni kuonesha kwamba, Serikali inafanya kazi ya kudhibiti vyeti feki. Suala la ufeki kwa sababu baadhi yetu hapa si ajabu mnatengeneza hivyo vyeti feki, hata Wabunge wapo na Kambi ya CHADEMA mnaye Mbunge ana cheti cha form *four fake* tunamjua.

**WABUNGE FULANI:** Mtaje.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Yeye mwenyewe anajijua, hajafika *form four* na ana cheti cha *form four,* kazi ya Serikali ni kudhibiti na hakuna cheti feki kinachoingia katika *system* ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tutulie kidogo ili twende vizuri. Tuko kwenye hoja ya Mheshimiwa Rajab, alikuwa anataka Waheshimiwa Wabunge wachangie, hoja ya Mheshimiwa Rajab ni ya kweli, nilipokuwa Mjumbe nikiwakilisha Bunge hili kwenye Chuo cha *UDOM,* kwenye Baraza la Chuo, wakati ule Chuo kinaanza, Chuo kili-*advertise* kupata Maprofesa na watu wenye *Phds* kutoka maeneo mbalimbali.

Tulishangaa sana katika maombi yale tulipata maombi feki kutoka Uganda, maombi feki kutoka Kenya ya Maprofesa, maombi feki kutoka India, maombi feki kutoka maeneo mengi sana hapa hapa *UDOM*. Kwa hiyo, ni tatizo kubwa hili, siyo kwamba Waziri wa Elimu peke yake, nimekumbana nalo.

Mheshimiwa Rajab malizia ndugu yangu. Kwanza Mheshimiwa Waziri kwa kumalizia kabisa!

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kusema kwamba, Serikali imechukua hatua nyingi na muhimu na kupitia vitengo vyake siyo tu kile ambacho Mheshimiwa Rajab amekitaja cha Baraza la Mitihani, lakini pia Baraza la Elimu ya Ufundi *(NACTE)* na pia kupitia Tume ya Vyuo Vikuu ambayo kila Taasisi katika hizo imehakikisha inaweka mpango wa kudhibiti wa utumiaji wa vyeti feki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rajab ametoa takwimu ya 6% wana vyeti feki kutoka kwenye mitandao, siyo *credible data*. *Credible data* inasema *reference* fulani ambayo ama ni ya Kiserikali au ya Kitaasisi, kwenye mtandao kuna kila kitu ambacho unaweza ukakusanya sasa hivi na mitandao iko chungu nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Rajab aamini kwamba, juhudi hizi za Serikali ndiyo zimewezesha hivi sasa tuwe na amani kuwa Serikalini tuna-*comfort* kwamba hatuna Madaktari feki, Walimu feki, Polisi feki na kadhalika.

Sisi kama Wabunge tuna dhamana kubwa kwa sababu Halmashauri zetu zinaajiri, kama vile Polisi wanavyofanya kuthibitisha vyeti hivi kwa kuvipeleka kwenye Baraza, Halmashauri zetu sisi ndiyo Madiwani, ni lazima tuzisimamie kuhakikisha kwamba katika ajira wanazozitekeleza na ndiyo ajira nyingi, tusaidie Serikali katika kuhakikisha kuwa, hatuchukui wananchi wale ambao wanataka

*shortcut*. Kwa hiyo, namsihi Mheshimiwa Rajab azitambue juhudi hizi za Serikali na akubali kuniachia shilingi yangu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rajab unarudisha shilingi?

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sirudishi shilingi na inabaki kama ilivyo. Kuhusiana na *reference* nataka nimwambie kwamba *reference* niliyoichukua kama ambavyo nilimtaja hapa Bwana Kassim Nyaki ambaye ndiye *Information Officer* wa *Public Service Recruitment Secretariat* ambaye alifanya mahojiano na gazeti la *Citizen* na yeye ndiye ambaye ametoa taarifa hiyo na akaendelea kusema zaidi kuwa *most forged are those from VETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa siyo kwamba hii taarifa nimeokota tu mitaani, lakini lingine ni kwamba Mheshimiwa Waziri anasema vyeti hivi vinatengenezewa mitaani, siyo kweli kuwa vyeti hivi vinatengenezwa mtaani. Shule zinauza vyeti, vyuo vinauza vyeti na ninyi hili Wizara mnalijua na mnakaa kimya na hamlifanyii kazi wala hakuna Waziri alichokieleza kwamba, kuna hatua zozote za kinidhamu labda ziliwahi kuchukuliwa kwa watu ambao wamekamatwa na tatizo kama hili, wakati tatizo hili lipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo Vikuu vinajulikana kwa kutoa vyeti feki na hili Waziri analijua na Baraza la Mitihani linabariki haya mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuzi ni wako, labda hapa tupige kura mimi siko tayari kurudisha shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana mimi sina uamuzi katika hili, mtakaoamua ni ninyi.

Waheshimiwa Wabunge, tumeshajadili tayari na utaratibu wote umefuatwa, sasa naomba niwahoji, nitawahoji wale ambao wanakubaliana na Mheshimiwa...

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rage taarifa hiyo anapewa nani sasa?

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Aliyekaa.

**MWENYEKITI:** Hiyo tumeshavuka Mheshimiwa Rage kwa heshima na taadhima, samahani sana.

Sasa tuko katika wakati wa kupiga kura, ninaanza na kuwahoji watakao kubaliana na mtoa hoja ambaye ni Mheshimiwa Rajab, halafu na ambao watakaokuwa hawakubaliani. Tumeelewana eenh!

**WABUNGE:** Ndiyo.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina suala nyeti la Mloganzila. Chuo Kikuu cha Mafunzo ambacho kinajengwa kwa mkopo kutoka Korea na hivi juzi Mheshimiwa Rais ameweka jiwe la msingi na chuo kimeanza kujengwa, lakini hakiwezi kuendelea kama Serikali haitolipa dola milioni kumi na nane. Sasa nimeangalia katika vitabu vyote, hotuba ya Mheshimiwa Waziri, lakini pia vitabu vingine vyote vya kasma mbalimbali hizo, pesa hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Mkandarasi yupo pale *site,* ujenzi umeanza, *certificate* ya kwanza siku yoyote italetwa, lakini fedha hizi Mheshimiwa Rais alikwishaagiza zitolewe na Wizara ya Fedha iliji-*commit* kuzitoa na huo ni wakati mrefu, wakati kabla marehemu Mheshimiwa Mgimwa hajafariki na iko *commitment* ya Serikali *in writing* kwamba, watalipa, lakini kama hela hizi hazikulipwa vitu viwili vinavyoweza kutokea ni kwamba, kile chuo hakiwezi kuendelea kujengwa sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tutakacho-*suffer* ni *liquidated damages*, lakini huyu Mkandarasi mpaka leo hajaweza kumwajiri Mkandarasi Mkazi kwa sababu pesa hizi hazijapatikana. Sina haja ya kushika shilingi, lakini nataka *commitment* ya Serikali kama sikupata *commitment* basi nilitupe kwa sababu hiki chuo kitakapojengwa, kinajengwa na fani zote na ndio India ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Serikali inatumia fedha nyingi sana kupeleka watu India. Chuo hiki kitakuwa na fani mbalimbali ya kutibu magonjwa ya moyo, figo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa shilingi kama itakuwa sikupata jibu ambalo litaridhisha. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa ni dakika tatu, ni vizuri sana mkaji-*squeeze,* mtapata nafasi mlio wengi. Mheshimiwa Waziri ufafanuzi Mloganzila!

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi ufuatao kuhusu hoja ya Mheshimiwa Zarina kwanza niungane nae kwamba hii ndio India ya Tanzania na huu ni Mradi mkubwa ambao tunatarajia kuufanikisha chini ya Serikali shupavu ya Chama cha Mapinduzi, kuleta ukombozi katika Sekta ya Afya. Ule ni Mji wa Afya, sio Hospitali ya Afya bali ni Hospitali Kuu pamoja na Chuo cha Mafunzo ya sayansi za tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba, Mradi ule ulikuwa umefadhiliwa kimkopo na wahisani kutoka nchi ya Korea, lakini kwa sababu Mradi ule ulipoasisiwa miaka minne iliyopita pesa zile ambazo zilidhaniwa kwamba zingeweza kujenga hospitali ile wakati ule, hivi sasa wakati Mkandarasi anaanza kazi hazitoweza kutosha kufanya kazi hiyo.

Kwa hiyo, Serikali ya Tanzania ilipewa mawili na Serikali ya Korea aidha, kushusha hadhi ya Hospitali ile, kwa maana ya kupunguza ukubwa wa Hospitali ile ama kutoa *commitment* ya kuongeza dola milioni 18 katika mchakato wa ujenzi wa Hospitali ile. Mheshimiwa Rais ameagiza Hazina na imeshatoa *commitment* ambayo imewasilishwa kwa Serikali ya Korea kusema kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, haitapunguza ukubwa wa Hospitali hiyo, bali Serikali ya Tanzania inaji-*commit* kuongeza dola milioni 18 katika Mradi ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaanza kutumia pesa za Mhisani, lakini katika mchakato wa ujenzi huu tutazitenga pesa hizi kwa ajili ya ujenzi huu kwa sababu ujenzi huu hautamalizika ndani ya mwaka mmoja, ujenzi huu utaendelea katika kipindi hiki mpaka tutakapoanza mwaka wa fedha unaofuata, tutaweza kutenga pesa na ikishindikana tutafute taratibu zingine ambazo tutaweza kulipa hela ambayo tayari Serikali imechukua dhamana kwa Serikali ya Korea kuzitoa pesa hizo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Zarina natumaini umeridhika!

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani sana, lakini hicho sio kitu kilichopo *site*. Ilivyo *site* ni kwamba, wakati Mkorea analeta, huu ni Mradi mkubwa kweli ni wa dola milioni 76.5 ambazo Mheshimiwa Rais amezipata katika bei nafuu sana, *interest* ya 0.01, *grace period* ya miaka kumi, *repayment* ya miaka 15.

Sasa hivi yule anashindwa kuajiri Mkandarasi Mkazi kwa sababu hela hizo hakuna ambazo zilikuwa zitolewe mwaka huu wa fedha, sasa kama hazipo hata kwenye kitabu mwaka kesho zitatoka wapi? Atalipwa nini na wale wa Korea wanalipa *the foreign component, the local component* inalipwa na Serikali ya Tanzania. Nataka *commitment* ya Serikali kwamba hizi hela

watakwenda kuzilipa aidha, kabla ya bajeti kwisha ama *within the budget* hii nyingine, lakini hizi hela kama hazikulipwa huu Mradi hauendelei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja ya Mheshimiwa Zarina ni ya maana sana, nafikiri sio ya kubishana hapa, sijui labda Naibu Waziri wa Fedha kama una habari za ziada! Vinginevyo jambo kama hili inabidi tuwakabidhi Kamati yetu ya Bajeti kwa sababu kule mwisho ndio tutapambana na Waziri wa Fedha, bado Mheshimiwa Zarina una nafasi kule mwisho.

Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. A. MALIMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hili suala la chuo kama alivyosema Mheshimiwa Waziri tulikuwa na hizo *option* mbili za kupunguza ili na *contribution* yetu ibaki vile tulivyoitaka mwanzoni, lakini kwa sababu ya mahitaji yetu, tukasema hapana acha twende nayo hivyo hivyo.

Sasa ninachotaka kumuahidi Mheshimiwa Zarina, tumeshazungumza hilo jambo, ni kwamba kwa upande wa Hazina pamoja na vipengele vingine ambavyo vimo kwenye Sekta ya Afya, kama ulivyosema Mwenyekiti tunakwenda kwenye Kamati ya Bajeti na tunataka tulifanyie kazi, lakini hili linaonekana lina hiyo *time problem* aliyosema ya kwamba labda kabla ya *financial year* hii pawe na pesa fulani imeshakwenda hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuseme kweli pamoja na hili, yako mengine pia ambayo yana *deadline* hiyo ya kabla ya tarehe 30 *June* kabla hatujamaliza mwaka wa fedha. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Zarina akubali kwamba tunalifahamu, lina uzito wa kipekee, lakini pamoja na mambo hayo mengine mengine tunataka tuliweke humo ili tuangalie namna tutakavyolishughulikia, lakini Serikali tunaahidi kwamba, tutalifanyia kazi ili lisishindwe kwa sababu ya umuhimu wake kwa jamii na nchi yetu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ni ahadi hiyo, tunaipeleka katika Kamati ya Bajeti waliangalie. Kwa hiyo, tukifika kule mwisho sio lazima awe Mheshimiwa Zarina, tukumbuke wote kwamba kuna hili jambo la kulibeba kwa umoja wetu kwa pamoja.

Mheshimiwa Margaret Sitta!

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii nami niombe Serikali kutoa kauli kutokana na swali lifuatalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongea kwa niaba ya Kamati ya huduma za jamii nikiwa Mwenyekiti wa Kamati. Kwa kweli huu ni mwaka wa tatu mfululizo, sisi kama Kamati tumekuwa tukiomba Serikali kuona umuhimu wa kuunda chombo cha kuhudumia Walimu ili hata hayo malengo ya Serikali yanayotakiwa ya kupata matokeo makubwa sasa yapatikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wana matatizo ya kupata haki zao kutokana na mfumo wenye urasimu, hivi kuna ambaye hajui hili? Sasa imetubidi sisi kama Kamati kwa miaka mitatu, someni vitabu vya taarifa zetu, kwa miaka mitatu mfululizo mpaka tumekwenda ngazi za juu, jambo ni hilo hilo moja kwa moja bila kupata hatua zozote za utekelezaji.

Je, Mheshimiwa Waziri anasemaje kuhusu kutoa kauli ya kuunda chombo kimoja? Ama sivyo itabidi tutoe shilingi hapa tusiporidhika, lakini asitufikishe kwenye kutoa shilingi, ila ikibidi tutatoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka imebidi Kamati iazimie kuleta azimio Bungeni la kuitaka Serikali iunde chombo hicho. Wewe huoni kwamba Kamati imechoka? Kwa hiyo, nini kauli ya Serikali. Namwomba Waziri asinilazimishe kutoa shilingi. Nini kauli ya Serikali kuhusu kuunda chombo cha Walimu ili Walimu wapate huduma kwa haraka, wafanye kazi vizuri zaidi, tupate Matokeo Makubwa Sasa, nini kauli ya Serikali? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mama Margaret Sitta. Mheshimiwa Waziri wa Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mheshimiwa Celina Kombani ufafanuzi!

**MHE. CELINA O. KOMBANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili ni kweli, limeshaletwa mara nyingi na sisi Serikali hatukukaa kimya. Hatua ya kwanza ambayo tuliichukua, ni kuhakikisha kwamba, tunaimarisha zile *TSD* katika ngazi ya Wilaya, Mkoa mpaka Taifa, kuwapatia hela nyingi ili waweze kufanya vikao vyao vya kawaida.

Kwa hiyo, sasa hivi fedha za *TSD* zinafika katika *level* ya Wilaya na hiyo ni hatua ya kwanza wakati tunashughulikia kwamba tuwe na chombo kimoja au tufanyeje. Kwa hiyo, kwa mara ya kwanza kuanzia mwaka jana, *TSD* Wilaya wanapata fedha kwa ajili ya vikao vine; ambavyo ni *promotion,* nidhamu na vikao vyao vya kawaida. Hii ni kuimarisha ule uongozi wa walimu.

Pili, *paper* kuhusu chombo kimoja cha Walimu. *Paper* hiyo ipo katika ngazi ya Baraza la Mawaziri. Tutawasilisha katika Baraza la Mawaziri, baada ya kutoa msimamo, tutakuja kuwaeleza kwamba msimamo wa Serikali ni upi! Kwa

hiyo, hatua hiyo nilimweleza Mheshimiwa Mama Sitta kwamba tumefikia hapo na yeye akanishauri kwamba onana tena na wadau na nimemkubalia kwamba nitaonana nao. Sasa zaidi ya hapo tufanye nini?

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kwa mamlaka mliyonipa ndani ya kanuni, naomba niongeze nusu saa ili tumalizie malizie baadhi ya hoja zilizopo.

Mheshimiwa Mama Sitta!

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naiomba Serikali kama wengi walivyotanguliwa kwamba Serikali ya CCM ni sikivu. Usikivu ambao nawaza kuukubali siku ya leo, ni kuukubali ushauri alioutoa Mheshimiwa Celina kwamba tutakutana mara moja, mimi hiyo naikubali. Kwa sababu nilipoambiwa chombo kilichokwenda, kwanza kwa kusema kwamba, *TSD* inaimarishwa, *TSD* ni Idara ndogo sana ndani ya Tume ya Utumishi imeshindwa kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jawabu lake hapa ni kukaa pamoja na kuona mfumo gani wa chombo kimoja unaweza kufanya kazi kwa mazingira yetu hapa. Tunajua Serikali ina wasiwasi, Ma-*DED* wana wasiwasi, lakini mfumo huu unaweza ukaangaliwa, tukaona nafasi ya Ma-*DED* ni nini? Tusing'ang'anie kitu kilichoshindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa heshima na taadhima, tupate kauli ya Serikali kwamba tunaitwa kuzungumzia suala hili, mimi nakaa salama kabisa, Kamati yangu itafurahi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mama Sitta kwa ushauri uliotoa. Ni matumaini yetu kwamba, mwakani tutakapokutana patakuwa na hadithi nyingine. Kwa hiyo, hatua hii tuvuke.

Mheshimiwa Susan, Waziri kivuli!

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana…

**MHE. MAGRETH S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niwie radhi, sikusikia kauli ya mwisho ya Serikali imesemaje. Nisamehe!

**MWENYEKITI:** Ushauri uliotoa na majibu yaliyotoka ni kitu ambacho nyinyi Kamati na wao Serikali mwendelee kulifanyia kazi. Tukasema tu kwamba tutakapokutana mwakani matumaini yetu ni kwamba…

**MHE. MAGRETH S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakutana wapi?

**MWENYEKITI:** Majibu hayatakuwa haya haya kwamba, *paper* imeandikwa na Baraza la Mawaziri itakuwa na majibu mengine.

**MHE. MAGRETH S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisaidie tafadhali, hili jambo ni la muhimu, nini kauli ya Serikali? Ndio lilikuwa swali langu la msingi, naomba kauli ya Serikali, tunaitwa lini au kwa utaratibu gani? Nakuomba kabisa Mheshimiwa usirahisishe hili jambo.

**MWENYEKITI:** Sasa kutakuwa na kauli mpya basi haya, ruhusa tena…

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitoa shilingi basi…

**MWENYEKITI:** Sasa hukutoa Mama ndio maana tukaendelea!

**MHE. MAGRETH S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba hili suala la Walimu ni muhimu sana, nakuomba sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mama Sitta, Mwenyekiti wangu yaani tufuate tu utaratibu kama unatoa shilingi unatoa, tunaendelea na zile taratibu zile zingine za kawaida.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa tuongee.

**MWENYEKITI:** Umetoa eeh!

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Huo ndio utaratibu wake tunakwenda namna hiyo. Vinginevyo unakuwa umetoa ushauri wa kufanyiwa kazi. Kwa hiyo, shilingi imetoka, majibu ya Mheshimiwa Waziri, halafu mnachangia, halafu tunamalizia.

Mheshimiwa Waziri, majibu kwanza!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naona kwamba…

**MWENYEKITI:** Nimekosea utaratibu kidog, nadhani ni kwenye kuchangia kwanza, halafu Waziri si ndio? Kuchangia kwanza ili muweze kuandika.

Mheshimiwa Serukamba, Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Masoud na CHADEMA Mheshimiwa Mnyika! Mnatosha. Mheshimiwa Serukamba, haya!

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama hapa kuunga mkono hoja ya Mama Margaret Sitta, lakini niliomba kuongea, nilitaka niseme jambo ambalo kwa kweli linafanana sana na hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi wakati nachangia niliomba Serikali kwamba umefika wakati tuunde Tume, kujadili matatizo yetu yote ya Walimu na elimu ili tusitatue matatizo ya elimu *in a piece mill*, huyu anasema tutatue tatizo la wanafunzi, huyu atakuja kesho atatatua la *University,* nadhani umefika wakati tuunde Tume ya Elimu itakayoangalia mfumo wetu wote kuanzia *kindergarten* mpaka *University*, kuangalia matatizo ya Walimu, kuangalia kila kitu Mihtasari, vyote itatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikiunga mkono hoja hii, nadhani umefika wakati Serikali ikubali iunde Tume ya Elimu, ya watu waliobobea kwenye Elimu ili tuangalie tatizo la Elimu katika mapana yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ameunga mkono. Mheshimiwa Bulaya Ester!

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia. Naomba niseme moja kwa moja namuunga mkono Mheshimiwa Mama Margaret Sitta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mama Margaret Sitta ni Mwenyekiti wa Kamati amezungumzia miaka mitatu mfululizo, wamekuwa wakizungumzia tatizo hilo hilo na bila shaka majibu yalikuwa yale yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua ni jinsi gani Walimu wetu wanavyofanya kazi katika mazingira magumu na jiografia ya nchi yetu, Walimu walikuwa wakienda katika Halmashari unaona ni jinsi gani wanavyopigwa dana dana, wakienda huku wanaambiwa nenda kule, wakienda huku wanaambiwa waende huku. Sasa mwisho wa siku wanapoteza muda kwa ajili ya kushughulikia masuala yao katika Wizara zaidi ya moja, wakati kungekuwa na chombo kimoja, ingewarahisishia na hata kuweka utaratibu mzuri wa madai yao na kuweka mfumo mzuri kwa ajili ya kushughulikia matatizo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi najua ni sikivu, toeni *commitment,* lini mnaanza? Hilo ndio jambo la msingi, Mama Margaret Sitta analolihitaji ni hilo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Mheshimiwa Masoud dakika mbili pia!

**MHE. MASOUD A. SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta juu ya kupatikana kwa chombo kimoja cha kusimamia haki za Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwajiri anakuwa ni mwingine, lakini anayetunza nidhamu ni mwingine. Walimu wana matatizo mengi, fedha zao za kupandishwa madaraja imeongelewa kwa muda mrefu, fedha za likizo ni tatizo na matatizo mengine ya hapa na pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wamekuwa ni watu wa kutangatanga, kuhamahama, hawajui chombo gani wakamate, hawajui wapi waende, malalamiko yao ni mengi. Tatizo letu hatujakuwa na chombo kimoja mahsusi, maalum ambacho kitasimamia Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya CCM kama sikivu mbona hamsikii kwa hili? Kama hamsikii mnasikia jambo gani? Semeni kuanzia lini, kesho ama kesho kutwa, muda fulani tunakaa tunamaliza hili jambo. Sasa usikivu uko wapi? Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, ni hoja maalum, hoja nzuri ili kuweza kuwasaidia Walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, kifupi!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Margaret Sitta ya kuondoa shilingi. Ningependa Serikali izingatie, hoja hii si ya Mheshimiwa Margaret Sitta peke yake, ukisoma taarifa ya Kamati ukurasa wa 14, kipengele cha 5.6, Kamati yenye Wabunge kutoka Vyama vyote inasema:

"Serikali iangalie upya mfumo wa kuhudumia Walimu kwa kuanzisha Tume ya Utumishi wa Walimu ili kukabiliana na adha zinazowakabili Walimu nchini." *(Makofi)*

Kwa hiyo, hatutarajii katika mazingira kama haya, jambo hili liwe na kura ya hapana. Mheshimiwa Waziri amesema kwamba na amesema kauli mbili tofauti; kauli ya kwanza alisema Waraka umeandaliwa utapelekwa kwa Baraza la Mawaziri, mara ya kwanza alisema limepelekwa kwa Baraza la Mawaziri.

Sasa ili Bunge litekeleze wajibu wake vizuri wa kuisimamia Serikali, tunahitaji kauli ya Serikali hapa ni lini hasa chombo hiki kitaundwa na kama

Serikali haitoi kauli basi Serikali iulete mbele ya Bunge hili iuweke mezani, huo waraka ambao Serikali inasema imeshaandaa, ili tuwe na ushahidi wa kweli, hilo pendekezo limeandaliwa, muundo wake ni upi, tuwe na uhakika chombo kinaundwa kweli kweli, kwa sababu maslahi ya Walimu ni jambo linalotuunganisha wote, kwa sababu elimu bora inategemea Walimu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa na chombo cha Walimu, tutakuwa na chombo ambacho kitaungana na madai ya Walimu katika kuhakikisha madeni ya Walimu yanalipwa, mazingira ya Walimu yanaboreshwa badala ya sasa ambapo sauti ya Walimu haisikiki vizuri. Kwa hiyo, naunga mkono jambo hili na naamini Wabunge wote watapiga kura ya pamoja ya kulikubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hawa Ghasia, mchangiaji wa mwisho!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nisiunge mkono hoja ya Mheshimiwa Mama Sitta, kwa sababu alisema anaomba *commitment* ya Serikali, aliiomba wakati Waziri wa Utumishi anatoa hiyo hoja na Waziri wa Utumishi alimkubalia kwamba, ataitisha kikao cha wadau tujadiliane kwa sababu waraka upo ndani ya Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aliomba lazima tukae na wadau kwa sababu unapokaa na wadau unachelewesha muda wa kukaa kwenye Baraza la Mawaziri. Si hivyo tu, Waziri amemkubalia wakutane na wadau na leo ameomba *commitment* ya Serikali, Serikali wamemwambia iko kwenye Baraza la Mawaziri na tuko tayari kukutana na wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *commitment* zaidi ya hapo ni nini? Yaani amwambie kesho kinaanzishwa? Unapoanzisha chombo ni lazima ustadi, ni lazima upite kwa wadau, upite kwenye Baraza la Mawaziri, uangalie faida zake na hasara zake. Nikiwa Utumishi nilishapeleka Waraka kwenye Baraza la Mawaziri kuomba hicho chombo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara ya kwanza nikarudishwa kwa sababu hata kwenye Baraza la Mawaziri unaweza ukaenda na kitu Mawaziri wenzako wakakupiga kikumbo, ukarudi. Nilipeleka mara ya kwanza nikarejeshwa, nikaenda mara ya pili, tukapitisha. Ilivyopita mara ya pili, kikaonekana kile kitu hakitekelezeki kitazamwe upya na ndiyo kazi ambayo inatazamwa sasa hivi, hicho ambacho mimi nilikipendekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukatai analolipendekeza, tunalikubali, lakini atupe muda, ameomba tukutane na wadau tumekubali, tupo kwenye Baraza la Mawaziri sawa, sasa *commitment* ipi zaidi ya hiyo anayoitaka, ndiyo maana siungi mkono hoja.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali, kuhusu utaratibu.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo inaeleweka kwa mujibu wa Ibara ya 63, kazi ya Bunge ni kuishauri Serikali na kuisimamia Serikali. Ni ajabu sana kama tutaendelea ku-*rely* kwenye *opinion* za viongozi wanaotokana na Serikali kwamba Waziri anaweza akapeleka kitu kwenye Baraza la Mawaziri, ikapigwa kikumbo halafu na Bunge lako likakubali kana kwamba Serikali ndiyo inatoa *directives* kwa Bunge, chombo ambacho kina mamlaka ya kuisimamia. Ninadhani itakuwa siyo sahihi, ni wakati sasa Bunge liiagize Serikali itoe *commitment* juu ya masuala haya. Haiwezekani kwamba tukawa tunaisikiliza Serikali, tuoneshe mamlaka ya kuisimamia Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali naona unateka nyara hoja, hoja siyo ya kwako, yupo mwenye shilingi yake, hayo maneno kama ni maneno ya maana atayasema yeye. Naomba uzime *microphone* yako. Waziri anayehusika na jambo hili!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti…

**MWENYEKITI:** Naona Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu amesimama, utamalizia Mheshimiwa Waziri Celina.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya mtoa hoja, nataka nimwombe, hata mimi nimeshawahi kuzungumza na Mwalimu Margaret Simwanza. Mheshimiwa Margaret anaumia kwa sababu naye ni Mwalimu, lakini nyuma yake ana Walimu wengi na kwa kweli jambo hili ni kubwa. Humu ndani Makofi mengi yanapigwa wadau ni wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kumwomba mama yangu Margaret ni kutaka kumhakikishia kwamba, kama Serikali tutahakikisha ile *commitment* ya Waziri inatekelezwa. Serikali itakaa na wadau, wadau hao muhimu ni pamoja na Kamati yako mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo *commitment* ya mwisho ambayo nataka nikupe mama Margaret, kama hii unaridhika basi ukubali tu kwamba,

Serikali tunakubaliana na *commitment* hii kwamba tutakaa na wadau ikiwemo Kamati yako katika kupitia upya jambo hili ambalo tayari tumesha-*advance*. Kama hilo unaridhika Mheshimiwa Margaret, basi nitafurahi sana kama ukitoa shilingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Celina una jambo la kuongezea ili umalizie, baadaye tumpe Mama Sitta.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikubaliane tu na Mheshimiwa Lukuvi, ndiyo jibu letu hili kwamba tutakutana na wadau.

**WABUNGE FULANI:** Lini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI:** Hiyo lini unajua huwezi ukatoa *commitment* wewe peke yako kama Celina Kombani, natoa *Commitment* kama Serikali, kama tumeji-*commit* kama Serikali kwamba tutakutana nao, tutakutana nao kwa wakati muafaka.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza nikarudisha shilingi, Serikali ikubali kwamba, tukutane kabla Bunge la Bajeti halijakwisha, hapo nakubali, kabla Bunge la Bajeti halijakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni la miaka mingi, kabla ya Bunge la Bajeti halijakwisha, nakubali kurudisha shilingi, naomba hilo. Namshukuru Mheshimiwa Lukuvi ameongea vizuri, Mheshimiwa Celina Kombani ameongea vizuri, sasa wamalizie kwamba kabla ya Bunge la Bajeti halijakwisha, hapo nitarudisha shilingi kwa raha kabisa.

**MWENYEKITI:** *Commitment*, nini tatizo kukutana kabla ya bajeti kwisha?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana naye, wadau namba moja ni Kamati yake, lakini kuna wadau wengine.

**WABUNGE FULANI:** Aaah! Kamati ni wadau namba moja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI:** Yeye kwa Kamati yake ni sawa, lakini *stakeholders* wa Elimu ni wengi sana. Kamati yake *yes* kabla ya Bunge.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa mama Sitta, kwa kifupi sana.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba wamekubali na *Hansard* naomba iandikwe hivyo kabla ya Bunge la Bajeti

halijakwisha. Idadi ya Wadau hata wakiwa wote waje tu, lakini kabla ya Bunge la Bajeti kwisha. Nawashukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mama Margaret Sitta kwa hoja hiyo na bahati nzuri katika mfumo wetu wa uongozi, Waheshimiwa Mawaziri wote ni Wabunge, wanaona joto lililopo hapa. Hivyo, ikija mwakani Mawaziri wamekaa na kurudisha hicho kitu, basi tutaelewana hapa ndani.

Waheshimiwa Wabunge, Mama Sitta amerudisha shilingi, kwa hiyo, hatutahoji chochote. Waziri Kivuli sasa kwa heshima yako.

**MHE. SUZAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa nataka kuweka mambo sawa kidogo, nataka nimhakikishie Waziri kwamba Kambi ya Upinzani inafanya tafiti za kutosha na huo utafiti tulioutoa, tumeutoa kwenye *Southern African Region Universities* na ndiyo huo ulituambia kwamba idadi ya wasomi katika Vyuo Vikuu vya Tanzania ni 2.9 ambayo na ninyi mnaikubali. Hii niliyoitoa ya tafiti ni ya mwaka 2010 na siyo 2013 kama ulivyosema. Hivyo, nataka nikuhakikishie kwamba tunafanya utafiti wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la kisera na nitazungumzia suala la miundombinu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni Chuo kikongwe kuliko Vyuo vyote hapa nchini hamna anayelikataa na nina hakika Wabunge wengi humu ndani ambao ni *graduate* wamepita katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo kile sasa hivi kina takribani wanafunzi 22,000, lakini nataka nikwambie chuo kile ambacho na wewe ulipita kama mwanafunzi wangu nikiwa nakulea, kwamba Chuo kile kina matatizo makubwa sana ya miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwaka jana chuo hiki *of course* ni pamoja na Chuo Kikuu cha Ardhi ambacho kilikuwa ni sehemu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kwa hiyo ninapoongelea Chuo Kikuu cha Dare s Salaam naongelea pia na Chuo Kikuu cha Ardhi sasa hivi. Majengo yale yanatisha, wanafunzi wameongezeka Vyuo viko vile vile, bweni namba tano na namba mbili ni hatarishi. Mwezi wa Tatu nakumbuka kulikuwa na tetemeko, wanafunzi wakakimbia kwa sababu jengo lile la *hall five* huwa linatetemeka sana, kwa hiyo wanafunzi wako hatarini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ongezeko kubwa hilo la wanafunzi na miundombinu kuwa mibovu kiasi kwamba sasa hivi hata *seminars* hawaingii tena kutokana na matatizo haya, lakini hali ni mbaya na hakuna utaratibu wowote wa kukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *commitment,* naona hapa wametoa shilingi bilioni mbili na laki saba kwa mwaka huu, lakini mwaka jana walikuwa hawajatoa. Kibaya zaidi ni kwamba kwenye randama inaonesha ni milioni mia saba.

**MWENYEKITI:** Malizia Mheshimiwa.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua kwamba Vyuo hivi Vikuu vikongwe vinakarabatiwa lini na kama sitapata ufafanuzi wa kina, naomba kusema kwamba nitatoa shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Susan anachosema ni kweli, miaka hiyo nikijiunga Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka wa kwanza nilimkuta pale akiwa msimamizi wa bweni Namba Sita na alinikabidhi godoro. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Susan Lyimo kama ifuatavyo:-

Moja, sijawa mwanafunzi wake. Usi-*judge* upya wa kitabu kwa *cover* yake…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan Lyimo alimaanisha mimi siyo wewe Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, randama ninayo hapa Fungu 46 kama inavyosoma, ukurasa wa 88, kwamba ukarabati ambao tumeutenga kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni shilingi bilioni mbili na milioni mia saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kinalikumba pia Vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu Vishiriki vingi vya Umma ambavyo jumla yake ni Vyuo 11. Serikali inalitambua jambo hili na ni changamoto ya kimaendeleo kwamba hatukubaki na chuo kimoja kama tulivyoanza wakati wa uhuru na wala siyo vichache vile ambavyo vilikuwepo wakati Awamu ya Nne ikiingia madarakani. Hii ni changamoto ya Maendeleo ambayo rasilimali fedha namna ya kuzigawa katika eneo letu hili la sekta ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanzisha mpango ambao tumewashirikisha wahisani Benki ya Dunia chini ya Mpango wa *Science*, *Technology, Higher Education Program* ambayo kwa kifupi tunaita *(STEP)*. Kule tuna dola milioni mia moja za benki ambazo tumezigawa katika Vyuo vyetu Vikuu kwa ajili ya kazi ya ukarabati na ujenzi mpya ili tuvihuishe na tuviwezeshe kuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kufundisha. Vyuo kadhaa vimefaidika katika mpango huu kikiwemo

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu Huria, Chuo cha *SUA*, *MUCE* ambayo iko Iringa, *DUCE* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kwamba haijatosha wala haijaturidhisha sisi kama Serikali pale tulipofikia, lakini juhudi hii tutaendelea nayo. Mojawapo tumeshafanya maongezi na *World Bank* kwa ajili ya kuendeleza mradi wa *STEP,* awamu ya kwanza imekwisha lakini tumeanza *negotiation* ili tuingie kwenye awamu ya pili ambapo tutapata fedha zingine kwa ajili ya kuendeleza mradi huu, ili Vyuo vyetu tuweze kuvirudisha katika hadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimesomea Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, nimefundisha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na sasa ni Waziri na ninavitembelea Vyuo Vingi vyetu vya Umma hasa vile vikongwe, kweli tuna tatizo ambalo sasa tunalishughulikia. Ukitembea sasa hivi sivyo kama ilivyokuwa kabla hatujaanza mkakati wa kuvikarabati na kuvirudisha katika hali nzuri ya kuweza kufundisha na kujifunza.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshiiwa Waziri, bado sijaridhika kwa sababu kama nilivyosema, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni Chuo Kikongwe na cha zamani sana na kwa maana hiyo, ukarabati wake unatakiwa uwe *unique*. Waziri anajibu kusema kwamba Vyuo vimeongezeka lakini kuna Vyuo kama *University* of Dodoma hivyo ni vipya, hivyo bado vile Vyuo vya zamani kama Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ninachokisemea hawajakifanyia ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumuuliza Waziri, Vyuo vyetu vingi kazi kubwa ya Vyuo ni *consultancy, research* na kufundisha. Ninachotaka kujua, *University of* Dar es Salaam ina mradi mkubwa sana wa Mlimani *City*, ni kwa nini fedha ambazo zinapatikana kutoka Mlimani *City* ambayo kimsingi kwa mfano athari zozote zitakapotokea pale Mlimani *City* kama ilivyotokea kule *West Gate* Nairobi, waathirika wakubwa watakuwa *University of* Dar es Saalam, wakazi wa pale na wao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mradi ule ni mkubwa sana na unaingiza fedha nyingi sana, ni kwa nini Wizara au Serikali isiruhusu fedha kiasi fulani zinazotokana na mradi huo ziwe zinatumika kukarabati Chuo Kikuu. Nazungumza hivi kwa sababu mfano Chuo cha Ardhi pamoja na kwamba wanatoa watalaam wengi sana, wanafanya *consultancy*, kutokana na mafunzo waliyonayo wamekuwa wakifanya kazi nyingi sana. Mwaka jana wameweza kujenga ofisi zao sita wenyewe kwa fedha zao za ndani.

Najiuliza kwa Chuo Kikubwa kama Chuo Kikuu chenye miradi mbalimbali kwa nini Serikali isiruhusu waweze kuchukua miradi kwa mfano kama walivyosema wa Mlimani *City* ili wenyewe waweze kujigharamia, waweze

kukarabati angalau tuone mwaka huu wamekarabati, *let say hall five*, mwaka ujao wanakarabati kitu kingine ili Chuo kile kirudie hadhi yake. Ukizingatia kwamba Mawaziri wengi Wakuu wamepita Chuo hiki, kwa nini tusiweke heshima ya Chuo hiki. Bado nasisitiza kwamba natoa shilingi na naomba Wabunge waniunge mkono.

**MWENYEKITI:** Sasa kwa sababu muda haupo upande wetu, naomba tupate watu wawili tu wachangie Mheshimiwa Esther Matiko na Mheshimiwa Rashid.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nimesimama kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Susan, Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kabisa kwamba Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni kikongwe na kwa bahati mbaya zaidi siyo tu kwamba ni zile *hostel* zimechoka, miundombinu yote pale kwa ujumla imechoka. *Lecture theater* zake zimechoka na kwa sasa hivi haziwezi ku-*absorb* idadi ya wanafunzi wanaokwenda pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijawa Mbunge nilikuwa nafundisha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, unafundisha wanafunzi wengine mpaka wanakaa nje. Mheshimiwa Waziri anasema kwamba, wanatenga fungu kwa ajili ya kukarabati hivi vyuo na kuvijenga vingine na kuviendeleza. Najiuliza Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni Chuo cha kwanza kabisa Tanzania na ni chuo ambacho kimesomesha watu wengi humu Mawaziri na Wabunge ambao hawana vyeti feki, ni Chuo ambacho kinatambulika duniani na Afrika. Kwa nini wasikipe *priority* kuboresha miundombinu ya kile chuo, kuanzia *hostel, lecture theater* hata *teaching aids* mpaka sasa hivi Wahadhiri wa Chuo Kikuu wanafundisha kwa chaki, kipindi hiki! Una wanafunzi wengi hauna hata zile *speaker* ambazo unaweza ukawa unaongea wanafunzi wasikie kwenye *lecture theater* zingine. Kwa hiyo ni aibu sana.

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kuwa na elimu nzuri na bora, isiyokuwa na vyeti feki na Mawaziri feki na Wabunge feki, tuboreshe kile chuo ambacho ni cha mwanzo kabisa kudumisha elimu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Susan Lyimo. *(Makofi)*

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Susan kuhusiana na Chuo chetu Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Dar es Salaam ni Chuo cha kihistoria, ni chuo ambacho kimetoa mazao ya kuendesha Taifa hili. Nashangaa sana kwa Serikali hii kukiangalia Chuo kile bila kukipa uwezo ambao unastahiki. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ndiyo sura ya Taifa, ukienda Kenya na Marais mbalimbali wamepitia Dar es Salaam. Tanzania imefika hapa kwa mazao ya Chuo kile. Leo Waziri anakuja hapa anatoa maneno mepesi kabisa. Hakuna *discussion* katika suala hili. Ni lazima chuo kijengwe na kiwe kizuri na kivutie Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, nashukuru sana.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Moja ni kukiri kwanza kwamba tuna kazi kubwa ya kukarabati miundombinu ya Vyuo vyetu vikongwe kikiwemo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kampasi ya Muhimbili *MUHAS* na Vyuo vingine ambavyo ni vya Serikali. Hiki ambacho ndiyo cha awali kabisa kina *particular significance* kwa nchi hii, lakini kwa kutambua uzito wa tatizo hilo ndiyo maana katika bajeti ya mwaka huu, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni mbili na milioni mia saba kwa ajili ya ukarabati wa Chuo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni fedha za ndani za Serikali ili kuweza kuungana na fedha za mkopo za *World Bank* katika programu za *STEP* ambayo imefanya upanuzi na ukarabati katika chuo hicho, lakini pia Serikali haizuii chuo kile ambacho kina mapato yake chenyewe kuweza kujipangia kutumia katika ukarabati mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha hela hizi za ukarabati mwaka huu wa fedha Serikali imekitengea Chuo Kikuu cha Dar es Salaam maduhuli ya jumla ya shilingi bilioni hamsini na sita milioni mia tano na kumi na sita, laki sita na elfu sitini na nane, ili kuweza kuendesha chuo kile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ambayo wanaifanya pamoja na *consultancy* au mradi wa Mlimani *City* ambao hivi sasa unawapa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wastani wa shilingi milioni mia kila mwezi ambayo inakuja kama bilioni na kitu kwa mwaka, pesa zile zinabaki chuoni na zinaweza zikatumika kwa mipango ya chuo kwa kila hali ambayo wangependa kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba inatenga pesa zaidi kwa ajili ya kuviweka Chuo hiki katika hali nzuri na hiyo ndiyo *commitment* ya Serikali na hivyo ndivyo ambavyo tutaendelea kufanya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan kwa kifupi sana kwani muda haupo upande wetu.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza nataka niweke mambo sawa, Waziri anaposema habari ya Maduhuli, haya maduhuli hata siku moja hayaendi kwenye miradi, haya mara nyingi inakuwa ni matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *sorry*, wakati Mheshimiwa Rais anakwenda Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wakati kinatimiza miaka hamsini akiongozana na Mheshimiwa Mnyika na mimi nilikuwepo aliahidi kwamba wakati wa michango alichanga shilingi milioni tatu na laki tano na baada ya hapo akasema kwamba wangekuja kuongeza kwenye bajeti ili waweze kufanya ukarabati. Vile vile akaahidi kwamba wangetengeneza *Student Centre* ya bilioni 18 lakini hela hiyo haionekani mahali popote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri anasema kwamba kuna fedha za *World Bank,* kwenye kitabu cha maendeleo hakuna mahali panaonesha hela za *World Bank* zinakwenda kufanya ukarabati Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. *Concern* yangu sasa hivi ni kwamba, wanafunzi wako katika hali hatarishi sana, yale mabweni yako hatarini kuanguka. Sasa hivi bweni moja lililokuwa linachukua wanafunzi 300 sasa hivi linachukua wanafunzi takribani 800-1000. Hivi yakianguka yale majengo ina maana tunakuwa na wanafunzi zaidi ya 1500 wanafia mle ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itoe *commitment,* watakarabati lini hasa *hall five* na *hall two* ambayo yapo katika hatari ya kuanguka.

**MWENYEKITI:** Umesharudisha shilingi enhee?

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Hapana.

**MWENYEKITI:** Tumefika mahali pa maamuzi sasa utaratibu wetu ni ule ule wanaoafikiana na Mheshimiwa Susan Lyimo na ambao hawataafikiana nao.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan Lyimo hoja yako imetupwa.

Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda kama mnavyoona saa yetu, naomba tuingie katika utaratibu wa *guillotine*. Wengine mniwie radhi majina yenu ninayo lakini muda hauko upande wetu. Katibu tafadhali!

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts … … Tshs.*1,258,016,000/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning… … … Tshs.* 3,984,782,000/=
Kif. 1004 - *Internal Audit Unit… … … … …Tshs.* 609,113,000/=
Kif. 1005 - *Procurement Management Unit… … … … … … … … … Tshs.* 968,097,000/=
Kif. 1006 - *Government Communication Unit… … … … … … … … … Tshs.* 458,490,000/=
Kif. 1007 - *Legal Unit… … … … … … … Tshs.* 603,842,000/=
Kif. 2001 - *Commissioner for Education… … … … … … Tshs.* 12,513,888,000/=
Kif. 2002 - *Inspectorate… … … … … Tshs.* 18,220,232,000/=
Kif. 3001 - *Basic Education… … … … … Tshs.* 641,580,000/=
Kif. 3002 - *Adult Education and Non Formal Education… … … … Tshs.* 1,256,007,000/=
Kif. 4001 - *Secondary Education… … … Tshs.* 364,172,000/=
Kif. 5001 - *Teachers Education… … … Tshs.* 48,491,490,000/=
Kif. 7001 - *Higher Education… … … Tshs.* 218,618,924,000/=
Kif. 7002 - *Tech. and Vocation Training Division… … … … Tshs.* 13,125,415,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**FUNGU 46 - WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**

Kif. 1001 - *Admnistration and Human Resource Management … … … … … ..Tshs.* 600,000,000/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning… … … Tshs.* 322,783,288,200/=
Kif. 2001 - *Commissioner for Education… … … … … … Tshs.* 1,931,920,240/=
Kif. 2002 - *Inspectorate… … … … … … Tshs.* 750,000,000/=
Kif. 3001 - *Basic Education… … … … Tshs.* 15,405,840,860/=
Kif. 4001 - *Secondary Education… … Tshs.* 12,210,570,100/=
Kif. 5001 - *Teachers Education… … … Tshs.*12,961,280,000/=

Kif. 7001 - *Higher Education… … … … Tshs.* 85,600,433,600/=
Kif. 7002 - *Tech. and Vocational*
*Training Division… … … … …Tshs.* 2,570,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge naomba tukae. Mheshimiwa Waziri taarifa.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Taasisi zake kwa mwaka 2014/2015, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo, naomba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali na kuyapitisha makadirio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka 2014/2015, Yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu kwa Wizara yetu hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu Profesa, Wakurugenzi wote, Makamishana na Watumishi wote na kipekee Walimu wetu kote nchini kwa kazi nzuri na kubwa wanayofanya.

Pia mzipokee pongezi za Waheshimiwa Wabunge ambazo wamezitoa, kwa sababu ninyi ndiyo roho ya Taifa letu. Tunajua kabisa bajeti tuliyowapa ni ndogo, lakini ni hali halisi ya uchumi wetu, kadri itakavyowezekana wakati ujao, bajeti hii itakuwa ikiboreshwa. Kwa niaba ya Bunge hili, niwapongeze tena na kuwatakia kila la kheri katika mwaka wa fedha ujao.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno hayo, kwa vile kazi zilizopangwa kwa siku ya leo zimekamilika na muda haupo upande wetu, naomba sasa nichukue fursa hii kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 2.27 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne,*
*Tarehe 20 Mei, 2014, Saa Tatu Asubuhi)*